# Mwana Mkuu wa Ibrahim

**Majibu ya "Wana wa Ibrahimu"**

Na

Jamil R. Rafiq B.Sc.

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

# Mwana Mkuu wa Ibrahim

Majibu ya "Wana wa Ibrahimu"

**Mwandishi:**

Jamil R. Rafiq B.Sc.

Chapa ya Kwanza: 1977
Chapa ya Pili: 1981
Chapa ya Tatu: 2000
Chapa ya Nne: 2025

**© Islam International Publications Ltd.**

**Kwa Maelezo Zaidi:**

**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031
Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

For further information please visit:
www.alislam.org

Cover design: Nauman Hadi

**ISBN:** 978-1-84880-644-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# YALIYOMO

**KISHA UKAJA MSAADA WA MWENYEZI MUNGU**.....i
**NENO LA MBELE** ........ iii
**UTAMBULISHO WA MWANDISHI** ........ v
**BI. HAJIRA, BINTI WA MFALME**........ 1
Ismaili na Isaka wote Watabarikiwa ........ 3
Jiwe Kuu la Pembeni ........ 4
Namna Tatu za Wana wa Ibrahimu........ 4
**SEHEMU YA KWANZA**........ 9
Wauza Watumwa ni Waisraeli........ 9
Hakuwaiga Wayahudi ........ 9
Tofauti katika Kurani na Biblia........ 10
Kuumba Ndege ........ 11
Maisha ya Mtume[saw]........ 13
Mume Mwaminifu........ 14
Vitabu Mbinguni........ 15
Vinywa vya Manabii........ 16
Fumbo la 'Utatu'........ 17
Wapagani Wapingwa........ 17
Wayahudi ........ 18
Mtume[saw] na Wakristo........ 19
Mungu Habadili Nia ........ 22
Vita vya Muhammad[saw] ........ 24
Dini na Siasa Kuandamana........ 26
Abu Sufyan........ 28
Vita ya Uhud ........ 29
Ndoa za Muhammad[saw] ........ 30

Amri Kuu ya Yesu .................... 31
"Tumerahisisha Mambo" .................... 32
Mwana wa Kupanga .................... 33
Hiana Nyingine .................... 34
Zainabu Anaolewa na Mtume[saw] .................... 35
Kisa cha Uwongo .................... 37
Si Mjakazi, Bali Mke .................... 39
Uwongo Mwingine .................... 39
Haki za Pekee .................... 41
Adabu za Kuingia Nyumbani .................... 42
Cheo cha Wakeze Mtume[saw] .................... 42
Sheria ya Shungi .................... 43
Utume wa Muhammad[saw] .................... 45
Mtume na Nabii .................... 45
Kuhani .................... 46
Idadi ya Mitume .................... 47
Ardhi Inazunguka .................... 47
Hakuweka Msingi Mpya .................... 48
Mwana Sio Mwisho .................... 48
Bwana ni Nani? .................... 51
Matarishi Wengi, Habari Moja .................... 52
Maandiko Yametimia .................... 53
Mtume Muhammad[saw] kwa Dunia Nzima .................... 55
Maana ya Utume .................... 57
Pombe .................... 58
Watumwa wa Mungu .................... 59
Msaidizi: Roho wa Kweli .................... 60
Yesu – Mtumishi wa Mungu .................... 63

Torati, Injili na Kurani .......... 64
Vitabu vya Mungu Hutokea Wapi? .......... 66
Miujiza ya Mtume[saw] .......... 67
Siyo Mashairi .......... 67
Kurani na Injili .......... 68
Uthman[ra] Hakukusanya Kurani .......... 71
Waalimu wa Kurani .......... 71
Kurani katika Jalada Moja .......... 72
Waandishi wa Kurani .......... 73
Uhakikisho Zaidi .......... 73
Uthmani[ra] Alifanya Nini? .......... 74
Usahihi wa Kurani .......... 77
Mitume wa Yesu .......... 77
Upungufu wa Imani .......... 78
Kutayarisha Vita? .......... 79
"Mti na Matunda yake" .......... 79
Kutangua Dini zote .......... 79
Unabii Uliotimilika Zamani .......... 80
Ujamaa wa Kiislamu .......... 80
Kwa Nini Agano la Kale? .......... 81
Uislamu Umetimiza Vitabu Vya Kale .......... 81
Sheria za Zamani .......... 81
Kupenda Usafi .......... 84
Wasemaje Juu ya Nafsi Yako? .......... 85
Asionekane Mpole .......... 85
Mambo ya Ahera .......... 86
Kutenda Dhambi .......... 86
Hana Mamlaka .......... 87

Kwa Waarabu? ..... 87
Kundi Moja ..... 87
Kuomba Mara Sabini ..... 88
Wasitoke Bila Ruhusa ..... 88
**SEHEMU YA PILI — UENEZI WA ISLAM** ..... 91
Abu Bakr[ra], Khalifa wa Kwanza ..... 91
Dhimmi ..... 92
Umoja Unavunjika ..... 94
Jina Ali ..... 94
Khalifa ..... 95
Umoja Utapatikana Tena ..... 95
Islam katika Afrika ..... 96
Afrika ya Mashariki ..... 97
Utumwa ..... 97
Picha ya Mtumwa ..... 98
Msaada wa Waarabu ..... 98
A. Njia ya Biashara ..... 98
Mitume wa Kristu ..... 100
Hirizi na Upali ..... 102
Ukristo na Uislamu ..... 103
Utumwa ..... 103
Kanisa la Katoliki Liliendesha Utumwa Afrika ..... 104
Papa Afundisha Utumwa ..... 105
Watumwa Walichukuliwa na 'Yesu' ..... 106
Mbwamwitu ..... 109
Utawala ..... 110
Sababu Nyingine ..... 111
Uislamu Chini ya Ukoloni wa Kikristo ..... 112

Masomo Yana Faida ........................................................ 113
Hila ya Padre ........................................................ 114
Katika Taifa la Kisasa ........................................................ 116
Taifa Liandamane na Dini ........................................................ 117
Dini Iandamane na Maisha ........................................................ 118
Maisha ya Mwislamu ........................................................ 119
Mtoto Azaliwapo ........................................................ 119
Jando ........................................................ 120
Chuo ........................................................ 120
Ndoa ........................................................ 120
Talaka ........................................................ 121
Nguzo za Dini ........................................................ 122
Ramadhani ........................................................ 122
Zaka ........................................................ 122
Sikukuu ........................................................ 122
Kuaga Dunia ........................................................ 122
Umoja Uliovunjika ........................................................ 123
Ahmadiyya ........................................................ 123
Jihad ........................................................ 124
Ahmadiyya na Wakristo ........................................................ 124
Yuz Asaf ........................................................ 126
**SEHEMU YA TATU** ........................................................ 127
Somo 1. Nani Aliye Mwana wa Ibrahim ........................................................ 127
Somo 2. Vitabu Mbalimbali Tatizo ........................................................ 127
Mungu ni Baba ........................................................ 128
Usafi wa Moyo ........................................................ 129
Matayarisho ........................................................ 131

Somo 3. Waislamu na Wakristo Wanategemea Mitume Mbalimbali ........ 132
Mpendwa Wangu ........ 135
Sallallahu 'Alaihi Wasallam ........ 136
Padre Anajipinga ........ 137
Somo 4. Mungu Mmoja Yesu na Maria ........ 137
Kurani Yataja Utatu ........ 138
Ufunuo wa Yesu ........ 139
Baba Aabudiwe ........ 140
Mungu Yu Karibu ........ 140
Mungu ni Rahmani ........ 142
Utatu ........ 143
Ufunuo Kukamilika ........ 144
Mama Wa Mungu ........ 144
Somo 5. Mwanadamu Mbele ya Mungu ........ 145
Ajali ........ 147
Kipeo cha Mwislamu ........ 147
Mungu Akipenda ........ 148
Kujifanya Mdogo ........ 148
Sujuda ........ 149
Ibada ........ 150
Mapendo ........ 151
Somo 6. Mwanadamu Mbele ya Mungu Kiumbe Huru ........ 153
Utiifu ........ 158
Bahati Nasibu, Ajali ........ 160
Somo 7 - Imani Ni Kitu Kikuu ........ 161
Malaika ni Wema tu ........ 161
Kuficha Imani ........ 162

Somo 8. Mwanadamu Mbele ya Mungu – Sala ........................ 164
Si Tendo Dhahiri tu ................................................................ 165
Kuosha Roho ........................................................................ 167
Sujuda ................................................................................... 168
Somo 9. Mwanadamu Ajilinda Na Unajisi ............................... 169
Vitu Najisi ............................................................................. 170
Kukoga ................................................................................. 171
Kabadili Nia .......................................................................... 172
Unajisi Unaingia ................................................................... 173
Ndoto ya Petro ...................................................................... 174
Kuungama au Kutawadha ..................................................... 175
Somo 10. Hali ya Wanadamu Tangu Asili ............................... 176
Adamu .................................................................................. 177
Mungu Hafuti Kazi Yake ....................................................... 177
Mungu Hataki Uovu .............................................................. 177
Amri za Mungu ..................................................................... 178
Mfano wa Dunia .................................................................... 179
Je Tukubali Uovu? ................................................................. 179
Neema Hutoka kwa Mungu .................................................. 180
Ujinga, Maradhi, Ufukara ....................................................... 181
Maradhi ................................................................................ 182
Ufukara ................................................................................. 184
Tiba ya Haraka ..................................................................... 185
Mpango wa Kudumu ............................................................. 186
Kukombolewa ....................................................................... 188
Kifo ....................................................................................... 189
Hali ya Giza .......................................................................... 190
Somo 11. Mwanadamu ni Mkosefu, Mwenye Dhambi ......... 192

Utajuaje? 194
Kumpenda Mungu na Jirani 195
Kuishi Kitawa 196
Dhambi Moyoni 196
Mungu Halazimishwi 197
Sadaka 198
Saumu 198
Somo 12. Hukumu Ya Ahera Dhambi Husamehewa 199
Kadiri ya Mungu 201
Kwenye Heri 204
Tutaulizwa Nini? 204
Tutahukumiwa lini? 205
Tutahukumiwa na Nani? 206
Hukumu Itafanywaje? 206
Uje Bwana Yesu 207
Somo 13. Adhabu ya Milele kwa Wahalifu 208
Adhabu ya Moto ni Nini? 210
Maelezo 210
Sababu ya Kutokuonekana 212
Wake Huko Ahera 215
Jahanamu 215
Somo 14. Heri ya Milele 218
Wanawake Watulizao Macho 219
Pepo ya Waislamu 219
Somo 15. Asili ya Ubaya na Mauti 219
Shari ya Alivyoviumba 220
Sheria za Maumbile 222
Mizimu, Pepo 222

Somo 16. Maadui na Wasaidizi wa Mwanadamu .................... 224
Jini, Malaika Na Shetani .................... 224
Maelezo .................... 224
Majini Walisilimu! .................... 226
Wenye Hasira Kali .................... 227
Somo 17. Mungu na Kaisari .................... 228
Utekelezaji wa Sheria .................... 230
Utawala wa Kikristo .................... 231
Kutumia Nguvu .................... 232
Somo 18. Dini ya Moyo na ya Maungo .................... 233
Imani .................... 235
Mti wa Kiislamu .................... 236
Somo 19. Mwanadamu katika Taifa .................... 237
Kujitolea kwa Wenzake .................... 238
Kuwatendea Wengine .................... 238
Somo 20. Kujenga Ujamaa .................... 239
Matendo ya Kujenga Ujamaa .................... 239
Sikukuu .................... 240
Sikukuu za Wakristo .................... 241
Kuhiji .................... 241
Fadhila za Ujamaa .................... 242
Kusaidiana .................... 243
Somo 21. Hali ya Wanawake .................... 244
Kuwa Mwili Mmoja .................... 244
Mwanamume Bora Kuliko Mwanamke .................... 245
Islam na Wanawake .................... 247
Usawa Katika Ndoa .................... 248
Tofauti za Dhahiri .................... 248

Wanaume ni Wasimamizi ........ 249
Shungi ........ 250
Daraja Moja Zaidi ........ 252
Talaka ........ 253
Kuolewa na Kutokuolewa ........ 254
Kutunza Mali ........ 255
Alama ya Unyonge ........ 255
Bikira Maria ........ 256
Kuzaliwa Bila Baba ........ 258
Somo 22. Mwanadamu na Viumbe Wengine ........ 259
Safi na Najisi ........ 261
Hatima ........ 261
Mwujiza? ........ 264
**LULU ZENYE THAMNI** ........ 269
Muhammad ni Nuru ........ 269
Kazi Yetu ni Kunadi ........ 271
Msaada Wenye Shani ........ 274
**FAHARASA** ........ a

# KISHA UKAJA MSAADA WA MWENYEZI MUNGU

Nilipomaliza kuandika jawabu la *Wana wa Ibrhimu*, nikalikuta ni jawabu thabiti fika linalofutilia mbali shutuma zote za Padre. Basi nikatamani nikiite kitabu hiki jina lishindalo jina la kitabu cha Bwna Padre, nisipate. Nikashauriana na baadhi ya Wanajumuiya, Mzee Rashidi Msabaha – Mwenyekiti wa Jumuiya yetu ya Dar-es-Salaam – akiwa mmojawapo, hatukumudu.

Hatimaye, nikakubali, shingo upande, jina *wajukuu wa Ibrahimu*, na kupeleka mswada mtamboni.

Baada ya siku kadha, nilipokuwa nimesahau kabisa habari hii, niliamka usiku mmoja kwa sala ya nafali, ghafula nikatiliwa kwa nguvu rohoni ( إلقاء ) **Mwana Mkuu wa Ibrahim**. Nikashtuka, nini hii! Haraka nikafahamu, hili ndilo jina la kitabu changu. Nikamshukuru Mola Karimu. Asubuhi nikaenda matbaa na kubadili jina la kitabu kuwa **Mwana Mkuu wa Ibrahim**, aliye Mtume Mtukufu[saw]. Alhamdu Lillahi.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 12 Juni 2024

# NENO LA MBELE

Naweka mbele ya wasomaji kitabu hiki – *Mwana Mkuu wa Ibrahim* – nilichokitunga kwa kusikia malalamiko mengi kutoka kwa Waislamu, Waahmadiyya kwa Wasunni, waliotaka Jumuiya ya Ahmadiyya itoe majibu ya kitabu cha Padre H.P. Anglars kiitwacho *"Wana wa Ibrahimu"* ambamo dini tukufu ya Kiislamu imelaumiwa na kusingiziwa sana.

Padre amejaribu kuhakikisha ya kwamba Wakristo ndio wana hasa wa Ibrahimu waliorithi baraka alizoahidiwa Ibrahimu. Lakini hakika yenyewe ni kwamba ingawaje Waisraeli walibarikiwa na unabii kwa muda mrefu sana, lakini kwa sababu ya wao kuvunja Agano la Mungu, ufalme wa mbinguni ulinyang'anywa kwao baada ya Yesu, bali wakapewa Wana wa Ismaili sawa na ahadi ya Mungu. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

> "Hakika watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye na Mtume huyu na walioamini." (Aali 'Imraan 3:69)

Ndiyo kusema kwamba katika zama zilizopita watu waliomfuata Ibrahimu ndio waliomkurubia, na katika zama hizi Mtume Muhammad[saw] na waaminio wanamkurubia kuliko wengine wote. Yaani Waislamu ndio wana wa Ibrahimu hasa kwa kiroho na *Mtume Muhammad[saw] ndiye Mwana Mkuu wa Ibrahimu.*


Kabla hawajaanza kusoma kitabu hiki, wasomaji wanapaswa kuelewa ya kwamba nikijibu upinzani wa Padre sikurejesha zaidi kwenye Agano la Kale, bali nimelitaja kila mara Agano Jipya. Sababu yake ni kuwa sawa na imani ya Wakristo, zama za sheria za Agano la Kale zilipita pindi alipotundikwa Yesu msalabani; sasa, wafikirivyo, wamo katika zama za Agano Jipya. Hivyo, kuwarejesha kwenye Agano la Kale katika mambo ya sheria si hoja kwao. Wanalitumia Agano la Kale kihistoria au kwa kutafuta humo bishara za ujaji wa Yesu. Padre anakataa kukubali Kurani kwa sababu sheria zake zinafanana na sheria za Agano la Kale, ilhali jambo hili ni dalili kubwa ya ukweli wa Kurani, kwani Musa alitabiri ujaji wa Nabii atakayefanana naye (Kumbukumbu 18:18).

Pia ijulikane ya kwamba sawa na imani ya Islam, manabii wote huwa hawatendi dhambi. Kwa hiyo, wasomaji wakisoma mahali kadha kwamba Yesu alionyesha hulka mbaya wakati fulani, basi hayo nimezungumza sawa na maneno ya Injili wala siyo kabisa kulingana na imani ya Kiislamu juu ya Yesu.

Jamil R. Rafiq,
Amiri na Mbashiri Mkuu,
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania.

Masjid Salaam,
20 Februari1977
Dar es Salaam.

# UTAMBULISHO WA MWANDISHI



Jamil R. Rafiq, mtungaji wa kitabu hiki, alizaliwa Pakistan mwaka 1936. Katika mwaka 1956 alipata, shahada ya B.Sc. katika Panjab University. Mnamo mwaka 1961 alihitimu masomo ya dini katika chuo cha Jamia Ahmadiyya Rabwah, na akapata shahada ya **shahid**. Katika mwaka 1962 alipelekwa na Khalifa Mtukufu wa pili[ra] nchini Tanganyika (sasa Tanzania).

Yu mtungaji wa mashairi ya Kiswahili. Kwa miaka kadha alikuwa Mhariri wa "East African Times" na "Mapenzi ya Mungu". Miongoni mwa vitabu vyake, kitabu cha Tajwid kinajulikana zaidi kati ya masheikh na waalimu wa Afrika Mashariki.

Kwa miaka kadha alikuwa Amiri na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Kenya.

## BI. HAJIRA, BINTI WA MFALME

Katika dibaji ya 'Wana wa Ibrahimu', Padre H. P. Anglars amevuruga ukweli kusudi ili kushusha hadhi ya Nabii Ismaili na mamaake Bi. Hajira. Amedai kwa kuifuata Biblia yake ya kwamba Bi. Hajira alikuwa mjakazi. Kwa kweli waandishi wa Biblia wamevuruga historia ya mnyororo wa wana wa Ismaili tangu kuanzia mama yao mtukufu, Bi. Hajira. Ukweli wenyewe ni kwamba Bi. Hajira[ra] alikuwa binti wa Mfalme wa Misri, wala si mjakazi hata kidogo. Mfalme wa Misri alipoona miujiza na utukufu wa Nabii Ibrahimu, ndipo akampa binti yake Hajira katika ndoa. Mfasiri mashuhuri sana wa Biblia, Bwana Rashi, ambaye ni Myahudi ameandika kwa uwazi mno katika maelezo ya Biblia ya kumhusu Bi. Hajira ya kwamba:

> 'She was the daughter of Pharaoh'.
>
> (Tafsiri ya Rashi, chini ya Mwanzo mlango wa 16).

Yaani alikuwa binti wa Firauni.

Ijulikane ya kuwa wafalme wa Misri waliitwa kwa lakabu ya Firauni. Yule Firauni aliyeangamizwa wakati wa Musa[as] alikuwa vile vile mfalme wa Misri, lakini ni mwingine wala siye yule aliyekuwa baba mzazi wa Bi. Hajira.

Basi, mfasiri Myahudi ameisha kubali ukweli huu, lakini Padre Anglars asikubali. Chuki ya mtu humpeleka mbali

na ukweli. Na mwanaye Ismaili ndiye ambaye Ibrahimu alitaka kumchinja sawa na ndoto yake, lakini Mwenyezi Mungu Alimkataza kutekeleza nia yake. Waandishi wa Biblia wamejaribu bure kumnyang'anya Ismaili heshima hiyo, wakisema eti huyo ni Isihaka[as] aliyetakiwa kuchinjwa. Ebu someni:

> "Mungu Alimjaribu Ibrahimu, Akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, mimi hapa. Akasema, umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka Nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa." (Mwanzo 22:1-2)

Ijapokuwa waandishi wa Biblia wameandika jina Isaka badala ya Ismaili, lakini hiana hiyo haikuweza kuuficha ukweli ulivyo. Kwani Biblia inasema kuwa aliyetakiwa kutolewa sadaka ni "Mwana wako wa pekee." Na ni hakika ya kuwa Ismaili alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Ibrahimu, na alikuwa mkubwa kuliko Isaka aliyezaliwa miaka 14 hivi baada ya kaka yake. Kwa hiyo Isaka hakuwa mwana wa pekee wakati wowote. Naam, Ismaili alikuwa mwanaye wa pekee kwa muda wa miaka 14. Hivyo maneno yenyewe ya Biblia yanatoboa hakika ilivyo na kudhihirisha hiana iliyofanywa na waandishi wa Biblia kwa ajili ya chuki ya Kikaini juu ya Ismaili. Tena ni ujasiri wa Padre Anglars kusema kuwa Biblia haisemi

kuwa wazao wa Ibrahimu waliahidiwa baraka, bali ni ‘mzao’ (mmoja) tu. Padre ameandika hivi:

> “Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake.” (Mwanzo 12:7)

Kumbe ukisoma Biblia yenyewe utakuta maneno yafuatayo:

> “Bwana Akamtokea Abrahamu, Akasema, uzao wako Nitawapa nchi hii.” (Mwanzo 12:7)

Kwa hiyo Biblia haisemi mzao mmoja bali uzao, na kisha neno ‘Nitawapa’ lahakikisha kuwa ni zaidi ya mmoja.

## Ismaili na Isaka wote Watabarikiwa

Padre hataki Ismaili naye apate baraka bali Isaka tu ndiye amependelewa na padre. Ile sehemu isemayo ‘agano la milele’ kwa Isaka, inaonekana ni nyongeza ya baadaye. Au ‘milele’ maana yake hapa ni mpaka zama ambapo wenyewe wana wa Israeli watavunja ahadi hiyo. Na kweli alipofika Mtume Muhammad[saw] katika uzao wa Ismaili, wana wa Israeli walikuwa wamevunja ahadi, na kwa hivyo baraka zikaondolewa kwao na kuhamishwa kwa wana wa Ismaili. Kwa ajili ya maovu ya wana wa Israeli, Yesu akawaambia:

> “Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake.” (Mt. 21: 43)

## Jiwe Kuu la Pembeni

Ieleweke ya kuwa 'Jiwe kuu la pembeni' lililokataliwa na waashi, ndiye Ismaili ambaye hao waandishi wa Biblia walimkatalia heshima aliyopewa na Mungu; lakini limekuwa ni jiwe la pembeni. Habari hii ilitolewa na Zaburi (118: 22, 23) mapema sana kwa kuonyesha jinsi Ismaili na wazao wake watakavyokataliwa na 'waashi'. Katika wazao wake akatokea Mtume Muhammad[saw] ambaye alitimiza bishara hii:

> "Naye aangukiaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika, naye yeyote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki" (Mt. 21:44).

Habari hii ilijulikana dhahiri katika maisha ya Mtume Muhammad[saw] katika vita vyake. Lakini Yesu mwenyewe alivunjwa na msalaba sawa na imani ya Wakristo. Kwa hiyo, bure tu padre amejaribu kuhakikisha bishara hii ndani ya dhati ya Yesu. (uk. 35).

## Namna Tatu za Wana wa Ibrahimu

Padre ameandika namna tatu za wana wa lbrahimu: Kwanza ni wale waliozaliwa kwa Hajira, yaani kwa mwili bila ya ahadi. Hii siyo sawa, kwani Ismaili alizaliwa kwa ahadi. Malaika wa Mungu alizungumza na Bi. Hajira akimpa ahadi ya kuzaliwa kwa Ismaili (Mwanzo 16: 7-12), ilhali Bi. Sara hakuambiwa na Malaika moja kwa moja, bali Nabii Ibrahimu akapewa habari ya Isaka.

Hii yaonyesha utukufu wa Hajira. Pengine sababu ya Sara kushushwa hadhi ni kuwa yeye alimtesa Hajira pasipo haki, na akamwambia lbrahimu kumfukuza bibi huyo pamoja na mwanaye. Huu ni ukatili mkubwa sana uliorithiwa na wana wa Israeli baadaye.

Ni la ajabu kuwa mwanamke mwenye hulka za aina hii — sawa na Biblia — amesifiwa lakini aliyezungumzwa na Malaika wa Mungu amedharauliwa.

Juu ya Ismaili ahadi inasema: "Nimembariki" (Mwa. 17:20). Basi Ismaili naye amebarikiwa.

Kama padre aseme kuwa ahadi hiyo ilikuwa kuhusu mambo ya dunia tu wala si ya roho, basi atambue ya kuwa 'Nimembariki' laonyesha ahadi kuhusu dini, na maneno ya baadaye,

> "Nitamzidisha, Nami Nitamwongeza sana sana…"

Ndiyo yahusuyo maendeleo ya dunia. Basi zipo ahadi kuhusu maendeleo ya dini na dunia.

Aina ya pili ya wana wa Ibrahimu ni wale waliozaliwa kwa ahadi, nao ni Wayahudi. Tumeisha eleza juu kuwa watoto wote wawili walizaliwa kwa nguvu ya ahadi.

Kisha ametaja wengine ambao si wana wa Ibrahimu kwa ukoo, lakini ni wazao wake kwa imani ambao ndio Wakristo. Hii haionekani kuwa sawa, kwani Yesu amesema:

> “Kama mngekuwa watoto wa Ibrahimu, mngezitenda kazi zake Ibrahimu.” (Yn. 8:39)

Yesu ametupatia kipimo cha kupimia utoto wa Ibrahimu; ni kutenda kama alivyotenda Ibrahimu. Sasa imani ya mtu haiwezi kupimwa ila matendo yake yanaweza kuonekana. Hebu tuangalie kuwa Wakristo wanamfuata Ibrahimu katika matendo yake? Tunasikitika kusema kuwa hawamfuati. Kwani Ibrahimu alianzisha sheria ya kutahiriwa kwa amri ya Mungu ambayo sheria hiyo imepuuziliwa mbali na Kanisa. Bali hata Padre Anglars ameidharau ndani ya kitabu chake tunachochambua wakati huu. Tohara ni alama ya dhahiri ya agano la Mungu kwa wazao wa Ibrahimu.

> “Mungu Akamwambia Ibrahimu, nawe ulishike **Agano** Langu, wewe na uzao wako kwa vizazi vyao baada yako. Hili ndilo agano Langu utakalolishika, kati ya Mimi na wewe, na uzao wako baada yako. Kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa" (Mwanzo 17:9-10).

Na asiyetahiriwa ‘amevunja agano Langu’ (Mwa. 17:14).

Basi kwa kuwa Wakristo wamevunja Agano hili, kwa hiyo hawatapata zile baraka alizoahidiwa Ibrahimu. Wakristo wanasema kuwa tohara ni ya moyo siyo ya mwili. Kwa kweli tohara ya mwili na ya roho zote mbili ni za muhimu. Kudharau tohara ya mwili ni kitendo

kibaya na kupuuza tohara ya moyo au roho pia ni jambo baya. Tohara ya mwili ni alama ya nje ya kuwa mtu huyo anathamini Agano la Mungu.

Padre amesema kuwa wenye tohara na wasio na tohara ni ndugu. Ni sawa, lakini waliopuuza amri ya Mungu ya tohara wamevunja Agano la Mungu; ni watoto waasi.

## SEHEMU YA KWANZA

### Wauza Watumwa ni Waisraeli

Padre amesema kwenye ukurasa 11 kuwa Waarabu kazi yao ilikuwa tangu zamani kufanya biashara ya hata watumwa sawa na (Mwanzo 37:25). Kumbe hiyo sehemu ya Biblia inasema ya kuwa watoto wa *Israeli walimwuza Yusufu* kwa Waishmaeli. Padre amesahau kuwa waliouza ni wana wa Israeli, amekumbuka tu kwamba walionunua ni Waishmaeli. Padre amenaswa na mtego wake mwenyewe.

### Hakuwaiga Wayahudi

Padre amesema (uk. 13) kuwa Mtume[saw] aliwaiga Wayahudi katika sheria ya kuelekea Yerusalemu wakati wa ibada. Uhakika wenyewe ni kuwa Mtume[saw] aliambiwa na Mungu kuelekea Baitul-Mukaddas, na shabaha yake ilikuwa kudhihirisha nani anamfuata Mtume na nani anakataa:

> "Na Hatukukifanya kibla ulichokuwa nacho ila tupate kujulisha yule anayemfuata Mtume kutoka yule anayegeuka kwa visigino vyake." (Al-Baqara 2:144).

Waislamu waliambiwa kuelekea Yerusalemu walipokuwa Makka ilhali watu wa Makka walipenda Kaaba, kwa njia hii ikajulikana nani anafuata amri ya

Mungu. Na hapo Madina, Wayahudi walikuwa wengi, kwa hiyo wakajaribiwa hao ambapo Mungu Aliifanya Kaaba kuwa kibla cha daima. Kwa vyovyote, siyo kwamba Mtume aliwaiga Wayahudi, bali alifuata amri ya Mungu iliyokuwa na hekima ndani yake.

## Tofauti katika Kurani na Biblia

Padre amedanganyika aliposema kuwa sababu ya tofauti zilizopo kati ya maneno ya Biblia na Kurani ni kuwa Mtume[saw] alisikia mambo hayo kwa watu waliosimulia habari kwa masimulizi tofauti na kwamba Mtume[saw] mwenyewe hakujua kusoma. Ni kweli kuwa Mtume[saw] hakujua kusoma wala kuandika, lakini hiyo haiwezi kuhakikisha sababu mbovu aliyoleta padre.

Hakika hasa ni kuwa kila mahala Kurani ilipotengana na Biblia, uchunguzi utaonyesha kuwa Kurani imesema haki, bali Biblia imepotoka kwa kuwa haipo katika hali yake ya asili.

Kuhusu Injili inajulikana dhahiri ya kuwa haielezi historia kamili ya Yesu. Kwani inaeleza kuzaliwa kwake, kidogo hali zake nyingine na kisha mara Yesu anaonekana akihubiri na kuonyesha miujiza na kisha katundikwa msalabani. Historia ya miaka zaidi ya 40 hivi haiwezi kuwa kiasi hicho.

Tumesema miaka zaidi ya 40, ijapokuwa Wakristo wana-

sema kuwa Yesu alitundikwa msalabani katika umri wa miaka 33. Nabii anapata utume katika umri wa miaka 40, na kisha Yesu alihubiri pia kwa miaka kadha, basi kwa vyovyote alitundikwa katika umri uliozidi miaka 40. Siku hizi wapo Wakristo wasemao kuwa tukio la msalaba lilipatikana katika umri wake wa miaka 45 hivi.

## Kuumba Ndege

Padre amesema kuwa Kurani inaeleza miujiza ya Yesu isiyoelezwa na Biblia, kama vile kutengeneza ndege kwa udongo (uk. 14). Padre amedai kuwa Mtume[saw] akasikia visa kama hivyo kwa Wakristo wa zama hizo ambavyo si vya kweli, naye akaandika ndani ya Kurani.

Kwa hakika hicho si kisa, bali ni jambo linalopatikana kwa kila nabii. Aya hiyo ya Kurani (Al-Maaida 5:111) inaeleza jinsi kila nabii anavyowalea wafuasi wake kama ndege anavyototoa vifaranga vyake na kuwalea. Watu wanakuwa wa udongo, yaani wenye mawazo ya kidunia, lakini nabii akiwapatia ulezi bora anawafanya wawe watu wa kimbinguni wanaoanza msafara wao wa kuruka angani kumfikia Mola wao. Hii ni mithali tu ambayo padre alitazamiwa kuitambua haraka, kwani Yesu aliwazoesha wafuasi wake kusikia mafumbo na kuyaelewa. Kwa hiyo, sio mwujiza katika maana wanayofikiria watu; lakini ni mwujiza katika hii maana ya kuwa nguvu ya nabii inawafanya watu waipendao dunia

kuwa watu wa mbinguni.

Upo mfano wa aina hii hadi leo katika Injili:

> "Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" (Mathayo 23:37; Luka 13:34).

Ingawa hayo yanaonyesha kuwa Yesu alitaka kuwalea kama ndege avileavyo vifaranga, lakini hakufaulu katika shabaha; Kurani inaeleza kuwa alifaulu. Ingawa si wote, lakini wengine walikubali kulelewa kama vifaranga. Wakakubali uongozi wake.

Padre amefurahi kuandika upinzani wa Wapagani wa Makka kwamba kundi la watu lilimsaidia Mtume[saw] kwa kuandika Kurani (Al-Furqaan 25:5-6). Lakini padre ajue ya kuwa Kurani inawaita watu wote kukusanyika pamoja na kuweza kuandika hata sura moja tu kama ya Kurani. Lakini mpaka leo hii hakuna aliyeweza kufaulu kupokea mwito huu. Kama Mtume[saw] aliweza kuandika kwa msaada wa watu, basi na wao pia walete mfano wake kwa msaada wa watu wote. Lakini hawawezi mpaka Kiyama!

Padre ameandika kuwa katika zama za Mtume Muhammad[saw] Wakristo wa aina tatu walipatikana: Unestori, Umonofisti na Waariani (uk. 15). Hao walikuwa na imani tofauti juu ya Yesu, na Mtume[saw] akaandika imani hizo ndani ya Kurani kwa kuupinga

Ukristo. Kwa kweli Kurani haikupinga kila imani iliyokuwapo wakati huo, bali imani nyingine ikaisadikisha na nyingine ikaipinga iliyokuwa mbovu. Kwa mfano, Wakristo wa Kimonofisti waliamini kuwa Yesu ni Mungu wala hakuwa mwanadamu hata kidogo. Kurani inaipinga imani hii pamoja na hoja. Na Wanestori waliamini kuwa Yesu hakufa msalabani bali mtu mwingine aliyefanana naye akafa. Imani hii nayo haipo katika Kurani ijapokuwa padre amesema kuwa imo hiyo imani katika (An-Nisaa 4:158). Aya hiyo haisemi hivyo; bali inasema kuwa Yesu alifananishwa na maiti juu ya msalaba, lakini hakufa huko. Yaani alizimia msalabani na watu walifikiri amekufa.

Imani ya Wakristo wa Kiariani imehesabiwa na padre kuwa mbovu ilhali hiyo ndiyo iliyo sawa; yaani Yesu si Mungu hata kidogo bali ni mtume wa Mungu.

Padre anasema Wakristo wale hawakuwa na umoja. Tunasema je, na leo wanao umoja? Leo pia wapo katika makundi mbalimbali chungu nzima.

## Maisha ya Mtume[saw]

Wasomaji wanaelekezwa kusoma kitabu *"Maisha ya Mtume Muhammad[saw]"* kilichotangazwa na Jumuiya ya Ahmadiyya. Padre amevuruga huko na huko alipoandika maisha ya Mtume[saw]. Kwa mfano amesema kuwa baada ya mama mzazi wa Mtume[saw] (Bi Aaminah)

kufariki, Abdul-Muttalib, babuye Mtume[saw], alimkabidhi Muhammad[saw] kwa mama mmoja aitwaye Halima. Kwa hakika siyo baada ya kufariki mamaake mzazi, bali baada ya kuzaliwa ambapo mzazi wake alikuwa hai.

Hii ilikuwa ni desturi ya Waarabu ya kuwa watoto wote baada ya kuzaliwa walikuwa wanakabidhiwa kwa wanawake wa vijijini waliokuwa wakiwachukua na kuwanyonyesha na kuwalea kwa miaka kadha na kisha kuwarudisha kwa wazazi wao. Sawa na desturi hii Mtume[saw] naye akapelekwa kijijini alipozaliwa. Na shabaha hasa ilikuwa ni kuwa mtoto apate afya nzuri akikulia katika hewa safi ya vijijini kuliko mijini, na pia ajifunze lugha safi ya Kiarabu, kwani lugha ya watu wa mijini ilichanganyika na lugha nyinginezo kwa ajili ya kutembelewa na watu wa nchi na lugha mbalimbali.

## Mume Mwaminifu

Padre amesema kuwa Mtume[saw] baada ya kumwoa Hadija akaendelea kuwa mume mwaminifu kwa miaka 20, kwani hakuoa mke mwingine. Padre atambue kuwa kuoa wake wengi siyo kinyume cha uaminifu. Naam, kinyume na uaminifu ni mtu kuchanganyika na wanawake wageni ambao wanamimina mafuta yenye thamani miguuni pake na kuipangusa miguu yake kwa nywele zao (Luka 7:37).

## Vitabu Mbinguni

Padre hakuelewa imani ya Waislamu wanaposema kuwa kitabu fulani kimeshuka kutoka mbinguni. Siyo maana yake kuwa huko mbinguni kuna vitabu vilivyoandikwa katika karatasi. Bali maana yake ni kuwa sheria zote zipo katika Elimu ya Mungu, Naye Anateremsha, kwa kuwafunulia manabii sawa na hali ya watu wa zama.

Kama Mkristo anashangaa kwa kuona kitabu kingine kimeteremka kutoka mbinguni baada ya Injili, basi Wayahudi wana udhuru wanaposhangaa juu ya Injili iliyokuja baada ya Torati.

Kurani imekuja sawa na bishara za Biblia. Someni kitabu chetu *"Mtume Muhammad[saw] Katika Biblia."*

Padre amejasiri kusema kuwa Mtume[saw] akaacha kuhubiri kwa muda, akaanza kutangatanga milimani akitafuta nuru (uk. 19). Habari hii ni ya uwongo. Inaonekana padre anakumbuka Yesu alipotangatanga jangwani akijaribiwa na Ibilisi (Mat. 4:1). Hakika ni kuwa kabla hajaletewa wahyi wake wa kwanza, Mtume[saw] alikuwa ameisha anza kupata ndoto zilizokuwa zikitimia kama 'mwanga wa asubuhi' (Bukhari). Padre anasema kuwa hapo Hadija akamtumainisha akisema:

> "Je, Mola wako Hakukukuta ukihangaika (kuongoza watu) naye Amekuongoza." (Adh-Dhuhaa 93:8)

Historia nzima haihakikishi kwamba Hadija akasema hayo. Bi. Hadija alimwambia:

> "Sivyo, Mungu Hatakufedhehesha kamwe, kwani unawatendea wema jamaa na kuwasidia wanyonge na kutenda hulka njema zilizopotea, na kuwakaribisha wageni na kusaidia katika haki." (Bukhari)

Hayo yalisemwa na Hadija mara baada ya kufunuliwa wahyi wa kwanza ambapo Mtume[saw] aliogopa isije akashindwa katika kutangaza ujumbe wa Mungu barabara na kwa hiyo Mungu Akamkasirikia. Ile aya aliyoandika padre ilishuka baadaye sana.

## Vinywa vya Manabii

Padre ameshangaa kwa nini Mungu Hakuendelea kujijulisha kama kale kwa vinywa vya manabii. Je, padre hajashangaa bado kwa nini Mungu Aliacha desturi Yake ya kale ya kuleta manabii kwa kuwaongoza binadamu bali kaleta Mtoto wake ili auawe msalabani?

Kwa kweli kila nabii kaletewa maneno kwa njia ya Jibrili au akaonyeshwa maandishi aliyosoma na kuandika. Hata mara moja haukushuka ubao ulioandikwa kutoka mbinguni. Pengine Mungu Anamwotesha nabii habari fulani. Kwa vyovyote ni nabii anayewaeleza watu mpango wa Mungu.

## Fumbo la 'Utatu'

Padre anasema kuwa haijulikani kama mtu asiyesoma anaweza kuelewa vya kutosha fumbo hili la 'utatu'. Je, na wale wavuvi waliweza kulielewa hilo? Siyo kwamba halieleweki kwa asiyesoma tu, bali kwa aliyesoma halieleweki asilani, kwani ni kinyume cha akili.

Juu ya Utatu wa Mungu, Mariamu na Yesu tutaandika mbele katika mahali pafaapo.

## Wapagani Wapingwa

Mtume Muhammad[saw] alipinga imani ya wapagani walioyaabudu masanamu. Na ni sawa pia kuwa Mtume[saw] aliwaambia baadhi ya waaminio kuhamia Uhabeshi kwa sababu ya mateso. Lakini padre hakueleza kuwa watu wa Makka waliwafuata hadi Uhabeshi (Ethiopia) na kumchochea mfalme Mkristo wa hapo ili awarudishe hao Waislamu huko Makka kwa sababu eti ni watumwa wao waliowakimbia. Lakini mfalme, kwa busara yake, akawaita hao Waislamu barazani pamoja na hao watu wa Makka. Watu wa Makka wakamwambia mfalme Najashi kuwa Waislamu wanamdharau Yesu. Mfalme alipowauliza, Masahaba wakamsomea aya za sura Maryam (sura ya 19) ambamo imani ya kweli juu ya Yesu imeelezwa. Hapo mfalme akachukua kijiti kidogo na akasema, "siongezi hata sawa na kijiti hiki katika sifa za

Yesu zilizotajwa na Waislamu", na akasilimu. Mtume[saw] alipohamia Madina, huyo mfalme akafariki, na Mtume[saw] akasalisha sala yake ya jeneza.

## Wayahudi

Padre amesema kuwa Wayahudi walipomkataa Muhammad[saw] hapo yeye akaanza kuwapinga na kuwafukuza. Ukweli ni kuwa hao Wayahudi hawakuwa raia waaminifu. Hata padre amekubali kwamba katika hali ya vita, Wayahudi wa Madina waliungana na watu wa Makka. Yaani kuna vita kati ya nchi mbili, Makka na Madina, na Wayahudi walio raia wa Madina wakaungana na nchi adui katika siku za vita hasa. Na pia Wayahudi walipanga kumwua Mtume[saw], je, katika hali kama hiyo wasingechukuliwa hatua?

Basi padre amevuruga historia aliposema kwamba Mtume[saw] akawafukuza Wayahudi eti kwa sababu hawakusadiki madai yake. Naam, Yesu kweli aliwaghadhabikia Wayahudi kwa sababu alikataliwa, na akawaita 'kizazi kibaya na cha zinaa' (Mt. 12:39).

Mwishowe padre ameandika kuwa uhusiano kati ya Wayahudi na Waislamu ulipovunjika, ndipo Waislamu wakaacha kuelekea Yerusalemu, na wakaanza kuelekea Kaaba (Makka). Tumeisha eleza hapo juu ya kuwa kugeuza kibla kulikuwa na hekima, pia sawa na bishara ya Biblia 'Yerusalemu Mpya' ilipaswa kupatikana.

Yerusalemu ilikuwa ni kibla cha manabii; kwa hiyo 'Yerusalemu mpya' maana yake ni kibla kipya kupatikana. Basi bishara ya Biblia ikatimia kwa njia hii (Ufunuo 3:12).

## Mtume[saw] na Wakristo

Kwenye ukurasa wa 23, Padre amesema ya kwamba mwanzoni uhusiano kati ya Wakristo na Muhammad[saw] ulikuwa mzuri. Ingawa Wakristo hao wangeweza kumpinga Muhammad[saw] mapema kwa kukumbuka maneno ya Yesu: "Jihadharini na manabii wa uongo", lakini kipimo cha uzuri wa mti ni matunda yake, kwa hiyo Wakristo hawakumpinga Muhammad[saw]. Lakini baadaye walipomsikia akipinga imani yao juu ya Yesu kuwa mwana wa Mungu, ndipo wakampinga, kasema padre. Lakini tukifanya uchunguzi tutaona ya kuwa tangu mwanzo Mtume[saw] alitangaza imani iliyo kinyume cha imani ya Wakristo. Sura ya 112 (Al-Ikhlaas) iliyoshuka Makka inatangaza waziwazi kuwa Mungu "Hakuzaa wala Hakuzaliwa." Na uhusiano tunaozungumzia ni wa zama za baadaye sana ambapo Mtume[saw] alikuwa ameisha hamia Madina.

Tena padre amejasiri kutumia neno 'kujidai' kwa ajili ya Mtume[saw], je, alama gani ya uwongo ilionekana ndani ya huyo Mteule wa Mungu? Naam, alama ya uwongo iliyotajwa ndani ya Biblia ni kuuawa kwa nabii mwongo

(Kumbukumbu la Torati, 18:20; 13:5). Sawa na hii alama mwasemaje juu ya Yesu aliyeuawa msalabani sawa na imani ya Wakristo?

Padre amesema kuwa Wakristo wa zama hizo walimkataa Muhammad[saw] walipoona kuwa yeye anajifanya Mtume sawa kama Yesu. Ijulikane ya kuwa imani ya Waislamu siyo kwamba Muhammad na Yesu ni sawa; bali Mtume[saw] ni mkuu kuliko manabii wote, Yesu akiwa mmojawao. Ndiyo kusema kuwa Muhammad[saw] si sawa na Yesu bali ni mkubwa sana kuliko Yesu. Hata Musa alikuwa mkubwa kuliko Yesu sawa na imani yetu.

Hii siyo sawa ya kuwa Wakristo walikubaliana na Mtume[saw] mwanzoni kwa kuona kuwa yeye anamwamini Mungu mmoja sawa na Wakristo ambao nao wanaamini:

> "Wakujue wewe, Mungu wa kweli wa pekee, na Yesu Kristo uliyemtuma." (Yn. 17:3)

Kwani ijapokuwa hayo ni maneno ya Yohana, lakini kwa kitendo Wakristo hawayaamini: Mungu wa pekee ni mmoja tu na Yesu ni Mtume wake (uliyemtuma) si mwanaye!

Na ile aya isemayo kuwa Yesu na mamaake walifanywa kuwa ishara, siyo shabaha yake kuwakuza kuliko binadamu; bali kinyume chake inamaanisha kuwa kwa ajili ya ujeuri wa Wayahudi usio na mipaka, Yesu aliyezaliwa bila baba, na Mariam aliyemzaa, ni ishara

isiyo nzuri, kwani sasa ufalme wa mbinguni utanyang'anywa kwa wana wa Israeli na watapewa Wana wa Ismaili. Kuzaliwa bila baba siyo heshima, bali inaashiria kuwa sasa hakuna kati yao mwanamume ye-yote anayestahili kupewa heshima ya kuwa baba wa Nabii. Kuzaliwa bila baba kunawezekana sawa na elimu ya utibabu. Tutazungumza habari hii baadaye.

Tena siyo sawa kusema kuwa ujaji wa Mtume[saw] uliwaachia Wakristo kumchagua mmoja wa hawa wawili: Yesu na Muhammad; bali Waislamu wanamwamini Yesu vilevile kuwa nabii. Kwa hiyo, siyo kuchagua mmojawapo, bali kuwakubali wote wawili. Na ieleweke kwanza kwamba fikira hii ya kuwa anaweza kutokea aliye sawa na Yesu au kumpita yeye katika zama zijazo ilipatikana kati ya Wakristo wa zamani. Mtaalamu mkubwa wa Theologia aitwaye D. F. Strauss aliandika kitabu 'Leben Jesu' yaani maisha ya Yesu, katika mwaka 1835 na akaandika ndani yake:

> "Yesu alijionyesha kuwa mfano wa maendeleo ya wanadamu lakini hatuna hakika kwamba wakati ujao mwingine hatatokea kuwa sawa naye au **Kumpita**".
>
> (Historia ya. Ukristo, J.3, kilichoandikwa na Robert M. Glen.)

Ingawa bwana huyo alipingwa na Wakristo wengi lakini pia alipata urafiki wa wengine kama Halmashauri ya

Zurich, waliompa kazi kama Mtaalamu wa Theologia chuoni mwaka wa 1839 (uk. 129 kitabu hicho).

Kwa hakika Bwana D. F. Strauss aliyekuwa mtaalamu wa Kikristo alipata ukweli, kwani mwaka huo (mwaka 1835) alipoandika kitabu hicho, alizaliwa Seyidna Ahmad[as], Masihi wa Muhammad[saw], aliyempita Yesu katika cheo cha roho.

*Roho Itokayo Kwake:* Hayo na maneno mengine yaliyotumika ndani ya Kurani Tukufu kwa ajili ya Yesu yanakusudia kumwondolea lawama aliyoletewa na Wayahudi ya kwamba amezaliwa kwa njia isiyo halali. Mungu Amemtukuza ili kusudi asionekane kuwa kizazi cha zinaa.

## Mungu Habadili Nia

Kumbe Wakristo hawamkubali Mtume[saw] kwa sababu Mungu Aliisha leta mwanaye wa pekee duniani ili kuiokoa dunia, na sasa kufika kwa nabii mwingine kutaonyesha kana kwamba Mungu Amebadili nia yake.

Uhakika wenyewe ni kuwa Islam inakubali kabisa ya kuwa Mungu Habadili desturi Yake:

> "Lakini hutapata mabadiliko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu, wala hutakuta mageuko katika kawaida ya Mwenyezi Mungu." (Al-Faatir 35:44)

Kwa hiyo, kumleta Mtume[saw] baada ya Yesu siyo maana yake Mungu Amegeuza nia. Bali yeye ametumwa kwa kukamilisha mpango ule ule wa Mungu Alioupanga Alipoumba binadamu kwa kumpatia mwongozo na wokovu. Ijapokuwa mitume mbalimbali wana daraja tofauti, lakini wote wanakuja kufanya kazi moja na kuiendeleza dini mbele zaidi.

> "Sema: Mimi si mpya katika Mitume." (Al-Ahqaaf 46:10)

Ndiyo kusema kuwa Mtume[saw] si mtume mgeni katika ule mpango wa Mungu, bali amekuja sawa na mpango na nia ya Mungu.

> "Sema: Mwaonaje ikiwa kama ametoka kwa Mwenyezi Mungu nanyi mmemkataa, na shahidi miongoni wana wa Israeli alishuhudia juu ya mfano wake na akaamini, lakini ninyi mnafanya kiburi; kwa yakini Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu wadhalimu." (Al-Ahqaaf 46:11)

Aya hii ni wazi kutangaza kuwa Mtume[saw] amekuja sawa na bishara ya Musa aliyetabiri katika Kumbukumbu la Torati (18:18) juu ya ujaji wa nabii aliye mfano wake. Yesu hakudai hata mara moja kuwa yu mfano wa Musa; bali Padre Anglars amepiga kelele nyingi sana katika kitabu chake kuwa Muhammad[saw] anaturudisha tena

kwenye Agano la Kale na kuwa mafunzo ya Islam yanafanana na mafunzo ya Musa.

Kwa neno zima, Mungu Hakubadili nia, bali nia ndiyo ile ile. Naam, imani hii yenyewe si sawa ya kuwa Mwana wa Mungu alikuja kuuawa msalabani ili kutwaa dhambi za wengine. Bila shaka hapo ndipo kubadili nia ya Mungu; kwani daima Akaleta mitume na manabii kwa kuwaongoza wanadamu, imekuwaje ghafla Akabadili nia na kaleta mwana wake. Tena siku zote mpango na nia ya Mungu ilikuwa ni kwamba kila mwenye dhambi ataadhibiwa au atasamehewa, lakini haitawezekana mtu mwingine awe kafara ya dhambi za wengine. Nabii Musa alijitolea kwa hiari yake kama kafara kwa dhambi za wana wa Israeli, lakini Mungu Akakataa Akisema kuwa:

> "Mwenye dhambi ndiye atakayeadhibiwa." (Kutoka 32:32, 33)

Kwa vyovyote Wakristo wasiwe na wasiwasi eti Mungu Amebadili nia; la, Hakubadili nia, bali Amemleta Mtume Muhammad[saw] sawa na mpango Wake Alioutaja ndani ya Biblia.

## Vita vya Muhammad[saw]

Ni kujipumbaza kusema kuwa Waislamu ndio walioanzisha vita walipoteka msafara mmoja wa Makka

uliokuwa na bidhaa nyingi za thamani, na kwamba sababu ya vita ilikuwa ni tamaa ya mali.

Ukweli ni kwamba fikra hii ya padre imepotoka kabisa bali yaonekana kusudi amesema uwongo ili kuharibu jina zuri la Islam kwa ajili ya husuda.

Hakuna msafara wowote uliotekwa na Waislamu. Hakika yenyewe ni kuwa misafara ya watu wa Makka ilikuwa inapita karibu na Madina siku zote ambayo baada ya Waislamu kuhamia Madina iliendelea kupita kama kawaida. Na ilikuwa ni kawaida yao daima kuwa na wanavita pamoja nao kwa ajili ya ulinzi. Baada ya Waislamu kuhamia Madina idadi ya wanavita iliongezwa pia kwa sababu ya hofu, lakini Waislamu hawakuizuia misafara hiyo hata siku moja.

Kabla ya vita ya kwanza (vita ya Badr) kupiganwa kati ya Waislamu na Wapagani wa Makka, misafara miwili ya bidhaa ilipitia huko salama kabisa bila kuzuiliwa. Kisha msafara mwingine wa tatu ulioongozwa na Abu Sufyan (ambaye baada ya Makka kutekwa alisilimu) ulitakiwa kupita huko uliotoka nchi ya Shamu. Pamoja na msafara huo, wanavita kama 500 walikuwapo kwa ajili ya kuulinda. Wapagani wa Makka walileta jeshi la watu 1,000 ili kuishambulia Madina kwa kujisingizia kwamba limekuja kuulinda msafara wao. Mtume[saw] alipopata habari ya jeshi hilo akachukua watu 313 bila

matayarisho yoyote ili kulizuia jeshi la Wapagani. Msafara ukapita salama, bali majeshi mawili yakagongana, na Waislamu wachache wenye silaha hafifu waliweza kupata ushindi mkuu katika mwaka mmoja tu baada ya kuhamia Madina sawa na bishara ya Biblia (Isaya 21:16-17).

Hii ndiyo kweli iliyopotoshwa na chuki ya padre. Vita zote alizopigana Mtume[saw] zilikuwa na sababu maalum na kila mara adui alitangulia kupanga kuwashambulia Waislamu. Shabaha haikuwa hata mara moja biashara au utawala; bali kujitetea: Ndiyo jihadi inayoelezwa vibaya na Wakristo kila mara.

Padre ameuliza swali rahisi sana aliposema kuwa kama dini na siasa zisingaliandamana katika wakati wa Mtume[saw] "haijulikani vizuri watu wangapi wangalijiunga naye" (uk. 26). Bila shaka wangekuwa zaidi kuliko idadi ya watu aliopata Yesu katika maisha yake. Kabla Waislamu walikuwa hawajahamia Madina idadi yao ilikuwa si ndogo sana hata baadhi ya masahaba waliposumbuliwa na Wapagani walimwomba Mtume[saw] ruhusa ya kupigana nao, lakini hawakupewa.

## Dini na Siasa Kuandamana

Padre anafikiri kuwa Islam lazima inataka kuwa dini na siasa ziandamane. Sivyo. Bali njia zote mbili

zimeruhusiwa: Dini na utawala kuandamana pamoja au kuwa mbalimbali. Hii inategemea hali iliyopo.

Lakini je, padre hajui historia ya Ukristo? Kanisa Katoliki na serikali ziliandamana kwa muda mrefu mno.

> "Mara nyingi mtu mmoja aliweza kuwa askofu na mtawala wakati mmoja mahala pamoja. Tena Kanisa lilifundisha kwamba serikali pia inahitaji kupata mamlaka yake ya kutawala kwa idhini ya kanisa." (Historia ya Ukristo J. 2 uk. 88, Dean A. Peterson).

Papa hakuzitenganisha hizo mbili bali Luther (mwaka 1525) 'alifundisha kwamba serikali na kanisa ni viwanja viwili mbalimbali' (Kitabu hicho uk. 88).

Isitoshe, Ukristo ulienezwa na serikali:

> "Wakati huu shughuli zote za kueneza Imani ziliongozwa na Rumi yenyewe kwa njia ya Wizara ya Kueneza Dini. Vyama mbalimbali vya kimishionari viligawiwa maeneo yao ya kufanya kazi na bila kibali cha Wizara hiyo hakukuwa na ruhusa kwa ye yote kufungua kituo kipya. Jinsi uenezi huo ulivyosimamiwa na mwunganisho wa mamlaka huko Rumi iliwezesha Kanisa la Kiroma kufunika dunia nzima na wamishionari wake."

(Historia ya Ukristo, uk. 71, 72. J. 3).

Ndiyo kusema kwamba kwa msaada wa serikali Ukatoliki ulienea duniani kote.

Kuhusu uhusiano baina ya serikali na wamishionari maneno yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa:

> "Hata hivyo uhusiano wa uenezi wa kimishionari na serikali za kikoloni ni wa kutatanisha. Katika mahali pawili, yaani, Uganda na Vietnam, serikali zilijali wito wa wamishionari wao kuwasaidia na kuchukua utawala wa nchi zile"

(Historia ya Ukristo J. 3, uk. 68: Robert M. Glen)

Padre amesikitika juu ya kitendo hicho cha Wakristo cha kuunganisha utawala na dini. Lakini je, hajui mpaka sasa kiongozi wa serikali ya Uingereza ni kiongozi wa kanisa?

**Abu Sufyan**

Padre amekariri tena kwenye ukurasa wa 27 kuwa Waislamu waliuteka msafara wa biashara wa Abu Sufyan, huko Badr, wakachukua mali yao yote na watumwa. Tumeisha eleza, na wanahistoria wa Kikristo pia wanajua, ya kuwa msafara haukutekwa, ila tu padre Anglars amezusha uzushi huu usio na kifani. Inaonekana sheria ya kusema kweli pia imekuwa "laana".

## Vita ya Uhud

Padre amesema kuwa Waislamu walishindwa katika Uhud na mpaka sasa wanakumbuka Uhud kwa sikitiko na hasira (uk. 28). Ni sawa kuwa kwa ajili ya kosa fulani Waislamu walipata hasara kubwa katika Uhud, lakini mwishowe tena Wapagani kwa sababu fulani walipofikiri kuwa Waislamu wamepata msaada toka Madina wakakimbia uwanjani.

***Jemedari Mkuu*: ** Ni kweli ya kuwa mwana mkuu wa Ibrahimu, Mtume[saw], pamoja na kuwa Nabii Mkuu alikuwa Jemedari Mkuu vilevile. Lakini padre amefanya hiana alipoandika kwamba aya ifuatayo inahusu vita ya Khaibar:

> "Bila shaka Tumekupa ushindi ulio dhahiri, ili Mwenyezi Mungu Akufunikie makosa yako (unayosingiziwa) yaliyotangulia na yajayo, na kukutimizia neema Yake". ( Al-Fat'h 48:2-3)

Hii aya inauhusu 'Mkataba wa Hudaibiya' uliopatikana baina ya Wapagani na Waislamu kwa kutokupigana kwa miaka 10. Mungu Anasema kuwa mkataba wa amani ni ushindi wa Islam inayotaka amani daima, na kwamba katika hali ya amani Islam itapata wafuasi wengi kwa njia ya mahubiri. Historia inaonyesha ya kuwa katika muda wa amani, Islam ilienea sana kuliko miaka ya hapo kabla.

## Ndoa za Muhammad[saw]

Mwanzoni mwa Mlango wa 'Ndoa za Muhammad', padre ameandika maneno ya Injili: "Nao wawili watakuwa mtu mmoja" (Mt. 19: 5, 6), na kisha ameeleza ya kwamba Muhammad[saw] alioa wake wengi.

Kwa kweli mantiki ya padre ni ya ajabu. Kama wawili wanaweza kuwa mmoja, kwa nini watatu au wanne wasiweze kuwa mmoja? Baada ya ndoa mke na mume wanasaidiana katika mambo yote ya maisha na kwa njia hii wanakuwa kitu kimoja; siyo maana yake ya kwamba wanakuwa kiwiliwili kimoja, bali wanakuwa na umoja. Basi kwa hiyo, hata watatu au wanne wanaweza kuwa na umoja; bali taifa zima la watu mamilioni huwa kitu kimoja kwa sababu ya umoja wao.

Kwa kifupi, maneno hayo ya Injili hayafundishi kuwa mtu lazima aoe mke mmoja tu. Kwani funzo hili la kuwa 'mtu mmoja' au 'mwili mmoja' halikutolewa na Yesu, bali lilitolewa zamani sana katika Agano la Kale:

> "Naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa '**Mwili Mmoja.**" (Mwanzo 2:24)

Na katika zama za 'Agano la Kale', desturi ya kuoa wake zaidi ya mmoja ilishikwa. Manabii wa Agano la Kale walikuwa na wake zaidi ya mmoja. Kama 'Mwili mmoja' lingekuwa na maana ya kuoa mke mmoja tu, bila shaka hao waliofunzwa hilo wangejua habari hii.

Basi ni kupachika maana ngeni katika fundisho la 'Agano la Kale', ambayo haikujulikana kwa watu waliopewa hilo funzo.

Kama padre anafikiri ya kwamba ugomvi utatokea ikiwa mtu ataoa zaidi ya mke mmoja, basi atambue ya kuwa hata kati ya mume na mke mmoja pia ugomvi unatokea mara kwa mara ambao hurekebishwa.

Padre amesema kuwa:

> 'kwa Mwislamu ndoa siyo kubeba pamoja mzigo mmoja' (uk. 28).

Hakika yenyewe ni kuwa Islam tu ndiyo dini iliyotoa mafunzo kamili juu ya wajibu wa mke na mume ambao wajibu huo wasipoutekeleza wanahesabiwa wenye dhambi.

## Amri Kuu ya Yesu

"Ndoa ni namna ya kwanza kutimiza amri kuu ya Yesu ya kupenda mwenzake anavyojipenda mwenyewe", kasema padre. Lakini tukichunguza Biblia tutakuta ukweli wenyewe ni kinyume chake. Yesu amesema ya kwamba:

> "Wako matowashi waliojifanya kuwa matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kulipokea neno hili, na alipokee."(Mt. 19:12)

Ni wazi kuwa Yesu alipendelea watu wasioe kama wanataka kutumikia dini. Lakini kwa kuwa wengi hawawezi kuvumilia useja kwa hiyo wanaruhusiwa kuoa. Ndiyo kusema kwamba kwa Yesu ndoa si kitu kitukufu, bali ni njia ishikwayo na yule asiyeweza kuishi useja kwa ajili ya ufalme wa mbinguni.

Lakini Dini ya Kiislamu imemlazimisha kila mwenye uwezo kuoa au kuolewa. Mtume[saw] alisema:

> "Hakuna kuishi useja katika Islam."

Kisha alitangaza:

> "Asiyependa ndoa hahusiani nami."

Basi tunashangaa kwa nini Padre amesema kuwa ndoa ni njia ya kutimiza amri kuu ya Yesu! Katika Ukristo ndoa ni kitu duni na kwa hivyo watu watukufu kama mapadre wa kikatoliki hawataki kuoa.

**"Tumerahisisha Mambo"**

Akijadili habari za ndoa, Padre amesema, "Kwa Muhammad ndoa haikukusudiwa kumletea mwanadamu taabu na shida; Islam inataka kuyarahisisha hata maagizo ya kale:

> "Basi, Tutamrahisishia (mwanadamu) mambo kuwa mepesi." (Al-Lail 92:8)

Tunashangaa kuona kwamba padre ametaja aya hiyo ili kuwadanganya wasomaji. Aya hiyo haizungumzii kuondoa wajibu wa sheria bali inasema kwamba yule atakayesadiki jambo jema Tutamrahisishia mambo kuwa mepesi. Hebu someni wenyewe:

> "Lakini anayetoa (sadaka) na kumcha (Mungu) na kusadiki jambo jema, basi 'Tutamrahisishia mambo kuwa mepesi'."(Al-Lail 92:7-8)

Ni habari nyingine kabisa iliyoelezwa katika aya hiyo. Basi tunahuzunika juu ya Padre kuondokewa na tabia njema ya uaminifu. Kwetu Waislamu sheria ni baraka; lakini kwa ajili ya Wakristo sheria ni **'Laana'** (Wagalatia 3:13). Haieleweki kwa nini padre anatia mawazo ya Biblia yake ndani ya Kurani Tukufu?

## Mwana wa Kupanga

Kuhusu ndoa ya Mtume[saw] na Bi. Zainabu, padre amedhihirisha uchafu mwingi sana wa moyoni. Amemlaumu Mtume[saw] kwa nini akamwoa mke wa mwanaye wa kulelewa. Bali amesema ya kwamba watu walipomlaumu Mtume[saw] juu ya habari hiyo, Kurani ikawanyamazisha kwa kusema:

> "Haiwi kwa mwanamume aliyeamini na mwanamke aliyeamini kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao." (Al-Ahzaab 33:37)

Hakika yenyewe ni kwamba Bwana Zaid aliyekuwa mtumwa ambaye Mtume[saw] alimpa uungwana na kampanga mwana, alishauriwa na Mtume[saw] kumwoa Zainabu aliyekuwa binti wa shangazi wa Mtume[saw] Bi. Zainab mwenyewe na kaka yake hawakupenda shauri hilo, kwa sababu Zaid alikuwa mtumwa; bali walipenda Mtume[saw] mwenyewe amwoe binti huyo. Lakini Mtume[saw] alikazania shauri lake ili kuondoa fikara mbovu ya heshima ya kiukoo. Hapo Mwenyezi Mungu Akateremsha aya hiyo aliyoitaja padre ya kwamba shauri la Mtume[saw] likubaliwe na Zainabu aolewe na Zaid. Ndivyo ilivyotendeka. Lakini Padre mwenye fikara mbovu anasema kuwa aya hiyo ililetwa ili Mtume aweze kuwatuliza watu waliomlaumu Mtume kwa ajili ya kumwoa Zainabu.

## Hiana Nyingine

Ndoa ikafungwa baina ya Zaid na Zainabu, lakini haikuendelea kwa muda mrefu zaidi. Zainabu alikuwa mwenye tabia tofauti na mumewe ambaye alijiona hafifu mbele ya mkewe. Kwa hiyo Zaid akataka kumpa talaka. Mtume[saw] alipojua nia yake, akamsihi Zaid asimwache mkewe. Kurani ikieleza habari hii inasema:

> "Na ulipomwambia yule ambaye Mungu Amemneemesha na wewe umemneemesha: Shikamana na mkeo na umche Mungu." (Al-Ahzaab 33:38)

Padre Anglars ametumia hiana kubwa alipoandika aya hiyo kwa kuondoa maneno yake ya mwanzo yaani "Ulipomwambia…" na akaanzia kutoka "Shikamana na mkeo". Kwa njia hii alitaka kuhakikisha kwamba Mtume[saw] alipomwoa Zainabu watu wakamlaumu, ndipo aya hiyo ikaletwa ndani ya Kurani Tukufu kumwambia Mtume[saw] ashikamane na Zainabu wala asijali lawama za watu.

## Zainabu Anaolewa na Mtume[saw]

Zaid alijaribu sawa na maagizo ya Mtume[saw] kuishi na mkewe Zainabu, lakini alipoona ameshindwa kabisa akampa talaka. Eda yake ilipopita Mtume[saw] alimwoa Zainabu kwa amri ya Mungu na shauri ya jamaa zake Zainabu. Padre anamlaumu Mtume[saw] kwa nini akamwoa mke wa mwanaye wa kulelewa. Lakini padre anapaswa kutambua ya kuwa mwana wa kulelewa si mwana; ni mtoto wa mtu mwingine ila tu Mtume[saw] alimlea nyumbani kwake.

Waarabu wa zamani walifikiri kuwa mwana wa kupanga ni kama mwana hasa wa mtu, lazima atarithi pia na kutendewa anavyotendewa mzaliwa hasa wa mtu. Mtume[saw] alimpanga Zaid kuwa mwana wa aina hiyo kabla haijashuka sheria ya Kurani kuhusu habari hiyo. Lakini kisha Mungu Aliteremsha aya ndani ya Kurani Tukufu ya kwamba:

> "Wala Hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa wana wenu hasa; hayo ni maneno yenu ya vinywa vyenu; na Mwenyezi Mungu Husema kweli, Naye Huongoza njia. Waiteni kwa (ubini wa) baba zao, maana huo ndio uadilifu mbele ya Mungu. Na kama hamwajui baba zao, basi ni ndugu zenu katika dini na rafiki zenu." (Al-Ahzaab 33:6)

Aya hii iliposhuka Bwana Zaid aliyekuwa akiitwa Zaid bin Muhammad akaanza kuitwa tena Zaid bin Harith, kwani Harith alikuwa babaake mzazi. Mungu Akavunja desturi ya Waarabu na Akafundisha haki na uadilifu, lakini padre bado anang'ang'ania kushikilia desturi mbovu ya zamani. Kwa padre sheria ni ***'laana',*** kwa hiyo anao udhuru. Lakini kwa ajili ya Mwislamu sheria ni rehema. Sheria imekomesha ile desturi ya kupanga mwana, kwa hiyo Zaid akafanyiwa adili kwa kupewa ubini wa baba yake hasa.

Padre akiwadanganya wasomaji wake ameandika:

> "Baadaye akampenda Zainabu, isipokuwa huyu alikuwa mke wa Zaid, mtoto wake wa kulelewa. Zaid alimpenda sana mkewe Zainabu, lakini, kwa jinamizi kubwa, akampa Zainabu talaka, ili apate kuolewa na Muhammad." (uk. 29)

Maneno ya Padre yanaonyesha kana kwamba Zaid alimwacha mkewe ili Mtume[saw] aweze kumwoa. Hiyo ni fikira chafu ya Bwana Padre.

Kama Mtume[saw] angelitaka kumwoa Zainabu, angemwoa tu hapo mapema alipokuwa bikira bali hata jamaa zake wakataka Zainabu aolewe na Mtume[saw]. Lakini Mtume[saw] alipendelea Zaid amwoe bibi huyu. Hata mjinga wa mwisho anaweza kutambua habari hii, lakini padre asielewe!

## Kisa cha Uwongo

Kisha padre ameeleza kisa cha uwongo kabisa kisichokuwa na msingi ndani ya Kurani wala katika Hadithi za Mtume[saw]. Kusema kwamba siku moja Mtume[saw] alipokwenda nyumbani kwa Zaid akawahi kumwona Zainabu na akapendezwa na uzuri wake ndipo mambo yote yalitendeka, ni ushenzi mtupu. Zainabu akiwa binti wa shangazi yake hakuwa mgeni kwa Mtume[saw]. Yeye alimjua siku zote, bali akaombwa na kaka yake Zainabu amwoe bibi huyo, lakini Mtume[saw] alikataa. Imekuwaje baada ya kuolewa na Zaid uzuri wake umpendeze?

Inaonekana padre, kila mara anampima Mtume[saw] kwa kukisia hali ya Yesu jinsi ilivyoelezwa katika Biblia. Katika (Luka 7:37), Yesu anaonekana na mwanamke ambaye alimbusu Yesu. Alipolaumiwa kwa kitendo

hicho akaanza kujitetea na kutoa mifano. Yohana (11:5) anatoboa kuwa Yesu alikuwa na mapenzi kwa mwanamke aitwaye Martha. Yohana anaeleza tena katika (11:36) kwamba Yesu alimpenda sana mwanamke fulani mpaka Wayahudi walisema: "Angalieni jinsi alivyompenda."

Licha ya wanawake, Injili inaeleza kuwa Yesu alikuwa na mapenzi ya mvulana fulani:

> "Palikuwa na mmoja wa wanafunzi wake, ameegemea kifuani pa Yesu, ambaye Yesu alimpenda." (Yohana 13:23)

> "Petro akageuka akamwona yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu anafuata; ndiye huyo aliyeegemea kifuani pake wakati wa kula chakula cha jioni, akasema, Bwana, ni nani akusalitiye." (Yohana 21:20, 21)

Lo, mapenzi makubwa yaliyoje mpaka haachi kuegemea kifuani pake hata wakati wa chakula!

Athari mbaya ya kitendo kama hicho imeonekana wazi wazi siku hizi ambapo padre mmoja akafungisha ndoa kati ya wanaume wawili ndani ya Kanisa hasa, na akabariki ndoa hiyo kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu! Someni gazeti "News of the World" la tarehe 9.7.1967. Bila shaka padre huyo amechukua ruhusa ya kufungisha ndoa ya kilawiti kwa kusoma sehemu kama

hizo za Biblia hapo juu. Bahati mbaya ni kwamba mapadre wanapochunguza maisha ya Mtume[saw] huwa wanampima sawa na mwenendo wa Yesu.

## Si Mjakazi, Bali Mke

Padre akiwafuata baadhi ya watu wengine amemtaja Bi. Maria Kibtiyya kama mjakazi wa Mtume[saw]. Hakuwa mjakazi bali alikuwa mkewe. Hata Padre Dale amekubali kwamba bibi huyo alikuwa mkewe Mtume[saw]. Kwa kweli Mtume[saw] hakuwa na suria yeyote.

## Uwongo Mwingine

Padre anasema kwamba safari moja Mtume[saw] alitaka kuwafukuza wakeze wote, hata akajitenga nao kwa mwezi mzima. "Lakini, je, ni halali kufanya vile?", Padre anauliza. Na kisha anasema kwamba Kurani ilijibu swali hili hivi:

> "Ewe Nabii, mbona unaharimisha Alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unataka radhi ya wake zako? (Nabii akiwapeni talaka) yumkini Mola wake Atamletea badala yenu wake wengine walio bora kuliko ninyi!" (Al-Tahriim 66:6)

Padre amechanganya aya ya pili na ya 6 pamoja, hata kwamba madhumuni yakavurugika.

Padre anasema kuwa Mtume[saw] alitaka kuwafukuza wakeze wote, lakini aya anayoandika yasema kuwa

“Ewe Nabii, mbona unaharimisha Alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unataka radhi ya wake zako?” Je, kweli aya hii inaonyesha kuwa Mtume[saw] alitaka kuwafukuza? Aya inasema Mtume[saw] alitaka radhi ya wakeze.

Kwa hakika tukio lingine kabisa limeelezwa hapo. Ni hivi kwamba Mtume[saw] alizoea kutumia asali. Siku moja baadhi ya wakeze walimwambia kuwa wanasikia harufu (ya asali) kinywani mwake. Hapo Mtume[saw] alinuia kuacha kabisa kutumia asali, ndipo aya hii ilishuka iliyosema kwa nini yeye anaharimisha Alichokihalalisha Mungu.

Naam, sehemu ya pili ya aya alivyopanga Padre ndiyo aya ya 6 nayo inaeleza kwamba kama Mtume[saw] akiwapa talaka wakeze kwa sababu fulani, basi Mungu Atampa wake bora zaidi kuliko hao. Lakini kwa kuwa Mtume[saw] hakuwapa talaka, hata mmojawao, kwa hiyo ilihakikishwa kwamba wake hao wote walikuwa ni wema na bora sana.

Ijulikane kwamba hitilafu ndogo ndogo zaweza kuzuka kati ya mke na mume katika mambo ya maisha na zinarekebishwa pia mara kwa mara. Hili ni jambo la kawaida katika maisha. Lakini padre mseja hawezi kuelewa mambo ya maisha ya ndoa.

## Haki za Pekee

Padre ameandika ya kuwa Muhammad[saw] alidai haki ya pekee kuhusu ndoa. Ile haki ya pekee aliyosema padre imeelezwa katika aya hii:

> "Na mwanamke mwaminio akijitoa mwenyewe kwa nabii, na kama nabii akitaka kumwoa; ni halali kwako tu, si kwa waaminio wengine." (Al-Ahzaab 33:51)

Ni sawa ya kuwa Mtume[saw] alipewa ruhusa ya kumwoa mwanamke mwaminio aliyejitoa kwa ajili ya nabii. Lakini padre atashangaa ya kuwa Mtume Muhammad[saw] hakutumia hiyo ruhusa maisha mazima. Basi lawama ya padre ni bure ya kuwa Mtume[saw] alijipendelea kuliko waaminio wengine na akaandika katika Kurani ruhusa kwa ajili yake. Swali linazuka ya kuwa kama Mtume[saw] hakutumia ruhusa hiyo, basi ilikuwa na maana gani kutoa ruhusa ya aina hiyo. Jibu ni kuwa aya inamtolea ruhusa kila nabii siyo Mtume Muhammad[saw] peke yake kama yanavyoeleza maneno ya Mungu. Yaani Muhammad[saw] hakupewa haki hiyo ya pekee bali ni haki ya manabii wote, wa zamani na hata wa baadaye. Inawezekana nabii yeyote wa baadaye atumie haki hiyo.

Jambo jingine ni Mtume[saw] kuoa zaidi ya wake 4. Kwa kweli nabii anapaswa kueneza sheria kati ya wanawake pia, kwa hiyo ni vizuri aoe zaidi ili kuwafunza dini hao

wakeze ambao watawafunza wanawake wengine. Ndivyo ilivyotukia. Wakeze Mtume[saw] walifunza elimu kubwa sana, hususa zile zilizowahusu wanawake. Hata Manabii wa Biblia walioa wake wengi, pengine kwa shabaha hiyo.

## Adabu za Kuingia Nyumbani

Padre amesema ya kwamba waaminio walikatazwa kuingia nyumbani kwa Mtume[saw] bila ruhusa eti ili kuepushana na fujo zilizoweza kutokea kati ya ahali zake, au kati yao na watu wengine. Kwa kweli huu ni msiba mkubwa wa fahamu ya padre. Kwa hakika Islam inafundisha kutokuingia katika nyumba ya mtu yeyote isipokuwa kwa ruhusa ya mwenye nyumba:

> "Enyi mlioamini, msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka mwombe ruhusa, na mwatolee salam waliomo humo. Hayo ni bora kwenu, huenda mtakumbuka." (An-Nuur 24:28)

Na sheria hiyo hiyo inaihusu pia nyumba ya Mtume[saw]; kuna jambo gani la ajabu! Kwa kweli padre hakufundishwa adabu ya kuingia nyumbani katika Injili, kwa hiyo anashangaa.

## Cheo cha Wakeze Mtume[saw]

Padre amechukia kuona heshima kubwa ya wakeze Mtume[saw] baina ya waaminio, kwani heshima kama

hiyo hata Yesu hakuipata kati ya wanafunzi wake waliomkimbia na kumlaani na kumsaliti. Kurani Tukufu inasema:

> "Nabii ana haki zaidi kwa waaminio kuliko nafsi zao; na wakeze ni mama zao." (Al-Ahzaab 33:7)

Na kwa kuwa wakeze Mtume[saw] ni mama wa waaminio kwa kiroho, hivyo haifai kuwaoa baada ya Mtume[saw] kufariki. (Al-Ahzaab 33:54).

Padre amepotoka tu alipotaka kuhakikisha heshima ya wakeze Mtume[saw] mbele ya wanawake wengine wa Kiislamu akitaja aya hii:

> "Ewe nabii, waambie wake zako, na mabinti zako, na wake wa waaminio, wateremshe juu yao shungi zao (yaani wafunike vichwa vyao kwa shungi). Hivyo inaelekea zaidi wajulikane na wasiudhiwe." (Al-Ahzaab 33:60)

Kwa hakika aya hii haionyeshi tofauti baina ya wakeze

Mtume[saw] na wanawake wengine walioamini, kwani wote hao wameambiwa kuteremsha shungi zao juu ya vichwa vyao. Fikara ya padre inahangaika bila kutafakari.

## Sheria ya Shungi

Mwisho wa mlango huu wa *"Ndoa za Muhammad",* padre amelaumu desturi ya wanawake wa Kiislamu kuvaa

shungi, na amesema desturi hii ni 'hatari' na kwamba siyo kazi ya dini kuzuia maendeleo. Upande mmoja padre anaona kujisitiri kwa heshima ni hatari na upande mwingine anataka kuondoa umalaya nchini. Dawa moja ya muhimu kwa kuondoa umalaya ni wanawake kujifunika vizuri wakitoka nje, kwa sababu chanzo cha vitendo viovu ni wavulana na wasichana kuchanganyika ovyo katika vilabu na makanisa. Inajulikana dhahiri kuwa vijana wengi zaidi wanaofika kanisani shabaha yao inakuwa kutafuta wapenzi, siyo ibada.

Padre anataka kukomesha mavazi mafupi, lakini dawa yake haikubali. Kama mwanamke atalazimika kuvaa shungi, atakuwa na haja gani tena kuvaa miniskati?

Ni kitu gani hayo maendeleo anayofikiria Padre? Je, vilabu vya pombe, vilabu wanamopiga dansi wanawake walio uchi wa nyama, na kutenda vitendo vya kinyama ambavyo vyote hivyo vinapatikana katika nchi za magharibi ndiyo maendeleo? Maendeleo ndiyo wavulana na wasichana kuchanganyika ovyo na kubusana barabarani bila kuona haya? Waislamu waliposhikamana na sheria ya Kiislamu pamoja na wanawake wao kujisitiri, katika zama hizo maendeleo ya kweli yalipatikana hata Wazungu walilazimika kupata shahada ya elimu ya juu katika vyuo vikuu vya Kiislamu katika nchi za Kiislamu. Waislamu wamerudi nyuma kwa kusahau sheria ambayo itasimamishwa tena kwa

njia ya Jumuiya ya Masihi aliyeahidiwa. Tutaandika zaidi juu ya shungi mbele.

## Utume wa Muhammad[saw]

### Mtume na Nabii

Padre ametofautisha kati ya Mtume na Nabii. "Nabii ni kama mhubiri au mwonyaji" kasema padre, "mtume ni yule anayetumwa kwa taifa fulani ili kuwaongoza watu." Kisha anashangaa kuwa Muhammad[saw] anadai kuwa mtume na nabii pamoja.

Kwa kweli nabii na mtume ni kitu kimoja. Nabii maana yake ni mtoaji habari na mtume ndiye anayetumwa. Kwa hiyo, mtu anayeitwa kuwa nabii kwa sababu ya kuleta habari kutoka kwa Mungu pia anaitwa mtume kwa sababu ya kutumwa na Mungu ili kutoa habari hiyo. Haiwezekani Mungu Amtume mtu bila kumpa habari yoyote ya kutolewa kwa wanadamu. Kwa hiyo kila nabii ni mtume pia na kila mtume ni nabii vile vile. Hii ndiyo sababu Mtume[saw] ameitwa Nabii na pia Mtume ndani ya Kurani.

Wakristo wanaweza kuwaita watu kuwa mitume wanaotumwa na binadamu pia, kama vile mitume walioteuliwa na Yesu. Kwa kweli sisi Waislamu hatuwaiti kuwa mitume. Mitume au Manabii hutumwa na Mungu pekee.

Pia ieleweke hapa ya kuwa baadhi ya Waislamu wanafikiri kuwa yule anayeleta sheria mpya huitwa nabii na mtume pamoja; lakini asiyeleta sheria mpya huitwa Nabii peke yake si Mtume. Fikira hii haiafikiani na Kurani. Kwani, Waislamu wote wanakubali kuwa Harun[as] ni nabii asiyeleta sheria, bali sheria alipewa Nabii Musa; lakini Kurani inawaita wote wawili – Musa na Harun – kuwa mitume (Rasuli). Tazameni Sura Twaa Haa 20:48 ya Kurani Tukufu.

Pia Nabii Saleh anajulikana kuwa hakuleta sheria mpya, lakini ameitwa Rasuli wa Mungu (Mtume wa Mungu) ndani ya Kurani (Al-Balad 91:14).

**Kuhani**

Padre ametafuta kitu kikubwa sana alipoandika kuwa Muhammad[saw] hakudai kuwa Kuhani (uk. 33). Itambulikane kuwa katika Islam Mtume huwa anawapita wote katika daraja la roho. Ukuhani ni daraja ndogo kuliko Utume; kwa hiyo haina haja kudai Ukuhani baada ya kupata cheo kikubwa zaidi.

Inaonekana kuwa Biblia, wakati mwingine, inawaita manabii wasio na sheria mpya kuwa Kuhani. Kama vile katika Waebrania 5:4, Nabii Harun alivyoitwa kuwa Kuhani. Sawa na fundisho la Kurani, Nabii Haruni ni Mtume asiyeleta sheria mpya. Katika maana hii pia Muhammad[saw] hakuwa Kuhani, kwani alileta sheria

mpya. Naam, Yesu anaweza kuitwa Kuhani kwa sababu hakuleta sheria mpya. Na kweli Biblia inamwita hivyo (Waebrania 5:10).

## Idadi ya Mitume

Padre amejiingiza katika kutafuta idadi ya mitume waliofika duniani. Ameandika idadi mbalimbali kama vile 313 au 315. Ifahamike kuwa katika Hadithi moja ya Mtume[saw] idadi ya mitume imesimuliwa kuwa 124,000. Lakini hii kwa kweli inamaanisha kuwa mitume wengi mno walifika. Mara nyingi katika lugha yetu pia tunasema kuwa: "Nimekuambia mara elfu lakini hunisikii." Sasa siyo maana yake kuwa ulisema mara elfu sawasawa; bali maana yake ni mara nyingi. Kwa hiyo ile Hadithi ya Mtume[saw] inakusudia kueleza wingi wa manabii.

## Ardhi Inazunguka

Naam, ni hakika kwamba ardhi inazunguka pembezoni mwa jua ndipo usiku na mchana hupatikana. Padre anasema kuwa kukataa jambo hili si busara. Hapo tunawakumbusha wasomaji ya kuwa ukweli huu ulipotangazwa na mwanasayansi mmoja wa Kikatoliki, Bwana Galileo Galilie (1564-1642), akakufurishwa na Papa na kufukuzwa katika Kanisa. Sababu iliyotolewa ni kuwa bwana huyo amesema kinyume cha Biblia. Basi sawa na kauli ya Padre Anglars, Papa hakuwa mtu mwenye busara?

Katika miaka ya nyuma habari zilitangazwa magazetini kuwa sasa Papa ameteua kamati kwa kufikiria upya kukufurishwa kwa Bwana Galileo na kumkubali tena katika Kanisa ilhali tangu miaka zaidi ya 300 ameisha kufa bwana huyo! Kwa kweli siku zote kulikuwa ugomvi baina ya Kanisa na elimu ya sayansi. Someni "Historia ya Ukristo", jalada la 3, uk. 5,6; iliyoandikwa na Robert M. Glen.

## Hakuweka Msingi Mpya

Muhammad[saw] hakuweka msingi mpya, bali alikuja katika mnyororo wa mitume. Hata padre amekubali, bali ameshangaa kwa nini Muhammad[saw] alileta tena mafunzo kama ya Agano la Kale. Hii yaonyesha kuwa Mtume aliendelea na msingi ule ule uliowekwa katika Biblia, ila tu Yesu amegeuza msingi sawa na imani wanayoitakidi Wakristo wa siku hizi.

Kwa kweli kuna agano lile tu liitwalo Agano la Kale; ndiyo sheria ya Mungu. Kwa kuwa Yesu hakuleta sheria mpya, basi hakuna nafasi ya Agano lolote Jipya. Naam, Agano Jipya ni Kurani Tukufu, kwani ndiyo sheria mpya. Injili ilikuwa ni bishara kwa ujaji wa Muhammad[saw] ambaye kwa njia yake Ufalme wa mbinguni ulitazamiwa kuja.

## Mwana Sio Mwisho

Padre ameeleza kuwa mwanzoni Mungu Akaleta mitume na mwishowe Mwana. Baada ya Mwana kuja

haina maana atokee tena Mtume yeyote. Padre akihakikisha habari hii ameeleza ule mfano wa shamba la mizabibu aliotoa Yesu. Lakini padre hakueleza mfano huo mzima bali ameacha sehemu yake ya mwisho inayoonyesha Mtume atakuja baada ya Yesu. Yesu alisema:

> "Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa na mtu mwenye nyumba naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawakamata watumwa wake, huyu wakampiga, na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumwa wengine wengi kuliko wa kwanza, wakawatenda vile vile. Mwishowe akamtuma mwanaye kwao, akisema: Watamstahi mwanagu. Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao: 'Huyu ni mrithi', haya tumwue, tutwae urithi wake. Wakamkamata, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, Atawatendaje wale wakulima? Wakamwambia; Atawaangamiza vibaya wale wabaya;

> na shamba la mizabibu Atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda yake wakati wake. Yesu akawaambia; Hamkupata kusoma katika maandiko:
>
> Jiwe walilolikataa waashi,
> Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni;
> Neno hili limetoka kwa Bwana,
> Nalo ni ajabu machoni petu?
>
> Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lenye kuzaa matunda yake. Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; na yeyote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki." (Mathayo 21:33-44).

Katika mfano huu, shamba la mizabibu ni maisha haya ya dunia, wakulima ni watu (au wana wa Israeli katika mfano huu); watumwa wa bwana ni mitume wa Mungu; mwana kwa njia ya mfano ni Yesu. Ni sawa aliyosema padre ya kuwa maana yake ni kwamba Mungu Alituma mitume kwanza ambao walisumbuliwa na kuuawa na wana wa Israeli; na kisha Akatuma mwana yaani Yesu. Mfano huu unasema kuwa mwana akauawa. Padre akamalizia mfano hapa hapa ilhali mfano unaendelea kusema kuwa baada ya mwana kuuawa, Bwana mwenyewe atakuja na kuwaadhibu hao wakulima

wabaya, yaani wana wa Israeli, na kuwapa wakulima wengine shamba la mizabibu ambao wataleta matunda katika wakati wake. Ndiyo kusema kwamba baada ya Yesu mpango sio basi, bali wakulima wengine watapewa kazi ya kutunza shamba la mizabibu. Na imetabiriwa mapema ya kuwa hao wataleta matunda sawasawa, yaani Waislamu waliopewa Utume na Unabii baada ya wana wa Israeli hawatanyang'anywa shamba hilo tena.

Ndivyo ilivyotokea. Mungu Akawaadhibu wana wa Israeli vikali sana na tangu hapo ufalme wa mbinguni wakapewa Waislamu kwa njia ya Mtume Muhammad[saw]. Na katika shamba hili la mizabibu mara kwa mara watumwa watapelekwa kuchukua matunda, yaani mitume wataendelea kutokea sasa kati ya Waislamu tu pekee, na wanadamu wote watalazimika kuingia katika Islam wakitaka baraka za milele.

## Bwana ni Nani?

Bwana katika mfano huo hapo juu, bila shaka ni Mungu mwenyewe. Lakini Mungu Hana mke wale mwana, bali Yesu ameitwa mwana kwa njia ya mfano tu. Kwa hiyo na hata Bwana kimfano ni Mtume[saw] ambaye amedhihirisha utukufu mkuu wa Mungu. Musa ameitwa mfano wa Mungu (Kutoka 7:1); kwa hiyo katika mfano wa shamba la mizabibu, Bwana ni yule aliye ‘mfano wa Musa’; na Mtume Muhammad[saw] ni Mtume aliyefanana

na Musa (Kumbukumbu 18:18; na Al-Muzzammil 73:16). Basi habari ya Mtume[saw] imo katika mfano wa shamba la mizabibu. Ni wazi kwa nini padre amekoma mpaka kuuawa kwa Mwana bila kuendelea kuandika mbele mfano wa shamba la mizabibu!

Kwa vvovyote Mtume[saw] ametokea sawa na mfano wa shamba la mizabibu, wala mwana sio mwisho wa mambo yote! Padre amewaomba Waislamu kuelewa vizuri maana ya mfano huu, basi tumeuelewa vizuri sana ila sasa padre anapaswa kuzingatia maana yake ya ndani na kutenda sawa nayo.

## Matarishi Wengi, Habari Moja

Padre amesema kuwa Mtume[saw] hawezi kuwa mkweli kwa sababu kulikuwa na maagano mawili tu wala siyo matatu. Yesu alileta agano jipya ili kukamilisha agano la kale. Kwa kweli Yesu hakuleta agano jipya, kwani alikamilisha tu lile lile la kale, alivyokubali padre. Maana yake ni kuwa yeye alikuwa mtume wa mwisho wa zama za Agano la Kale. Na kwa njia ya Mtume Muhammad[saw] Agano Jipya la milele limeanza. Yesu hatangui sheria ya Torati. Kwa kweli mitume wote walileta habari moja tu ya kwamba Mungu ni Mmoja wala Hana mshirika. Basi atakayesema kuna Mungu baba, Mungu mwana na Mungu roho mtakatifu, bila shaka huyo hawezi kuwa mkweli, kwani amegeuza habari.

## Maandiko Yametimia

Padre anasema kuwa siku aliyofia Yesu akasema (matabiri) yote yametimia (Yn. 19:30). Siyo maana yake kuwa kila bishara ya Torati imetimia wala haikubaki bishara yo yote kumhusu nabii mwingine kutokea. Bali Yesu alikuwa na maana ya kuwa matabiri yote yaliyohusu tukio la msalaba yametimia. La, sivyo, kauli hii haitaonekana kuwa sawa, kwani kuna habari chungu nzima zilizoelezwa katika Biblia (kama vile katika kitabu cha Danieli) ambazo zilikuwa hazijatimia wakati huo.

Ieleweke kinaganaga kuwa maneno haya ya Yesu kuwa 'yote yametimia', yanahakikisha kuwa yeye hakutazamiwa kufa msalabani, kwani hayo aliyasema alipokuwa bado hai msalabani. Basi alijua ya kuwa yote yameisha timia tayari, hakuna zaidi ya hayo ya kuwa atakufa pia msalabani na atafufuka. Ndiyo sababu alipofikiri katika hali ya taabu kuwa pengine ataweza kufa akalia akisema:

> "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona Umeniacha?"

Yaani haikuandikwa kuwa atafia msalabani, bali alipaswa kulindwa na kifo cha laana. Na kweli Mungu Hakumwacha, bali Akamwokoa katika kifo cha laana cha msalaba. Alizimia tu na akafikiriwa kuwa amekufa.

Padre ameandika bure ile bishara ya Ezekieli (34:11-12) kuwa Mungu Atakuja kuchunga kondoo Zake kwa kuokoa dunia nzima. Kwa kweli bishara ya Ezekieli inazungumza wazi wazi juu ya Israeli.

> "Nitawatoa katika watu wa mataifa, na kuwa-kusanya katika nchi zote, Nami Nitawarudisha katika nchi yao wenyewe; Nami Nitawalisha juu ya milima ya Israeli."(Ezekieli 34:13)

Padre ameandika aya ya 11, 12 tu; kumbe ile ya 13 inazungumza waziwazi juu ya Israeli. Kondoo watatafutwa kati ya watu wa mataifa, sio watu wenyewe wa mataifa. Na ni sawa kuwa Waisraeli walitawanyika kati ya mataifa mbalimbali; Yesu alikuja kuwatafuta kati ya mataifa. Kwa hiyo, Yesu hakuja kwa mataifa yote.

Tena Yesu mwenyewe alikiri kuwa kuna mambo mengine ambayo yeye hakuwaambia watu, kwani hawawezi kuyavumilia (kama vile kusali sala tano, wanawake kujisitiri kiungwana, kujiepusha na anasa na ulevi n.k.w.k.), bali atakapokuja yule roho wa kweli atawaambia kweli yote (Yn. 16:13). Kwa hiyo, Yesu hakutimiza mambo yote ila yale ya Agano la Kale tu. Lakini kweli yote ilielezwa na Roho wa kweli aliye Mtume Muhammad[saw].

## Mtume Muhammad[saw] kwa Dunia Nzima

Padre ameandika kwamba Yesu ametumwa kwa ajili ya mataifa yote, imekuwaje baada ya miaka 600 tena Mungu Amtume mtume mwingine kwa kubadili nia Yake. Tumeisha eleza hapo nyuma (uk. 18) kuhusu nia ya Mungu ya kuwa haikubadilika kwa ujaji wa Muhammad[saw]. Ila hapa tunataka kueleza kuwa Yesu hakuja kwa ajili ya wanadamu wote. Kusema kwamba Yesu hasa alitumwa kwa Waisraeli, lakini kwa jumla alitumwa kwa dunia nzima, si sawa hata chembe; kwani Yesu alitamka:

> "**Sikutumwa** ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." (Mt. 15:24)

La sivyo yeye angesema kuwa japo nimetumwa kwa wanadamu wote lakini hasa nimetumwa kwa Waisraeli.

Kusema kwamba Mtume Muhammad[saw] naye alisema kwanza alikuja kwa ajili ya Waarabu peke yao na kisha akasema kuwa ametumwa kwa wote, haina msingi. Yeye alitumwa kwa watu wote (Al-A'raaf 7:159), kwa hiyo na kwa ajili ya Waarabu pia. Aya: "Ili uwaonye watu wa Makka na walio pembezoni mwake" haisemi kuwa alitumwa hasa kwa ajili ya Waarabu, bali maana yake ni kuwa siku zote hao waliachwa, lakini sasa Muhammad[saw] ametumwa kwa ajili yao pia na wengine wote pia, ili

wasiseme kuwa siku zote mitume walitokea kwa ajili ya Waisraeli tu:

> "Wasije wakasema: Mola wetu, mbona Hukutupelekea Mtume." (Al-Qasas 28:48)

Muhammad[saw] hakusema kwanza: "Sikutumwa ila kwa Waarabu" na kisha akageuka alipokataliwa na akasema: "Nendeni kwa mataifa yote."

Mtume[saw] mwenyewe aliwahubiri watu wa mataifa mbalimbali katika uhai wake. Katika mwaka 628 yeye aliwaandikia barua wafalme wa Uajemi, Rumi, Misri na Ethiopia. Mfalme wa Ethiopia, Najashi, aliyekuwa Mkristo alisilimu kwa mahubiri ya masahaba wa Mtume[saw]. Wakristo kwa Wayahudi walisilimu katika zama za Mtume[saw]. Waarabu, Waajemi na Waafrika pia walisilimu.

Yesu, aliwakataza wanafunzi wake wasiwahubiri wowote ila Waisraeli tu; bali alikataza pia kuwahubiri Wasamaria (Mat: 10:5) ambao ndio machotara wa Kiyahudi; wengi wao ni wazao wa Wayahudi kwa wake wasiokuwa Wayahudi. Sasa kama walikataliwa walio Wayahudi nusu-nusu, watapokelewaje wasio Wayahudi kabisa!

Yule mwanamke Mkananayo asiyekuwa Myahudi kwanza alikataliwa lakini alipojifananisha na mbwa akasaidiwa. Ndiyo kusema kwamba Wayahudi ndio

watoto machoni pa Yesu waliompigilia msalabani, lakini wasio Wayahudi ni kama mbwa tu hata wakiwa wema namna gani!

Basi kama Yesu alisema baadaye kuwa hata watu wa mataifa mengine pia wanaweza kubatizwa, alikuwa na maana hiyo hiyo kuwa watabatizwa kimbwa. Kwani katika uhai wake alimpokea kimbwa mama asiye Mwisraeli. Ndio mfano aliowaachia wafuasi wake.

Pia maana ya 'Mataifa' inaweza kuwa 'mataifa ya Kiisraeli', yaani makabila 12 ya wana wa Israeli. Alizungumza juu ya viti 12 tu (Mt. 19:28).

Kwa vyovyote ni Muhammad[saw] tu aliyetumwa kwa dunia nzima. Nchi ya Arabu si mbali sana na nchi ya Israeli; kwa nini Yesu hakuchukua jukumu la kupeleka ujumbe wake huko? Alijua kuwa hakutumwa kwa wengine!

## Maana ya Utume

Padre hakuelewa kabisa habari za utume sawa na imani ya Kiislamu; amesema kila nabii analeta habari kutoka kwa Mungu wala hakuna wa kukamilisha mwingine wala wa kuendeleza utume wa mtume mwingine. Imani ya Islam ni kuwa mitume wachache walileta sheria mpya, lakini wengi sana walitumwa kuendeleza utume wa mitume hao.

Kurani Tukufu inafundisha:

> "Na bila shaka Tulimpa Musa kitabu na Tukawafuatisha Mitume (wengine) baada yake." (Al-Baqara 2:88)

Ndiyo kusema kwamba Nabii Musa alipewa sheria na waliokuja baada yake walikusudiwa kuendeleza utume wa Musa. Hata Yesu alikuja kuendeleza utume wa mitume wengine (Al-Hadiid 57:28). Sawa na imani yetu, Yesu hakuleta dini mpya, bali alikuja kuhubiri Torati.

Hatusemi kuwa mabaya waliyokatazwa zamani yanaweza kuhalalishwa na Mtume mwingine. Bali ni Wakristo wenyewe wanaokubali upuuzi huu, kwani wanapuuzilia mbali sheria za Musa, wakisema Yesu ametuokoa katika *'laana ya sheria.'* Kumbe, kwao sheria ni laana, ilhali ni baraka kubwa kwa kupata maendeleo ya roho.

## Pombe

Ni fikara mbovu kusema kwamba pombe iliruhusiwa na Kurani kwanza na kisha ilikatazwa. Aya hii: "Na katika matunda ya mitende na mizabibu ambayo mnaitengeneza kileo na riziki nzuri" (An-Nahl 16:68) haikuhalalisha pombe. Bali inaeleza kuwa wanadamu wanatengeneza kileo katika zabibu na tende, na pia wanapata **Riziki Nzuri**; ndiyo kusema kuwa kileo si riziki nzuri. Wapi kuhalalishwa kwa pombe? Aya hii Akiimalizia Mungu, Anasema:

> "Hakika katika hayo imo ishara kwa watu watumiao akili." (An-Nahl 16:68)

Basi, tunawaelekeza watumiao akili kuisoma aya hiyo na kupeleleza kuwa je, inahalalisha pombe au inaitaja kama ni kitu kibaya?

**Watumwa wa Mungu**

Hatuelewi kwa nini padre anachukia kuitwa mtumwa wa Mungu. Yale yaliyonenwa na Yesu kuwa: "Siwaiti tena watumwa" (Yn. 15:15) hayaelezi 'watumwa wa Mungu'; bali 'watumwa' tu. Kwa kweli alikuwa na maana ya kuwa wanaomkubali nabii hawabaki kuwa watumwa wa wanadamu au watumwa wa dhambi (Yn. 8:34). Kuwa watumwa wa Mungu si jambo lililo kinyume cha heshima ya binadamu. Paulo aliwaandikia Wakorintho:

> "Maana mlinunuliwa kwa thamani." (1 Kor. 6:20)

Hapa Wakristo wameitwa watumwa (wenye kununuliwa). Tena:

> "Mlinunuliwa kwa thamani; msiwe watumwa wa wanadamu." (1 Kor. 7:23)

Ni dhahiri kuwa waaminio si watumwa wa dunia, bali ni watumwa wa Mungu.

Ni sawa pia ya kuwa waaminio ni marafiki wa Mungu. Yaani kwa sababu ya kufuata amri za Mungu wameitwa watumwa au watumishi wa Mungu; lakini kwa kuwa

Mungu Anawatendea vizuri, hivyo wameitwa pia marafiki wa Mungu. Lakini "Mwenyezi Mungu ni Rafiki wa wamchao." (Al-Jaathiya 45:20)

Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa Urafiki wa Mungu unapatikana kwa ajili ya 'kumcha Mungu.'

**Msaidizi: Roho wa Kweli**

Kwenye ukurasa 41, padre amedai ya kuwa ile bishara ya Msaidizi haimhusu Mtume Muhammad[saw] bali ilitimia siku hamsini baada ya Pasaka ambapo Roho Mtakatifu aliwashukia mitume. (Matendo 4:31).

Kwa kweli, habari ya Msaidizi imeelezwa na Yesu mahala kadha katika Biblia. Katika Yohana 14:26 Msaidizi ameitwa pia Roho Mtakatifu; katika Yohana 15:26, ameitwa Msaidizi (na Roho wa kweli); katika Yn. 14:16-17, Msaidizi mwingine na Roho wa kweli lakini katika Yohana 16:13 ameitwa Roho wa Kweli. Na katika Yn. 16:7 ameitwa msaidizi.

Hii inahakikisha kuwa bishara hii inamtabiri Msaidizi tu ambaye kwa ajili ya kuwa Mtukufu sana amepewa sifa ya kuwa roho mtakatifu; au kwa sababu ya kueleza kweli yote amepewa sifa ya kuwa Roho wa Kweli. Ameitwa mara moja tu kuwa Roho Mtakatifu na mara tatu Roho wa Kweli, lakini mara nne akaitwa Msaidizi. Kama aliyetabiriwa ni yule Roho Mtakatifu aliyemshukia Yesu alipobatizwa na Yohana, bila shaka kila mara angetajwa

kwa hilo jina, kwani ni kitu kinachojulikana. Bila shaka hapa aliyekusudiwa si yule Roho Mtakatifu aliyekuwa akishuka mara kwa mara katika uhai wa Yesu (Mt. 3:16-4:1; Yn 20:22), kwani yule Msaidizi hangeweza kutokea ilhali Yesu yupo (Yn. 16:7).

Tena, kazi ya Msaidizi ilikuwa ni kuwafundisha yote na kuwakumbusha yote (Yn. 14:26), yaani kufundisha yale asiyofundisha Yesu, ili kuwaongoza kwenye kweli yote (Yn. 16:13), na pia kukumbusha yaliyofunzwa na Yesu. Kazi hiyo haikufanywa na Roho aliyewashukia mitume siku ya Pentekoste. Huyo roho mtakatifu aliwatia tu mitume ujasiri ili waweze kusema waliyofunzwa na Yesu bila kuogopa. Lakini mapya asiyoyafundisha Yesu hakuwafunza Roho huyo. Pia Msaidizi aliye Roho wa Kweli alitakiwa "kunena" maneno maalumu kwa kusikia kutoka kwa Mungu. Hatuoni ndani ya Biblia kuwa siku ya Pentekoste yule Roho aliyewatilia mitume ujasiri akanena maneno aliyoyasikia kutoka kwa Mungu. Hakunena lo lote.

Lakini Mtume Muhammad[saw] ndiye aliyenena maneno maalumu yaliyotoka kwa Bwana Mungu bila kuchanganya hata neno moja lake ndani yake. Tena akaeleza kweli yote (Al-Maaida 5:68). Akafundisha mapya yasiyofunzwa na Yesu, na pia akawakumbusha aliyoyafunza Yesu. Lakini ndugu Wakristo wanachukia kumpokea huyu Msaidizi.

> "Maneno hayo nimewaambia, msije mkachukizwa." (Yn. 16:1)

Yule Msaidizi alipaswa kumshuhudia Yesu (Yn. 15:26). Kweli Mtume[saw] alishuhudia kuwa Yesu hakuwa mwongo bali alikuwa Nabii mkweli, ijapokuwa Wayahudi walimkataa. Lakini siku ya Pentekoste, roho mtakatifu aliwatilia tu ujasiri mitume ambao mapema walimkubali Yesu.

> "Nanyi pia mnashuhudia, kwa kuwa tangu mwanzo mmekuwapo pamoja nami." (Yn. 15:27).

Roho wa Kweli, au Msaidizi, alipaswa kumtukuza Yesu (Yn. 16:14). Kazi hii alifanya sana Mtume[saw] kwa kumwondolea lawama zote alizoletewa Yesu na Wayahudi, hata kwamba Padre Anglars ameandika aya za Kurani kwa furaha kwa kuonyesha kuwa Yesu ametukuzwa ndani ya Kurani.

Kwa kweli 'Msaidizi' ndiye yule Nabii aliyetabiriwa katika Kumbukumbu la Torati (18:18) ambaye:

> "Nitatia maneno Yangu kinywani mwake, naye atawaambia **Yote** Nitakayomwamuru."

Yaani atawaambia kweli yote. Kwa kuwa Yesu alizoea kuzungumza katika mafumbo, amesema roho wa kweli,

roho mtakatifu na msaidizi; lakini Musa anaeleza wazi wazi kwamba atakayekuja ni Nabii.

**Yesu – Mtumishi wa Mungu**

Padre kinyume na wasia wa Yesu amechukizwa (Yn. 16:1), ilhali yule Msaidizi, Mtume Muhammad[saw], hampingi Yesu hata mara moja. Kusema kuwa Yesu kuitwa 'Mtumishi wa Mungu' ni sawa na kumpinga, ni kosa kubwa kabisa, kwani katika (Matendo 4:27), Yesu ameitwa Mtumishi wa Mungu:

> "Walikusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu."

Je, na Biblia pia inampinga Yesu ikimwita Mtumishi wa Mungu? Ebu someni pia:

> "Ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu." (Matendo 4:30)

Mbele ya Mungu, wote ni watumishi bali watumwa:

> "Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie **Watumwa** wako kunena neno lako kwa ujasiri wote." (Matendo 4:29)

Hakuna fedheha kujiona mdogo mbele ya Mwumba wa mbingu na ardhi, Mungu Aliye Bwana ni Mkuu kuliko Yesu (Yn. 14: 28).

## Torati, Injili na Kurani

Ni sawa alivyosema padre ya kwamba Waislamu wanaamini vitabu hivyo vilivyotajwa juu. Lakini pia tunaamini ya kuwa Torati na Injili vilikuwa vimeharibiwa na wafuasi wake kabla haijafika Kurani. Vile vile ni imani yetu ya kwamba Injili ilikuja kuitumikia Torati, kwani Yesu alifika kutilia nguvu sheria za Musa (Al-Maaida 5:47). Yesu mwenyewe alisema:

> "Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza." (Mt. 5:17)

Pia alitamka:

> "Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo katika ufalme wa mbinguni." (Mt. 5:19)

Alisisitiza habari hiyo aliposema:

> "Waandishi na Mafarisayo wameketi kiti cha Musa; basi, yoyote watakayowaambia, myashike na kuyatenda." (Mt. 23:2-3).

Hayo yanaonyesha dhahiri ya kuwa Yesu ailkuja kuitumikia Torati siyo kuitangua. Na sababu yake ni kuwa alipofika Yesu, Wayahudi walikuwa wamesahau

kiini cha sheria ila waliishika kijuu-juu tu, pamoja na kugeuza baadhi ya sehemu za Torati. Yesu aliposema kuwa alikuja 'kutimiliza', maana yake ilikuwa ni kufundisha upya yaliyokuwa yamefutiliwa mbali katika Torati. Kwa mfano Yesu anaonekana akisema:

> "Mmesikia kwamba imenenwa; jicho kwa jicho, na jino kwa jino; lakini nawaambia, Msishindane na mtu mwovu...."(Mt. 5:38-39)

Maana yake ni kwamba katika Torati mliyo nayo fundisho la kisasi linaonekana, lakini mimi nikiwaambieni fundisho la kusamehe ninatimiliza hiyo Torati. Yaani siyo kwamba habari ya msamaha haikuwamo ndani ya Torati, bali Mungu Alifundisha kusamehe pia sawa na hali, lakini Wayahudi wa baadaye waliondoa hiyo sehemu kwa sababu ya ugumu wa moyo wao. Kurani inaeleza ya kuwa Torati ilifundisha msamaha pamoja na sheria ya kisasi:

> "Na humo (katika Torati) Tuliwaandikia ya kwamba mtu kwa mtu, na jicho kwa jicho, na pua kwa pua, na sikio kwa sikio, na pia itakuwa kisasi katika jeraha. Lakini **Atakayesamehe**, basi ni kafara kwake." (Al-Maaida 5:46)

Basi habari ya msamaha walifunzwa, lakini wakabadili hiyo sehemu, kwa hiyo Mungu Akamtuma Yesu aje

kuitimiliza Torati kwa njia hii pia. Isaya pia alitangaza ya kuwa watu wamebadili sheria.

> “Kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele”. (Isaya 24: 5)

Ni bahati mbaya ya kwamba Musa alidhaniwa kuwa hakufunza kusamehe ilhali alifundisha kama tulivyoisha eleza, na pia ni la ajabu ya kuwa Yesu alipowakumbusha habari ya msamaha watu wakadhani kwamba amefuta sheria ya kisasi ilhali alisema wazi wazi ya kwamba:

> “Asiye na upanga, na auze joho lake akanunue.” (Luka 22: 36)

Basi popote pale Yesu anapoonekana akipinga Torati, kwa kweli haipingi ila anaeleza sheria ya Musa iliyoeleweka vibaya, au iliyofutiliwa mbali ndani ya Torati. Na pia inawezekana kuwa mahala fulani hata waandishi wa Injili wameharibu – lakini si waandishi wa mwanzo kabisa, bali wa baadaye waliogeuza Injili.

## Vitabu vya Mungu Hutokea Wapi?

Waislamu wasemapo kuwa kitabu kimeshuka kutoka mbinguni wanamaanisha ya kuwa Mungu Alimtuma malaika (Jibrili) aliyemshukia nabii na kumwambia maneno yaliyotamkwa na Mungu. Kurani pia ilishuka kwa njia hiyo. Inawezekana wakati mwingine nabii

aonyeshwe maandishi kwenye ubao ambayo ayasome na kuandika au aambiwe habari katika ndoto.

Mtume[saw] alipokuwa akiletewa wahyi (ufunuo) kutoka kwa Mungu kwa njia ya malaika Jibrili, alikuwa akiyakumbuka kwa ghaibu pale pale, kwani yalikuwa ni machache, na kisha baada ya malaika kuondoka, alikuwa akimwita mwandishi mmojawapo ambaye akamwandikia maneno hayo. Kwa njia hii Kurani Tukufu nzima ilishuka na ikaandikwa yote pale pale.

## Miujiza ya Mtume[saw]

Padre amesema ya kuwa Mtume[saw] hakuonyesha mwujiza ila tu kwamba Kurani Tukufu ilikuwa ni Mwujiza mzima kwani hakuna anayeweza kuleta mfano wake.

Ni kweli kabisa ya kuwa Kurani ni mwujiza mkuu wa Mtume[saw] lakini hata hivyo kaonyesha miujiza mingine pia. Wasomaji wanaelekezwa kusoma kitabu chetu kiitwacho *"Miujiza ya Mtume Muhammad[saw]."*

## Siyo Mashairi

Padre amedai kuwa Kurani ni mashairi. Kumbe hajui mashairi ya Kiarabu ni kitu gani. Kurani yenyewe inakatalia mbali upuuzi huu: "Wala hatukumfundisha shairi, wala haimpasi, huo sio ila ni ukumbusho na Kurani ibainishayo." (Yaa Siin 36:70)

## Kurani na Injili

Padre amepandisha cheo cha Injili bure aliposema kuwa Kurani na Injili ziliandikwa miaka 20 hivi baada ya kuteremshwa. Ukweli ni kuwa Mtume[saw] aliandikisha Kurani katika uhai wake, bali pale pale kila aya iliposhushwa akaiandikisha, kama tulivyoeleza hapo juu. Lakini hali ya Injili ni tofauti kabisa:

(1) Yesu anasema kuwa sikuja kuitangua Torati, lakini Injili inafunza pahala kadha kinyume cha Torati. Ndiyo kusema kuwa mahali hapo Injili imevurugwa.

(2) Injili siyo maneno ya Mungu, wala hata maneno ya Yesu (yaani Injili zilizopo duniani wakati huu). Kwani hamtakuta ndani yake 'Mungu Akinena', bali waandishi kadha wameandika maisha ya Yesu jinsi walivyotaka. Na hao waandishi Mathayo, Marko, Luka na Yohana wamehitilafiana pia katika mambo kadha wa kadha. Kwa mfano:

Inaonekana katika Yohana (1:19-44) ya kuwa Yesu alikwenda Galilaya moja kwa moja siku mbili baada ya kukaa na Yohana Mbatizaji (haikutajwa kabatizwa kwake). Lakini Mathayo (4:1) na Luka (4:1) na Marko (1:12) wanaeleza kuwa Yohana alimbatiza Yesu na kisha Yesu alijaribiwa na Shetani kwa siku arobaini nyikani.

Luka anatuambia ya kuwa Yusufu seremala alikuwa mtoto wa Eli (3:23); lakini Mathayo anasema hapana yeye alikuwa mwanaye Yakobo (1:16).

Luka anasema kuwa Yesu alichukuliwa mbinguni huko 'Bethania' (24:50-51); lakini katika Matendo (1:12) tunasoma alipaazwa kutoka mlima ulioitwa Mizeituni.

(3) Injili hazikutamkwa na Yesu, kwani Yesu alikuwa Myahudi na wanafunzi (mitume) wake nao walikuwa Wayahudi. Kama Yesu angetamka hayo au hata wanafunzi wake, bila shaka Injili za mwanzo kabisa zingekuwa katika lugha ya Kiyahudi (Kiebrania). Lakini miswada ya zamani kabisa inayojulikana katika historia ni ile ya Kigriki. Hata Injili moja haionekani katika Kiyahudi. Kwa hiyo, ni dhahiri ya kuwa mafunzo yaliyotolewa katika hizo Injili siyo lazima yalitolewa na Yesu. Naam, maneno machache yaliyotamkwa na Yesu yametiliwa ndani ya Injili kwa Kiyahudi moja kwa moja hadi leo. Kwa mfano: 'Hosana' (Mt. 21:9); 'Eloi, Eloi, lama sabakthani'; (Mt. 27:46) 'Rabi'; (Yn. 3:2); 'Talitha kumi' (Mk. 5:41).

Ilmuradi, minghairi ya maneno machache ya Kiyahudi mengine yote ni ya Kigriki ambayo yalifasiriwa katika lugha mbalimbali.

(4) Isitoshe, wataalamu wameisha kubali tangu zamani ya kwamba Agano Jipya liliandikwa tangu asili katika lugha ya

Kigriki kwa ajili ya Wagriki; na kwamba mabadiliko yalifanywa kusudi ndani yake siyo kwa bahati mbaya (Encyclopaedia Biblica J. 4, uk. 4980).

(5) Katika 'Commentary of Bible' iliyoandikwa na Horn tunasoma ya kuwa Injili ziliandikwa baina ya mwaka 37 hadi 98. (J. 4, sehemu 2 mlango 2)

(6) Wataalamu kama Baur na wengineo walisema kuwa Agano Jipya liliandikwa katika karne ya pili. Wengine walikanusha habari hii. (Historic ya Ukristo, J. 3, uk. 100 – Robert M. Glen)

(7) Katika karne ya nne tafsiri ya Biblia kwa Kilatini ilionekana ni maneno yaliyovurugika mno, kwa hiyo, Papa aliamuru kunyosha maandiko na kisha kati ya mwaka 383 na 400 Biblia iliandikwa iitwayo 'Jerome's Revised Version', iliyochukua mahali pa Biblia ya zamani ya Kilatini baina ya Wakristo.

(Encyclopaedia Biblica J. 4, uk. 4993)

Kwa vyovyote hakuna haja tuseme zaidi juu ya habari hii, kwani hata wataalamu wa Kikristo wenyewe wameisha kubali jambo hili ya kuwa Agano Jipya bali Biblia nzima waliyo nayo siyo ya asili. Kwa hiyo, tunashangaa juu ya padre kuilinganisha Biblia ya aina hii; na Kurani Tukufu ambayo iliandikwa siyo tu katika zama za uhai wa Mtume Muhammad[saw] bali kila aya iliposhuka ikaandikwa pale

pale kwa uangalifu. Hapa chini tutazungumza kidogo kuhusu kuhifadhiwa Kurani Tukufu.

## Uthman[ra] Hakukusanya Kurani

Tulivyoisha eleza hapo juu ya kuwa kila aya ya Kurani iliandikishwa na Mtume[saw] mara ilipokuwa ikishuka. Kwa hiyo, Mtume[saw] aliacha nyuma yake Kurani Tukufu nzima ikiisha andikwa tayari. Zaidi ya hayo kati ya Waislamu walipatikana wale waliokumbuka kwa ghaibu Kurani nzima neno kwa neno.

## Waalimu wa Kurani

Mtume Muhammad[saw] aliteua masahaba wanne waliokumbuka Kurani nzima kwa ghaibu chini ya usimamizi wa Mtume[saw] mwenyewe. Waalimu hao ndio wafuatao:

1. Abdullah bin Masuud[ra].

2. Salim Maula Abi Hudhaifa[ra].

3. Muadh bin Jabal[ra].

4. Ubayy bin Ka'b[ra].

Hao waalimu waliwafunza wengine Kurani Tukufu neno kwa neno jinsi walivyojifunza kwa Mtume[saw]. Mtume[saw] mwenyewe alikuwa anajua Kurani nzima kwa ghaibu. Bali kila mwaka malaika Jibrili alikuwa akishuka katika mwezi wa Ramadhani na kusoma Kurani Tukufu pamoja na Mtume[saw]. Katika Ramadhani ya mwisho

Mtume[saw] alisoma Kurani nzima mara mbili pamoja na malaika Jibrili.

## Kurani katika Jalada Moja

Katika Ukhalifa wa kwanza, masahaba 500 waliokuwa wamehifadhi Kurani nzima walipouawa katika vita iliyotokea baina ya Waislamu na jeshi la Musailamah, hapo Seyidna Umar[ra] alimwomba Khalifa Abu Bakr[ra] kuchukua hatua ya kuhifadhi Kurani, kwani waliokumbuka Kurani japokuwa ni wengi lakini wamepungua kati yao 500. Na kama katika vita mbalimbali wataendelea kuuawa, basi inaweza kutokea hatari kwa kuhifadhi Kurani. Kwanza Seyidna Abu Bakr[ra] hakujali shauri la Seyidna Umar[ra], lakini baadaye alikubali na akamkabidhi Zaid bin Thabit[ra] kazi ya kukusanya Kurani katika jalada moja kutokana na maandishi aliyoacha Mtume[saw] katika vipande vya mitulinga na kadhalika, pamoja na kusadikishwa na masahaba wawili waliokuwa wamekumbuka Kurani nzima kwa ghaibu. Zaid bin Thabit[ra] alikuwa miongoni mwa wale waandishi walioandika aya za Kurani zilipokuwa zikishuka.

Kwa vyovyote kazi hii ya umuhimu ilifanyika chini ya usimamizi wa Khalifa Abu Bakr[ra] mwenyewe ambaye pia alikuwa miongoni mwa waandishi wa Kurani ilipokuwa ikishuka. Kwa hiyo, Kurani ilikuwa imeandikwa tayari katika zama za uhai wa Mtume[saw] lakini ilikuwa katika

vipande. Abu Bakr[ra] aliikusanya katika jalada moja bila ya kugeuza mpango wa aya au wa sura au kuigeuza kwa njia yoyote iwayo.

## Waandishi wa Kurani

Ni bora zaidi tuandike majina ya waandishi wa Kurani waliokuwa wakiandika aya za Kurani mara zikishuka. Kati yao masahaba 15 wametajwa katika vitabu vya Hadithi za Mtume[saw] (Fat-hul Baari J. 9, uk. 19), nao ndio wafuatao:

1. Zaid bin Thabit[ra]. 2. Ubayy bin Ka'b[ra]. 3. Abdullah bin Sa'd bin Abi Sarh[ra]. 4. Zubair bin Al-'Awwam[ra]. 5. Khalid bin Said bin al-'As[ra]. 6. Abaan bin Said bin al-'As[ra]. 7. Handhala bin al-Rabii[ra]. 8. Mu'aiqib bin Abi Fatima[ra]. 9. Abdullah bin Arkam[ra]. 10. Shurahbil bin Hasana[ra]. 11. Abdullah bin Rawaha[ra]. 12. Seyidna Abu Bakr[ra]. 13. Seyidna Umar[ra]. 14. Seyidna Uthman[ra]. 15. Seyidna Ali[ra].

## Uhakikisho Zaidi

Siyo ya kuwa tumezusha leo kwamba kila aya ya Kurani ilikuwa imeandikwa na kupangwa tayari katika uhai wa Mtume[saw] bali hapa chini tunaandika ushahidi wake wa maandiko:

> "Kurani ilikuwa imekusanywa tayari katika uhai wa Mtume[saw]. Kila mara aya mpya iliposhuka, Mtume[saw] akawaita waandishi na kuwaamuru

kuiandika mahala maalum katika sura maalum."

(Tafsiri Neshapuri uk. 9)

Habari hiyo pia imeelezwa katika vitabu vingine vya Hadithi za Mtume[saw] kama vile Abu Daud, Tirmidhi, Mishkaat, Fat-hul Baari. Na katika Majma'ul Bayaan, uk. 196 tunasoma waziwazi ya kuwa mpango wa aya za Kurani haukufanywa na mtu yeyote hata Mtume[saw], bali malaika Jibrili alikuwa akieleza kila mara ya kuwa aya fulani itawekwa mahali fulani. Kusema kwamba sura zimepangwa kwa kuangalia urefu wa kila sura – yaani kwanza sura ndefu zimepangwa na baadaye sura ndogo ndogo – si sawa. Kwani sura ya kwanza kabisa (Al-Faatiha) ni ndogo sana, ina aya 7 tu, ilhali sura ya pili (Al-Baqara) ina aya 287. Sura ya tano (Al-Maaida) ina aya 121, lakini ya sita (Al-An'aam) aya zake ni 166. Na kwa njia hii sura zote zikichunguzwa itaonekana kuwa katika mpango wa sura urefu wake haukuangaliwa. Bali Mungu Amepanga sura za Kurani sawa na madhumuni yaliyoelezwa humo.

Kwa hiyo, imejulikana wazi ya kuwa hata ule mpango wa aya za Kurani ulipangwa sawa na wahyi wa Mwenyezi Mungu ulioletwa na malaika Jibrili.

## Uthmani[ra] Alifanya Nini?

Hapa swali lazuka kuwa kama Kurani ilikuwa imeandikwa nzima katika uhai wa Mtume[saw], na kisha

ilikusanywa katika jalada moja katika zama za Abu Bakr[ra], je, Uthman[ra] alifanya nini kuhusu jambo hilo mpaka yeye anatajwa-tajwa kila mara?

Jibu lake haliko mbali. Ni hivi kwamba katika zama zake Uthman[ra] alipokea habari ya kuwa watu wa baadhi ya makabila fulani hutamka maneno kadha ya Kurani kwa matamshi tofauti kidogo huku wakisema kuwa wemejifunza hivyo kutoka kwa Mtume[saw]. Na hiyo ni sawa.

Sababu yenyewe ni kuwa Kurani ilishuka kwa lugha halisi ya Kiarabu ya Kureish. Lakini baadhi ya makabila mengine ya Kiarabu yalikuwa na vilugha vyao ambavyo vilugha hivyo vilikuwa na matamshi tofauti kidogo kwa baadhi ya maneno fulani. Hao watu waliruhusiwa na Mtume[saw] kwa wahyi wa Mungu kutamka maneno hayo maalum kwa matamshi tofauti. Ijulikane kuwa matamshi yalikuwa tofauti kidogo lakini maana ilikuwa ni ile ile.

Katika zama za Khalifa Uthman[ra], Waislamu ambao hapo kabla waliishi zaidi katika mazingira ya kikabila, wakavuka ukabila na wakawa kitu kimoja, na lugha halisi ya Kiarabu ikawa lugha moja kubwa kwa watu wote. Kwa hiyo, Uthman[ra] alitengenezesha nakala za Kurani iliyokuwa imekusanywa katika jalada moja katika zama za Abu Bakr[ra] na kuzituma nakala hizo mahala mbalimbali, na akatoa amri yenye busara ya kuwa sasa haina haja ya kuendelea na ile tofauti ya matamshi

iliyoruhusiwa kwa ajili ya shida, kwani sasa watu wote wamejua lugha moja kubwa.

Kwa hiyo, padre haambiwi "kungoja hadi Ahera" kupata jibu la swali hili ya kuwa kwa nini Uthman[ra] alichukua hatua ya kukataza vikali kila tamshi lingine ghairi ya lile lililokuwa limeandikwa katika jalada hizo.

Asiyejua Kiarabu anaweza kuingiwa na wasiwasi ya kuwa nini maana ya 'matamshi tofauti'! Basi ijulikane ya kuwa ilikuwa ni tofauti ndogo ndogo za 'irabu' sawa na lahaja za makabila, zisizoleta tofauti katika maana. Mpaka leo, hizo zimeandikwa katika vitabu vya maelezo ya Kurani. Kwa mfano katika sura (Al-Baqara) 2:21 neno 'yakhtafu' maana yake ni inanyakua, lakini 'Yakhattifu' (ambalo lilikuwa yakhtatifu) pia maana yake ni hiyo hiyo, na yote mawili yametokana na asili moja. Basi matamshi hayo yote mawili yaliruhusiwa na Mungu (Tafsiri Baidhawi chini ya Sura Al-Baqara 2:21). Mfano mwingine ni neno Jibriil (malaika Gabrieli). Hili liliruhusiwa kutamkwa Jabraiil, Jabriil, Jabrail na Jibriil. Tamshi la mwisho limehifadhiwa katika Kurani, lakini watu wa makabila mbalimbali waliruhusiwa kutamka sawa na lahaja zao. Na ni dhahiri ya kuwa tofauti hizi za matamshi hazileti hitilafu katika maana. Neno Jibriil limetumika katika

sura Al-Baqara 2:98. Tazameni matamshi hayo katika Tafsiri Baidhawi chini ya aya hiyo.

Matamshi hayo tofauti ya makabila mbalimbali mpaka leo hii yamehifadhiwa katika vitabu, ila tu ndani ya Kurani Tukufu linaandikwa sawa na lugha ya Kureish kwa amri ya Mungu.

Mfano wake kwa Kiswahili ni kama vile neno 'mke' ambalo hutamkwa na watu wa kusini kuwa 'nke' na 'mtoto' kuwa 'ntoto'. Ni tofauti ya matamshi tu lakini maana haigeuki hata kidogo. Kwa Kimvita 'njia' hutamkwa 'ndia', 'uchaguzi' kuwa 'utaguzi'. Wengine wanatamka 'dito' badala ya 'jicho'.

### Usahihi wa Kurani

Wataalamu wa Kikristo waliochunguza usahihi wa Kurani

wamekubali kabisa ya kuwa:

> "Juhudi za wanazuoni wa Ulaya kuhakikisha kuwa yaliingia mabadiliko katika Kurani zimeshindwa".

(Encyclopaedia Britannica chini ya neno 'Kurani').

## Mitume wa Yesu

Padre amesema ya kuwa hakuna 'mtume', aliyeandika Kurani baada ya Muhammad[saw] "kama walivyofanya mitume wa Yesu" (uk. 45). Hii ni sawa kwani Kurani

ilikuwa imekwisha andikwa tayari mbele ya Mtume[saw]. Na hadi leo tunayo Kurani ile ile bila ya tofauti yoyote iwayo.

Lakini Injili ziko katika hali isiyoaminika kabisa kama tulivyokwisha eleza nyuma.

## Upungufu wa Imani

Mtume[saw] alieleza hoja zilizo wazi kuhakikisha ubatili wa uungu wa Yesu, na kisha akawaita Wakristo kushindana naye kiroho kwa kumwomba Mungu Awaadhibu wenye imani mbovu. Wakristo walikataa kupokea wito huo. Padre anasema kuwa sababu yake labda huenda wakaogopa ukatili fulani, au upungufu wa imani, au kwa sababu nyingine, kama kuogopa kuvunja amri ya Yesu:

> 'Usimjaribu Bwana Mungu wako.' (Mt. 4:7)

Kwa kweli ilikuwa ni upungufu wa imani uliowazuia wasikubali wito huo, kwani baada ya kumsikiliza Mtume[saw] wakatambua kuwa imani yao haina msingi.

Padre amesema kuwa:

> "Wakaahirisha ubishi wao mpaka siku ya Kiyama."

Lakini itambulikane ya kuwa hakuna busara kuahirisha hadi Kiyama, kwani huko kutakuwa ni 'kilio na kusaga meno' (Mt. 24:51). Bora tujadili hapa hapa duniani na kuamua vizuri.

## Kutayarisha Vita?

Padre amepotosha ukweli alipoandika ya kwamba baada ya kufanya ibada ya Umra (Haji ndogo), Mtume[saw] akarudi Madina "kutayarisha 'vita' ya mwisho."

Hii siyo kweli hata kidogo, kwani kulipatikana mkataba baina ya Waislamu na Wapagani wa Makka kutokupigana vita kwa miaka 10. Hivyo, haina maana kusema kuwa Mtume[saw] alikwenda kutayarisha vita. Naam, kabla ya kumalizika hiyo miaka 10, Wapagani walivunja mkataba, ndipo Mtume[saw] aliiteka Makka pamoja na masahaba watakatifu elfu kumi sawa na bishara ya Biblia (Kumbukumbu 33:2), bila kumwaga damu.

Tazameni Biblia ya Kiingereza, kwani kwa Kiswahili wamebadili na kuandika "Meribeth-Kadesh" badala ya neno 'elfu kumi.'

## "Mti na Matunda yake"

Padre anasema ya kuwa hatuwezi kumhukumu Muhammad[saw], lakini tunaweza kuhukumu matunda ya mti wake. Na kisha ametaja baadhi ya mambo kwa kuilaumu Islam.

## Kutangua Dini zote

Padre anachukia kwa nini Muhammad[saw] ametangua dini zote za kale.

Sawa na mafunzo ya Kiislamu, manabii wote wa kabla ya Mtume[saw] walitumwa kwa ajili ya watu maalum na zama maalum, na kwa hiyo sheria zao ziliwahusu watu fulani tu kwa ajili ya muda fulani. Basi ilibidi ije sheria itakayowahusu watu wote na zama zote hadi Kiyama. Na hiyo ndiyo sheria ya Islam. Yesu wanayejivunia pia alitumwa kwa ajili ya kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli (Mt. 15:24). Mathayo akitaja bishara ya Mika kumhusu Yesu ameandika:

> "Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda; kwa kuwa kwako atatoka mtawala atakayewachunga **watu wangu Israeli**." (Mt. 2:6)

Kumfanya Yesu awe mwokozi kwa dunia nzima ni kubatilisha bishara ya Mika.

## Unabii Uliotimilika Zamani

Padre ameingiwa na husuda juu ya Mtume[saw] kwa nini amepata unabii. Kumbe Kitabu chake kinatoa bishara za ujaji wa Nabii Muhammad: Agano la Kale na pia Agano Jipya. Someni kitabu chetu kiitwacho *"Mtume Muhammadsaw katika Biblia."*

## Ujamaa wa Kiislamu

Padre anashangaa kwa nini sasa baada ya ujaji wa Muhammad[saw] ujamaa wa Kiislamu upokelewe. Ni

dhahiri ya kuwa kama Mtume[saw] kweli ametumwa na Bwana Mungu, lazima mambo yake yote yakubaliwe.

## Kwa Nini Agano la Kale?

Padre anasema kwa nini Uislamu unaturudisha kwenye Agano la kale? Jibu lake ni kuwa hata Yesu hakuja kutangua Agano la Kale (Mt. 5:17). Padre anasema sheria ni laana; huku ni kujiepusha na wajibu waliolazimishwa wanadamu na Mungu. Lakini kwa Mwislamu sheria ni baraka. Basi lazima tuwarudishe Wakristo kwenye Agano la Kale ili wasiwe wazembe na kutegemea damu ya Yesu, bali wenyewe watie bidii.

## Uislamu Umetimiza Vitabu Vya Kale

Ni sawa kwamba Uislamu umetimiza vitabu vya kale. Ule upungufu uliokuwa ndani ya hivyo umeondolewa na Islam, na sheria kamili imeletwa katika Kurani Tukufu.

## Sheria za Zamani

Padre amedai bila kuchunguza ya kwamba kwa nini sheria za zamani kama ndoa, amri za upendo na kadha wa kadha zilizoletwa na Kristo hazimo tena ila tunayakuta ya Agano la Kale (unajisi, kufunga, kusali...).

Padre hataki kujiondolea unajisi wala hataki kufunga au kusali. Yesu mwenyewe alisali akianguka kufudifudi alipoogopa kukamatwa na Wayahudi na kuangamizwa

msalabani (Mt. 26:39). Ama kufunga pia kumethibitika katika maisha ya Yesu. Someni:

> "Akafunga siku arobaini mchana na usiku." (Mathayo. 4:2)

Yesu aliwaeleza wanafunzi wake jinsi ya kufunga saumu. (Mathayo. 6: 16-17)

Wanafunzi waliposhindwa kumponya kijana fulani, Yesu

alimponya. Hapo wanafunzi walipomwuliza Yesu kwa nini wao hawakuweza kumponya kijana yule, akasema Yesu:

> "Lakini namna hii haitoki ila **kwa kusali na kufunga."** (Mt. 17:21).

Kwa hiyo, faida ya kusali na kufunga imekubaliwa na Yesu, bali kwa nguvu ya kusali na kufunga akaweza kutoa pepo mchafu wa kijana huyo. Padre hataki kujisumbua katika kujitakasa, hii ndiyo sababu katika zama hizi hata Mkristo mmoja hawezi kutenda alivyoahidi Yesu.

Padre anasema kwa nini sheria kuhusu ndoa na amri ya upendo zilizoletwa na Kristo hazimo katika Islam. Jibu lake ni kuwa sheria iliyokamilika sana kuhusu ndoa imo katika Kurani kuliko kitabu chochote cha dini yoyote iwayo. Na habari hii ilijulikana wazi ilipotungwa sheria ya ndoa na urithi nchini humu.

Juu ya upendo pia fundisho lipo katika Islam, lakini upendo umfaao mwenzako; sio upendo wa bandia wa kimdomo tu. Upendo wa kweli unamtuma mtu awatendee wema watu wote. Someni Kurani Tukufu sura An-Nisaa 4:37; Haa Miim 41:35; Ash-Shuuraa 42:41 na penginepo ambapo Mungu Ameeleza kuwatendea wema jamaa wa karibu, wazazi, marafiki na watu wote.

Kurani inasema kuwatendea vizuri walio jamaa na wengine. Lakini Yesu alipofikiwa na mama yake mzazi na nduguze hakuwakaribisha bali akasema:

> "Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani? Akawanyoshea mkono wanafunzi wake, akasema, Tazama, Mama yangu na ndugu zangu! Kwa maana yeyote atakayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu na umbu langu na mama yangu." (Mat. 12: 49,50)

Hii yaonyesha adabu yake mbaya mbele ya mzazi wake; bali pia yaonyesha ya kuwa mama yake hakumwamini Yesu. Je, padre anataka huluka ya aina hii ifundishwe na Kurani. Huu ndio upendo wa Yesu? Kurani inafundisha juu ya wazazi:

> "Wala usiwakemee, na useme nao kwa heshima." (Banii Israaiil 17:24)

Au padre anataka kutuambia upendo wa Yesu alioueleza aliposema:

> "Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la, sikuja kuleta amani, bali upanga." (Mt. 10:34)
>
> "Nimekuja kutupa moto duniani; na ukiwa umekwisha washwa, ni nini nitakalo zaidi?" (Luka 12:49)

## Kupenda Usafi

Padre amedai Kurani haifundishi juu ya usafi. Elimu ya padre ni haba juu ya Kurani. Hebu someni:

> "Na nguo zako uzisafishe, na uchafu uuondoe." (Al-Muddaththir 74:5-6)
>
> "Kisha wajisafishe taka zao." (Al-Hajj 22:30)

Mtume[saw] alisema kuwa: *An-nadhafatu minal-imani*, yaani usafi ni sehemu ya imani.

Tunauliza, Yesu amefundisha usafi gani? Je, kula chakula kwa mikono michafu ndilo fundisho la kutunza usafi? Wanafunzi wa Yesu walikuwa wakila chakula bila kunawa (Marko 7:2). Na Yesu akawatetea walipopingwa na wengine (Marko 7:15).

Hoja ya Yesu ni bure kwamba kinachoingia tumboni mwa mtu hakiwezi kumtia unajisi, kwani shabaha ya kunawa kabla ya kula ni kupata usafi ambao Yesu hataki.

Angalieni hususa katika nchi yetu kwa jumla ndugu wanakula chakula kwa kumega na mkono wakichanganya mchuzi na wali au ugali. Sasa kama mtu hanawi kabla ya kula, bila shaka anafanya kinyume na usafi, na anaweza kupata maradhi. Hata kama mtu akifikiri kuwa mikono yake ni safi, lakini bila wasiwasi katika muda kidogo tu kwa ajili ya vumbi mikono hutakiwa kuoshwa kabla ya kula waila vumbi na takataka zote zitaingia tumboni mwako na utaugua.

Neno unajisi si balaa kubwa sana, bali maana yake ni kitu kilicho kinyume na usafi. Tuangalie usafi wa roho na pia wa mwili.

## Wasemaje Juu ya Nafsi Yako?

Padre ameandika kuwa Muhammad[saw] alilelewa katika upagani. Kwa kweli katika zama za Mtume[saw] upagani ulienea katika Arabu, lakini Mtume[saw] ingawaje kakulia huko lakini hakulelewa kipagani. Ile aya aliyoitaja yeye (Adh-Dhuhaa 93:8) haielezi shabaha yake. Yesu alilelewa Kiyahudi.

## Asionekane Mpole

Padre amezusha kuwa aya 160 ya sura 3 Aali 'Imraan inasema kuwa Muhammad 'hana budi kujishinda ili asionekane kuwa mpole mno'. Ebu someni wenyewe aya hii:

> "Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao; na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu, bila shaka wangelikukimbia." (Aali 'Imraan 3:160)

Aya hii inasema kuwa Mtume[saw] ni mpole na laini kwa rehema ya Mungu. Siyo kwamba 'asionekane kuwa mpole mno'.

## Mambo ya Ahera

Padre anasema Mtume[saw] hakujua mambo ya ahera. Kwa kweli ni Mungu pekee Anayejua kikamili mambo ya ahera. Binadamu anajua kiasi tu alichoambiwa na Mungu.

Hata Yesu hakujua alivyokiri mwenyewe:

> "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba." (Marko 13:32)

Basi ujuzi kamili ni wa Baba tu yaani Mwenyezi Mungu.

## Kutenda Dhambi

Padre ametaja aya ifuatayo kuhakikisha kuwa Mtume[saw] anatenda dhambi:

> "Ili Mwenyezi Mungu Akufunikie makosa yako (unayosingiziwa) yaliyotangulia na yajayo." (Al-Fat'h 48:3)

Hapa panaeleza kufunikiwa makosa anayosingiziwa na watu kama Padre Anglars. Sawa na imani ya Kiisiamu siye

tu Muhammad[saw] bali manabii wote hawatendi dhambi. Mungu Anawalinda na kila dhambi.

Lakini Yesu mwenyewe anakiri kuwa yeye siye mwema:

> "Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? hakuna aliye Mwema ila Mmoja, ndiye Mungu." (Marko10:18)

Asiye mwema bila shaka anatenda dhambi! Fikiri bwana Padre!

## Hana Mamlaka

Kweli mtu yeyote hana mamlaka ya kweli juu ya mwingine ila ni Mungu tu. Kazi ya Manabii ni kufikisha ujumbe na kuwaonya watu; hawawashurutishi kukubali dini. Yesu naye alikuwa hana mamlaka, waila Waisraeli wote wangelimkubali. Kama mamlaka yanadaiwa ndani ya Injili, basi ni ya bandia.

## Kwa Waarabu?

Mtume[saw] alitumwa kwa ajili ya wanadamu wote (Al-A'raaf 7:159). Ile aya aliyoitaja padre (Al-Baqara 2:130) inaeleza dua ya Nabii Ibrahimu na Ismaeli kwa kuinuliwa Mtume kati ya wazao wao.

## Kundi Moja

Padre amepotoka kuelewa maana ya (Al-Maaida 5:49). Anasema Mungu Hataki kuwafanya watu wote kundi

moja. Kwa kweli aya inasema kuwa Mungu Angewafanya kundi moja kama Angetaka hivyo kwa nguvu. Lakini Hatumii nguvu, bali Anawajaribu. Yaani Ameleta sheria itakayowaunganisha pamoja lakini baada ya kujaribiwa watakapoielewa kwa makini.

## Kuomba Mara Sabini

Padre anasema Mungu Hawezi kuwasamehe watu hata kama Mtume awaombee mara sabini. Ametaja (At-Tauba 9:80). Kwa kweli mkisoma aya hiyo pamoja na za kabla yake, mtajua ya kuwa habari hiyo ni ya wale wanafiki ambao kazi yao daima ni kuicheka Islam na kufanya masihara, siyo kwamba watu wote hawatasamehewa. Hao ni watu maalumu ambao madhali hawaachi unafiki wao hawatasamehewa. Lakini wakiuacha unafiki bila shaka watasamehewa.

## Wasitoke Bila Ruhusa

Padre amesema kwamba Kurani iliwakataza watu wasitoke mbele ya Mtume bila kuomba ruhusa kusudi cheo chake kikubaliwe, wala wasiwe kati ya watu wabaya wasioamini (uk. 49).

Aya aliyotaja padre kuhakikisha habari hiyo ni (An-Nuur 24:63) ambayo wasomaji wenyewe waisome kutambua maana yake ni nini:

> "Waaminio ni wale waliomwamini Mwenyezi

> Mungu na Mtume wake; na wanapokuwa pamoja naye kwa jambo linalohusiana na wote, hawaondoki mpaka wamwombe ruhusa." (An-Nuur 24:63)

Ni wazi ya kuwa hapa maana yake ni kwamba wanapokuwa katika mkutano kwa kufikiria jambo la muhimu linalohusu umma, waaminio hawapaswi kuondoka kwa haja fulani ila baada ya kuomba ruhusa kwa Mtume[saw]. Kwa kweli hiyo siyo kujikuza bali ni adabu ya vikao vya kushauriana. Hata katika bunge, mbunge anapotaka kwenda nje mara moja anamwomba spika ruhusa. Padre kwa ajili ya chuki yake aliyo nayo kwa Mtume[saw] humlaumu katika kila jambo bila kutafakari zaidi.

Tena aya hiyo haimhusu Mtume[saw] pekee, bali katika mkutano wowote unaoitishwa kwa kujadili jambo fulani wahudhuriao wanalazimika kumwomba ruhusa mwenyekiti kabla ya kuondoka. Je, katika vikao vya Kikristo adabu hii haiangaliwi? Kama hapana basi mjifunze hiyo adabu!

## SEHEMU YA PILI — UENEZI WA ISLAM

Kwenye uk. 51, padre amesema kwamba Uislamu ulienea kwa kutanua utawala, yaani kuingia nchi fulani, kuchukua madaraka yote kuifanya dini ya washindi kuwa dini ya watu, ama kwa lazima, ama kwa shuruti fulani, na kwamba uenezi huo kwa Waislamu huitwa Dar-el-Islam.

Padre amepotosha ukweli. Dar-es-Salaam au Dar-el-Islam au hata Dar-el-Aman maana yake ni ile nchi ambayo haina vita na Waislamu au baada ya kupigana vita ikashindwa mbele yao na ikatekwa na Waislamu. Katika maana hiyo hiyo India iliitwa na wataalamu kadha wa Kiislamu kuwa Dar-el-Aman au Dar-el-Islam ilhali ilikuwa ikitawaliwa na Wakoloni wa Kikristo.

Kinyume cha Dar-el-Islam ni Dar-el-Harb yaani nchi ya vita; ni kila nchi inayopigana na nchi ya Kiislamu. Padre ajisahihishe kuwa wakati huu Palestina siyo Dar-el-Islam bali ni Dar-el-Harb.

### Abu Bakr[ra], Khalifa wa Kwanza

Padre amesema ya kuwa katika zama za Abu Bakr[ra], Islam ilivuka mipaka ya bara Arabu kwa sababu Wakristo wa hapo walikuwa wakichukia wafalme wa Rumi na Uhabeshi (Ethiopia) na Uajemi, kwa hiyo waliona afadhali wapate msaada wa Waislamu, kujitenga na wafalme waovu. (uk. 51)

Padre amekiri kuwa utawala wa Waislamu haukuwa mwovu, ndio maana Wakristo walitaka msaada wa Waislamu. Lakini anaposema kuwa hii ndiyo sababu Uislamu ulivuka mipaka ya bara Arabu, hapo hakusema sawa. Waislamu hawakuhitaji msaada wa Wakristo. Je padre hajui ya kuwa Wayahudi walipoleta fitina walishindwa namna gani? Wakristo pia kama wangelileta fitina hawangefaulu. Bali wao wenyewe walihitaji msaada wa Waislamu nao wakapata pia kama alivyokiri padre.

## Dhimmi

Padre ametoa udhuru mbovu sana. Wasiokuwa Waislamu walitakiwa kutoa kodi hafifu sana kama dinar moja kila mwezi, bali hata Dirham 4 pekee kwa mwezi na badala yake walipewa ulinzi kamili katika serikali ya Islam na wakapewa haki zote za kibinadamu bila kutwishwa wajibu mzito wa kulinda nchi katika siku zile ngumu za vita. Lakini Waislamu walitakiwa kutoa uhai wao ili kuwalinda 'Dhimmi' hao na kuilinda nchi pia. Bali Waislamu nao walitakiwa kutoa kodi maalum iliyokuwa kubwa zaidi kuliko waliyotozwa wasiokuwa Waislamu; kodi hiyo huitwa Zaka ambayo kima chake ni kikubwa zaidi kuliko dinari moja au dirham 4 pekee. Juu ya hayo Waislamu walipotakiwa kupigana vita, walikuwa wakijitegemea kuhusu silaha na chakula na hata nguo; yaani kila

mwanavita alipaswa kujitegemea bila kupata vitu hivyo kutoka kwa serikali.

Kwa hiyo, walipotozwa kodi hafifu sana bila kubebeshwa mzigo mkubwa wa kutoa uhai kwa ajili ya nchi, ilikuwa ni raha kwa wasiokuwa Waislamu. Bali baadhi wa watu walifikiri pengine kodi hiyo ilikuwa ni sababu ya watu kadha kutokusilimu, kwani wakisilimu watatakiwa kutoa kodi (zaka) kubwa.

Kuitwa 'dhimmi' hakukuwa ni sababu ya watu kuchukia. Bali 'dhimmi' maana yake ni yule anayepata amani na ulinzi wa mali yake na nafsi yake na kila kitu chake. Yaani hao walipewa ulinzi kamili chini ya serikali ya Kiislamu. Hilo halikuwa ni tusi, bali ni neno linaloonyesha kuwa Waislamu walilazimika kuwapa ulinzi wa kila aina nchini ili waishi bila taabu yo yote.

Basi kama watu walisilimu, bila shaka walifanya hivyo kwa kuona mafunzo bora ya Kiislamu na vitendo vizuri vya Waislamu.

Historia inatuambia ya kuwa Waislamu walipolazimika kwa muda kuondoka Palestina wakawarudishia Wakristo (wenyeji wa hapo) kodi yao, na Wakristo waliwasindikiza Waislamu kwa machozi wakisema wanawapenda Waislamu kuliko Watawala wa Kikristo!

## Umoja Unavunjika

Padre ameeleza kuwa Waislamu waligawanyika katika makundi mbalimbali. Hii ni sawa. Lakini hali kama hiyo imezipata dini zote zilizopo duniani. Baada ya muda kupita kutoka kwa zama za nabii, watu huanza kugawanyika kwa ajili ya fikara zao tofauti. Katika zama za uhai wa nabii, watu wakihitilafiana wanamwuliza nabii naye anawaamulia, hivyo wanabaki katika umoja. Lakini baada ya nabii kufariki, polepole hitilafu zinapozuka kati yao, kunakuwa hakuna wa kuwaamulia anayekubaliwa na wote. Hii ndiyo sababu hata Ukristo umegawanyika katika madhehebu mengi sana.

## Jina Ali

Padre amepotoka aliposema kuwa:

> "Ukikuta jina Ali katika jina la Mhindi (Hasan Ali, Rajab Ali, n.k.) basi ujue yeye ni Shia."

Kwa kweli Waislamu wa kila dhehebu wanatumia jina hili, sio Washia tu pekee. Katika India wako Waahmadiyya wengi wanaoitwa kwa jina Ali kama vile Muhammad Ali, Husain Ali. Na pia kati ya Wasuni wa Kihindi wapo wengi sana wenye jina hilo. Hakika yenyewe ni kuwa jina Ali halijulishi kuwa mtu fulani ni Mshia. Basi padre asahihishe mawazo yake.

## Khalifa

Padre amesema kuwa Wasuni walimkubali Muawiya kuwa Khalifa, Kwa hakika Waislamu Wasuni (na Waahmadiyya pia, kwani tu Wasuni, wanaamini kuwa Ukhalifa ulikoma baada ya Ali, Khalifa wa nne. Hapo baadaye ufalme ulipatikana. Ingawaje wafalme hao walitumia lakabu ya ukhalifa, lakini hawakuwa Makhalifa bali ni wafalme.

Ili kutofautisha kati ya Ukhalifa wa makhalifa wanne wa mwanzo, na wafalme waliojipatia lakabu ya Khalifa, Waislamu mara nyingi wanawaita wale wanne kuwa *Khulafai Rashidiin*, yaani makhalifa walioongoka, ndio makhalifa hasa; wengine walikuwa ni wafalme. Kwa hiyo, kama baadhi ya wafalme fulani kati yao hawakufuata barabara mafunzo ya Kurani, ni kosa lao wenyewe. Lakini Makhalifa Abu Bakr[ra], Umar[ra], Uthman[ra] na Ali[ra] ndio mifano kwa Waislamu.

## Umoja Utapatikana Tena

Padre anaandika ya kuwa baada ya umoja wa Waislamu kuvunjika, mpaka sasa umoja haujapatikana tena, wala hapana mtu yeyote anayetumaini kwamba utapatikana tena kama ulivyokuwa wakati wa Waumeyya na Waabasi.

Padre asijifurahishe na wazo hilo bovu. Si mtu mmoja tu bali wanajumuiya wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya walio karibu milioni kumi duniani kote wana

imani ya kuwa kwa njia ya hii Jumuiya ya Ahmadiyya umoja ule ule uliokuwa zamani utapatikana mara nyingine, na Mungu Amesimamisha hii Jumuiya kwa shabaha hiyo hiyo.

Bali na Waislamu wengine wote nao wanaitakadi kuwa katika zama za mwisho Uislamu utaenea kila mahala atakapotokea Masihi kati yao. Kwa hiyo Wakristo wanaotaka kusilimu wasivunjike moyo kwamba umoja hautapatikana tena kati ya Waislamu; watulie tu, utapatikana katika muda usio mrefu sana. Hadi ya mwisho ni mpaka miaka 200 tangu sasa. Na muda huo si mrefu katika maisha ya dini kubwa sana.

## Islam katika Afrika

Tangu uk. 58, padre ameanza kueleza jinsi Islam ilivyoenea katika Bara la Afrika. Ameeleza kuwa kwa bahati mbaya silaha pia zikatumika kwa kueneza dini. Lakini padre haelezi kwamba kulikuwa na sababu kadha wa kadha za siasa zilizolazimisha vita, na vitani bila shaka silaha zinatumika. Lakini vita vyenyewe havikuwa kwa kueneza dini.

Padre amemtaja Uthman dan Fodio aliyeeneza dini mpaka pande za Adamawa. Huyo Hadhrat Uthman bin Fodio (dan = bin) alikuwa mcha-Mungu sana; hakupigana vita kwa dhuluma bali alilazimishwa na maadui.

## Afrika ya Mashariki

Padre amesema kuwa ingawaje Islam iliingia Afrika ya Mashariki kwa upole na amani zaidi lakini siyo maana yake kwamba Islam inakataa silaha zinapohitajika. (uk. 59).

Padre amejaribu kuwahakikishia wasomaji kwamba Islam inaruhusu kueneza Islam kwa silaha kama haienei kwa njia nyingine. Padre hawezi kuwapumbaza watu katika zama hizi za elimu ambapo tumeisha fasiri Kurani kwa Kiswahili inayoeleza wazi wazi kuwa:

> "Hakuna karaha katika dini." (Al-Baqara 2: 257)

Padre mwenyewe amekiri katika kitabu chake kuwa watu hawakulazimishwa kusilimu.

## Utumwa

Padre amesema kuwa:

> "Biblia inataja kazi hiyo ya Waarabu." (Mwanzo 37:27)

Vyema. Lakini ukifunua Biblia sehemu hiyo utakuta ya kuwa nduguze Nabii Yusufu wakamwuza Yusuf kwa Waishmaeli. Lakini bwana padre amesahau kwamba waliouza ni wenyewe wana wa Israeli, kabila la Yesu. Tutaandika zaidi juu ya Utumwa baadaye.

*Biashara na Ukazi*: Waarabu walikuja Afrika Mashariki kwa ajili ya biashara na pia kukaa. Padre amesema ya

kwamba hizo pia zikawa ni sababu ya Islam kuingia huku kwetu. Pia padre amekubali kuwa Islam haikuingia Afrika Mashariki kwa vita. Basi kuna lawama gani tena!

**Picha ya Mtumwa**

Kwenye uk. 62, padre amechora picha ya mtumwa na chini yake ameandika maneno ya Isaya:

> "Walio utumwani watawekwa huru."

Lakini tutahakikisha katika sehemu nyingine ya kitabu hiki jinsi kanisa lilivyoendesha biashara ya Utumwa. Bishara hiyo ya Isaya imetimia kwa njia ya Mtume[saw].

Kwenye ukurasa huo huo padre amekubali kuwa dini ya Kristo iliweza kustawi tu kwa sababu ya Wareno na utawala wao.

**Msaada wa Waarabu**

Padre amesema kwamba Waarabu walieneza "lugha ya Kiswahili mpaka miji na vijiji vya ndani, walisaidia maendeleo, na muungano kati ya makabila" (uk. 66). Na hii kwa kweli si jambo baya bali ni faida kubwa sana kwa taifa.

**A. Njia ya Biashara**

Padre ameeleza jinsi Waarabu walivyokuja hapa Afrika Mashariki kwa ajili ya biashara. Alivyosema padre, hakuna Mwarabu aliyekwenda shambani kuhubiri Islam; bali watu walipoona Waarabu walivyoishi,

wakavutika na wakaingia katika Islam – lakini siyo mara moja bali pole pole. Hapa tunauliza je, njia hii ya watu kusilimu si halali?

Siyo tu kwamba njia hiyo ni halali sana, bali hii pia inahakikisha kuwa bila kuhubiriwa watu walivutika kwenye Uislamu, na jambo hilo linahakikisha kwamba desturi za dini hii ziliwaathiri wenyeji nao wakakubali kusilimu.

Padre amesema ya kuwa wale tu walisilimu, wasiokuwa wameridhika na mila zao za zamani. Tunasema kwamba waliosilimu bila shaka wakaona mila nzuri za Kiislamu kuliko zile zao. Kama wangesilimu huku wakizipenda bado mile zao, bila shaka wangelikuwa Waislamu wabovu. Padre amesema kuwa haijulikani kama wengi walipenda kutahiriwa. Ieleweke ya kwamba kutahiriwa kulipatikana mapema katika mila za baadhi ya makabila ya Kiafrika, bali na Biblia pia inalazimisha kutahiriwa. (Mwa. 17: 9-14).

Padre amesema tena ya kuwa sababu ya watu kusilimu ni kwamba wenyeji walipata kutoka kwa Waarabu ujamaa ambao ni kitu cha lazima kwa wanadamu. Basi, hapo Waarabu wangesifiwa waliowapa wenyeji wa zamani kitu cha lazima sana kwa wanadamu.

Padre amekubali mwishowe kwamba Waarabu hawakutumia njia isiyo halali. Anakiri ya kuwa Waarabu

hawakutumia nguvu kwa kueneza dini; mvuto wa ustaarabu na upendeleo wa kidini vilitosha. Sawa. Na Ukristo pia uliingia kwa njia ya hospitali na mashule. Tutaeleza habari hii zaidi mbele katika mahali pafaapo.

## Mitume wa Kristu

Padre ameeleza kwamba Ukristu uliingia nchini kwa njia nyingine katika miaka ile ile, na mpaka sasa. "Yaani wabashiri wa Ukristu hawakuja kwa ajili ya biashara, bali walikuja kwa nia ya kubashiri dini" kasema padre. Lakini mahubiri yao yanajulikana kwa watu wote. Wakatumia njia fulani ya kuwavuta watu kwa mfano kwa kujenga mahospitali. Kwa kuwa watu walihitaji msaada wa hospitali, hivyo wakavutika kwa wajengaji wa hizo hospitali ambao wakaanza kuwabatiza kwa jina la baba na mwana na roho mtakatifu kwa kufaidika na taabu za watu waliolazimika kupata matibabu. Ingawaje watu wote wanatibiwa humo, lakini Wakristo walianza kupendelewa, na kwa njia hii watu kadha walitanasari si kwa kuuelewa Ukristo wenyewe, bali kwa kupata matibabu kwani hakuna aliyetambua 'Utatu' ni kitu gani kwa kuwa eti ni siri.

Wakati huu mbele yetu iko taarifa iliyotolewa katika gazeti la 'Urdu Digest' la mwezi Aprili 1968 ambayo taarifa hiyo inamsikitisha kila mwenye kuthamini ubinadamu. Taarifa yenyewe inahusu hospitali za misheni.

Imeelezwa humo wazi wazi ya kuwa mgonjwa asiye Mkristo, hususa mama mwenye maradhi ya hatari sana anatendewa kwa hila mbaya sana. Anapokelewa kwa huruma na mara moja daktari anamwandikia dawa na kisha mwuguzi hachelewi kutayarisha ile dawa mbele ya mgonjwa na kumwambia, 'kunywa kwa jina la Mtume'. Mgonjwa Mwislamu anafurahi kwani amesikia jina la Mtume – ingawaje ni ujinga wa mwuguzi huyo wa Kikristo, kwani Mwislamu anamtaja Mungu, siye Mtume, wakati wa kutenda jambo lolote. Kwa vyovyote mgonjwa anakunywa kwa kutamka 'Bismillahi.' Kila siku hutendeka hivyo, lakini mgonjwa haoni nafuu. Na kisha baada ya siku tatu au nne anapewa dawa ya rangi hiyo hiyo akiambiwa; "kunywa kwa jina la Yesu." Mgonjwa kwa kuwa huwa taabani, hivyo mwenye imani dhaifu anaitika na kusema 'nanywa kwa jina la Yesu.' Kumbe, kweli dawa imefanya kazi leo. Basi mgonjwa anakuwa na imani kuwa Yesu amemponya, na hapo anatanasari.

Makala hiyo ya 'Urdu Digest' inatoboa ya kuwa mwanzoni mgonjwa anapewa maji tu ya rangi, siyo dawa, kwa hiyo haileti nafuu 'dawa' hiyo; lakini kisha dawa hasa inatolewa ambayo inaleta nafuu kwa mgonjwa ambaye anadanganyika kufikiria eti Yesu amemponya!

Basi, hii kwa jumla ni hali ya hospitali za misheni. Hatusemi kila mahala wamefanya hivyo; lakini kwa

vyovyote inahakikisha habari hii ya kuwa hospitali zilitumika kama chambo.

Hali ya mashule yao pia inajulikana kwa wote. Katika nchi yetu wapo Waislamu waliolazimika kuchukua jina la Kikristo ili kupata masomo katika shule za misheni. Tunaye ndugu fulani katika Jumuiyya ya Ahmadiyya pia ambaye alilazimika kufanya hivyo alipokuwa Msuni katika zama za utoto wake.

Katika India Wakristo waliingia kwa njia ya biashara. Kampuni ya biashara ya Uingereza iitwayo 'East India Company' iliingia India kwa njia ya biashara wakati wa enzi ya mfalme wa Kiislamu Jahangir, katika mwaka 1613, na kisha polepole India ikafanywa Koloni la Kikristo kwa njia ya hii hii ya kampuni ya biashara. Baada ya kupata utawala katika India, Wakristo waliwaingiza wenyeji wenye hali ya chini katika Ukristo kwa hila mbalimbali.

## Hirizi na Upali

Padre amedai kuwa wamishonari walipokuja nchini wakafuta mila za zamani kama vile hirizi na upali. Hapo bila shaka padre anadokeza juu ya mambo ya baadhi ya Waislamu. Itambulikane ya kuwa hirizi hazina msingi katika dini ya Kiislamu. Kama Waislamu walianzisha jambo hili, ni kosa lao binafsi.

Naam, Upali, yaani kuoa wake wengi, ni desturi iliyokuwapo mapema katika baadhi ya makabila ya Kiafrika na pia desturi hii imeruhusiwa katika Kurani pamoja na masharti kadha wa kadha, bali na Biblia pia haikatazi kuoa wake wengi.

## Ukristo na Uislamu

Padre amesema kuwa Uislamu ulitoka mijini na kuingia vijijini; lakini Ukristo ulianzia vijijini na baadaye ukaingia mijini. Kwa kweli sababu yake ni kwamba mijini Uislamu ulikuwa na nguvu, hivyo Ukristo uliona afadhali uanzie vijijini.

## Utumwa

Hii ndiyo silaha kubwa katika fikara za Wakristo kwa kuharibu jina zuri la Uislamu; lakini sasa hivi wasomaji wataelewa uhakika wake hasa kwamba kwa kweli ni Ukristo ulioendesha Utumwa kidini na ili kujificha ukailaumu Islam.

Kwanza kabisa tuelewe kuwa Biblia inasemaje juu ya Utumwa. Je, inauharimisha, au hapana? Ebu someni kitabu cha Walawi (25:44):

> "Nao watumwa wako na wajakazi wako, utakao kuwa nao, wa mataifa waliowazunguka ninyi kwa hao mtanunua watumwa na wajakazi."

Tena katika Waefeso twasoma hivi:

> "Enyi watumwa, watiini walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili, kwa hofu na kutetemeka, kwa unyofu wa moyo, kana kwamba ni kumtii Yesu". (Waefeso 6:5)

Ndiyo kusema kwamba mtumwa kumtii bwana wake ni kama yeye kumtii Yesu! Je bado padre anadai kuwa utumwa ni haramu katika Ukristo? Badala ya kuleta fundisho la kuwapa watumwa uungwana, wanaambiwa hao wadhulumiwao kutetemeka mbele ya bwana zao na kuwatii kama vile kumtii Yesu. Na kwa kuwa Yesu ni mungu sawa na imani ya Wakristo wa siku hizi, hivyo mtumwa anaambiwa kumtii bwana kana kwamba yu Mungu!

## Kanisa la Katoliki Liliendesha Utumwa Afrika

Wasomaji watambue kinaganaga ya kuwa ni Wakatoliki hasa walioendesha biashara ya utumwa katika Afrika. Na leo kwa kujificha wameanza kutangaza kuwa Waarabu walifanya kitendo hicho. Tunasema kwamba kama baadhi ya Waarabu walifanya hivyo, basi walifanya kinyume cha fundisho la Kurani; lakini **Kanisa Katoliki** lenyewe **liliendesha utumwa.** Hebu someni aliyoyaandika mwenyewe padre mmoja wa Kijerumani katika kitabu chake kiitwacho "Christianity in Africa" kwenye ukurasa wa 125:

> "Hata kukamata watumwa na biashara ya watumwa vilifahamiwa kuwa ni vitendo vya

> ucha-Mungu vya Kikristo, kwa sababu vilionekana hivyo tu ndiyo njia iliyokuwako ya kuweza kuokoa roho za washenzi."

Tena kwenye ukurasa 126 anaandika hivi:

> "Hapa pia tunaona uhusiano mchafu wa Kanisa kuhusiana na utumwa; nyumba ya Majesu (Chama cha Makasisi wa Kikatoliki kilichoanzishwa na Ignatius Loyola katika mwaka 1533) katika Sao Paulo de Loanda (Angola) hawakuruhusiwa kuondoka ila baada ya kuwafikia Askofu wa Loanda na kuwabariki."

Kitabu kiitwacho "The New Congo" kinatoboa ya kuwa:

> "Kwa miaka 350 mfululizo mapadre hao wakaendesha kazi ya kukamata watumwa ili kuokoa roho zao; kwani walisadiki ya kwamba si vibaya kama miili yao iteseke **Utumwani** endapo roho zao zitaokoka huko mbinguni kwa Bwana Yesu."

## Papa Afundisha Utumwa

Ndani ya kitabu "Labour and Slavery in Christianity", tunasoma ya kuwa Papa Leo II aliwaandikia barua maaskofu wa Brazil kuwa Yesu hasemi neno lolote liwalo la kupinga utumwa, na kwamba amekubali

utumwa kama vile alivyokubali maneno mengine, na ya kwamba watumwa hawamtumainii Yesu msaada wowote."Encyclopaedia of Religions", jalada II, uk. 602, inapasua kwa kusema:

> "Katika mafunzo ya Mungu wetu hakupatikani kuchukia utumwa, na hakuna hata dalili moja ionyeshayo kuharimisha utumwa."

**Watumwa Walichukuliwa na 'Yesu'**

Ni jambo la kusikitisha mno ya kuwa Papa alitoa ruhusa ya kukamata watumwa, wamishonari walishika watumwa, na tena zile meli zilizochukua shehena za watumwa zilipewa majina **"Yesu"** na **"Maria"**. Kuzipa meli hizo majina hayo pia huhakikisha kuwa kazi ya kuwakamata watumwa ilihesabiwa takatifu sana.

Hii ndiyo hali ya Ukristo, lakini padre amejasiri kuilaumu Islam. Na mara kwa mara amesema katika kitabu chake ya kuwa kama Kurani haikukataza Utumwa, kwa nini Waarabu walikamata watumwa. Kama Waarabu walifanya biashara ya utumwa, waliiasi sheria ya Kurani, Tena hao Waarabu walikuwa ni wafanya biashara tu sio masheikh; lakini mapadre wazima walifanya tendo hilo bovu kwa kupata kibali cha Papa Leo II. Fundisho la Islam tunaandika hapa chini kwa kila apendaye kusikia.

Kurani Tukufu inafundisha wazi wazi ikisema:

> "Je, Hatukumpa (binadamu) macho mawili, na ulimi, na midomo miwili, na Tukamwongoza njia mbili zilizoinuka? Lakini hakupita njia ya mlimani. Na nini kitakujulisha njia ya mlimani ni nini? Ni kumpa mtumwa uungwana." (Al-Balad 90:9-14)

Padre anasema kama Kurani ilikataza utumwa kwa nini mara kwa mara ndani ya Kurani waaminio wanaambiwa kumwachia mtumwa huru kwa ajili ya baadhi ya makosa fulani. Jibu lake ni kuwa fundisho la Islam liliteremka polepole. Islam ilipokuja, desturi ya utumwa ilikuwapo mapema. Basi Islam ilipotaka kuuondoa utumwa, ilitumia hekima na kuuondoa polepole, hatua kwa hatua. Watumwa waliokuwapo wakati huo waliambiwa kuachwa kwanza kwa kufidia makosa fulani. Hii pia yahakikisha ya kuwa tangu mwanzo Islam iliuhesabu utumwa kuwa jambo baya.

Waislamu walipoona kuwa Mungu Anapenda watumwa kuachiwa huru, wakawapa wengi sana uhuru. Mtume[saw] pamoja na masahaba wakaanza kuwapa uhuru watumwa kwa kuwanunua kutoka kwa washirikina wa Makka. Kwa njia hii, jamii ikafunzwa ubaya wa utumwa. Na kisha ikija aya ndani ya Kurani iliyosema:

> "Haimpasi nabii kuwa na mateka mpaka apigane na kushinda katika nchi." (Al-Anfaal 8:68)

Desturi ya watu wakati huo ilikuwa ni kuwakamata tu watu na kuwafanya watumwa. Katika aya hii Mungu Anakataza kukamata wafungwa au watumwa ila tu vita vikipiganwa ndipo iko ruhusa ya kuwakamata wafungwa wa vita. Na desturi hii ya kukamata wafungwa wa vita ni halali, bali hata siku hizi pia hufuatwa. Lakini Kurani inafunza tena juu ya hao wafungwa wa vita ya kuwa:

> "Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru, wapigeni shingo mpaka mmeshinda, kisha wafungeni sana, tena **waacheni** kwa hisani au kwa kujikomboa." (Muhammad 47:5)

Angalieni jinsi Kurani inavyochukia utumwa. Hata wafungwa wa vita ambao walistahili kukamatwa, kwani walikuja kupigana na Waislamu na wakakamatwa katika uwanja wa vita, wanastahili kuachwa huru kwa njia ya hisani, au kwa kujikomboa. Vipi kukamata tu hivi watumwa!

Padre anasema ya kuwa kwa kuwa Kurani inaposema kwamba kama mtu anakosea katika kutimiza sheria fulani, ajikomboe kwa kumpa mtumwa uhuru wake. "Ndiyo kusema watumwa watakuwapo siku zote; la, sivyo, watatimizaje agizo la Kurani?", Padre auliza. Kweli juu ya baadhi ya makosa, Kurani, ikieleza fidia yake, inasema kuwa mtumwa apewe uhuru wake. Kama mtu hana, basi anaambiwa fidia nyingine pia:

> "Mwenyezi Mungu Hatawakamateni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini Atawakamateni kwa viapo mlivyoviapa kwa nia. Basi kafara yake ni kuwalisha maskini kumi kwa kadiri ile mnayowalisha watu wa majumbani mwenu au kuwavisha, au kumpa uungwana mtumwa. Lakini asiyeweza kupata, basi afunge saumu kwa siku tatu." (Al-Maaida 5:90)

Bwana padre atambue ya kuwa kama hakuna mtumwa, hata hivyo sheria itafuatwa tu, kwani zipo fidia nyingine pia.

Badala ya padre kuisifu sheria ya kumwachia mtumwa huru akaipinga. Kurani ilipoweka uhuru wa mtumwa kwa fidia ya kosa fulani, ilikuwa na makusudi ya kupunguza desturi hii. Na kisha baadaye ikaifuta kabisa hiyo desturi mbovu kama tulivyoisha eleza hapo juu. Padre anastahili kuilaumu Biblia isiyokataza utumwa, bali amlaumu Papa na Kanisa kwa ajili ya kukuza desturi ya utumwa duniani.

Basi wasomaji wasidanganyike wakisoma ndani ya kitabu chake mara kwa mara juu ya watumwa ya kwamba Waarabu walifanya biashara hiyo.

**Mbwamwitu**

Chini ya kichwa hicho cha maneno padre ameandika kwamba:

> "Wale walioendesha utumwa katika nchi yoyote,

> ndio watu wasiojali Mungu, wala dini, wala dhamiri, wala damu ya wenzao; ni watu wanaopenda faida yoyote, kwa njia yoyote; wako tayari kuharibu chochote na kuvunja sheria yoyote ili kujipatia faida."

Tunakubaliana na padre katika kauli hii, ila tunasema kuwa sasa amwamulie Papa Leo II na Kanisa zima la Katoliki pamoja na mapadre walioendesha utumwa kwamba kweli hawakujali Mungu wala dini, bali walitaka tu faida yoyote kwa njia yoyote, na papo hapo tunamwelekeza padre asome maneno yafuatayo:-

> "Wamishonari wa Kikristo hawakulalamika kamwe kuilaumu biashara hii ya utumwa ingawa (wasemavyo) ni kinyume cha fundisho la kanisa lao, maana biashara hiyo iliwapatia faida yoyote."

(H. G. Ravenstein, The Hakluyty Society, London)

Bila shaka imeisha julikana dhahiri ya kuwa nani alikuwa ni mbwamwitu katika ngozi ya kondoo.

## Utawala

Chini ya kichwa hicho cha maneno padre ameshindwa kuleta jambo lolote la maana. Ila sasa tunauliza kwa nini bado Wakristo wanang'ang'ania kushikamana na utawala katika nchi za Zimbabwe na Namibia? Je, Smith siye Mkristo na Vorster je? Mbona, padre hakusema lolote juu ya utawala haramu na dhalimu wa hao wakoloni wa Kikristo? Padre alisema kweli kabisa alipoandika kuwa

utumwa bado ungali unaendelea (uk. 72). Waafrika katika Zimbabwe na Namibia ndio watumwa wanaodhulumiwa na mabwana wao wa Kikristo, kina Smith na Vorster! Padre anapaswa kuwasihi hao kuliko kutaja-taja mambo ya zamani ya Waarabu akitia-tia chumvi nyingi.

## Sababu Nyingine

Padre amesema sababu nyingine ya watu kusilimu ilikuwa ni **upagazi**. Akieleza zaidi anasema kuwa Wanyamwezi na Wasukuma ndio waliowasindikiza Waarabu katika misafara yao, wengine wakiwa viongozi na wengine wanyapara au wasimamizi, na wengine wapagazi; waliporudi kwao kumaliza siku zao, wengi walikuwa wamekwisha kushika dini. (uk. 74)

Hapa padre amekubali ya kuwa hao Wanyamwezi na Wasukuma hawakushurutishwa na Waarabu; bali tu walisafiri pamoja nao kwa siku kadha na wakashika dini. Tunaona hii inathibitisha ubora wa dini ya Kiislamu ya kwamba hao ndugu walipotembea na Waislamu wakaanza kupenda dini yao bila kuhubiriwa au kushurutishwa. Waliona kwa macho yao vitendo vya hao Waislamu ndipo wakavutika na wakasilimu.

Kisha padre ametaja ujamaa mara nyingine. Habari hii tumeisha eleza hapo kabla.

*Lugha ya Kiswahili:* Padre anasema kuwa mwanzoni lugha ya Kiswahili ilikuwa ni lugha ya Waislamu tu

pekee. Lakini hakuweza kuhakikisha kuwa jambo hili liliwezaje kueneza Islam. Ila tu amejaribu kuwatenganisha wananchi juu ya suala la lugha. Katika nchi fulani mchafuko ulitokea kati ya wananchi juu ya suala la lugha. Na sasa padre amejaribu kukoroga nchini humu suala hili.

Kwa hakika Kiswahili ni lugha nzuri sana iliyoweza kuwaunganisha wananchi wote wa Tanzania, bara hadi visiwani. Katika Afrika Mashariki, Tanzania imebarikiwa na kupata lugha moja ya Taifa zima, Na kwa msaada wa Mungu, sasa ziko alama za kuhakikisha ya kuwa lugha hii itaweza kuunganisha Waafrika wote pamoja. Na ni jambo la kufurahisha na kutuliza ya kuwa wazo la kukifanya Kiswahili kiwe ni lugha ya bara zima la Afrika limetolewa na Nigeria, nchi ya Afrika Magharibi. Lakini padre anataka kukifuta hata katika Afrika Mashariki kwa kuleta suala la dini katikati.

## Uislamu Chini ya Ukoloni wa Kikristo

Padre ametia kichwa cha maneno "Uislamu chini ya Ukoloni wa Kizungu"; lakini ingekuwa kweli zaidi kama angetumia neno 'Ukoloni wa Kikristo' kuliko 'Ukoloni wa Kizungu.'

Padreameficha ukweli aliposema kuwa katika ukoloni, dini haikuendeshwa na serikali. Ukweli ni kwamba kisirisiri dini iliendeshwa na serikali. Au tuseme ya kwamba Kanisa lilikuwa ni idara tu ya serikali. Katika

siku za ukoloni, mapadre waliweza kusafiri katika gari la moshi kwa kutoa nusu ya nauli. Ingawaje dini haikuwekwa rasmi chini ya serikali, lakini kwa hakika ni serikali iliyowasaidia mapadre hata kwa mali. Serikali za nje zilikuwa zikileta msaada wa aina hiyo. Juu ya utawala na kanisa tutaandika mbele.

## Masomo Yana Faida

Padre amesema kuwa Waingereza (Wakoloni wa Kikristo)

hawakuipendelea sana Tanganyika; wakawaachia waliotaka kuanzisha shule na hospitali zao – wenyewe wakawa walinda amani tu.

Kumbe hii ilikuwa ni hila ya serikali ya Ukoloni wa Kikristo kwa kuwarudisha nyuma Waislamu. Kwani walijua kuwa Waislamu hawana shule, bali Wakristo wanazo zao au wanayo mipango ya kuzianzisha pamoja na kufungua hospitali; hivyo bora serikali isishughulikie hizo ili Waislamu wapate hasara. Na ndivyo ilivyotokea. Waislamu waliotaka watoto wao waelimishwe katika shule za Kanisa, wakawakuta watoto wao wamekwisha pewa majina ya Kikristo tayari wakati wa kuwapokea shuleni.

Hali ya hospitali za misheni tumeeleza katika kitabu hiki mahali pengine.

## Hila ya Padre

Padre ameuliza swali analoona ni 'gumu' kujibiwa, nalo ni kwamba je ni haki ya wazazi kulinda imani ya watoto wao na kuwapatia nafasi ya kuiimarisha; na hasa si haki tu, bali ni wajibu pia?

Swali lenyewe si gumu hata kidogo, na jibu lake ni kuwa kama ni halali kwa wazazi, bali ni wajibu wao, kulinda manufaa ya kidunia ya watoto wao, bila shaka ni wajibu wao pia kulinda manufaa yao ya kiroho. Hakuna mzazi anayependa kumwona mtoto wake katika maafa ya kiwiliwili, kwa nini avumilie kumwona katika maafa ya roho? Je padre anapenda kuwaona watoto wa Kikristo kuelimishwa kipagani? Kama hapana, basi swali lake limejibiwa tayari. Robert M. Glen, mwandishi wa 'Historia ya Ukristo' ameandika akieleza mateso kwa Wakristo katika Urusi ya kwamba:

> "Bado (Wakristo) wanasumbuliwa kila siku kwa kunyimwa haki zao za kumwabudu na kumshuhudia Mungu. Sheria mpya, kama sheria ya ndoa ya mwaka 1968, zimewaondolea wazazi haki ya kuwalea watoto wao kufuata imani yao wenyewe. Lazima wawalee watoto wao kwa kufuata malezi ya mjenzi wa Ukomunisti. Kama wakijitahidi kutumia malezi ya wazazi ya Kikristo yaliyohesabiwa na serikali kama 'mvuto

> wenye madhara' juu ya watoto, serikali itawaondosha watoto kwa wazazi wao. Bado siku za ukiwa zimetanda mbele ya Wakristo wa Urusi." (j. III, uk. 157)

Islam inafundisha kuwalea watoto Kiislamu maadamu ni watoto; wakiisha balehe wanaweza kujichagulia dini yoyote waipendayo. Hakuna kushurutisha katika dini sawa na mafunzo ya Islam; kuhubiriana na kuelekezana kuna ruhusa.

Padre ametumia udanganyifu aliposema kuwa shule zinakuza akili ili kila mmoja aweze kupatiwa nafasi ya kuchagua dini kwa akili timamu. Kauli hii inaweza kuwa sawa kama shule hazifundishi dini yoyote iwayo bali masomo ya kawaida tu yanasomeshwa bila kumwelekeza mwanafunzi kwenye dini yoyote. Hapo bila shaka kila mtoto baada ya kuwa mkubwa anaweza kujichagulia mwenyewe dini yoyote aitakayo. Lakini hali ya shule za Kikristo haikuwa hivyo; bali watoto walilazimika kupata mafunzo ya Kikristo, hata walilazimika kufanya ibada ya Kikristo bila kujali mtoto anapenda hivyo ama hapana. Kwa hiyo, shule za Kanisa hazikukuza akili ya mtoto kwa usawa, bali zikamlea katika mazingira ya Kikristo.

Kwa hivyo Waislamu waliopenda watoto wao wasipotee wakawazuia watoto wao wasiingie shuleni mwa misheni.

Kwa njia hii bila shaka wakabaki nyuma katika elimu ya kidunia, lakini wakaweza kwa vyovyote kuwaokoa watoto wao katika balaa kubwa la kuabudu binadamu mfile.

Kwa kweli, ilikuwa ni kazi ya serikali kufungua shule kwa ajili ya watu wote. Lakini haikufanywa hivyo ili kulisaidia Kanisa liweze kueneza Ukristo kwa njia ya shule.

Hapa panafaa tutoboe siri hii pia ya kwamba katika zama za enzi ya Wajerumani, ilipoamuliwa waalimu wa Kiislamu waajiriwe katika shule kwa kuwafunza watoto, hapo Kanisa likapeleka barua ya malalamiko huko Ujerumani kwa nini Mwislamu amepelekwa katika shule. Kanisa liliisihi serikali ya Kijerumani kujisahihisha na kutokurudia tendo kama hilo. Tunayo picha ya barua hii iliyoandikwa kwa lugha ya Kijerumani. Je padre bado anadai kuwa hana mawazo ya kiubaguzi hata katika shule.

## Katika Taifa la Kisasa

Padre amepotoka aliposema kuwa Waislamu wanaona ni vigumu kuwa raia kamili katika Taifa linalojengwa kwa mtindo wa kisasa. Hakika yenyewe ni kuwa Waislamu ni raia kamili wala sio nusu-nusu. Anasema padre kwamba Waislamu hawawezi kuacha desturi za kale. Padre mpaka kufa atatamani Waislamu waiache dini yao lakini hawataacha. Je Mkristo anaweza kuambiwa na padre kuacha desturi za Kikristo hata zikiwa mbovu namna gani kama vile kumwabudu

binadamu aliyeisha kufa tangu miaka kama 2,000 hivi? Kama hapana, kwa nini padre anamtaka Mwislamu aiache sheria yake nzuri imfaayo binadamu siku zote?

## Taifa Liandamane na Dini

Kama nia ya padre ilikuwa kuichochea serikali eti Waislamu hawawezi kuridhika na utawala wa kisasa, bali wanakumbuka siku za Harun-ar-Rashid (uk 77), aelewe ya kuwa Waislamu sawa na imani yao katika Kurani wamekubali serikali ya sasa nao ni watiifu. Serikali hii ni ya watu wote: Waislamu, Wakristo na wengineo pamoja. Na madaraka katika serikali pia hayatengwi kwa ajili ya mtu wa dini fulani. Na hii inajuzu sawa na dini yetu. Kwa hiyo, padre hataweza kufaulu katika nia yake hiyo. Anaweza kuona kwa macho kwamba Waislamu wamejitolea mhanga kujenga taifa pamoja na wananchi wengine bila kasoro yoyote.

Kila mmoja anapenda kwamba wengine wote waingie katika dini yake. Wakristo wanapenda watu wote waingie katika dini yao na Waislamu hali kadhalika wanapenda kuwa dunia nzima isilimu. Lakini siyo maana yake ya kuwa Mwislamu anataka kuwa serikali ichukue dini ya Kiislamu kuwa dini ya serikali. Serikali ya hapa petu si ya dini; wala haiipendelei dini yoyote. Na kwa kuwa nchini humu watu wa dini mbalimbali

wanaishi, kwa hiyo siasa hii ya serikali ya kutokuwa na dini fulani maalum ndiyo bora sana.

Ni sawa ya kuwa Mwislamu anaamini ya kwamba Islam tu ndiyo dini inayokubaliwa na Mungu. Na pia Waislamu wanapenda watu wote waifuate dini hiyo, lakini si kwa nguvu, bali baada ya kuielewa vizuri watakapoikubali. Na je padre hapendi ya kwamba Ukristo ufuatwe na watu wote?

## Dini Iandamane na Maisha

Padre anasema kuwa Mwislamu anataka mila na desturi za Kiislamu ziwe desturi za ujamaa kwa wote. Hatusemi hivyo. Tunapenda watu waelewe ukweli wa dini ya Kiislamu ndipo wafuate desturi zake. Hatusemi walazimishwe kuzifuata.

Juu ya kufunga, padre anasema Waislamu wanapenda watu wote wafunge, kwani wengi wanapata vishawishi wakiwaona walao. Padre amepotea vibaya sana. Waislamu hawashawishiki wakiwaona wengine wakila. Bali wanapenda sana kufunga saumu. Hata watoto wadogo ambao hawapaswi kufunga sawa na sheria ya Islam, nao wanapenda kufunga.

Naam, padre amesema kweli alipoandika kuwa Islam haimruhusu binti wa Kiislamu kuolewa na Mkristo. Je na padre anapenda mabinti wa Kikristo waolewe na Wapagani?

## Maisha ya Mwislamu

### Mtoto Azaliwapo

Mambo aliyoyaeleza padre kuhusu mtoto kuzaliwa siyo yote ya Kiislamu. Mathalan, mtoto wa aina fulani kuwekwa msikitini hadi kucha siyo desturi ya Kiislamu hata kidogo. Utasa hauhesabiwi kuwa laana katika Islam, bali ni kasoro tu ndani ya mwanamke; laana maana yake ni kufukuzwa mbali na Mungu. Mwanamke tasa hana ila yoyote kiroho, akitenda mema atakubaliwa na Mungu kama mtu yeyote mwingine.

Siyo desturi ya Kiislamu kwamba mtoto aonyeshwe jua siku ya saba, au kumvika Yasin. Vilevile siyo sheria ya Kiislamu mtoto kueuliwa siku ya arobaini baada ya kuzaliwa; bali mtoto azaliwapo, pale pale anaogeshwa ili kumsafisha. Basi tu. Naam, mwanamke wa Kiislamu baada ya kuzaa anaoga siku damu ile ya uzazi inapokwisha kutoka. Na hii ni muhimu kwa ajili ya usafi wa mwili. Na mengine kama 'kuvunja mtoto' ni uzushi; hakuna msingi wake katika Islam.

Kutoka nje kabla ya siku ya 14 baada ya kuzaa si mwiko katika Islam. Wala siyo desturi ya Kiislamu mwalimu kufika kila siku na kumsomea Yaa-Siin. Hakuna mambo kama jina la kuzaliwa au jina la kupanga au jina la msibu katika sheria ya Kiislamu. Kuna jina tu analopewa mtoto azaliwapo — hasa baada ya siku 7 anapotahiriwa.

Mwalimu kumsomea 'akika' mtoto afaye akiwa bado mchanga pia ni bidaa, wala siyo sheria ya Kiislamu.

**Jando**

Chini ya kichwa hicho, padre ameandika yote yasiyokuwa ya Kiislamu, bali ni mila za baadhi ya makabila ya Kibantu. Habari hiyo haimo katika Islam asilani. Mtoto anatahiriwa baada ya siku 7, kama alivyosema padre mwenyewe; basi kuna jando gani tena iliyobaki. Je, kila Mwislamu anatahiriwa mara mbili: baada ya kuzaliwa na tena anapobalehe? Kufichua mwali na mengine yote ni mambo ya kikabila tu. Msichana hatahiriwi katika Islam.

**Chuo**

Ni kweli ya kuwa Waislamu waliwafundisha watoto wao katika vyuo ili wajifunze Kurani Tukufu. Padre anaposema kuwa mwalimu analipwa 'ada' na mengineyo, hayo yote kwa kweli ni njia ya kumpa malipo kidogo kwani mara nyingi mwalimu hana kazi nyingine. Katika Jumuiya ya Ahmadiyya watoto wanafunzwa bila kutolewa ada ya aina yoyote.

**Ndoa**

Mambo kama 'utashi' na 'kuchagua siku njema', 'kifungua mlango', 'kipakasa' na 'kufichua', hayo yote siyo desturi ya Kiislamu, bali ni mila tu za watu.

Hakuna chakula cha 'fungate' alichoeleza padre, bali kuna karamu ya walima inayoandaliwa na Bwana arusi

kwa ajili ya furaha ya ndoa. Ndoa ya muda haikubaliwi na Waislamu wote, bali ni Washia tu wanaoikubali. Ndoa ya siri ni uzushi wa padre; hiyo hakuna katika Islam. Mtume[saw] alisema: 'Itangazeni ndoa'; kwa hiyo lazima ndoa itangazwe.

## Talaka

Islam inamruhusu mume na mke kuachana kama sababu za kweli za kutosha zimepatikana na imekuwa vigumu mke na mume kuendelea vema katika maisha.

Padre hakusema sawa alipoandika kwamba mke aliyepewa talaka anakaa eda kwa miezi minne sawa na eda ya yule aliyefiwa na mume. Kwa kweli eda hizo ni tofauti. Eda ya aliyefiwa na mumewe ni miezi minne na siku 10; bali eda ya aliyepewa talaka ni miezi mitatu.

Padre amesema kuwa aliyetalikiwa hawezi kuolewa na yule aliyemwacha, mpaka aanze kuolewa na mtu mwingine na kisha aachike. Kwa kweli, talaka ziko za aina mbalimbali. Ni talaka ya aina ya *'mughalladha'* (nzito) tu iliyo na sharti aliyoeleza padre. Talaka za aina nyingine hazimzuii mke huyo kuolewa na mumewe yule upya.

Hata Biblia inaruhusu kutoa talaka sharti mke amezini. (Mt. 5:32). Sharti hii ni ya hatari kwani mume akishindwa kuishi na mke mwenye tabia chafu, atalazimika kumsingizia ili aweze kumwacha.

## Nguzo za Dini

Kuhusu saa za sala padre atambue ya kuwa sala ya adhuhuri haisaliwi saa 6 za mchana, kwani jua huwa kichwani saa hiyo ambapo sala imekatazwa. Sala hiyo husaliwa jua linapopinduka baada ya saa 6 za mchana.

## Ramadhani

Padre amesema kufunga Ramadhani ni lazima. Itambulikane kuwa kuna masharti ya saumu, na wapo watu wa aina fulani ambao wanaambiwa wasifunge. Ni Mwislamu mkazi mwenye afya anayelazimika kufunga. Aliye safarini atafunga baada ya kumaliza safari yake. Mgonjwa atafunga baada ya kupona.

## Zaka

Padre amechanganya sadaka ambazo hutolewa kutokana na ukarimu wa mtu, na zaka ambayo ni kitu cha lazima kwa kila aliye na mali sawa na kiwango kilichowekwa na Islam.

## Sikukuu

Sikukuu zilizowekwa katika Islam ni mbili tu, Idul Fitri na Idul Haji. Zingine zimebuniwa na watu.

## Kuaga Dunia

Padre ameandika mengi yaliyo bidaa kuhusu habari hii. Kwa kweli mtu anapofariki, sheria ya Islam inafundisha huyo aoshwe (na mtu yeyote) kisha avishwe sanda na

asaliwe sala ya jeneza ndipo azikwe. Matanga na kumimina maji na mengineyo yote aliyoandika padre hayamo katika sheria ya Islam ijapokuwa baadhi ya Waislamu wa nchi hii wamezoea kufanya hivyo kinyume cha sheria za Kiislamu.

## Umoja Uliovunjika

Padre ameeleza kwamba Waislamu siku hizi wamegawanyika katika makundi mbalimbali na ametaja madhehebu ya Waislamu. Ni sawa. Tumeisha eleza hapo nyuma ya kuwa hata Wakristo wameisha farakana tayari katika makundi mengi sana.

## Ahmadiyya

Padre amesema kuwa "Farakano kubwa linalotuhusu hapa ni Ahmadiyya, kwa sababu wako humu Afrika mashariki". Hapa tunauliza, je Wasunni, Washia na wafuasi wa madhehebu mengine ya Kiislamu hawamo humu Afrika Mashariki? Kwa nini Ahmadiyya tu inawahusu Wakristo?

Padre ameandika kuwa Sayidna Ahmad[as] alizaliwa mwaka 1839. Kwa kweli tarehe ya kuzaliwa kwake ni 13.2.1835.

*Mtume wa Mwisho:* Waahmadiyya wanasema kuwa baada ya Mtume Muhammad[saw] hakuna mtume atakayeleta dini mpya au kitabu kipya badala ya Kurani. Manabii

watakaotumikia Islam wataendelea kutokea sawa na matakwa ya Mungu.

## Jihad

Hatusemi kwamba badala ya jihadi afadhali mahubiri ili kueneza dini. Bali tunasema ya kuwa kwa ajili ya kueneza dini mahubiri ndiyo jihadi. Hatukatai jihadi katika maana ya vita, ila tunasema kuwa vita haviwi kwa ajili ya kueneza dini. Naam, maadui wakitangulia kupigana, hapo Mwislamu analazimika kupigana kama masharti kadha wa kadha yapatikane.

*Maelezo Halisi ya Kurani:* Hatusemi kwamba maelezo halisi ya Kurani hayawezi kupatikana katika vitabu vya wataalamu wa Kiislamu. Bali tunasema kuwa mahala kadha wa kadha baadhi ya wataalamu hawakuweza kutoa maelezo barabara.

## Ahmadiyya na Wakristo

Padre anasema kuwa vitabu vya Ahmadiyya vinamchukiza Mkristo kwa sababu zifuatazo:

(I) Tafsiri ya Kurani iliyotolewa na Ahmadiyya inaonyesha 'kwa uteuzi maneno yote yanayoonyesha tofauti kati ya Ukristo na Uislamu'. Je ni jambo baya kudhihirisha tofauti baina ya Ukristo na Uislamu? Hata padre amejaribu kuonyesha tofauti kati ya dini hizo mbili katika kitabu chake tunachochambua

wakati huu. Anasema padre kuwa Waahmadiyya wanatumia utaalamu wa juujuu tu bila kuangalia asili ya mambo. Je padre anaona huo utaalamu wa juujuu katika majibu yetu haya? Au ni kukagua mpaka kiini cha mambo yalivyo?

Padre amesema kuwa Waahmadiyya wanajaribu kuonyesha Biblia nzima ikimtabiri Muhammad[saw]. Siyo kujaribu tu bali tumefafanua hasa katika vitabu vyetu pamoja na kitabu kiitwacho ***"Mtume Muhammad[saw] katika Biblia"***. Si neno moja moja tulichukua, bali tumeeleza kwa urefu bishara za Biblia juu ya ujaji wa Muhammad[saw].

Padre anadai Waahmadiyya kuwa tofauti na Wasuni wanaposema kuwa Yesu hakufa msalabani. Padre atambue kuwa hata Wasuni wanasema Yesu hakufa msalabani. Ila tu wanasema kuwa Yesu alichukuliwa mbinguni lakini tunasema alitundikwa msalabani ambako alizimia na akafikiriwa kuwa mfu; na kisha baada ya kutibiwa na wafuasi wake akazinduka na kuhamia Kashmir.

## Yuz Asaf

Padre amevuruga ukweli aliposema kuwa lile kaburi linalodaiwa na Waahmadiyya huko Kashmir kuwa kaburi la Yesu ni la nabii fulani aitwaye Yusuf Asaz. Sivyo hata kidogo. Bali kaburi hili ni la nabii aitwaye 'Yuz Asaf' ambalo ni 'Yesu' tu katika lugha nyingine. Someni kitabu chetu "Jesus in India" mkaelewe uhakika wa jambo.



Kaburi la Yesu nchini Kashmir

## SEHEMU YA TATU

Chini ya 'Imani ya wana wa Ibrahimu', padre amesema jambo lisilo na msingi hata kidogo. Amesema kwamba Waislamu wanamheshimu Maria Bikira, hata wakaweza kumwomba kwa ibada (uk. 88).

Huu ni uwongo mbaya sana kusema kuwa Waislamu wakaweza kumwomba Maria. Waislamu hawamwombi hata Mtume Muhammad[saw], bali wanamwomba Mungu tu Mmoja. Hatujui kwa nini padre anataka kumpa Maria heshima ya bandia ya kwamba hata Waislamu wakaweza kumwomba bibi huyo.

### Somo 1. Nani Aliye Mwana wa Ibrahim

Tazameni kurasa 1-7

### Somo 2. Vitabu Mbalimbali Tatizo

Padre anasema kwamba Kurani ilidai kuwa inasadikisha yaliyo mbele yake (Yuunus 10:38); lakini tunaona tofauti kubwa katika Kurani na Biblia. (uk. 89).

Pole, bwana padre, ukichunguza Kurani utaelewa kuwa wafuasi wa Biblia wamelaumiwa humo kwa ajili ya kugeuza maneno ya Biblia (An-Nisaa 4:47). Na kweli ziko sehemu nyingi sana ndani ya Agano la Kale na pia Agano Jipya zinazohakikisha ukweli wa kauli ya Kurani.

Na pia Kurani inasema kwamba Biblia ilikuja kwa ajili ya wana wa Israeli tu, kwa hiyo sheria ya Biblia

iliwahusu hao pekee. Kurani ilileta sheria ya kudumu kwa wanadamu wote, kwa hiyo sheria zote zilizokuwamo ndani ya Biblia zilizokuwa zinafaa kwa wote zimekusanywa humo.

Itambulikane kuwa Kurani inaposema kuwa inasadikisha yaliyo mbele yake, maana yake ni kusadikisha zile bishara za ujaji wa Muhammad[saw], yaani bishara hizo zimetimia kwa njia ya Kurani Tukufu.

## Mungu ni Baba

Padre amesema kwamba kwa Waislamu Mungu si baba. Hapo padre amepungukiwa elimu. Kurani Tukufu inasema:

> "Na mwishapo kuzitimiliza ibada zenu (za haji), basi Mkumbukeni Mwenyezi Mungu kama mnavyowakumbuka baba zenu au kumbukeni zaidi." (Al-Baqara 2:201)

Hapa panaeleza kuwa tumkumbuke Mungu kama baba yetu. Lakini pale pale imesemwa 'au kumbukeni zaidi.' Hii yaonyesha kuwa ijapokuwa neno baba linaeleza mapenzi na huruma, lakini Mungu ni zaidi kuliko baba. Hii ndiyo sababu ingawaje mithali ya baba kwa Mungu ipo katika Kurani, lakini Islam haitii mkazo juu ya Mungu kama baba, bali Mola, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Kimfano Mungu Anaweza kuitwa baba, lakini mfano huu una kasoro zote zile zilizo katika baba; lakini Mungu Hana kasoro. Tena kwa kuwa imani juu ya ubaba wa Mungu imewapoteza watu wengi sana wasiouelewa mfano huu na wakamchukua Yesu kuwa mtoto wa Mungu, kwa hiyo Islam haitaki kumfananisha sana Mungu na baba. Kwa ajili ya hatari hiyo na pia kwa sababu ya kasoro ya ubaba, Waislamu hawakupenda kumwita Mungu kuwa baba. Kwani matokeo mabaya sana ya matumizi ya neno hili yako mbele ya macho yao!

**Usafi wa Moyo**

Padre amejasiri alipodai kuwa Islam haifundishi usafi wa moyo, upole na unyenyekevu. Katika Islam matendo huhesabiwa sawa na usafi wa moyo wa mtu. Mtume Muhammad[saw] alisema ya kuwa:

> "Mungu Haangalii sura zenu na mali zenu; bali Huangalia mioyo yenu na vitendo vyenu". (Muslim)

Kurani Tukufu inasema:

> "Hayo ni safi kabisa kwa mioyo yenu na mioyo yao" (Al-Ahzaab 33:54).

> "Na anayeziheshimu alama za Mungu, basi hilo ni katika utawa wa moyo." (Al-Hajj 22:33)

> "Hao ndio Ameiandika imani mioyoni mwao na

Akawasaidia kwa roho itokayo kwake." (Al-Mujaadila 58:23)

"Siku ambayo haitafaa mali wala watoto isipokuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo safi." (Ash-Shu'araa 26: 90)

Kuhusu upole padre ajue ya kuwa:

"Mungu Aliyeleta Kurani ni Mpole." (Aali 'Imraan 3: 31); "Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu." (Al-Faatiha 1: 1)

Na Mtume Muhammad[saw] pia ni mpole na mrehemevu (At-Tauba 9:128). Juu ya unyenyekevu Kurani inatuambia:

"Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu." (Al-Furqaan 25:64)

"Je, wakati haujafika kwa wale walioamini ya kwamba mioyo yao inyenyekee kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kwa mambo ya haki yaliyoteremka? Wala wasiwe kama wale waliopewa Kitabu zamani na muda wao ukawa mrefu, kwa hivi mioyo yao ikawa migumu, na wengi wao ni waasi." (Al-Hadiid 57:17)

Hii aya inawasihi Waaminio kuwa wanyenyekevu, na pia

inaeleza jinsi ambavyo mioyo ya wafuasi wa Biblia ikawa migumu kwa kupita muda mrefu.

*Upendo:* Mtume[saw] alisema kuwa mwaminio ni yule anayependa kwa nduguye yale anayopenda kwa nafsi yake.

Kurani inaeleza kwamba:

> "Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri lazima Rahmani Atawafanyia **upendo.**" (Maryam 19:97)

Mungu ni mwenye kusamehe sana na mwenye upendo sana (Al-Buruuj 85:15). Na juu ya waaminio kumpenda Mungu tumeambiwa katika Kurani:

> "Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana." (Al-Baqara 2:166)

**Matayarisho**

Kurani siyo matayarisho kwa kupokea Agano Jipya; bali maagano yote ya hapo kabla ni maagano ya kale; Kurani Tukufu ndiyo Agano Jipya kabisa. Na sasa hiyo ndiyo inayotakiwa kufuatwa:

> "Na atakayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu, basi haitakubaliwa kwake, naye katika akhera atakuwa miongoni mwa wenye hasara." (Aali 'Imraan 3:36)

## Somo 3. Waislamu na Wakristo Wanategemea Mitume Mbalimbali

Kuhusu Unabii, padre amepotea alipoeleza imani ya Waislamu. Padre atambue ya kwamba Waislamu tunasema ya kwamba Mwenyezi Mungu Hakuvunja mpango Wake maalum Alipoleta manabii mbalimbali duniani. Mpango wa Mungu ulikuwa ni kuwaongoza wanadamu katika njia iliyonyoka ili waweze kuungana na Mungu. Na ili kutekeleza mpango Wake huo, Yeye Akatuma manabii mbalimbali katika zama mbalimbali.

Kwa kuwa katika zama zilizopita njia za kusafiri hazikuwa nyingi au za haraka zaidi, hivyo mataifa mbalimbali hayakuweza kuungana pamoja, na kwa hiyo Mungu Akatuma manabii katika mataifa mbalimbali. Na Mungu Alikuwa Amekadiria ya kuwa katika zama za mwisho njia za kusafiri zitabuniwa na kwa hiyo mataifa mbalimbali ya dunia nzima yatakuwa ni kitu kimoja, hivyo itakuwa bora kuleta nabii mmoja kwa ajili ya watu wote wa dunia nzima. Na huyo nabii ndiye Muhammad[saw].

Pia Mungu Aliwatayarisha watu wote wa duniani kote kwa kumpokea huyo Nabii mteule Muhammad[saw] kwa njia ya kuleta manabii kadha wa kadha. Dini mbalimbali zilikuwa ni kama darasa mbalimbali za chuoni, ambapo Islam ni darasa la mwisho la chuo hiki. Hii ndiyo

sababu Mungu Akaleta mafunzo kidogo kwanza kisha Akaongeza na Akaendelea kufanya hivyo hadi Alipomleta Muhammad[saw]. Akaleta sheria kuu ambayo haikuacha jambo lolote liwalo la maana lililokuwa la lazima au la muhimu kwa ajili ya maendeleo ya roho ya binadamu.

Basi kwa jumla Mungu Hakubadili mpango wake Alipoleta manabii mbalimbali au Alipoleta Muhammad[saw] baada ya Yesu, bali Ametimiza ule mpango mkuu Aliokuwa Ameiwekea hii dunia.

Hivyo, kwa kweli kila nabii alikuwa ameingia katika mpango wa Mungu, Yesu akiwa mmojawapo. Hii ndiyo sababu Waislamu wanawaamini manabii wote na ni jambo la lazima kwa Waislamu kuwaamini wote hao. Ijapokuwa hao manabii wa zamani walifanana tu na waalimu wa shule ya msingi, wa daraja mbalimbali, au waalimu wa shule ya sekondari, lakini Muhammad[saw] ni Mwalimu Mkuu aliyekuja kuwapatia wanadamu digrii ya mwisho katika mambo ya dini na roho.

Basi, wakati mwingine Mungu Aliporudia sheria fulani ya zamani, Alikuwa na maana ya kuwa hiyo sheria iwe msingi na kisha amri kubwa zaidi pia zikafundishwa. Kana kwamba A.B.C.D zilizofundishwa na waalimu wa shule za msingi ziko sawa bali ziko pale pale na sasa masomo ya juu zaidi yanaanza.

Kwa vyovyote, Waislamu hawasemi kuwa kila mara Mungu Alipoleta nabii mpya Akabadili mpango wake. Na pia ijulikane ya kuwa kila nabii alitimiza matakwa ya mpango huo, kwani mpango huo ulitaka wanadamu wapate maendeleo hatua kwa hatua. Hivyo kila nabii (pamoja na Yesu) alitimiza shabaha ya Mungu.

Itambulikane hapa kwamba tumeandika nyuma pia ya kuwa Muhammad[saw] alitumwa kwa ajili ya wanadamu wote sio kwa ajili ya Waarabu pekee, lakini padre kila mara anakariri habari hiyo hiyo. Lakini wakati mwingine anataja pia imani ya Waislamu kuwa Muhammad[saw] alikuwa kwa ajili ya watu wote.

*Mateso:* Kusema kwamba Yesu alipata mateso, ni sawa; lakini kwa kweli kila nabii amepata mateso. Muhammad[saw] aliteswa ajabu pamoja na masahaba zake, ambapo wanafunzi wa Yesu walisalimika kwa kumkimbia au kumlaani au kumsaliti. Nabii Yahya (Yohana Mbatizaji) aliuawa ndani ya jela sawa na Biblia na kichwa chake kililetwa mbele ya mfalme kikiwekwa ndani ya sinia. Kweli Yohana mbatizaji aliteseka sana. Mateso ya kila nabii yalikuwa ya aina mbalimbali. Basi siye Yesu pekee aliyeteseka katika njia ya Mungu bali manabii wote, bali hata wengine wacha-Mungu wasiokuwa manabii nao waliteseka.

Vilevile padre aelewe kwamba siye Yesu tu aliyekuwa

ametabiriwa ndani ya Maandiko ya kale, bali manabii mbalimbali walitabiriwa. Hata Yohana mbatizaji alitabiriwa kuja. Mtume Muhammad[saw] kwa kuwa ni Nabii Mkuu, hivyo ametabiriwa zaidi sana katika Biblia na Vitabu vingine vya dini mbalimbali. Yule Msaidizi au Mfariji anayetajwa na Biblia ndiye Muhammad[saw].

## Mpendwa Wangu

Kweli Yesu ni mpendwa wa Mungu, lakini siye Yesu tu pekee, bali Manabii wote huwa wapendwa wa Mungu. Mtume Muhammad[saw] ni Mpenzi Mkuu wa Mungu hata kwamba anayetaka kupata mapenzi ya Mungu analazimika kumtii Muhammad[saw]. (Aali 'Imraan 3: 32)

Padre atambue ya kuwa Yesu akawa mpendwa wa Mungu kwa ajili ya kubatizwa na Yohana Mbatizaji. Baraka hii aliipata kutokana na ubatizo wa Yohana:

> "Akabatizwa na Yohana katika Yordani. Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka na Roho, kama hua, akishuka juu yake; na sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe." (Marko 1: 9-11)

Basi padre asione fahari, bali amshukuru Yohana mbatizaji ambaye ubatizo wake ukamfanya Yesu kuwa mpendwa wa Mungu. Lakini Muhammad[saw] akawa mpendwa wa Mungu bila kubatizwa na mtu yeyote; bali

Mungu Akamchagua kwa ajili ya wema wake ulio moyoni mwake. *Alhamdulillah.*

**Sallallahu 'Alaihi Wasallam**

Padre amewasifu Waislamu kwa kumwombea Muhammad[saw] kwa hayo maneno kila wamtajapo. Ahsante. Lakini bwana padre utambue ya kuwa tunapomwombea Mtume wetu kwa kusema 'Mungu Ambariki na kumpa amani', tunamaanisha kwamba daima Mungu Ailinde dini yake na kuibariki. Waila Mtume[saw] ameisha fariki, naye yuko kwa Mungu Mpenzi wake, wala hayuko katika hatari ya aina yoyote. Yeye ameungana na Mola wake kwa kudumu. Bali hatari iko kwa dini yake kutokana na mashambulio ya wale wajinga wasioielewa sheria aliyoleta na uhakika wake. Basi, Mungu mwenyewe Aliwafunza Waislamu kumsalia Mtume ili Waislamu wajue ya kuwa kila mara dini ya Kiislamu itakapokuwa katika hatari ya kushambuliwa, Mungu Ataleta msaada wake kwa kuilinda dini yake. Na ndivyo Alivyofanya Mungu daima. Katika zama hizi Mungu Ametimiza mara nyingine ule muradi wa kusema: "sallalahu 'alaihi wa sallama", kwa njia ya kuleta Seyidna Ahmad[as] ambaye aliunda jumuiya yake kwa idhini ya Mungu ili kumlinda Muhammad[saw] heshima yake na heshima ya dini yake. Majibu yetu haya ya kitabu cha padre ni alama tu moja ya kuhakikisha faida

ya kumsalia Mtume[saw].

### Padre Anajipinga

Padre amesema kwenye ukurasa 95, "Haifai sisi Wakristo kumkashifu mtume wa Waislamu", lakini mwenyewe padre amewahi kumkashifu katika hicho hicho kitabu chake, ingawaje kwa kujificha nyuma ya 'kuuhukumu mti.' Ni hila tu ya kinafiki kwa kumkashifu Mtume[saw].

## Somo 4. Mungu Mmoja Yesu na Maria

Kurani inaeleza upotevu wa wale waliowaabudu Yesu na mamaake Maria kuwa miungu. Padre amekubali kuwa:

> "Ni upuuzi wa baadhi ya Wakristo waliosema kuwa Utatu mtakatifu ni Mungu, na Maria, na Yesu. Utatu kama huo hata sisi tunaukataa." (uk. 97)

Kwa kweli huo ni upuuzi, tunakubaliana na padre. Lakini pia ijulikane ya kuwa hata kama Maria si mmojawapo wa Utatu, lakini mpaka leo hii anaabudiwa na Wakristo. Je, hao nao wanafanya upuuzi? Kurani inawasuta kwa ajili ya kuwaabudu Yesu na Maria bila kutaja 'Utatu' katika sehemu hiyo – yaani katika Al-Maaida 5:117. 'Utatu' umetajwa katika An-Nisaa 4:172.

## Kurani Yataja Utatu

Padre amesema Kurani haikuutaja utatu hata mara moja. Ebu soma aya ifuatayo ya Kurani:

> "Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume wake wala msiseme 'watatu,' jizuieni, itakuwa bora kwenu; bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu. Ni mbali na utakatifu Wake ya kwamba Awe na mwana. Ni vyake vilivyomo mbinguni na ardhini; na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa mlinzi". (An-Nisaa 4:172)

Basi imani juu ya utatu imevunjwa ndani ya Kurani. Na kama padre ana maana ya kuwa Kurani haikutaja kwa majina zile nafsi tatu, Mungu baba, mungu mwana na mungu roho mtakatifu, kweli kwa majina hakuna, lakini kuna sababu yake maalumu. Sababu yenyewe ni kwamba baadhi ya Wakristo walifikiri nafsi tatu za Mungu ni: Baba, Mwana na Maria; na wengine wakasema ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; hivyo ilifaa tu kueleza Utatu wenyewe ili kila mmoja asahihishwe: Mwenye kukubali zile tatu za mwanzo na pia mwenye kukubali zile tulizotaja nyuma.

Kwa hiyo, Kurani inakataa na kupinga kabisa utatu wa aina yoyote. Padre aliposema ya kuwa Muhammad[saw] alikutana na Wakristo waliokuwa wamejitenga na kanisa waliosema kuwa nafsi tatu ni Mungu, Maria na Yesu, alikuwa na maana kuwa utatu wa aina hii tu umekataliwa

ndani ya Kurani. Lakini kwa hakika utatu wa kila aina iliyokuwa au iliyopo au itakayokuwa umekataliwa vikali.

**Ufunuo wa Yesu**

Padre amedai kuwa Waislamu hawakubali ufunuo wa Yesu. Sivyo, bali tunakubali ufunuo wa Yesu. Hata tunakubali maneno haya ya Yesu:

> "Aliyeniona amemwona Baba" (Yn. 14:9).

Sababu yake ni kuwa manabii wote huja kwa kudhihirisha uwepo wa Mungu kwa njia ya hoja, dalili na miujiza. Kwa hiyo, katika zama mbalimbali waliowakubali manabii kwa uhalisi wa nyoyo walimwona Mungu. Juu ya Muhammad[saw] Kurani inaeleza:

> "Bila shaka wanaofungamana nawe kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao." (Al-Fat'h 48: 11)

Aya hii inasema kuwa waaminio walipofanya ahadi ya kumfuata Mtume[saw] kwa kuweka mikono yao katika mkono wa Mtume, kwa kweli waliweka mikono yao katika mkono wa Mungu. Kisha Kurani inasema:

> "Mwenye kumtii Mtume, basi amemtii Mungu." (An-Nisaa 4:81)

Basi katika maana hii hii Yesu naye akasema tuliyotaja juu.

**Baba Aabudiwe**

Biblia inasema:

> "Semeni, mnaposali: Baba yetu uliye mbinguni." (Mt. 6:9)

Ndiyo kusema kwamba Mungu Baba pekee Ataabudiwa siyo mwana au roho mtakatifu. Basi Mwana na Roho Mtakatifu hawana uungu.

**Mungu Yu Karibu**

Padre amewadanganya wasomaji aliposema kuwa Wakristo wanamwamini Mungu kuwa karibu nasi ilhali Islam inafundisha kuwa 'macho hayamfikii'. Ukweli ni kwamba Kurani haijasema kwamba Mungu Yu mbali nasi; bali imesema macho hayamfikii Mungu. Na tunajua kuwa kuna vitu ambavyo macho ya binadamu hayavifikii lakini vipo karibu sana na mtu, kama vile upepo, roho ya mtu.

Padre apanue elimu yake kwa kujua ya kwamba kama kitu kipo karibu mno au mbali mno, macho yanashindwa kukiona. Na Mungu Yu karibu mno na pia mbali mno kwani Yuaenea kila mahala. Kurani inasema:

> "Tu karibu naye kuliko hulkumu yake." (Qaaf 50:17)

Yaani Mungu Yuko karibu na binadamu kuliko mshipa wake wa moyo. Pia:

> "Basi mahali popote mgeukiapo, ndipo (mtaukuta) uso wa Mwenyezi Mungu." (Al-Baqara 2:116)

Pia someni aya hii:

> "Yeye Huwa pamoja nao popote walipo." (Al-Mujaadila 58:8)

Na sasa tugeukie aya aliyoitaja padre, lakini ametaja nusu-nusu. Aya kamili ndiyo ifuatayo:

> "Macho hayamfikii, bali Yeye Anayafikia macho; Naye ni Latifu, Mwenye habari." (Al-An'aam 6:104)

Hapa Mungu Anasema kuwa macho hayamfikii Mungu, bali Yeye Huyafikia macho. Basi Yu karibu. Muradi wa aya ni kuwa baadhi ya watu wanafikiri kuwa wanaweza kumjua Mungu kwa uwezo wao, ilhali hawawezi isipokuwa tu Mungu mwenyewe Ajidhihiriahe kwa watu. Hii ndiyo maana ya aya, bwana padre. Ama bishara kuhusu Imanueli, tukichunguza Agano la Kale, tunakuta ya kuwa hiyo ilitimia zaidi ya miaka 700 kabla Yesu hajazaliwa, katika dhati ya mtoto wa Isaya. Tazameni Isaya mlango wa 7 na 8. Na maelezo yake mwaweza kuelewa zaidi katika "The Wycliff Bible

Commentary" katika milango hiyo; angalieni hususa Isaya (7: 14 na 8:8).

Imanueli, maana yake ni Mungu Yu pamoja nasi. Je, kweli Mungu Alikuwa pamoja na Yesu daima? Yesu alipokuwa msalabani akahangaika na maumivu na akawahi kutamka:

> "Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha." (Mt. 27:46)

Yesu hayuko karibu, kwani kasema mwenyewe:

> "Hamtaniona kamwe tangu sasa." (Mt. 23:39)

Pia someni Jalada la 2 la 'Historia ya Ukristo', kwamba:

> "Njia moja ilikuwa kukaza huruma ya Mama Mariamu ambaye angechukua wajibu wa kuwaombea watu mbele ya mwana wake Yesu aliye mbali zaidi." (uk. 65)

## Mungu ni Rahmani

Padre anasema ya kuwa kwa Mkristo Mungu "Huwaangazia jua Lake waovu na wema, Huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." Ni sawa. Lakini Islam inafundisha ya kwamba Mungu ni Rahmani (Al-Faatiha 1:1), na Rahman maana yake kwa Kiarabu ni Yule ambaye Anatoa vitu vyote, si jua tu, bure kwa viumbe vyote, sio tu

kwa wanadamu wema na waovu, bali hata kwa wanyama na ndege na kila kiumbe. Tena:

> "Wote Tunawasaidia, hawa na hawa, katika kipawa cha Mola wako; na kipawa cha Mola wako hakikuzuiliwa." (Banii Israaiil 17: 21)

Pia padre amesema kuwa kwa Waislamu, Mungu "Hukunjua riziki kwa Amtakaye". Je kwa Mkristo, Mungu Hakunjui riziki kwa Amtakaye? Bila shaka katika dunia hii tunaona wengine wamejaaliwa riziki nyingi na wengine hawakujaaliwa sana. Hii yote ni kwa ajili ya kanuni iliyowekwa na Mungu katika hii dunia.

Siyo maana yake kuwa Mungu Humnyima fulani riziki na kumpa mwingine kwa kuwabagua; bali mradi wake ni kwamba Mungu Ameweka kanuni za uchumi katika ulimwengu, anayefuata barabara hizo kanuni huchuma mali nyingi, na yule aliye mvivu na mzembe hujinyima kwa ajili ya kanuni hii ya Mungu ya kuwa mzembe atanyimwa.

Lakini kama kwa Mkristo Mungu Anampenda kila mtu, kwa nini wengine ni maskini na wengine ni matajiri? Au je Mungu Anao ubaguzi katika kuwapenda watu mbalimbali?

**Utatu**

Padre amesema kuwa Utatu ndiyo asili ya upendo, lakini hakueleza uhakikisho wa usemi wake.

Waislamu hawakatai mafumbo yote ya Yesu, bali baadhi yake ambayo hayawezi kukubaliana na Maandiko wala akili ambayo kwa kweli ni nyongeza ya baadaye.

Waislamu tunasema kuwa wema watapata maisha ya Peponi, na wabaya baada ya kutakaswa katika Jahanamu wataingizwa Peponi. Lakini je, Wakristo nao wanaamini kuwa wasio Wakristo wataingia Peponi? Hapana!

## Ufunuo Kukamilika

Kusema kwamba Yesu amekamilisha ufunuo wa kale, na

sasa ufunuo mwingine hautakuja, ni kumpinga Yesu aliyesema:

> "Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote." (Yohana 16:12-13)

Kwa hiyo upo ufunuo wa Roho wa kweli ambaye ndiye Mtume Muhammad[saw]. Someni kitabu chetu *"Mtume Muhammad[saw] katika Biblia."*

## Mama Wa Mungu

Padre amesema Maria si Mungu ingawaje ni Mama wa Mungu, kwa sababu Mama mzazi wa Kardinali Rugambwa mwenyewe si Kardinali japo yu Mama Kardinali. Kwa kweli hiyo siyo hoja ya kweli. Kardinali

ni cheo ilhali Mungu si cheo kinachoweza kupatikana kwa mtu yeyote. Bali Mungu ni dhati maalum. Basi kama mzaa simba ni simba na mzaa binadamu ni binadamu, mzaa Mungu ndiye Mungu.

Mzaliwa huwa wa jinsi ya wazazi wake, ila tu kama wazazi wanakuwa wa jinsi tofauti hapo mzaliwa anakuwa wa hali ya katikati ya wazazi hao wawili. Kwa mfano farasi na punda wakikutana nyumbu anazaliwa aliye katikati ya farasi na punda. Basi kama Yesu alikuwa mtoto wa Mungu baba na Maria binadamu, hapo bila shaka Yesu yuko hali ya katikati, yaani nusu binadamu na nusu Mungu, siyo binadamu kamili wala Mungu kamili. Isipokuwa tu tukikubali kwamba Maria naye alikuwa Mungu kamili ndipo Yesu atahesabiwa Mungu kamili. Ule mfano wa Mama Kardinali ni hoja ya uwongo.

Pia itambulikane kwamba mzaliwa wa wazazi wa jinsi tofauti hawezi kuzaa tena. Je, hii ndiyo sababu Yesu hakuoa au kuzaa, sawa na imani ya Wakristo?

## Somo 5. Mwanadamu Mbele ya Mungu

Padre amesema kuwa Mkristo anakataa kumfananisha Mungu na Bwana Mkubwa akataye kila shauri, bila kujali viumbe vyake. Anasema kwamba Mungu ni Mwumba wa mbingu na nchi, lakini ni Baba pia.

Padre ameipinga Injili ambayo inafundisha ya kwamba:

> "Hata alipokuwa akipita alimwona mtu, kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake wakamwuliza wakisema, Rabi, ni yupi aliyetenda dhambi, mtu huyu au wazazi wake, hata azaliwe kipofu? Yesu akajibu, huyu hakutenda dhambi, wala wazazi wake; bali kazi za Mungu zidhihirishwe ndani yake." (Yohana 9:1-3)

Maneno hayo ya Yesu yanahakikisha ya kuwa mtu huyo akazaliwa kipofu kwa sababu Mungu Alitaka kuonyesha kazi zake. Je Mungu bado Hajafanywa 'Bwana Mkubwa' anayekata shauri bila kujali viumbe wake? Mmoja anamwamulia kumfanya kipofu na mwingine mwenye macho! Je yupo baba yeyote apendaye mtoto wake kuwa kipofu? Mapenzi ya Baba Mungu wa Kikristo yako wapi sasa?

Ieleweke hapa ya kuwa Islam inaposema kwamba Mungu Hufanya Apendavyo na kwamba Mungu ni Mwenye Hekima, maana yake ni kuwa Mungu Haamrishwi, bali Anatenda Anavyotaka, lakini matakwa yake huwa yenye hekima; yaani ziko sababu maalum Anazoangalia Mungu Akikata shauri.

Hata hakimu binadamu pia anaamua apendavyo, lakini kupenda kwake huwa na sababu kadha wa kadha. Basi na Mungu pia Humwongoza Amtakaye na kumhukumu amepotea Amtakaye; yaani Mungu baada ya kuona

wema wa mtu Humwamulia ameongoka, na Akiona uovu wa mtu Humwamulia kuwa amepotea. Kuna mushikili gani hapo? Naam, Anapoona watu wanapotea, Mungu Huleta manabii ili kuwaongoza.

## Ajali

Ajali au kadiri ya Mungu maana yake siyo kwamba binadamu hana uhuru wa kutenda kwani eti Mungu Ameisha mwamulia atende maovu au mema; sivyo. Bali maana ya kadiri ya Mungu ni kanuni zake Alizoweka katika ulimwengu; yaani mtu akitenda hivi matokeo yake yatakuwa ya namna fulani, na akitenda kinyume atapata matokeo kinyume.

Kuna mengine yaliyoisha amuliwa kabisa na Mungu. Kwa mfano, kila mtu atakufa. Sasa, mtu yeyote hata akifanya nini lazima atakufa siku moja. Asipofuata kanuni za afya, mtu ataugua; ndiyo kadiri ya Mungu uugue usipoangalia sheria za afya. Hii ndiyo maana ya kadiri au ajali katika Islam. Aya zingine alizoandika padre zinaweza kuelezwa kwa njia hii hii.

## Kipeo cha Mwislamu

Kipeo cha Mwislamu si kumtii tu Mungu; bali ni kupata Mapenzi ya Mungu, na njia yake ni kumtii Mungu na Mtume wake: "Sema, Ikiwa ninyi mwampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu Atawapendeni." (Aali 'Imraan 3:32)

## Mungu Akipenda

Padre amesema kuwa Mwislamu anapaswa kufanya kazi kama mtumishi wa Mungu. Kwa kweli kila kitu ni mtumishi wake hata Yesu:

> "Tazama mtumishi wangu Niliyemteua." (Mathayo 12:18)

Pia padre alisema Islam inafundisha kumtii Mungu; tunamwelekeza kila apendaye haki aisome Biblia isemapo:

> "Basi mtiini Mungu." (Waraka wa Yakobo 4:7)

Je Biblia nayo haifundishi kumtii Mungu?

Padre amewatania Waislamu waliofundishwa kusema 'Mungu akipenda' (insha-Allahu) wanapotaka kutenda jambo, ilhali mwenyewe anasema kwamba hiyo ilikuwa ni desturi ya Wakristo wa kwanza (Yak. 4:15). Hii inahakikisha ya kuwa Wakristo wa baadaye wameiacha desturi hiyo ya kumtegemea Mungu, kwa kuwa wameingia katika anasa za dunia.

## Kujifanya Mdogo

Naam, lazima mtu ajifanye mdogo mbele ya Mungu, bali hata Yesu alijua yu mdogo mbele ya Bwana Mungu:

> "Bwana ni mkuu kuliko mimi." (Yohana 14:28)

**Sujuda**

Padre akidharau sujuda iliyo muhimu sana katika ibada ya Kiislamu amesema kuwa:

> "Mungu Anastahili kuabudiwa, lakini ibada yenye kumpendeza siyo ile ya kutusha kichwa vumbini; Mungu Anataka kuabudiwa moyoni mwa mtu." (uk. 101)

Lakini Yesu ametenda vingine kuliko apendavyo padre:

> "Akaenda mbele kidogo kaanguka kifudifudi, akaomba akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke." (Mt. 26:39)

Yesu akajidhalilisha mbele ya Mungu kwa kuanguka kufudifudi alipohuzunika kujua kwamba Wayahudi wanataka kumpigilia msalabani. Hatujui kwa nini padre anaona aibu kumsujudia Mungu. Ni sawa ya kuwa kusujudu bila roho safi hakuleti faida, lakini siyo maana yake usisujudu kabisa; bali unapaswa kumsujudia Mungu kwa roho safi na kunjufu.

Kama Mungu ni baba, inafaa asiabudiwe, kwani hakuna baba anayeabudiwa. Padre amesema Mkristo si 'mtoto wa mjakazi', bali ni mtoto wa yule aliye mwungwana (Gal 4: 31). Ndiyo kusema kwamba kuna ubaguzi katika dini ya Kikristo kati ya mwungwana na mtumwa. Mtumwa adunishwa! Itambulikane kwamba hata wana

wa Ismaili sio watoto wa mjakazi. Ni uzushi wa Biblia iliyomwita Bibi Hajira kuwa mjakazi; bali alikuwa ni mkewe mwungwana halisi wa nabii Ibrahimu.

Padre amesema kuwa Mkristo hakuzaliwa kwa tone la shahawa, bali kwa maji na Roho. Padre aelewe kuwa shahawa nayo ni maji na roho; roho iliyomo ndani ya shahawa ndiyo roho inayojidhihirisha ndani ya mtu azaliwapo, ilhali hapo kabla ilikuwa imefichika humo.

Pia ijulikane kuwa ijapokuwa Yesu hakuwa na baba lakini hata hivyo alizaliwa na damu, kwani aliendelea kujilisha damu ya hedhi kwa miezi tisa tumboni mwa mamaake. Mkristo tu pekee siye mwana wa Mungu, bali hata waasi ni watoto wa Mungu (Isaya 30:1).

Kusema kuwa Mkristo ni kiumbe aliyekombolewa, ni madai tu matupu yasiyo na uhakikisho. Tunaona Wakristo walio wezi na waasherati; je, hao wote wamekombolewa? Alama ya kukombolewa ni kuungana na Mungu na kuwa mwema.

## Ibada

Hapo kabla padre akieleza tofauti kati ya Islam na Ukristo alisema kuwa 'kipeo cha Mwislamu ni kumtii Mungu' (uk. 100), lakini kwenye ukurasa wa 101 mwenyewe amesema kuwa "tunapaswa kutii hata mauti ya msalaba." Akimalizia akasema:

> "Basi ni utii wa mwana kwa babaye, katika roho na kweli."

Kwa hakika utii mbele ya Mungu sio kama utii wa mwana mbele ya baba. Kwani baba wakati mwingine anaweza kuamrisha kinyume cha ukweli. Hivyo kumfananisha Mungu na baba ni mfano usiokamilika. Bali Mungu ni Mola, Rahman, Rahim n.k.w.k.

**Mapendo**

Padre anasema kwamba Mkristo hana wasiwasi wa kuogopa yatakayompata (uk. 101). Kwa kweli hali ya mtu inastahili kuwa katikati ya kutumai na kuogopa ndipo anaweza kujirekebisha na kufaulu vizuri zaidi. Kutumaini ya kuwa Mungu ni Mwingi wa rehema na Mwingi wa ukarimu na Msamehevu huku kuogopa isije mtu akalegea katika imani na matendo mema na akawa mbali na rehema ya Mungu na upendo Wake. Ni fundisho linaloonekana tamu kwa nje kusema kuwa Mungu Husamehe kila akosapo mtu, lakini kwa kweli ni fundisho nusu, kwani mtu wa aina hii atajasiri kutenda dhambi kwa kutegemea kuwa atasamehewa dhambi. Na pia kuamini kuwa Mungu Ataadhibu kila akosapo mtu kunakatisha tamaa, kwani mtu akiisha kosea kwa bahati mbaya atavunjika moyo akifikiri kuwa sasa ataadhibiwa tu na Mungu wala hawezi kusamehewa. Kwa hiyo imani bora zaidi ni ile iliyofundishwa na Islam kwamba mtu akitubu kwelikweli husamehewa dhambi zote:

> "Sema, enyi watumishi wangu mliojidhulumu wenyewe, msikate tamaa katika rehema za Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote; hakika yeye ni Msamehevu, Mrehemevu. Na nyenyekeeni kwa Mola wenu na jitupeni kwake kabla ya kuwafikieni adhabu, kisha hamtanusuriwa." (Az-Zumar 39:54-55)

Basi mtu ajirekebishe ili asamehewe waila ataadhibiwa. Kwa njia hii tu mtu anaweza kupata maendeleo ya roho. Ile fikara ya kuwa hata nikifanya nini nitasamehewa tu kwani Yesu ameniondolea dhambi kwa njia ya kuuawa msalabani, ni imani inayorudisha nyuma katika wema.

Padre ajue ya kuwa si Injili tu bali hata Kurani inasema kuwa watu wema wataandaliwa karamu:

> "Ni karibisho litokalo kwa Msamehevu, Mwenye rehema." (Haa Miim 41:33)

***Kuogopa Miiko:*** Padre anajivuna kwa kusema kwamba: "Yesu ndio uhuru wa waana wasioogopa ajali wala miiko." (uk. 102)

Tunaona hii ni hatari kutokujali miiko. Makatazo ya Mungu lazima yaangaliwe, lakini padre hataki. Mwiko mmojawapo ni kujiepusha na uzinzi na wizi; je, usipoogopa kuangukia upotevu huo utaweza kusalimika? Hata! Na hii ndiyo sababu wengi wenye

imani ya aina hiyo huangukia maovu. Habari za ajali (kadiri) tumeisha eleza hapo nyuma.

Padre ameyahesabu mafundisho ya zamani kuwa manyonge na yenye upungufu (Gal. 4:6-9). Lakini hakika yenyewe ni kwamba kumwita Mungu kuwa baba kunamtia kasoro, kwani baba anazo kasoro nyingi na hizo zote zitakubaliwa katika Mungu pia kama Mungu Yu baba. Kuongeza sifa ya Baba katika sifa za Mungu ni kumtia upungufu. Padre amewashauri Waislamu kuongeza jina 'baba' katika majina ya Mungu. Padre ajue kuwa Waislamu hawajazoea kuzusha mambo jinsi watu wa Kitabu walivyozoea kuongeza-ongeza mapya katika Biblia.

## Somo 6. Mwanadamu Mbele ya Mungu Kiumbe Huru

Akijaribu kuwahakikishia wasomaji kwamba Islam inafundisha kuwa binadamu hana mamlaka kamili duniani, padre ameandika aya zifuatazo:

> "(Hamjui) kwamba habebi mbebaji mzigo wa mwingine na kwamba Mungu ndiye Anayechekesha na kuliza; na kwamba Yeye ndiye Atajirishaye, na Atoaye hazina; tukio lililo karibu linasogea, hakuna awezaye kuliondoa ila Mwenyezi Mungu… Basi msujudieni Mwenyezi Mungu na kumwabudu." (An-Najm 53: 39-63)

Padre ameacha katikati aya zinazohusu madhumuni yenyewe na akavuruga kusudi ukweli. Aya zenyewe zilivyo ndizo zifuatazo:

> "Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa? Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi kwamba habebi mbebaji mzigo wa mwingine; na ya kwamba mtu hatapata ila aliyoyafanyia juhudi; na ya kwamba juhudi yake karibu itaonekana; kisha atalipwa malipo yaliyo kamili; na kwamba mwisho ni kwa Mola Wako; na kwamba Yeye ndiye Anayechekesha na kuliza; na kwamba Yeye ndiye Aumbaye jozi ya kiume na kike, katika mbegu ya uzazi inapotiwa; na kwamba juu Yake ni ufufuo mwingine; na kwamba Yeye ndiye Atajirishaye na Atoaye hazina, na kwamba Yeye ndiye Mola wa (nyota) Shi'raa; na kwamba Yeye ndiye Aliyewaangamiza Waadi wa kwanza, na Wathamudi, Hakuwabakisha, na kabla yao watu wa Nuhu – hakika wao walikuwa wadhalimu na waasi sana – na miji iliyopinduliwa ndiye Aliyeiangusha. Vikafunikiza vilivyofunikiza. Basi juu ya neema gani ya Mola Wako unabishana? Huyu ni mwonyaji miongoni mwa waonyaji wa zamani. Tukio lililo karibu linasogea. Hakuna awezaye kuliondoa ila Mwenyezi Mungu. Je,

> mnastaajabia hadithi hii? Na mnacheka wala hamlii, na hali ninyi mmeghafilika? Basi msujudieni Mwenyezi Mungu na kumwabudu". (An-Najm 53: 37-63)

Hizo ndizo aya za Kurani alizovuruga padre alipojaribu bure kuhakikisha jambo lisilopatikana ndani ya Kurani Tukufu.

Aya zinasema kuwa kafara ya Yesu ni kitu kisicho na maana, kwani imeandikwa katika vitabu vya Musa ya kuwa hakuna mbebaji atakayebeba mzigo wa mwingine. Yaani kila mmoja atabeba matokeo mabaya ya dhambi zake yeye mwenyewe. Ndiyo kusema kwamba haina maana kwamba watu watende dhambi na badala yao Yesu asulubiwe msalabani. Na Kurani imesema haki kwani Vitabu vya Musa kweli vinanena hivyo. Katika Torati imeelezwa ya kwamba wana wa Israeli walipotenda dhambi na Mungu Alipowakasirikia, hapo Musa akajitolea kwa kumwomba Mungu kuwa:

> "Unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichokiandika. Bwana akamwambia Musa: Mtu yeyote aliyenitenda dhambi, ndiye Nitakaye-mfuta katika kitabu changu." (Kutoka 32:32-34)

Ndiyo kusema kwamba Mungu Alimwambia Musa ya kuwa atakayetenda dhambi ndiye ataadhibiwa, siyo

kwamba wana wa Israeli watende maovu lakini Musa apewe adhabu.

Tena kuna tofauti kati ya kafara aliyonuia Musa na ile anayosingiziwa Yesu. Kwani Yesu hakutaka kabisa kujitolea kufa msalabani, bali akaanza kulia na kuomba ili kikombe cha kifo kimwepuke. Lakini Musa kwa moyo wote anajitolea kwa ajili va watu wake na yuko tayari kufutwa katika daftari ya Mungu, lakini Mungu Hakukubali Akisema kuwa mwenye dhambi ndiye ataadhibiwa. Basi Kurani inaitaja habari hiyo isemapo "hakuna mbebaji atakayebeba mzigo wa mwingine." Kwa hiyo, kusema kwamba Yesu amebeba mzigo wa dhambi za watu ni jambo lisilo na msingi hata kidogo sawa na kitabu cha Musa wala sawa na akili ya binadamu.

Kisha Kurani katika aya hizo inaeleza waziwazi ya kuwa binadamu hatapata ila aliyoyafanyia juhudi. Habari hii inabatilisha kabisa masingizio ya padre kwamba Islam inafunza ya kuwa binadamu hana uhuru, na kwamba yote yanayotendwa, hutendeka sawa na furaha ya Mungu.

Ile habari ya kuwa Mungu Amtajirisha mtu au kumchekesha au kumliza na kadha wa kadha, maana yake ni kuwa binadamu hupata matokeo ya matendo yake lakini hayo matokeo yanatolewa sawa na kanuni iliyowekwa na Mungu katika ulimwengu huu. Ni kama mwalimu atoavyo matokeo ya mtihani wa mwanafunzi, lakini matokeo hayo

huwa sawa na juhudi aliyoonyesha mtoto katika mtihani. Kama mtoto anashindwa katika mtihani, si kosa la mtoaji matokeo ya mtihani huo. Basi Mungu Anapotoa matokeo ya amali za mtu, hapo Humchekesha au kumliza sawa na matendo ya mtu huyo.

Ile habari ya "tukio lililo karibu linasogea," muradi wake ni kuwa wapinzani wa Islam walioshika silaha ili kuangamiza dini hii watashindwa siku tukio kuu la kutekwa Makka litakapotukia, wala hakuna awezaye kuliondoa tukio hilo.

Hatuelewi kwa nini mwishowe bila kutaja aya yoyote ya Kurani, padre kaandika, "Mwanadamu hapandishwi cheo." Hii ni kinyume kabisa na fundisho la Islam. Kurani inasema waziwazi kwamba:

> "Watapata vyeo vitokavyo Kwake, na msamaha na rehema." (An-Nisaa 4:97)
>
> "Na wote wana vyeo sawa na yale waliyoyatenda. Na Mola wako si Mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda." (Al-An'aam 6:133)
>
> "Na atakayemjia hali yu mumini amefanya vitendo vizuri, basi hao ndio watakaopata vyeo vya juu." (Twaa Haa 20:76)

Ziko aya chungu nzima zihakikishazo kuwa binadamu hupandishwa cheo.

Padre amejasiri kusema kuwa mwanadamu hushiriki katika utawala wa Mungu, lakini Biblia yake inampinga:

> "Yeye Aliyehimidiwa, Mwenye uweza peke yake, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana; ambaye Yeye peke yake Hapatikani na mauti, Amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa; wala hakuna mwanadamu aliyemwona, wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una yeye hata milele." (1 Timotheo 6: 15, 16)

Kwa hiyo, Mungu peke yake ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, na yuko mbali, hawezi 'kukaribiwa.'

**Utiifu**

Padre amekariri mara nyingi juu ya utii kwamba Islam inamtaka binadamu kumtii Mungu. Kuna ubaya gani ndani yake? Je, Ukristo unamtaka mtu kumwasi Mungu? Si Biblia inamwita Mungu kuwa Bwana wa mabwana? Maana yake nini? Kama yu Bwana basi binadamu ni watumishi wake, na kazi ya watumishi huwa kumtii bwana!

Kurani inatia mkazo katika utii, kwani, ndiyo njia ya kumkurubia Mungu na kupata mapenzi Yake:

> "Sawa. ikiwa ninyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni Mwenyezi Mungu Atawapendeni." (Aali 'Imraan 3:32)

Padre amesema kuwa katika Ukristo badala ya Mungu kutiiwa, anatukuzwa na kushukuriwa kwa wema wake na ukarimu wake (uk. 104). Na ili kuhakikisha jambo hilo padre ameturudisha kwenye Agano la Kale, yaani ametaja aya za Zaburi, badala ya kututajia Agano Jipya. Kurani imejaa fundisho la kumtukuza Mungu na kutaja Wema Wake na Ukarimu Wake hata kwamba sehemu yake ya 100 haionekani ndani ya Biblia. Kila sura ya Kurani inaanzia na maneno "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa **ukarimu**." Aya hii imerudiwa mara 114 katika Kurani na tena ziko aya zingine chungu chungu zinazoeleza Ukarimu wa Mungu na Wema Wake na sifa Zake bora.

Padre amesema kuwa Mkristo anathamini kumshukuru Mungu badala ya kumtii. Lakini hakuandika hata aya moja ya Biblia ionyeshayo kuwa Mkristo amefunzwa hivyo. Lakini Kurani imejaa funzo hili la kumshukuru Mungu:

> "Na Nishukuruni wala msinikufuru." (Al-Baqara 2:153) "Kuleni katika riziki ya Mola Wenu, na mumshukuru." (Saba' 34:16)

Juu ya kumtukuza Mungu, Kurani inafunza hivi:

> "Na Mtukuze Mola Wako kwa kumsifu kabla ya kutoka jua, na kabla ya kuchwa na katika usiku Mtukuze na pia baada ya kusujudu." (Qaaf 50: 40-41) "Kinamtukuza Mwenyezi Mungu kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini;

> Ufalme ni Wake, na sifa njema ni Zake, na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu." (At-Taghaabun 64:2)

Kwenye ukurasa wa 104, padre amerudia habari za Mapenzi na Kudra ambazo aliziandika hapo nyuma pia na huko tumeisha eleza.

Juu ya **Riziki** padre amedhihirisha kana kwamba binadamu hapaswi kutia bidii sawa na Islam ili kupata riziki, bali Mungu Ameisha mwandikia kila mtu riziki yake. Hii siyo sawa. Hapo nyuma tumeisha eleza kuwa Kurani inafundisha kuwa:

> "Mtu hatapata ila aliyoyafanyia juhudi." (An-Najm 53: 40)

Lakini tunauliza kwa nini padre kila siku anamwomba baba yake aliyeko mbinguni:

> "Utupe leo **Riziki** yetu." (Mt. 6: 11).

Je, ndiyo kusema kwamba Mkristo hana haja ya kulima au kufanya kazi ili kujipatia riziki, bali inamtosha amwombe Mungu kila siku hiyo riziki?

## Bahati Nasibu, Ajali

Habari za ajali na kudura tumeisha eleza nyuma. Mwislamu hasemi kuwa binadamu amelazimishwa na Mungu kutenda vibaya au vema, bali amepewa uhuru, lakini atapatiwa matokeo sawa na matendo yake.

Lakini Yesu anaonekana na imani anayoipinga padre:

> "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe." (Mt. 26: 39)

Pia Yesu anaamini kuandikiwa:

> "Mwana wa Adam aenda zake, kama ilivyo-andikwa." (Mathayo. 26: 24)

## Somo 7 - Imani Ni Kitu Kikuu

Padre amesema kwamba kwa Mwislamu imani ni kubwa zaidi. Hii ni sawa. Bila imani mtu hawezi kuwa na nia ya kutenda. Bali hata Biblia inakazia imani, hatuelewi kwa nini padre hataki umuhimu wa imani kinyume cha kitabu chake:

> "Kwa maana, amin, nawaambia, mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, Ondoka hapa uende kule; nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu." (Mathayo. 17: 20)

Je, hii haionyeshi ukuu wa imani?

### Malaika ni Wema tu

Padre amesema kinyume na ukweli alipoandika kwenye ukurasa 108 ya kwamba Waislamu wanaamini kuna malaika wema na wabaya. Hii Siyo imani iliyofunzwa na Kurani. Bali kinyume chake Kurani inafundisha ya

kuwa malaika hawamwasi Mungu kamwe, bali daima wanamtii tu:

> "…juu yake wako malaika wakali, wenye nguvu, hawamwasi Mwenyezi Mungu Aliyowaamuru, na hutenda wanayoamrishwa." (At-Tahriim 66:7)

Basi kuna malaika wema tu; hakuna malaika wabaya sawa na dini ya Kiislamu. Kama yupo mtu anayefikiria kuwa ibilisi au shetani alikuwa malaika na kisha alipomwasi Mungu akawa shetani, basi ajue kuwa imani hiyo haiambatani na funzo la Kurani inayofunza kwamba malaika hawamwasi Mungu bali hutenda sawa na amri za Mungu. Shetani ni kiumbe tofauti na malaika.

**Kuficha Imani**

Padre anasema kuwa sawa na imani ya madhehebu ya Kishia iko ruhusa ya kuficha imani wakati wa dhuluma. Lakini padre atasemaje juu ya Paulo ambaye hata bila kushurutishwa alikuwa anajifanya miongoni mwa watu wa aina fulani ilhali hakuwa miongoni mwao:

> "Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria,) ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria

> mbele za Kristo) ili niwapate hao wasio na sheria." (1 Wakorintho 9:20-22)

Yaani Paulo anajisingizia kuwa miongoni mwa Wayahudi, Wapagani na wengineo kusudi awapate kwa wingi. Dini haienezwi kwa hila na udanganyifu!

Kwenye ukurasa 109, padre ameandika maneno ya Biblia yasemayo:

> "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba Aliyenipeleka." (Yohana 6:44)

Sasa padre atasemaje juu ya Mungu wa Biblia ambaye Akimvuta mtu, ndipo mtu huyo anaweza kuja kwa Yesu; kwa uwezo wake mwenyewe binadamu hawezi kumjia Yesu. Je, Biblia imenyima hiari yake na kumnyang'anya uhuru wake? Padre alifikirie jambo hili.

Vilevile someni:

> "Nakushukuru, Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo hayo uliwaficha wenye hekima na akili, Ukawafunulia watoto wachanga." (Mt. 11:25)

Je, si kwamba Mungu Ametumia nguvu kuwanyima wengine na kuwapa wengine? Je, huu ndio uhuru na hiari aliyopewa binadamu?

Padre amesema kweli kwamba “Wala hawatatupwa nje wale waliofuata maagizo ya Ibrahimu.” (uk. 110). Waislamu wanafuata maagizo ya Ibrahimu, lakini Wakristo wanakataa kumfuata, kwa mfano katika agizo la tohara ya kila mtoto wa kiume siku ya nane tangu kuzaliwa.

## Somo 8. Mwanadamu Mbele ya Mungu – Sala

Katika mlango huu wa Sala, padre amevuruga sana ukweli makusudi aidharau sheria ya Kiislamu. Padre amesema kuwa “Wanasali mara tano kutwa, kama walivyofanya watawa Wakristo” (uk. 111). Hatujui kama Wakristo watawa walisali sala tano kila siku kama Waislamu; lakini kwa vyovyote kama padre amekubali habari hii, kwa nini basi anaipinga tena? Kama Wakristo watawa walikuwa wakisali kama Waislamu, basi hii yahakikisha kwamba Wakristo wa siku hizi wamepotoka walipoacha kusali kama Waislamu!

Padre amesema ya kwamba Mwislamu kabla ya kusali anatawadha na maji au asipopata maji anafanya tayamumu na vumbi. Kwa hakika kutawadha kunaleta upole wa moyo na humwondolea mtu kiburi, kwani anakumbushwa kuwa ameumbwa na maji au na vumbi, yaani vitu hafifu sana. Kwa hiyo binadamu anapaswa asiwe na majivuno bali awe mnyenyekevu kwa kukumbuka chanzo chake. Pia kutawadha huleta usafi.

## Si Tendo Dhahiri tu

Padre amedanganyika aliposema kuwa kwa Mwislamu kusali ni tendo dhahiri. Hakika yenyewe ni kwamba Mungu Ametangaza ndani ya Kurani:

> "Basi ole kwa wanaosali, ambao wanapuuza sala zao, ambao hufanya ili waonwe." (Al-Maa'uun 107:5-7)

Ni dhahiri ya kuwa sala ya asili hutokana na moyo wa mtu. Yaani mtu hupaswa kuabudu kwa moyo pamoja na mwili wake, kwani Mungu Ameneemesha mwili na roho. Anayetaka ibada ya Roho tu kwa kuacha ibada ya mwili, humdharau Mungu, kwani mwili nao umeneemeshwa na Mungu. Na atakaye ibada ya mwili pekee bila kuwa roho humo vilevile hatapokelewa. Basi binadamu anapaswa kusali kiroho na kimwili: yaani afanye kitendo cha kimwili huku akinyenyekeza roho mbele ya Mungu ili Amsaidie kimwili na kiroho.

Pia ijulikane ya kuwa katika sala tano kuna sehemu tu moja inayoitwa faradhi ambayo husaliwa msikitini, lakini sehemu nyingine za sala hizo ambazo ni ndefu zaidi hupendelewa kusaliwa nyumbani. Ndivyo alivyokuwa akifanya Mtume[saw]. Sababu yenyewe ni kuwa kusali pamoja kunaleta faida ya umoja pamoja na baadhi ya faida nyingine; na kusali katika upweke kunaleta faida ya kwamba mtu hashawishiki na nia ya kuonwa na watu.

Basi Islam imewapatia wafuasi wake faida za aina zote mbili kwa kuamrisha kusali pamoja msikitini na pia kusali sehemu nyingine chumbani.

Vilevile ieleweke ya kuwa sala ya Kiislamu siyo tu maneno maalumu. Bali zaidi ya maneno hayo maalumu, mtu anapaswa kuomba maombi mengine mengi katika lugha yake sawa na shida zake na taabu zake.

Sasa tunauliza kwamba kama kwa Mkristo msikiti ndio moyo wake, kwa nini anahangaika kwenda kanisani? Padre amesema kwamba siyo amri ya Mungu kwenda kanisani kusali, bali ni amri ya kanisa; ndiyo kusema kwamba amri ya Mungu na amri ya kanisa zinahitilafiana. Basi dini hii si kamili, maana jambo la muhimu kabisa halimo katika dini ila tu kanisa limelibuni baadaye kwa kuona wafuasi wa dini nyingine wakifanya hivyo!

Pia kama kitendo cha mwili si kitu katika ibada ya kweli, kwa nini Mkristo hupiga magoti? Je, hicho sicho kitendo cha kimwili? Apige tu magoti ya moyo wake! Ni jambo la ajabu kuwa upande mmoja moyo hutiliwa mkazo sana na upande mwingine kiini cha sala yao ni kuomba, *"Utupe leo riziki yetu."* Katika Biblia ya Kiingereza wameandika *"Utupe leo mkate wetu wa kila siku"* (Mt. 6:13). Wanajifanya tu watu wa roho lakini maombi yao ni kuhusu chakula.

## Kuosha Roho

Padre amesema kuwa kwa Mkristo kutawadha ni kuosha roho. Ni kichekesho ya kuwa kama kutawadha si tendo la dhahiri kwa nini sala iwe ni tendo la dhahiri kama vile kupiga magoti na kutamka maneno kadha wa kadha; bali ingefaa kuelekeza roho bila kutamka lo lote. Lakini hii haiwezekani. Binadamu ameumbwa mwili na roho. Hivyo udhu wa mwili na udhu wa roho upatikane. Na vilevile sala ya roho na sala ya mwili iwepo. Hekima ya udhu ni kupata usafi wa mwili na pia kuahidi kuziweka safi kiroho sehemu hizo za mwili; yaani mtu anayetawadha hufunga nia mbele ya Mungu ya kuwa kama alivyozisafisha sehemu hizo za mwili kwa maji, ndivyo hivyo atakavyojaribu kwa uwezo wake wote kuziweka safi kiroho kwa kuzizuia hizo sehemu zisitende dhambi. Ziko dua maalum zinazoombwa wakati wa kuosha sehemu mbalimbali za mwili.

Ijulikane pia kwamba mwili unaathiri roho, na roho huathiri mwili. Kama mtu amehuzunika rohoni, alama zake zitaonekana katika mwili wake kwa sura ya machozi. Na kama amefurahika rohoni, uchangamfu utadhihirika usoni pake. Kwa hiyo, zile dini zinazopuuza mojawapo katika mwili na roho, hazina habari za tabia ya asili ya binadamu.

**Sujuda**

Padre anaona haya kujifanya mdogo mbele ya Mungu. "Kumbuka ukubwa wa Mungu na unyonge wa wanadamu," katania padre akiidharau sujuda mbele ya Mungu (uk. 112). Padre atambue ya kuwa 'Mungu ni Bwana wa Mabwana' (1 Tim. 6:15), na kwa hiyo wote ni kama watumishi mbele Yake. Mungu ni Mkuu kuliko hata Yesu (Yn. 14:28). Na kama Yesu aliye mdogo anaweza kusujudiwa na mwanamke (Mt. 15:25), kwa nini Mungu Aliye Mkuu Asisujudiwe na binadamu? Yesu mwenyewe alijidhalilisha mbele ya Mungu akianguka kifudifudi mbele ya Mungu (Mt. 26:39), kwa nini wanaojifanya wafuasi wake wanajivuna wasimsujudie Mungu? Lakini wapo Wakristo wengine wanaomsujudia Mungu katika ibada. Katika kijitabu kilichotolewa na Rev. Denis F. Wann tunasoma wazi wazi kuwa Mwinjilisti:

> "Kila siku aombe peke yake… amsujudie Mungu." (Mhudumu wa Kristo, uk.. 9)

Ni jambo la ajabu kwamba kati ya Wakristo walipatikana wengine ambao waliabudu divai na mikate na wakavisujudia:

> "Jambo jingine lililoandamana na mtindo huo ni jinsi walivyoanza kuabudu divai na mikate iliyokwisha kubarikiwa, wakaweka vyombo hivi

> katika kasha la kioo ambapo watu waliweza kuona na **kusujudu**."
>
> (Historia ya Ukristo, j. 2. uk 51 na Dean A. Peterson)

Padre ametania Waislamu wasalio hadharani, lakini hajui kwamba Kiongozi wa Kanisa, Bwana Tikhon:

> "alisimama katika gari lake akiwabariki maelfu elfu walipokuwa wamepiga magoti barabarani."
>
> (Historia ya Ukristo j. 3 uk. 151 – Robert M. Glen)

## Somo 9. Mwanadamu Ajilinda Na Unajisi

Katika Somo la 9, padre amepambanua kati ya Ukristo na Uislamu kuhusu kujilinda na uchafu. Ieleweke mapema ya kwamba Mwislamu anaposema unajisi maana yake ni uchafu ama wa kiwiliwili au wa kiroho. Tofauti baina ya Islam na Ukristo wa siku hizi ni kwamba Mwislamu anaona kujilinda na uchafu wa kila aina ni wajibu wake wa dini; lakini Mkristo anaona kujiepusba na uchafu wa roho tu ndiyo sehemu ya dini. Kuepukana na unajisi wa kiwiliwili ni ustaarabu wala sio wajibu wa dini kwa Mkristo.

Uhakika ni kwamba usafi wa roho au wa mwili haumfaidishi Mungu chochote; ni faida ya binadamu katika kujilinda na uchafu wa mwili na roho na kujipatia usafi wa kiwiliwili na moyo. Bali kila kitendo kinachofanywa kwa nia ya dini huwa cha dini sawa na

mafunzo ya Islam. Mtume[saw] amesema kuwa ni kitendo cha dini mtu kutia tonge la chakula kinywani mwa mkewe kwa mapenzi kama anatenda hivyo kwa ajili ya fundisho la Mungu kwamba mtu anapaswa kumpenda mkewe. Hii ndiyo tofauti baina ya Islam na Ukristo katika mambo yote yale. Mwislamu anafikiri kila kitendo kuwa cha dini kwa ajili ya nia ya mtu, lakini Mkristo anabagua, hiki cha dini na hiki cha dunia.

Islam inasema kuwa kitendo hutegemea nia ya mtu (Bukhari). Kama nia ni ya kidunia, hata sala itakuwa kitendo cha kidunia kama inasaliwa kwa kuonwa na watu. Na kinyume chake kumpenda mkeo ni kitendo cha dini kama unatenda hivyo kwa ajili ya mafunzo ya Mungu.

Sasa, asemavyo padre, Mkristo anajiweka safi kwa sababu ni "adabu tu na busara." Kwa hiyo akijiweka safi hapati radhi ya Mungu. Lakini Mwislamu anajiweka safi kwa sababu ya radhi ya Mungu, hivyo anapendwa na Mungu huku akiisha pata faida inayotakikana katika usafi.

## Vitu Najisi

Padre amesema kuwa Islam inafunza kwamba *jasho, machozi na mate ni najisi*. Hii siyo sawa. Mtu akipata jasho au akitokwa machozi hata ndani ya sala, udhu haubatiliki. Pia katika hali ya kutawadha mtu akitema mate, udhu upo pale pale, haujatanguka.

*Divai na pombe* ni vitu vichafu katika maana hii ya kwamba vinachafua afya ya mwili na pia ya roho. Vile vile pombe inanuka vibaya.

**Nguruwe** amehesabiwa najisi katika Biblia (Walawi, mlango wa 11); Islam haijasema hivyo ila tu kuila nyama yake ni haramu kwa sababu inaathiri vibaya afya ya mtu na kuziharibu khulka njema. Hali kadhalika ni uzushi wa padre kusema kwamba *mbwa ni najisi* katika Islam. Islam inaruhusu kumfundisha mbwa kwa kuwinda, na mawindo hayo ni halali kuliwa. Naam, Islam inasema kama mbwa amelamba katika chombo fulani, basi hicho kisafishwe vizuri sana kabla ya kukitumia, kwani bila kukisafisha mtu anaweza kupata ugonjwa. Padre hakutaja paka; lakini naye akilamba chomboni, lazima kukisafisha ili kulinda usafi kwa ajili ya afya.

## Kukoga

Baada ya mke na mume kujuana, wote wawili wanapaswa kukoga. Na sababu yake ni kwamba kitendo hicho kilichohalalishwa na Mungu kinamwathiri mtu sana mno mwili wake na mawazo yake. Na baada ya kitendo hicho ni muhimu kutuliza mawazo na viungo vya mwili. Na njia iliyo nzuri na rahisi ni kukoga, kwani maji huburudisha mwili na hutuliza mawazo. Vilevile uchafu mwingine unaotoka mwilini husafishwa kwa

kukoga. Huu ni ustaarabu mzuri, hatuelewi kwa nini Wakristo wanauchukia. Kwa neno zima Islam haikihesabu kitendo cha mke na mume kujuana kuwa kichafu. Bali kinyume chake Wakatoliki wanaona tendo hilo kinyume cha utawa na ucha Mungu, ndiyo maana wasiooa huhesabiwa 'Watawa'. Basi ile lawama yao wameitupia Islam kwa dhuluma.

*Nyamafu* ni haramu kula kwani inaharibu afya. Siyo najisi, kwa sababu Islam inaruhusu kuigusa, kuchuna ngozi yake na kuitumia hiyo kwa kutengeneza viatu na vitu vinginevyo.

Ni uzushi wa padre kusema kuwa katika mwezi wa Ramadhani kila chakula kinanajisika kwa Mwislamu ndiyo maana hawezi kukigusa. Mwislamu anaruhusiwa kukigusa chakula. Anakinunua sokoni, anakipika, anakiweka mbele ya mgeni (kwani mgeni hafungi), au anawapa watoto wake. Ila tu hakili, kwani amefunga saumu. Je, hii ndiyo kusema kwamba chakula kimekuwa najisi? Yesu alipohangaishwa na Shetani kwa siku arobaini nyikani na alifunga saumu kwa hizo siku, je, chakula chake kilinajisika? Kama kilichafuka kwa Yesu, sawa; lakini kwa Mwislamu hakichafuki.

## Kabadili Nia

Padre mara kwa mara anauliza je, Mungu Amebadili nia? Safari hii sisi tunamwuliza, kama Mungu Aliweka

sheria ya unajisi katika Torati, je, baada ya ujaji wa Yesu Mungu Amegeuza nia? Je, "yu geugeu?"

Ifahamike ya kwamba Islam *haikatazi nyama ya sungura* wala ya ngamia, ijapokuwa Torati tuliyo nayo siku hizi inakataza.

*Ukoma* ni ugonjwa tu wala sio unajisi. *Maiti* si kitu najisi; lakini anaogeshwa kwa ajili ya usafi ambao zaidi unawafaa walio hai ambao wanamshughulikia kumzika na wengineo walio karibu.

## Unajisi Unaingia

Badala ya kuona haya, padre ametangaza kwa fahari ule usemi wa Yesu usemao:

> "Hakuna kilicho nje ya mtu ambacho kikimwingia kinaweza kumtia unajisi." (Mk. 7:15)

Pombe imehesabiwa ni chakula kizuri na Wakristo wengi; lakini pombe ikiingia ndani ya mtu 'kutoka nje,' humchafua sana mpaka mtu anaweza kumtukana hata Mungu au kuwatusi wazazi na waalimu au mapadre wake. Katika hali ya kulewa anaweza kuzini pia. Je, si pombe iliyoingia ndani ambayo imemtia unajisi? Kauli hii ni hila tu ya kujihalalishia vilivyo haramu!

Padre amesema:

> "Kuvitumia ovyo vyombo vya mwili siyo kutenda machafu hasa ila ni kuharibu au

kukufuru matakatifu." (uk. 116)

Je, kukufuru matakatifu siyo kutenda machafu?

**Ndoto ya Petro**

Wakristo wamejitafutia hila kwa kuhalalisha kilicho haramu kwa kutafsiri vibaya ndoto ya Petro. Petro aliletewa katika ndoto wanyama wa kila aina, safi na najisi pamoja, na akaambiwa, 'Petro, uchinje ule' (Matendo 10:13). Bila shaka hii haina maana kuwa awachinje wanyama wote na kuwala. Sauti ilikuwa na maana kuwa achinje sawa na haja yake na atumie. Na maneno, "vilivyotakaswa na Mungu, usiviite wewe najisi" (Mdo. 10:15) yanahakikisha waziwazi ya kuwa kati ya wale wanyama, yeye alitakiwa kumchinja aliye safi na kula. Lakini Petro, inaonekana, akafikiri kwamba anaambiwa kuwala wanyama wote safi na najisi pamoja – jambo ambalo haliwezekani, kwani hata jitu kuu hawezi kumaliza wanyama wote wenye miguu minne pamoja na ndege wa kila aina na watambaao wote!

Ama Petro alivurugika mawazo ndani ya ndoto kwa sababu alikuwa na njaa nyingi wakati huo; bali akaona onyesho hili hali roho yake ikizimia; au waandishi, sawa na tabia yao, wamevuruga ndoto yenyewe walipoandika ndani ya kitabu ili kuhalalisha kilichoharamishwa na Mungu. Na Kurani imewalaumu sana waandishi wa Biblia kwa ajili ya kugeuza maneno ya kweli.

## Kuungama au Kutawadha

Padre amedharau kutawadha kabla ya sala, ila anasifu kusimama wima na kuinamisha kidogo kichwa na kujuta juu ya dhambi zake na kuungama kabla ya sala (tazameni picha uk. 117 wa kitabu chake). Kumbe kitendo hicho nacho ni cha kimwili jinsi alivyofikiri kutawadha kuwa kitendo cha kimwili. Je, kuinamisha kichwa si kitendo cha kimwili?

Tunamwuliza padre ya kuwa kama maji hayafai kuondoa dhambi, kwa nini anawabatiza watu kwa kuwamiminia maji au kuwazamisha ndani ya mto? Je, hayo maji yanawaondoleaje dhambi zote zile walizowahi kutenda hapo zamani?

Padre ameandika kwamba mbele ya Mungu unajisi ni dhambi ya moyo, hata kama maungo hayahusiki: Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake (Mt. 5:28). Hii ni sawa, na tunakubali hiyo katika dini yetu (Al-Mu'min 40:20). Lakini hiyo haimaanishi kuwa aliyemtazama mwanamke kwa tamaa ni sawa na yule aliyezini kimwili; kwani aliyezini ametenda maovu mawili: Kutamani mwanamke na kisha kutekeleza tamaa yake mbaya; ilhali aliyemtamani tu pekee ametenda dhambi moja.

Haitoshi kusafisha nje ya kikombe na chano (Mt 23: 25). Ni kweli. Lazima nje na ndani ziwe safi. Lakini

kuudharau usafi wa nje, ni kujichafua kiroho pia; kwani takataka za nje ya kikombe hazitabaki nje tu bali vidudu vya uchafu vikitembea nje ya kikombe vitaingia ndani pia. Kwa hiyo, katika mambo yote tuangalie usafi wa mwili na wa roho pamoja.

## Somo 10. Hali ya Wanadamu Tangu Asili

Padre amejaribu kuonyesha ubora wa Biblia juu ya Kurani; lakini maelezo aliyotoa yanaitilia aibu Biblia. Amesema:

> "Tangu asili wanadamu wanataka kusogea makao ya juu kwa Mungu, lakini Mungu Anawatawanya." (uk. 119)

Hii ni dhuluma kubwa ya Mungu kuwatawanya watu na kuchafua umoja wao.

Mungu Angefurahi kuona kwamba wanadamu wanatia bidii ili kupata makao ya juu Kwake Yeye, na Angewasaidia zaidi; lakini Akawachafua na kuwatawanya. Hili haliwezi kuwa fundisho lenye fahari kwa wafuasi wa Biblia. Kinyume chake Kurani Tukufu inasema:

> "Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia zetu. Bila shaka Mungu Yu pamoja na wafanyao mema." (Al-'Ankabuut 29:70)

Ni sawa kwamba ukombozi hutoka kwa Mungu; lakini siyo maana yake watu wasijitahidi kumpata Mungu. Watu wakionekana na shauku ya kumpata Mungu, Yeye Anapaswa kuwaongoza badala ya kuwachafua na kuwatawanya.

**Adamu**

Ni uzushi kusema kuwa Adamu alitaka kujifanya sawa na Mungu. Kama alitaka kujua 'mema na mabaya' (Mwa. 3:5), siyo maana yake alitaka kujisawazisha na Mungu. Bali Mungu Mwenyewe Anataka wanadamu wapambanue mema na mabaya, na kisha wajitenge na mabaya bali washike mema. Je hili ni kosa ama ni kuongoka?

**Mungu Hafuti Kazi Yake**

Kusema kuwa watu wabaya wanapoleta machafuko duniani, Mungu Analazimika kufuta kazi Yake, ni kauli mbovu. Mungu Hafuti kazi Yake. Kazi Yake huwa njema, bali Yeye Hufuta ubaya. Gharika la zama za Nuhu halionyeshi kuwa Mungu Alifuta kazi Yake; bali Akafuta uovu.

**Mungu Hataki Uovu**

Siyo imani ya Kiislamu ya kuwa Mungu Anataka kuona dunia katika hali ya uovu. Bali Kurani inafundisha:

> "Naam, anayechuma ubaya na makosa yake yakamzunguka, basi hao ndio watu wa Motoni;

> humo watakaa." (Al-Baqara 2:82)
>
> "Wala msifanye uharibifu katika nchi ikiisha tulia." (Al-A'raaf 7:57)
>
> "Bila shaka Mwenyezi Mungu Hawapendi wafisadi." (Al-Qasas 28:781)

Kwa kweli watu wanapotenda maovu, Mungu Huleta mitume ili kufuta maovu. Watu wasipowasikiliza na kujinyosha, wanaadhibiwa. Hii yaonyesha kuwa Mungu Anapenda mema na Anao mpango wa kuyaimarisha kati ya watu.

Ile aya isemayo: "Kama Akipenda Atawaondoeni, na

kuwaweka wengine Awapendao baada yenu" (Al-An'aam 6:134) haionyeshi kuwa Mungu Anaridhika na maovu, bali kinyume chake inaonyesha kuwa wasipojinyoosha watu, Atawaondoa kwa adhabu na kuleta wengine walio wema.

**Amri za Mungu**

Padre ameshindwa kuelewa maana ya aya isemayo:

> "Mwenyezi Mungu Huwatakieni yaliyo mepesi, wala Hawatakieni yaliyo mazito" (Al-Baqara 2:186).

Kwa hakika maana yake ni kwamba sheria za Mungu haziji ili kuwasumbua watu bali huwa kwa faida ya

binadamu kiroho na kimwili. Ndiyo kusema kwamba sheria siyo *'laana'* isemavyo Biblia, bali ni rehema, raha na faraja. Kwani laana ni kurudi nyuma bali raha na faraja ni kupata maendeleo.

## Mfano wa Dunia

Mfano wa dunia ulioelezwa katika Kurani (Yuunus 10:25), unamaanisha ya kuwa mtu anapojivunia kazi yake kwa kuona shamba lake limestawi wala hamshukuru Mungu Aliyeleta mvua kwa kulistawisha shamba, hapo Mungu Huleta adhabu kwa asiye na shukrani bali ana majivuno. Ndivyo ilivyo hali ya mataifa yanayojivunia maendeleo yao. Yaani yanapoanza kuwa na majivuno ndipo huanza kurudi nyuma. Hatuelewi kwa nini padre ameshangaa juu ya mfano huu wa Kurani.

## Je Tukubali Uovu?

Padre ameuliza je, tukubali maovu yaliyopo duniani? Kisha anasema kuwa Kurani imeeleza hadithi nyingi za watu waovu, lakini haitoi sababu nzuri ya kukomesha uovu huo. Kumbe padre haelewi kuwa Kurani inapoeleza historia ya waovu kwamba waliangamizwa na Mungu kwa sababu hawakuwakubali mitume na kuacha maovu yao, Kurani inamaanisha nini. Mungu Anawasimulia visa hivyo ili watu wamkubali Mtume kwani kwa baraka ya uongozi wake wataweza kuachana

na maovu ya kila aina. Basi, dawa ya kufuta maovu ni kuwafuata mitume waletao Amri za Mungu ambazo Amri hizo zikitekelezwa mtu anaepukana na maovu.

## Neema Hutoka kwa Mungu

Padre ameandika kuwa kwa Mwislamu neema hutoka kwa Mungu. Tunasema, naam; kwa mfano, jua, mwezi, nyota, hewa, maji na vingine vingi vinavyoonekana duniani ni neema za Mungu navyo vimetoka kwa Mungu. Je, Mkristo anaamini vimetoka kwa Belzebuli? Lakini ziko neema zilizo kwa kila kiumbe na kuna zingine wanazopewa watu wema tu. Kwa mfano, wema ni neema inayopatikana kwa watu wanaompenda Mungu na kufuata Amri Zake.

Padre amesema kwamba kwa Mwislamu hata vita hutokea kwa amri ya Mungu; ameandika aya inayoeleza ushindi wa Waislamu katika vita ya Badr:

> "Ninyi hamkuwaua lakini Mwenyezi Mungu ndiye Amewaua." (Al-Anfaal 8:18)

Aya hii muradi wake siyo kwamba Mungu Akaleta vita hiyo; bali Wapagani walifunga safari ya maili 300 hivi kuja kuwashambulia Waislamu, ndipo Waislamu wakaidhinishwa na Mungu kujitetea. Kwa hiyo vita ikaletwa na Wapagani, siyo na Mungu. Naam, ndani ya vita Mungu Akawasaidia Waislamu mpaka wakapata ushindi. Aya inaelaza kuwa Waislamu waliokuwa

wachache wenye silaha hafifu hawangeweza kuwashinda Wapagani waliokuwa wengi mara tatu kuliko Waislamu nao walikuwa na silaha nyingi na nzuri; lakini Mungu Akawasadia Waislamu.

Padre atasemaje juu ya Yesu aliyetamka:

> "Msidhani ya kuwa nimekuia kuleta amani duniani, la! Sikuja kuleta amani bali upanga." (Mt. 10:34)

## Ujinga, Maradhi, Ufukara

Islam haisemi tusiishughulikie dunia; bali kinyume chake inasema lazima tuishughulikie, hata tufunge ndoa ambayo inafikiriwa na kanisa Katoliki kuwa ni kitu kinichomzuia mtu asiweze kulitumikia kanisa vizuri, kwa hiyo imekatazwa kwa mapadre.

Islam inataka mtu ashughulike katika kazi za dunia kwa kujichumia riziki, na pia atie bidii kuondoa ujinga kwa kujielimisha, na kuisafisha dunia kwa kuyaondoa maradhi, na kuwasaidia maskini ili kuondoa ufukura. Lakini shabaha kuu iwe ni kuungana na Mungu kwa njia ya vitendo hivyo na vingine vya ucha Mungu na ibada.

Juu ya elimu, Kurani inafundisha kuomba daima: "Mola wangu, nizidishie elimu." (Twaa Haa 20:115)

Pia angalieni Al-Faatir 35:29, Az-Zumar 39:10, Al-Mujaadila 58:12. Mtume Muhammad[saw] aliagiza:

> "Kujielimisha ni wajibu wa kila Mwislamu, mwanamume kwa mwanamke"; na "Jitafutieni elimu hata kama ipatikane huko Uchina."

Je, Yesu naye alisisitiza kupata elimu kiasi hiki? Kama Wakristo walianzisha mashule, ni shauri yao wenyewe siyo amri ya Yesu. Lakini Waislamu wanapoanzisha shule zao, huwa kwa agizo la Mtume[saw].

**Maradhi**

Kuhusu maradhi Islam imefunza waziwazi ya kuwa "*Li-kulli da'in dawa'un illal-maut*," yaani kwa kila ugonjwa kuna dawa, ila mauti. Ndiyo kusema kwamba Mwislamu hawezi kukata tamaa kuwa eti ugonjwa fulani hautibiwi; bali lazima ipo dawa yake ila tu wanadamu hawajaweza kuigundua. Fundisho hili linamhimiza binadamu kutia bidii na kutafuta dawa za kila maradhi.

Lakini tukisoma maisha ya Yesu, tunaona yeye hakuhimiza juu ya habari za kutibu maradhi; bali kinyume chake visa visivyo na msingi vimeelezwa na waandishi wa Injili kwa kuwatupa wanadamu katika ujinga na magonjwa ya daima. Injili inasema kuwa Yesu alikuwa akiwatolea watu pepo bubu na pepo mchafu. Mathayo anaeleza hadithi ya kwamba:

"Watu wawili waliingiwa na pepo mpaka hao wakawa wakali mno hata mtu asiweze kupitia njia ile" (Mt. 8:28).

Kwa kweli hii inaonyesha kuwa hao wawili walikuwa na wazimu, yaani walirukwa na akili. Huu ni ugonjwa tu, lakini Injili inaeleza ya kuwa waliingiwa na pepo wa aina fulani. Hii ni kuua kabisa elimu ya utibabu.

Isitoshe, kisa kinaendelea hivi kwamba:

> Yesu alipotaka kuwatolea hao watu pepo, pepo hawa wakamsihi Yesu kwamba baada ya kutolewa kutoka katika hao Wagerasi, waruhusiwe kuingia kundi la nguruwe waliokuwako mbali nao. Yesu akafanya hivyo, hata hao pepo walipotoka wakaingia katika nguruwe. "Na kumbe, kundi lote wakateremka kwa kasi gengeni hata baharini; wakafa majini." (Mt. 8: 32)

Ndiyo kusema pepo wawili wakagawanyika kuwa wengi hadi kila nguruwe akaingiwa na pepo mmoja na hatimaye nguruwe wote wakaangamia majini. Mafunzo gani haya, jamani? Ndiyo kufunza elimu ya utibabu kwa kuondoa maradhi duniani?

Ni dhuluma kubwa kuwaruhusu 'pepo' hao kuingia katika

kundi la nguruwe, kwani kwa njia hii akawapatia hasara kubwa wenye mali. Lakini watu wa nchi hiyo wakaonyesha tabia nzuri kwa kutokumpiga Yesu bali 'walimsihi aondoke mipakani mwao' (Mt. 8: 34).

Kwa kweli hicho chote ni kisa tu wala hakina ukweli ndani yake. Mahali pengine Yesu anaonekana akimtoa mtu mmoja pepo bubu ambaye pepo huyo alipomtoka, mtu huyo akaanza kusema (Mt. 9:32). Ndiyo kusema kwamba ububu husababishwa na pepo fulani mchafu. Lahaula! Padre anajivunia hii Injili eti imefundisha kuondoa ugonjwa duniani?

Ni sawa kuwa wakati mwingine kwa baraka za mitume baadhi ya wagonjwa hupona; lakini kusema kuwa maradhi huletwa na pepo wanaowaingia watu, ni kuibatilisha kila aina ya elimu ya utibabu. Mtume Muhammad[saw] alifunza msingi wa elimu ya utibabu aliposema:

> "Hakuna maradhi yote yote ila kuna dawa yake pia."

Na katika vitabu vya Hadithi za Mtume[saw] ipo milango maalum juu ya 'Utibabu', humo dawa kadha wa kadha zimeelezwa na Mtume[saw] kwa maradhi ya aina kadha wa kadha. Islam imefungua mpango wa elimu ya utibabu uliofungwa kabisa na Yesu. Naam, ni bahati mbaya sana ya kuwa baadhi ya Waislamu wasio na elimu ya Dini Tukufu ya Kiislamu, wamejishughulisha katika vitendo vya kumtoa mgonjwa Shetani kwa kumfuata Yesu jinsi ilivyoelezwa katika Injili. Islam haifundishi hiyo katu.

**Ufukara**

Padre anauliza kwamba Islam imeleta mpango gani kuwasaidia maskini na mafukara. Amechora picha ya

maskini katika kitabu chake anayepewa sadaka na Mwislamu (uk. 145) na picha nyingine inaonyesha vipofu wanaoelekezwa kuingia katika shule ya vipofu (uk. 146). Ndiyo kusema kwamba Islam inasaidia maskini kwa kuondoa shida yake ya muda lakini Ukristo unasaidia kwa njia ya shule ili maskini ajitegemee.

Kwa kweli Yesu hakufunza mafunzo ya aina hii, bali Wakristo wenyewe kwa hiari yao wameanzisha shule za vipofu ili mradi shule hizo ziwe ni kama chambo cha 'kuwavua' watu na kuingizwa katika Ukristo.

Hakika yenyewe ni kuwa kuna taabu za aina mbili za mafukara; taabu zinazotakiwa kuondolewa mara moja, na taabu zinazotakiwa kuondolewa kwa kudumu. Kama kipofu hana kazi na anasikia njaa, haina maana kumwonyesha shule; bali kwanza anahitaji kupewa msaada wa chakula, ndipo baadaye anapaswa kufundishwa ili kupata ufundi kwa kujitegemea katika maisha. Biblia haifundishi hivyo, bali Kurani inaeleza njia hizo zote mbili.

## Tiba ya Haraka

Kama mtu ameonekana na njaa wala yeye hana msaada wowote anastahili kusaidiwa mara moja:

> "Au kumlisha siku ya njaa yatima jamaa, au maskini hohe hahe." (Al-Balad 90:15-16)

Ziko aya nyingi ndani ya Kurani juu ya habari hii.

## Mpango wa Kudumu

Islam inataka kuwa hali ya dunia iwe nzuri kiasi hiki hata kwamba kila aina ya umaskini itoweke:

> "Hakika hutakuwa mwenye njaa wala hutakuwa uchi, na kwa yakini hutapata joto." (Twaa Haa 20:119-120)

Ndiyo kusema kuwa sawa na fundisho la Kurani, Mungu Alitaka tangu wakati wa Adam kuwa jamii ipatikane duniani ambamo mtu yeyote asiwe na njaa, yaani apate riziki ya kutosha; asiwe uchi, yaani apate nguo pia; asiwe na kiu, yaani mipango ya maji iwe mizuri sana nchini; wala asipate joto (wala baridi), yaani kwa kila mtu nyumba pia ipatikane. Na Mungu Alipoeleza habari hii ndani ya Kurani Alikuwa na maana ya kuwa mipango mbalimbali ianzishwe kwa kuinua hali ya jamii nzima mpaka maskini asipatikane.

Amri ya kutoa zaka pia ina shabaha hiyo hiyo. Ndiyo sababu ijapokuwa sadaka kila mtu anaweza kumtolea maskini, lakini zaka lazima apelekewe imamu, yaani kiongozi, kwani atafanya mipango mbalimbali kwa kuinua hali za wanyonge, maskini na mafukara. Shabaha ya zaka ilivyoelezwa ndani ya Kurani inaonyesha ya kuwa fedha hizo siyo tu kwa kuwatolea maskini taslimu kwa kuwaondolea njaa kwa muda bali viwanda, shule na

mipango kadha wa kadha inatakiwa kuanzishwa sawa na hali kwa kuwasaidia wanyonge ili waweze kujitegemea.

Mtume[saw] kwa kitendo alifundisha habari hii. Alipofikiwa na maskini, alimwelekeza kwenda porini na kukata kuni na kuziuza sokoni. Mtu huyo akawa na hali nzuri sana katika muda usio mrefu.

Mtume[saw] alichukia sana tabia ya kuomba-omba barabarani, hata kwamba masahaba walijiepusha kabisa na kuomba. Sahaba mmoja aliyekuwa amepanda farasi, fimbo yake ikaanguka chini. Ndugu mmoja aliyekuwa pale alipotaka kumsaidia, sahaba huyo akamkataza bali mwenyewe akateremka kutoka kwenye farasi na akaokota fimbo yake huku akisema:

> "Mtume[saw] hakupenda tabia ya kuomba-omba."

Je kweli Yesu naye ametoa mafunzo ya aina hii? Je, Yesu anawahimiza watu wafanye kazi ili wajitegemee au anasema yafuatayo:

> "Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu mvae nini … Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti … Msisumbuke, basi, mkisema, Tule nini? au Tunywe nini? au Tuvae nini? … Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe." (Mt. 6:25-34)

Kwa hiyo padre amejibiwa na Yesu mwenyewe kuwa tujitahidi kuzalisha mali, kustawisha mashamba, kutengeneza viwanda vya nguo na vinginevyo ama tuishi kama ndege wanaolishwa na Mungu bila wao kulima (Mt. 6:26).

Juu ya mauti tuelewe kuwa hayo ni ya aina mbili. Mauti ya kiwiliwili, hayo hayana budi yatokee tu kwa kila kiumbe pamoja na Yesu. Na pili ni mauti ya roho, hayo yanapatikana kwa waovu wamkanao Mungu na Mtume wake. Lakini hao wafu wa roho watahuishwa kwa kutibiwa ndani ya jahanamu iliyo kama hospitali kwa wagonjwa wa roho na wafu wa roho. Kwa hiyo kila mtu ataponywa tu – moja kwa moja atakapomfuata mtume, au kwa kupitia jahanamu.

**Kukombolewa**

Kuhusu wokovu, padre amesema ya kwamba 'kwa Waislamu hakuna kukombolewa' (uk. 121), ilhali shabaha yenyewe ya ujaji wa Kurani ni kumkomboa binadamu katika dhambi na uasi. Mwenyezi Mungu Huwaokoa watu kwa njia ya mitume. Wanaowakubali wanaokolewa:

> "Hata mitume walipokata tamaa (na makafiri) wakadhani kwamba wameambiwa uwongo, msaada wetu ukawafikia, basi akaokolewa Tuliyemtaka. Na haiondolewi adhabu Yetu kwa watu wakosefu." (Yuusuf 12:111)

Ndiyo kusema kwamba Mungu Akawaokoa wema ila wakosefu hawaokolewi bali wanaadhibiwa maadamu hawawi wafuasi wa mitume.

> "Enyi watu wangu, mimi nina nini, nawaiteni kwenye **wokovu** nanyi mwaniita kwenye Moto! Mnaniita nimkufuru Mwenyezi Mungu na kumshirikisha na yule ambaye simjui, nami nawaiteni kwa Mwenye nguvu, Msamehevu" (Al-Mu'min 40:42-43).

Ilimradi, Kurani inawaita watu kwenye wokovu, lakini wokovu huo utapatikana kwa kuwafuata mitume na sheria zao walizoleta toka kwa Mungu. Naam, hatuamini kwamba wokovu unaweza kupatikana kwa kuamini kuuawa kwa binadamu fulani msalabani.

**Kifo**

Kifo cha roho ni kibaya; lakini kifo cha kiwiliwili ni jambo la lazima, kwani ndiyo njia ya kuhamia penye maendeleo makubwa zaidi ya roho. Yesu hakushinda mauti kwa kumfufua Lazaro, kwani hata kama alifufuliwa, lakini si baadaye alikufa tena? Au naye akapaa mbinguni? Hata msalabani Yesu hakuyashinda mauti, kwani yalipomkurubia tu akapiga, kelele:

> "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha!"

Katishika kweli kweli. Ndipo Mungu Akamhurumia na kumwokoa kwa ajili ya maombi yake asife kifo kibaya cha laana. (Waebrania 5:7)

Padre amewatania Waislamu akisema kuwa sawa na imani ya Waislamu mwanadamu anahitaji mwongozi amwongozaye katika **utii** (uk. 121). Ebu someni jinsi Yesu alivyookolewa kwa ajili ya Utii tu:

> "Yeye, siku hizo za mwili wake, alimtolea yule, awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti, maombi na dua pamoja na kulia sana na machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu; na ingawa ni Mwana, alijifunza **kutii** kwa mateso hayo yaliyompata." (Waebrania 5:7-8)

Ndiyo kusema kwamba Utii ni kitu kikubwa hata kwamba Yesu akajifunza hicho kwa njia ya kuvumilia mateso, ndipo akakombolewa. Basi Wakristo wanawezaje kukombolewa bila ya kutii?

## Hali ya Giza

Ni sawa aliyosema padre ya kuwa Yesu aliwatoa watu katika giza, kwani kila mtume na nabii hutumwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kila nabii huwa nuru kutoka kwa Mungu. Ila tu kwa kuwa Yesu alitumwa kwa Wana wa Israeli pekee, hivyo yeye alikuwa nuru kwa Waisraeli peke yao. Musa pia akaleta nuru kwa njia ya Torati:

> "Hakika sisi Tumeteremsha Torati yenye mwongozo na nuru." (Al-Maaida 5:45)

Mtume Muhammad[saw] alikuwa nuru kwa watu wote, kwa kuwa alitumwa kwa mataifa yote.

> "Mwenyezi Mungu ni Nuru ya mbingu na ardhi; mfano wa nuru Yake (yaani sheria ya Kiislamu) ni kama kishubaka kilichomo taa: taa ile imo katika tungi: tungi lile ni kama nyota ing'aayo, inayowashwa katika mti uliobarikiwa wa mzeituni, **usio wa mashariki wala magharibi**; ni karibu mafuta yake kung'aa ingawa moto haujayagusa, nuru juu ya nuru Mwenyezi Mungu Humwongoza kwenye nuru Yake Amtakaye, na Mwenyezi Mungu Hupiga mifano kwa watu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu." (An-Nuur 24:36)

Ndiyo kusema kwamba nuru hii ya Kiislamu siyo kwa ajili ya mashariki pekee wala kwa ajili ya mataifa ya magharibi pekee, bali ni kwa watu wote.

Tena Kurani inasema juu ya Mtume[saw] na Kurani Tukufu:

> "Enyi watu, bila shaka imewafikieni dalili kutoka kwa Mola wenu na Tukawateremshieni **nuru** dhahiri." (An-Nisaa 4:175)

> "Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na **nuru** ambayo Tumeiteremsha." (At-Taghaabun 64:9)

> "Kwa (Kitabu hicho) Mwenyezi Mungu Humwongoza mwenye kufuata radhi Yake katika njia ya salama, na Huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye nuru kwa idhini Yake." (Al-Maaida 5:17)

Kwa hiyo, Waislamu wamfuatao barabara Mtume Muhammad[saw] wamo katika nuru, na Wakristo pamoja na watu wote wanakaribishwa kuingia katika hiyo nuru.

## Somo 11. Mwanadamu ni Mkosefu, Mwenye Dhambi

Kila Mwislamu atashangaa kujua ya kuwa padre anafikiri ya kwamba Mwislamu hatendi kitendo kwa kumpendeza Mungu au haepukani na jambo kwa kuwa lamchukiza Mungu; bali anatenda kwa sababu sheria imemlazimisha. Ukweli ni kwamba Mtume Muhammad[saw] alifundisha:

> "Vitendo hupimwa sawa na nia ya mtu." (Bukhari).

Yaani hata kama kitendo kwa nje kinaonekana ni kizuri, lakini kama nia ni kuonwa na watu, kitendo hicho hakifai mbele ya Mungu.

Kurani imeshuka ili mtu apate radhi ya Mungu kwa kuifuata:

> "Kwa (Kitabu) hicho Mwenyezi Mungu Humwongoza mwenye kufuata **radhi** Yake katika njia za salama." (Al-Maaida 5:17)

Yaani kuifuata Kurani au kumtii Mungu sawa na sheria Yake ni njia tu ya kupata Mapenzi Yake na Radhi Yake. Radhi ya Mungu yaani furaha na upendo wa Mungu ni kitu kikuu:

> "Na radhi ya Mwenyezi Mungu ndiyo kubwa mno." (At-Tauba 9:72)

Matendo ya Waaminio husababishwa na upendo wa Mungu:

> "Na huwalisha chakula maskini na yatima na mfungwa kwa mapenzi Yake. (Husema): Tunawalisheni kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu tu." (Ad-Dahr 76:9)

Ni sawa kwamba Mungu Ameamrisha kuwalisha wenye njaa, na Waislamu wanatii amri ya Mungu, lakini shabaha katika kutii ni kupata mapenzi ya Mungu na radhi Yake.

Kwa jumla ni kuwa amri za Mungu au makatazo Yake huwa kwa faida ya binadamu kiroho na kimwili, na mtu akimtii Mungu Amri Yake hufaidika kiroho na

kimwili, na faida kubwa zaidi ni kupata Mapenzi na radhi ya Mola.

**Utajuaje?**

Padre amesema kuwa Mkristo hatendi tendo kwa kuangalia hilo ni halali au haramu, bali anaangalia kama linampendeza Mungu au linamchukiza. Lakini swali ni kwamba utajuaje hilo lampendeza au halimpendezi? Bila shaka kufuata maamrisho ndiyo kunampendeza na kutenda Aliyoyakataza kunamchukiza. Haiwezekani kuvunja amri Yake kumpendeza Yeye. Kwa hiyo, Mkristo akitaka kutenda sawa na upendo wa Mungu lazima afuate sheria ya Mungu. Bila hiyo atatangatanga tu na kutenda haramu huku akijipumbaza anampendeza Mungu eti yu mwana wa Mungu si mtumishi wake; ilhali Yesu mwenyewe alikuwa 'mtumishi wa Mungu'. (Mt. 12:18). Kurani pia inamwita kuwa mtumishi wa Mungu (An-Nisaa 4:173). Kwa hiyo, Wakristo wasichukie kuwa watumishi mbele za Mungu.

Padre amekariri tena kuwa Kurani inafundisha kwamba Mungu Anaweza kubadili nia Yake na akaandika aya ya Kurani (Al-Baqara 2:107). Aya hiyo haina ile maana aliyotaka padre kuivika. Bali maana yake ni kuwa Mungu Alitoa baadhi ya amri fulani kwa sababu maalum, na zile sababu zilipotimia Akaifuta hiyo amri na kuleta bora zaidi. Au kama amri ilikuwa kwa siku zote lakini watu

walisahau, Mungu Aliileta hiyo tena ndani ya Kurani. Nia ndiyo ile ile ya kuwa watu wapate mapenzi Yake na ukaribu Wake. Na kwa kuwa Mungu Anajua zaidi njia ya mtu kupata mapenzi Yake, hivyo Anazieleza hizo njia (yaani sheria hizo) kwa kuleta mitume.

## Kumpenda Mungu na Jirani

Padre amekariri mara nyingi kwamba amri kuu ya Yesu ni kumpenda Mungu na jirani, na kwamba huku ndiko kutimiliza sheria. Kumbe amri hiyo ya kumpenda Mungu na jirani siyo amri ya Yesu bali ni amri ya Torati ya Musa. Tazameni Agano la Kale: Kumbukumbu (6:5) na Walawi (19:18). Yesu mwenyewe amekubali kuwa hizo ni amri za Torati:

> "Mmoja wao, mwanasheria, akamwuliza, akimjaribu, Mwalimu, katika Torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea Torati yote na manabii." (Mathayo 22: 35-40)

Ndiyo kusema kwamba kumpenda Mungu na kumpenda jirani ni kiini cha Torati nzima, yaani hilo ndilo lengo. Na ili kulipata hilo lengo maamrisho na

makatazo yametolewa na Torati. Aliyekuambia lengo kuu, ndiye awezaye kukuelekeza kwenye njia ya kulipata hilo lengo vizuri zaidi. Basi iko haja ya sheria. Sheria siyo *'laana'* bali ni rehema kwa kumwongoza binadamu kwenye kupata lengo kuu la maisha yake.

## Kuishi Kitawa

Padre bali Wakristo wengine pia wanatumia neno *'utawa'* katika maana mbaya sana. Utawa ni utakaso na ucha Mungu. Maisha ya kitawa ni maisha mema. Mtu atimizaye haki za viumbe na haki za Mungu ndiye mtawa. Siye yule anayenuia kutokuoa maisha mazima; kwani tendo hili ni kinyume cha matakwa ya Mungu. Kurani inasema:

> "Na uruhubani (useja) wameubuni wenyewe. Sisi Hatukuwaandikia ila (walibuni) kuitaka radhi ya Mwenyezi Mungu tu, lakini hawakuufuata kama inavyotakiwa kuufuata." (Al-Hadiid 57:28)

Yaani Aliwaandikia kuitaka radhi ya Mungu; useja wakaubuni wenyewe, kisha wakashindwa kukaa useja kweli kweli, 'bali wengi wao ni waasi.' (Al-Hadiid 57:28)

## Dhambi Moyoni

Wote wanaamini kuwa chanzo cha dhambi ni roho. Lakini siyo maana yake kuwa vitendo usivinyoshe. Ni

sawa ya kuwa aliyemtazama mwanamke kwa tamaa ameisha mzini moyoni. Lakini je ni sawa yule aliyemtazama mwanamke kwa tamaa, na yule aliyemzini pia kimwili? Sivyo; bali aliyezini kidhahiri ametenda dhambi mbili; kwanza dhambi ya kuwa na tamaa, na kisha kwa ajili ya tamaa hiyo kumnajisi kiumbe mwenzake. Nia haionekani ila kwa njia ya vitendo, kwa hiyo lazima sheria iweke mipaka ya dhahiri ili kumsaidia mtu kujinyosha nia pia.

Si sawa kusema kuwa ushike sheria ya upendo tu kisha ufanye upendavyo. Kwani, kama Mkristo anampenda mwanamke jirani aliye mke wa mtu na mwanamke huyo naye ameridhika kulala naye, je itakuwa sawa eti kwa sababu yule mwanamke jirani naye akaridhika na tendo hilo chafu la zinaa? Padre hatamlaumu Mkristo huyo, kwani huyo hajamchukia jirani bali alimpenda na akatenda naye sawa na furaha yake. Lakini Torati itasema, yu mzinzi, aadhibiwe.

Tena kama amri kuu ni kumpenda Mungu na jirani tu, je yule asiye jirani utamtendeaje? Islam inafundisha kuwatendea viumbe wote vizuri.

## Mungu Halazimishwi

Padre amesema kuwa kama Mungu Hataki kumsamehe mtu fulani, basi Mungu Hawezi kulazimishwa kumsamehe. Anataka kusema kuwa Mungu

Anawabagua watu; huyu amesamehewa na huyu hakusamehewa eti kwa sababu tu Mungu Akapenda hivyo. Ni sawa kuwa hakuna awezaye kumlazimisha Mungu. Lakini Mungu Humsamehe kila anayesahihisha mwenendo wake (Al-An'aam 6:55). Na kama mtu hajisahihishi bali anaomba tu msamaha kwa midomo, huyo hasamehewi, kwani msamaha wa aina hiyo utakuwa bure kama mtu hajirekebishi.

**Sadaka**

Padre amesema kuwa Yesu anataka tutoe sadaka kwa moyo mwema. Hata Kurani inasema kuwa:

> "Nyama zao (dhabihu) hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia utawa wenu." (Al-Hajj 22:38)

Vilevile Waislamu wanaambiwa kutoa sadaka kwa ajili ya Mapenzi ya Mungu (Ad-Dahr 76:9).

**Saumu**

Kama Yesu alifunga kwa siku arobaini, Wakristo nao wanapaswa kufunga siku hizo; wamfuate Bwana wao. Lakini hawataki; wanataka zaidi anasa za dunia. Wametosheka na mateso ya Yesu; wenyewe hawataki kuteseka hata kwa kufunga. Padre amesema kuwa Waislamu wanapofunga hawakumbuki dhambi. Padre atambue kwamba Kurani inaeleza waziwazi ya kuwa

shabaha ya kufunga ni kumcha Mungu (Al-Baqara 2:184). Yesu alipohangaishwa kwa kujaribiwa na Shetani, akasalimika kwa kufunga saumu siku arobaini. Hapo Ibilisi alimwacha na 'akaenda zake kwa muda' (Luka 4:13). Ndiyo kusema Ibilisi atarudi tena kumshawishi, kwani alikwenda kwa muda tu. Basi kama Wakristo wanataka kusalimika na vishawishi vya kishetani wanapaswa kufunga, lakini kila mara, kwani Shetani hakuondoka kwa kudumu, bali kwa muda. Ndani yake kuna onyo kwa wafuasi wa Yesu. Kwani wakati mwingine mambo anayoambiwa nabii, hutimia kwa wafuasi wake.

## Somo 12. Hukumu ya Ahera Dhambi Husamehewa

Padre amesema kuwa katika Uislamu baadhi ya dhambi hazisamehewi, kama vile ukafiri na kuua Mwislamu kwa makusudi. Kwa kweli, kila dhambi husamehewa sawa na fundisho la Kurani. Alipofika Mtume[saw] watu karibu wote walikuwa makafiri, lakini waliposilimu wakasemehewa dhambi zote.

> "Sema, enyi watumishi wangu mliojidhulumu wenyewe, msikate tamaa katika rehema za Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu Husamehe dhambi zote; hakika Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu." (Az-Zumar 39:54)

Basi, sawa na Islam, dhambi zote husamehewa. Lakini sharti ya msamaha ni kuwa mtu atubu na kujirekebisha barabara. Ile aya isemayo: "Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehi kushirikishwa naye, na Husamehe yaliyo nyuma ya hayo kwa Amtakaye" (An-Nisaa 4:49) maana yake ni kuwa ushirikina ni dhambi kubwa zaidi kuzishinda zote zingine, na haiwezi kusamehewa kama mtu amekufa bila kuachana kabisa na dhambi hiyo; lakini dhambi zingine Mungu Anaweza kusamehe hata kama mtu alikufa bila ya kutubu – lakini kwa Amtakaye; yaani Akiona ya kwamba mtu huyo alitenda dhambi kwa bahati mbaya tu wala hakuwa na nia sana. Lakini mtu akiomba msamaha mwenyewe katika maisha ya dunia kwa moyo wote, atasamehewa kila dhambi.

Hata wale watakaokwenda Motoni, watatolewa baada ya kutibiwa kiroho, na wataingia katika msamaha wa Mola na kupata maisha ya Peponi, kwani "Rehema yangu hukienea kila kitu." (Al-A'raaf 7:157). Adhabu ya Motoni siyo ya milele kinyume na alivyoandika padre (uk. 131).

Padre ameona fahari kusema kuwa sawa na fundisho la Ukristo dhambi zote zinasamehewa, ila tu kukataa msamaha. Lakini Yesu anasema kwamba:

> "kila dhambi na kila neno la kufuru watasamehewa wanadamu, ila kwa kumkufuru Roho

> hawatasamehewa. Na mtu yeyote atakayenena neno juu ya Roho Mtakatifu hatasamehewa katika ulimwengu wa sasa wala katika ule ujao." (Mathayo 12:32)

Kumbe hata ahera mtu huyo hatasamehewa na atatupwa katika jahanamu kwa milele! Hiyo ndiyo huruma ya Baba?

**Kadiri ya Mungu**

Padre ametaja tena Kadiri ya Mungu ambayo tumeisha eleza hapo nyuma. Huko tulieleza pia ya kwamba hata Yesu aliamini kadiri aliposema kuwa aliandikiwa mateso yake mapema. Vilevi1e ieleweke ya kwamba hata kama Yesu angelijaribu kuepukana na mateso hayo, asingeliweza kwani ilitakiwa "maandiko ya manabii yatimizwe" (Mt. 26:56). Yesu alifundisha 'hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote' (Mt. 10:30).

Isitoshe, kwa sababu ya maneno hayo ya Injili, baadhi ya viongozi wa kanisa waliamini sana 'Kadiri' ya Mungu katika zama zilizopita. Kwa mfano Calvin alifundisha kabisa ya kwamba:

> "Kila tukio latokana na mapenzi ya Mungu."
>
> (Historia ya Ukristo, J 2, uk. 112, Dean Peterson)

Tena kitabu hicho hicho chasema:

> "Predestination (Kadiri) twaseme ni amri ya

> milele ya Mungu ambayo kwayo Ameamua Mwenyewe matokeo ya milele kwa kila mwanadamu ... Uzima wa milele umeamuliwa kwa wengine na hukumu ya milele kwa wengine. Kila mtu amekwisha kuwekewa mojawapo — uzima au mauti." (uk. 112)

Zaidi ya hayo imeandikwa mumo humo:

> "Mkazo wa Calvin si ajabu wala si mpya." (uk, 112)

Ndiyo kusema kwamba hii ilikuwa ni imani ya Wakristo tangu zamani.

Ikumbukwe kwamba hiyo siyo imani ya Waislamu. Kwetu sisi kuna namna nne za Kadiri ya Mungu, nazo ni hizi:

(1) ***Kadiri ya Kawaida*** ya Kimaumbile: Maana yake ni kwamba Mungu Amevipa vitu mbalimbali sifa kadha wa kadha zinazodhihirika kwa hivyo daima. Kwa mfano, moto unaunguza; maji yanazima moto. Moto kuandikiwa kuwa utaunguza maana yake ni kuwa Mungu Ameupa sifa hiyo. Pia mzabibu hauwezi kuzaa embe. Mambo kama hayo yanaingia katika namna ya kwanza ya Kadiri, yaani Kadiri ya Kawaida ya Kimaumbile.

Safari moja Khalifa Umar[ra] alipokuwa akiliendea jeshi la Kiislamu lililokuwa mahali fulani, njiani alipopata habari ya kwamba huko kwenye jeshi ugonjwa wa tauni

umezuka, pale pale akarudi. Alipoambiwa, 'Mbona unaikimbia Kadiri ya Mungu,' kasema Khalifa, 'Naam nakimbia kadiri ya Mungu na kuikimbilia kadiri ya Mungu.' Yaani Kadiri (kanuni) ya Mungu ni kuwa atakayekwenda katika mahala penye tauni ataugua, na pia ni kadiri ya Mungu ya kwamba mtu atakayejiepusha na kuingia katika mahala kama hapo atasalimika na tauni.

*Kadiri Maalum ya Kimaumbile*: Hii ni kadiri ambayo hutokea ilhali haitazamiwi. Kwa mfano, Mungu Anaamua kumpatia mtu fulani mtoto. Basi huyo mtu anapata tu hata kama mkewe ni tasa, kama vile Zakaria alivyopata mtoto Yohana ilhali mkewe alikuwa mzee na tasa, bali na Zakaria naye alikuwa mzee sana.

*Kadiri ya Kawaida ya Kidini*: Yaani ni kanuni ya dini kwa jumla inayofanya kazi duniani. Kwa mfano, ni kadiri ya kwamba ikiwa mtu atasali na kufunga saumu na kutimiza matakwa yote ya dini kwa nia safi, hapo lazima atapata maendeleo ya roho na polepole ataweza kuungana na Mungu. Asipofanya hivyo, hataweza kumkurubia Mola. Wapo wezi walioachana na mambo yote mabaya, bali wakafuata dini, nao wakawa mawalii wacha Mungu sana.

*Kadiri Maalum ya Kidini*: Yaani Mungu Anamsaidia mtu kwa msaada Wake maalum na kumpa vipawa vyake mahususi. Kwa mfano nabii hulindwa na dhambi kutoka katika utoto wake.

Kadiri hizo za aina ya maalum hutendeka kwa njia ya sababu zinazoonekana au bila sababu kuonekana.

Zaidi ya namna hizo nne za Kadiri ya Mungu hakuna kadiri yoyote nyingine inayosingiziwa Islam. Mwenyezi Mungu Hamwamulii yeyote kwamba atende maovu.

**Kwenye Heri**

Padre amesema kuwa Yesu anaita kwenye heri. Kwa kweli kila nabii huita kwenye heri; Yesu naye aliita lakini kawaita Waisraeli tu.

**Tutaulizwa Nini?**

Padre amesema kuwa hatuwezi kuulizwa na Mungu kama Yeye Mwenyewe Alituandikia tufanye hivi na vile. Hii ni sawa; lakini tulivyoisha eleza nyuma, Mungu Hakutushurutisha kutenda bali Ametueleza njia ya wokovu kisha Ametuachia nafasi tutende kwa hiari yetu. Basi tutaulizwa kwa nini tulitumia hiari yetu vibaya. Na ile habari ya vita, maana yake ni kuwa Mungu Aliwasaidia Waislamu vitani kwa sababu walidhulu-miwa. Siyo kwamba Mungu Alileta vita. Hii tumeisha eleza nyuma.

Naam, ni sawa kuwa Kurani inafunza kwamba kila atakayetenda dhambi ndiye atakayeadhibiwa siyo mwingine badala yake. Lakini akiomba msamaha kwa nia ya kujirekebisha, atasamehewa.

## Tutahukumiwa lini?

Padre amesema kuwa Kurani inafunza kwamba tutahukumiwa siku ya Kiyama; lakini Wakristo wanaamini hukumu imeisha anza. (uk. 132). Kwa kweli Kurani inafundisha ya kuwa kwa baadhi ya makosa na dhambi mtu huadhibiwa hapa hapa duniani kiasi fulani, lakini hukumu kuu itakuwa baada ya kufa.

> "Hao watapata fedheha katika dunia na katika ahera watapata adhabu kubwa." (Al-Baqara 2:115)

Lakini adhabu ya ahera si ya milele. Hukumu katika dunia:

> "Akateremsha Kitabu kwa haki ili Ahukumu baina ya watu katika yale waliyohitilafiana." (Al-Baqara 2:214)

Na hukumu huko ahera:

> "Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yenu siku ya Kiyama katika yale mliyokuwa mkihitilafiana." (Al-Hajj 22:70)

Na kwa hakika jibu la Kurani ni kamili zaidi, kwani tunaona baadhi ya watu wanaotenda maovu kama vile kuiba, kuua n.k.w.k. hawaonekani wameadhibiwa, basi hao wataadhibiwa siku ya Kiyama.

Padre amesema ya kuwa saa ile hakuna aijuaye ila Mungu, sawa na Kurani (Al-A'raaf 7:188); basi ajue ya kuwa hata Injili inasema ya kuwa:

> "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba." (Marko 13:32)

## Tutahukumiwa na Nani?

Tumeisha eleza nyuma ya kwamba Mungu ndiye Atakaye-

hukumu kati ya watu. Lakini mitume nao wanahukumu kwa amri ya Mungu sawa na sheria za Mungu:

> "Hakika tuliteremsha Torati yenye mwongozo na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mungu) waliwahukumu Mayahudi." (Al-Maaida 5:45)

Na kwa kuwa Yesu ni mfuasi wa Torati, hivyo naye amehukumu sawa nayo, lakini kawahukumu Wayahudi tu. Yesu hakuhukumu kwa kuwa yu Mwana wa Mungu, bali "naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu." (Yohana 5:27). Yaani akiwa ni nabii mmojawapo akahukumu walivyohukumu manabii wengine.

## Hukumu Itafanywaje?

Padre amekubali kuwa Kurani inaeleza jinsi ya kufanywa hukumu, lakini Injili 'haina maelezo', isipokuwa wema na wabaya watabaguliwa (Mt. 25:32). Kwa vyovyote ni wabaya watakaotengwa na wema sawa na Injili, bila kujali walikuwa Wakristo ama hapana.

Lakini baada ya ujaji wa Muhammad[saw] ni sharti la muhimu sana umwamini yeye pamoja na kutenda mema kwa kupata wokovu. Katika zama za kabla ya Muhammad[saw] ilikuwa ni lazima Waisraeli kumwamini Yesu na pia kutenda mema.

**Uje Bwana Yesu**

Ni kweli kabisa ya kwamba Yesu alitabiri kuja kwake mara ya pili duniani. Lakini ndugu Wakristo hawakuelewa dhamiri ya Yesu ijapokuwa alieleza waziwazi. Yesu alipoulizwa mbona Eliya aliyekwenda mbinguni hajarudi bado, basi wewe umekujaje kabla yake, akasema Yesu ya kuwa Yohana Mbatizaji ndiye Eliya, mwenye masikio na asikie (Mt. 11:13-141).

Sasa kama Yesu mwenyewe binafsi aje duniani, si ataulizwa, mbona, umekuja mwenyewe ilhali bishara ya ujaji wa Eliya ulieleza ya kwamba imetimia katika dhati ya Yohana? Kwa kweli ujaji wa Yesu mara ya pill ulikuwa na maana ya kuwa mtu mwingine badala yake atatokea jinsi alivyotokea Yohana badala ya Eliya.

Kwa hiyo, tunawatangazia Wakristo ya kuwa Yesu ameisha fika kwa sura ya Seyidna Ahmad[asw], mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, mwenye masikio na asikie. Alama za ujaji wake zimeisha timia tayari. Kama si yeye ni nani mwingine aliyetokea badala yake? Au, je, mtaendelea kung'ang'ania kumngoja yule

yule Yesu Mnazareti, jinsi Wayahudi walivyong'ang'ania kuona Eliya wa zamani? Lakini tambueni, wao mpaka sasa wanamngoja Eliya, lakini haji tena; ndivyo mtakavyochoka mkimsubiri Yesu mwenyewe atokee, lakini hatakuja katu.

Mnakaribishwa kupeleleza ukweli wa Islam na Seyidna Ahmad. Vipo vitabu chungu nzima vilivyotolewa kwa Kiswahili. Njooni mkapate uzima wa milele.

## Somo 13. Adhabu ya Milele kwa Wahalifu

Padre amekariri mara nyingine ya kuwa Kurani inafunza kwamba adhabu ya ahera itakuwa ya milele. Kwa kweli Kurani inafundisha kinyume chake.

> "(Jahanamu) ni makazi ya waasi, wakikaa humo karne nyingi." (An-Naba' 78:23-24)

Ndiyo kusema kwamba ijapokuwa adhabu hiyo itaendelea karne nyingi, lakini siyo ya milele. Na zaidi ya hayo amesema Mtume Muhammad[saw]:

> "Utafika wakati juu ya Jahanamu ambapo hakutakuwa humo yeyote, na upepo baridi utagonga milango yake." (Ma'alimut-Tanzi'il).

Lakini, Injili inatoa adhabu kali kiasi hiki ya kwamba malipo ya matendo maovu yaliyotendwa kwa muda maalum, yatakuwa ya milele hata milele (Mt. 25:41).

Pengine hiyo ndiyo njia ya Mungu kudhihirisha 'mapenzi' yake wanayojivunia Wakristo siku zote.

Padre amesema tena ya kuwa Kurani inaeleza kwamba "Heri ya mbingu siyo kuona Mungu." (uk. 135). Kwa kweli Kurani inatuambia ya kuwa:

> "Ewe mtu, hakika wewe ndiwe ufanyaye juhudi sana kwa Mola wako, basi utakutana naye." (Alinshiqaaq 84:7)

Maana ya aya (Al-A'raaf 7:157) siyo ya kuwa Mungu Atamwadhibu mtu yeyote amtakaye 'hata kama amefanya matendo mema,' asemavyo padre. Bali muradi wake ni kuwa Mungu Atakuwa na mamlaka ya kuadhibu au kusamehe; na bila shaka Mungu Hawezi kuamua ovyo, bali Ataangalia hali ya imani na vitendo vya mtu, ndipo Ataamua kumwadhibu au kumsamehe. Matakwa ya Mungu hayatatumika hovyo – jambo ambalo hata binadamu mwema hawezi kufanya.

Tena padre amesema ya kuwa aliyeandikiwa adhabu lazima atapewa tu hata akifanya mema. Hiyo siyo imani ya Kiislamu. Mtu haandikiwi afanye nini. Habari hii tumeisha eleza hapo kabla.

Agano la Kale linasema kuwa:

> "Sitatumia ukali wa hasira yangu; kwa maana mimi ni Mungu, si mwanadamu mimi." (Hos. 11:9)

Lakini Agano Jipya linabainisha kuwa adhabu itakuwa ya milele (Mt. 25:41). Ndiyo kusema kwamba hasira ya Mungu imeipita hata hasira ya binadamu.

Padre ameandika tena kwenye ukurasa wa 137 ya kuwa

Wakristo ni wana wa Mungu, sio watumwa au watumishi hata kwamba waadhibiwe. Tumeisha eleza hapo kabla ya kuwa Wakristo ni watumwa na Yesu ni mtumishi sawa na Injili.

**Adhabu ya Moto ni Nini?**

Padre amepotoka aliposema kuwa Kurani inataja adhabu za mwili (uk. 237). Kwa kweli mtu afapo, roho inajitenga na mwili ambao unazikwa na kisha huliwa na wadudu kaburini. Kuna wengine wanaochoma maiti zao. Lakini roho ya kila mtu hutoka na huwekwa na Mungu mahala fulani ambapo ndipo kaburi lake. Tutafufuliwa kiroho siku ya Kiyama; hivyo, adhabu au thawabu zote ni za roho.

**Maelezo**

Kwa hakika maisha ya ahera ni matokeo ya maisha ya hii dunia. Kila kitendo chetu huiathiri roho yetu. Hivyo, roho yetu huwa safi au chafu sawa na matendo yetu. Vitendo vyema hutia afya rohoni, na vitendo viovu huitilia roho maradhi. Roho hii baada ya kutoka mwilini, itakuwa kama mbegu ambayo itakua, na kutokana na

hiyo mbegu mwili mwingine wa kiroho utapatikana utakaokuwa na roho nyepesi zaidi ndani yake – ni kama mbegu inavyokua tumboni mwa mama na hutengenezeka mwili wenye roho ndani.

Na ni hakika ya kuwa mwili hulingana na mbegu. Hivyo huko ahera miili yetu ambayo ni ya kiroho, itakuwa na hali itakayolingana na hali ya roho zetu za hapa duniani. Wenye matendo maovu watakuwa na maradhi mbalimbali, ilhali wema watakuwa na afya njema sana. Na huruma ya Mungu itataka hao wagonjwa waponywe, kwa hiyo watapelekwa katika Jahanamu ambayo ni kama hospitali. Humo watatibiwa. Na ni dhahiri ya kuwa wagonjwa wanasumbuka wakitibiwa na kupewa dawa kali na yenye ladha mbaya; lakini hiyo ni heri kwani watapona.

Kwa hiyo, adhabu zote zilizoelezwa na Kurani, kwa kweli ni njia mbalimbali za kuwatibu; ni dawa za aina mbalimbali. Adhabu ya moto, maana yake ni tiba fulani, kama ilivyo hapa duniani pia ya kuwa baadhi ya maradhi yanapona kwa kuchoma zile sehemu.

Basi mambo ya Jahanamu yameitwa adhabu kwa sababu hao wagonjwa watasumbuka, lakini hizo ni dawa za kuwaponyesha. Na bila wasiwasi kila atakayepona, atatolewa nje na kupelekwa Peponi (yaani maisha ya kawaida yaliyo mazuri). Na mwishowe wote watawahi

kutoka, na Jahanamu itakuwa tupu, tulivyoisha eleza hapo nyuma.

Pia ijulikane ya kuwa minghairi ya Mungu kila kitu ni cha kiwiliwili, isipokuwa tu kiwiliwili cha aina fulani hakionekani na macho haya. Kwa mfano, upepo hauonekani kwa macho, lakini ni kitu cha kiwiliwili. Hali kadhalika malaika pia ni viumbe, kwa hiyo lazima wameumbwa na kitu fulani basi wanayo miili ila tu ni ya aina nyingine tusiyoweza kuiona kwa haya macho yetu.

**Sababu ya Kutokuonekana**

Sababu ya kutokuonekana kwa roho au hata malaika si kwamba eti hao hawana miili; bali sababu yake inaweza kuwa kuwepo kwao kwenye "frikwensi" (Frequency) tofauti.

Kwa hakika tunapoona kitu, maana yake ni kuwa miali ya nuru inayotoka kutoka hicho inaingia machoni mwetu mpaka ubongo ambao unahisi hiyo miali, na tunakiona hicho kitu. Sasa miali hupita hewani kwa sura ya mawimbi (waves), ambayo yanakuwa na mwendo kiasi fulani (frikwensi). Miali mbalimbali huwa na *frikwensi* tofauti. Kwa mfano, miali ya rangi nyekundu na rangi nyeupe au rangi nyingine ni ya *frikwensi* tofauti. Ziko rangi nyingine ambazo hatuzioni, lakini ziko duniani. Hatuzioni kwa sababu zinaenda katika *frikwensi* iliyo nje ya eneo la uwezo wa macho yetu. Kwa mfano,

X-rays ambazo hutumika sana hospitalini kwa kupiga picha ya sehemu za ndani ya mwili hazionekani kwa sababu tu zinakwenda kwa *frikwensi* isiyo katika uwezo wa macho yetu.

Basi malaika pia hatuwezi kuwaona, si kwa sababu hawana miili, bali miili yao iko kwenye *frikwensi* tofauti na uwezo wetu. Wakati mwingine malaika wanaonwa na wacha-Mungu. Hapo, kwa muda Mungu Anawajalia hao wacha-Mungu uwezo wa kuona miali ya *frikwensi* tofauti, lakini kwa muda.

Roho nayo haionekani kwa ajili ya tofauti ya *frikwensi*; lakini roho yenyewe ni kitu cha kiwiliwili, isipokuwa tu kiwiliwili hicho kina *frikwensi* tofauti na kiwiliwili cha huu mwili tulio nao hapa duniani.

Basi huko ahera, kwa kuwa sote tutakuwa katika hali moja katika ulimwengu wa *frikwensi* nyingine, hivyo tutaonekana sisi kwa sisi, pamoja na miili yetu ambayo miili hiyo haiwezi kuonekana na mtu aliyeko katika *frikwensi* ya hii dunia. Ni kama vile unavyogeuza mshale wa redio yako kwa kupata habari za nchi mbalimbali. Habari zile tu utasikia ambazo *frikwensi* yake inaafikiana na *frikwensi* uliyorekebisha kwayo redio yako.

Basi huko ahera miili itakuwapo, lakini *frikwensi* yake itakuwa ni kama *frikwensi* ya roho yetu hapa duniani, kwani miili hiyo itazaliwa kutokana na roho. Lakini

ndani ya hiyo miili mtakuwa na roho zilizo nyepesi zaidi ambazo hazitaonekana kwa sababu ya kuwa na *frikwensi* tofauti na uwezo wetu wa kuonea.

Hii ndiyo sababu, Kurani inaonekana ikieleza habari za ahera kama ni habari za kimwili. Isipokuwa tu mwili wa huko ni sawa na roho ya hapa, na roho ya huko ni nyepesi zaidi mno. Kwa hiyo, basi, binadamu atakuwa na uwezo zaidi wa kupata maendeleo, kwani uwezo wa roho ya hapa ni zaidi kuliko mwili wa hapa, na huko mwili utapata uwezo wa roho, na roho ya huko itakuwa na uwezo mwingi mno. Ni kwa sababu hii ya kuwa tutaweza kushuhudia uwezo na jalali ya Mungu kwa wingi zaidi kuliko tunavyoshuhudia hapa tukiwa katika mwili huu.

Maelezo hayo bila wasiwasi yanahakikisha ya kuwa tutaweza kumshuhudia Mungu zaidi kuliko tunavyofanya hapa duniani. Au tutamwona Mungu zaidi tunavyomwona hapa. Lakini kwa vyovyote haina maana kumwona Mungu ana kwa ana katika maana ya binadamu wawili kuonana, kwani Mungu Ameenea kote kote, bali binadamu hana uwezo huu, kwani ni kiumbe. Hivyo, kama Injili inasema kuwa tutamwona Mungu ahera kama tunavyomwona binadamu mwenzetu, haiwezi kuwa sawa. Na hii ndiyo sababu ya kuwa hata katika dunia hii hatuwezi kumwona Mungu katika maana hiyo. Haina maana kusema kuwa Mungu

Amekuja kwa sura ya binadamu, kwani hapo tutamfanya Mungu Asiwepo pahala pote, bali Atakuwa na mipaka na eneo maalum la dhati yake.

**Wake Huko Ahera**

Kurani imeeleza ya kuwa huko Peponi waaminio watapewa

watapewa wake wazuri. Hii ni haki, kwani binadamu akiwa binadamu atahitaji maisha ya familia, ila haya yatakuwa ya aina nyingine sawa na hali ya ule ulimwengu. Padre asitanie akieleza uzuri wa hao wake, kwani uzuri wa kimwili huko utalingana na uzuri wa roho waliyokuwa nayo hapa; hiyo roho ikiwa mbegu itazalisha mwili.

Padre amezungumza juu ya wavulana watakaowahudumia waaminio (Al-Waaqi'a 56:18). Hao wanaweza kuwa watoto wao waaminio. Neno 'watadumu', maana yake ni kuwa watadumu kuwa wema kwa wazazi wao sio waasi. Hii pia ni furaha kwa mzazi ya kuwa mtoto wake ni mwema, hamwasi.

Kule ahera ndiko maisha hasa, kwa hiyo juhudi na bidii zitahitajika kupata maendeleo, ila tu hakuna kurudi nyuma huko.

**Jahanamu**

Uovu ni maradhi ya roho, kwa hiyo waovu wataugua huko maradhi hayo, nao watatibiwa katika Jahanamu.

Wakiishapona watatolewa kuishi na wenzao Peponi kama kawaida.

Jahanamu siyo shimo kubwa ambamo moto unawaka;

bali ni hospitali, na ndiyo sababu wakati mwingine huko Peponi waaminio watawatembelea wabaya wasiudhike hata kidogo. Ni kama tunavyowatembelea wagonjwa hospitalini. "Basi akachungulia na akamwona katikati ya Jahanamu." (As-Saaffaat 37:56)

Na kwa kuwa Jahanamu ni hospitali, kwa hiyo padre asishangae kwa habari za vitanda, vifuniko na maji ya moto n.k.w.k., kwani hivyo vyote vinakuwapo hospitalini kwa ajili ya wagonjwa.

> "Atanyweshwa maji yaliyochemka; atayanywa kidogo kidogo wala hataweza kuyameza. Na mauti yatamfikia kutoka kila mahali, naye hatakufa." (Ibraahiim 14:17-18)

Aya hii inaeleza jinsi dawa za huko zitakavyomchukiza mtu hata kwamba ataona ni karibu kufa kwa sababu ya ukali wa dawa, lakini hatakufa, bali atatibiwa barabara. Aliyezoea kutumia maji ya barafu daima, akipewa maji ya bomba au maji ya moto kwa sababu ya ugonjwa wake anaona ni adhabu kubwa.

Jahanamu imeitwa gereza (Twaa Haa 20:75), na padre ameshangaa. Kwa kweli ni hospitali, lakini wagonjwa

hawatakuwa na ruhusa ya kutoka bila kupona. Kwa hiyo imeitwa gereza katika maana hii.

Ni ajabu ya kuwa adhabu za Jahanamu zilizoelezwa, kwa kweli ni dawa hata hapa duniani. Adhabu ya moto ni kuchomwa wakati mwingine au kutibu kwa umeme. Usaha ni kitu ambamo dawa ya vaksini (dawa ya chanjo) hutengenezwa. Zakkum (mpungate) ni dawa nzuri kwa ugonjwa wa uasherati. Padre aliyetaja adhabu hizo kitabuni anaelekezwa kutambua habari hii. Kwa njia ya kueleza adhabu hizo, Mungu Amewaelekeza binadamu kwenye njia za kutengeneza dawa kwa maradhi. Basi tunamshukuru badala ya kumtania kama alivyofanya padre.

Lakini fundisho la Biblia ya kuwa adhabu ni udhia tu wala siyo tiba, ni aibu; na pia adhabu kudumu milele, na kutengwa na Mungu milele ni kinyume na 'upendo' wa Mungu wanaoutangaza sana daima. Huku ni kushindwa kwa mpango wa Mungu, tena vibaya sana, kwani ni wengi walio wakosefu. Lakini sawa na maelezo ya Islam, mpango wa Mungu utafaulu, kwani mwishowe wote wataingia Peponi na kuungana na Mungu. Padre amekariri sana ya kuwa Waislamu wanaamini kuwa makafiri watadumu milele katika Jahanamu. Tumeisha eleza juu kuwa hiyo si sawa.

Neno la mwisho kuhusu habari ya ahera ni kuwa ule ulimwengu ni wa *frikwensi* nyingine, kwa hiyo vitu vyote vilivyotajwa kuhusu ulimwengu huo ni vitu hasa, ila tu viko kwenye hali inayolingana na ulimwengu huo. Hatuwezi kuvilinganisha na vitu vilivyo hapa duniani, jinsi tusivyolinganisha mwili na roho; lakini vyote hivyo vipo. Mtume[saw] aliposema kuwa neema za Peponi 'hakuna jicho lililowahi kuziona, wala sikio liliozisikia wala hazikuwazwa na moyo wa mtu,' maana yake ni dhahiri; kwani tuko katika ulimwengu wa *frikwensi* hii maalumu wala hatujawahi kushuhudia ulimwengu wa *frikwensi* tofauti.

## Somo 14. Heri ya Milele

Padre amepotosha aya aliyoandika hivi: "Kila mwanadamu tumemfungia nasibu yake shingoni mwake…" (Banii Israaiil 17:14); kwa hakika aya yenyewe ni hivi: "Na kila mwanadamu tumemfungia matendo yake shingoni mwake; na tutamtolea siku ya Kiyama daftari atakayoikuta imekunjuliwa. Soma daftari yako. Nafsi yako inakutosha kukuhesabia" (Banii Israaiil 17:14-15). Siyo ndege mbaya au njema, bali matendo yametajwa. Siyo kuwa kila mtu amekwisha andikiwa nasibu yake; bali kila tendo analotenda athari yake inabaki ndani ya roho. Kufungiwa na shingo, maana yake ni kuwa tendo halitapotea bure bali athari yake

itampata kwa vyovyote. Padre anaonekana hodari wa kupotosha ukweli!

### Wanawake Watulizao Macho

Padre ameandika kuwa huko Peponi kutakuwa na wanawake watulizao macho, sawa na Kurani. Ni kweli kuwa watakuwapo. Hao ni wake wema waaminio ambao waliinamisha macho yao hapa duniani wasiwatazame wanaume wengine kwa tamaa. 'Hawajaguswa' muradi wake ni kuwa wake hao ni wacha-Mungu waliotulia kwa waume zao wale hawakuguswa na wanaume wengine. Ijulikane hao sio viumbe wa huko Peponi, bali ni wanawake waaminio waliowaamini mitume wa zama zao pamoja na kutenda mema – Maria akiwa mmojawapo!

### Pepo ya Waislamu

Padre amesema kuwa Waislamu wanadhani kuwa Pepo ni kwa ajili ya Waislamu tu. Hatusemi hivyo; bali kila mtu aliyewaamini mitume wote na kutenda mema ataingia peponi. Waaminio wote tangu ulimwengu huu kuumbwa watakuwamo humo.

## Somo 15. Asili ya Ubaya na Mauti

Padre amesema sawa ya kuwa baadhi ya watu wanafikiri kwamba mabaya hayana budi kutokana na kiumbe kingine. Wakiugua, badala ya kutibiwa katika hospitali,

wanamkimbilia 'fundi' ili kutolewa pepo mchafu aliyesababisha maradhi hayo. Inaonekana kuwa 'fundi' mmojawapo bali 'Fundi Mkuu' alikuwa Yesu aliyefikiwa na wagonjwa wenye kifafa na wengineo, naye akawaponya kwa kuwatoa 'pepo' wachafu waliosababisha hayo maradhi. (Tazameni Mathayo 4: 24; 8:28-34; 9:32-33)

Ni bahati mbaya ya kuwa baadhi ya Waislamu nao wakamwiga Yesu 'ufundi' huo, kwa sababu ya mapenzi yao kwa Yesu, kwani yu Mtume wa Mungu katika imani ya Kiislamu. Ila tu hao wakawaita pepo wachafu kwa jina 'majini'. Ni mamoja tu kuita pepo au jini, lakini yaonekana ni kitu kile kile kimoja.

Habari za hirizi tumezieleza nyuma ya kuwa ni upuuzi, wala Kurani haifundishi kabisa jambo hilo.

Katika somo hili tena padre amekariri kadiri ya Mungu, ujinga, maradhi na ufukara – hayo yote tumeisha eleza vya kutosha mapema.

## Shari ya Alivyoviumba

Padre ameuliza maana ya "shari ya alivyoumba" Mungu ni nini? Hii ni aya ya sura 113 (Al-Falaq); humo mtu amefunzwa kumwomba Mungu kwamba Amlinde na shari ya vitu Alivyoumba. Kwa kweli Mungu Ameumba vitu kwa faida ya mtu, lakini wakati mwingine matumizi yake mabaya yanaleta shari kwa mtu. Basi mwaminio

anaomba kuwa aongozwe ili asipate kuvitumia vibaya mpaka vikawa shari. Pia kati ya viumbe kuna watu ambao wanaiba au wanaua. Basi mumini anamwomba Mungu Amlinde na shari za hao. Maana yake ni wazi, hatuelewi kwa nini padre ameshindwa kutambua. Pengine anawaza zile 'pepo' alizokuwa akitoa Yesu. Kwetu Waislamu hakuna pepo za aina hii.

Kwa Waislamu binadamu hakuumbwa katika hali duni; bali "bila shake tulimwumba mtu kwa umbo bora." (At-Tiin 95:5). Naam, chanzo cha binadamu ni dhaifu, yaani binadamu anapozaliwa huwa mtoto asiye na nguvu.

Na ile aya isemayo: "Najikinga kwa Mola wa watu katika shari ya wasiwasi wa Shetani" (Sura 114, An-Naas), maana yake ni dhahiri ya kuwa Shetani anamshawishi mtu kisirisiri, yaani bila kuonekana. Na hii imekubaliwa na Injili; hata Yesu alishawishiwa na Shetani (Mark 1:12-13). Padre anasema Yesu aliwapa mitume wake uwezo wa kutoa Shetani (uk. 144); lakini Yesu mwenyewe hakuweza kumfukuza, bali kila mahala alipomchukua Yesu, akaenda naye, kisha huyo Shetani kwa hiari yake akaenda lakini **kwa muda tu** (Luka 4:13). Kwa kweli Yesu aliwapa mitume wake uwezo wa kutoa 'pepo wachafu,' nao wakawa 'mafundi' wakubwa katika jambo hili.

Padre ametamka vizuri aliposema kuwa asili ya magonjwa siyo Mungu wala mashetani, wala pepo, wala

matashi ya mtu (uk. 145); lakini hapo alizipinga Injili zinazosema kwamba maradhi ya ububu na kifafa husababishwa na 'pepo', tulivyokwisha eleza nyuma.

Kwenye kurasa 145 na 146, padre amechora picha ili kuutania Uislamu, tumeisha jibu habari hii nyuma; yaani kuwasaidia maskini na shule za vipofu. Yesu hakufunza kuanzisha hospitali, bali aliwafunza 'ufundi' wa kuponya maradhi kwa kutoa 'pepo wachafu.'

**Sheria za Maumbile**

Padre amepotosha alipoandika kwamba kwa Waislamu

hakuna sheria za maumbile. Zile 'kawaida' alizosema kwa hakika ndizo sheria za maumbile. Na habari ya kusema 'Mungu Akipenda' tumeisha eleza nyuma.

Aya ile isemayo: "Wala msipende isipokuwa Anayopenda Mwenyezi Mungu" (Ad-Dahr 76:31), haisemi kuwa binadamu hana hiari katika kutenda; bali inaamrisha kufanya sawa na matakwa ya Mungu, yaani kufanya mema tu daima. Asiyefuata matakwa ya Mungu anayo hiari, lakini kwa kuwa amevunja amri iliyokuwa kwa kumnufaisha binadamu, atataabika.

**Mizimu, Pepo**

Hayo yote ni upuuzi sawa na Kurani Tukufu. Avishughulikiaye akiwa wa kawaida au 'fundi mkuu', ni mzushi tu. Hakuna ukweli wowote ndani ya habari ya

'pepo' au mizimu. Pia njia za kutoa pepo ziwe ni kumkaripia pepo na kumruhusu kuingia katika kundi la nguruwe au kumchomoa au kumchuchia, hizo zote hazina msingi; bali imani kama hiyo inapaswa kufutiliwa mbali katika jamii ili kufukuza adui mkubwa wa binadamu yaani ujinga.

Kauli yetu hapo juu imehakikisha kwamba padre amepotoka kabisa alipoandika kuwa 'Islam imepokea, bila ya kuipepeta sawasawa, imani katika viumbe ambao ni malaika…' (uk. 148).

Pia amepotosha padre akisema kuwa Islam inafunza kuacha matendo yanayoweza kumkasirisha pepo. Hatuamini pepo zo zote, tunawezaje kusema hayo. Habari ya ramli na Ya-Sin pia ni uzushi mtupu, ambao unafanana tu na ule 'ufundi' wa kutoa pepo wachafu katika bubu au mwenye kifafa.

Tumekubali maneno ya padre ya kuwa ni kazi ya dini kuwajulisha watu ya kuwa imani na pepo n.k.w.k. ni imani ya bure. Tumeisha timiza wajibu huo katika kurasa hizi. Ila tunawashauri Wakristo kuisafisha Injili na habari kama hizo. Pia tumekubali kuwaweka wanadamu huru na miungu ya bure. Tunatangaza siku zote kuwa Mungu wa kweli ni Mmoja tu, wenigine wote pamoja na Yesu sio miungu.

# Somo 16. Maadui na Wasaidizi wa Mwanadamu

## Jini, Malaika Na Shetani

Padre anasema kuwa kati ya viumbe hao wa aina tatu, viumbe wawili, Malaika na Shetani, wametajwa katika Biblia; lakini kiumbe Jin ametajwa katika Kurani pekee.

## Maelezo

Binadamu amepewa nguvu za aina nyingi; lakini, tuonavyo, nguvu hizo zinahitaji kitu kingine cha kuzisaidia ili ziweze kufanya kazi. Kwa mfano, tunayo nguvu ya kuonea. Lakini macho yetu hata yenye afya namna gani hayawezi kuona bila ya mwanga – kitu kilichoumbwa na Mungu. Kwani miali ya nuru ikiingia machoni hutuwezesha kuona. Hali kadhalika tunayo nguvu ya kusikia. Lakini masikio yetu hayatafanya kazi kama hakipo kitu kama upepo katikati, kwani mawimbi ya sauti (sound waves) hupita ndani yake ili kutufikia masikioni. Basi nguvu ya kusikia nayo huhitaji msaidizi, yaani upepo.

Sasa, ebu tuchunguze juu ya nguvu zetu za kutenda mema na mabaya. Kweli tunazo nguvu, lakini sawa na maelezo ya hapo juu lazima vipatikane vitu fulani vitakavyozisaidia nguvu zetu hizo za kutenda mema na mabaya. Katika dini ya Kiislamu kile kinachozisaidia nguvu za kutenda mema zifanye kazi huitwa **malaika**; na kile kisaidiacho nguvu za kutenda maovu ni Shetani. Ndiyo kusema kwamba Malaika hawawezi kutushu-

rutisha tutende mema, jinsi mwanga usivyoweza kutulazimisha tuone kitu fulani, kwani tunaweza kugeuza uso upande mwingine au hata kufumba macho. Msaada wa nuru uko tayari kama tunayo nguvu ya kuonea. Hivyo, msaada wa Malaika upo tayari, kama tunataka twaweza kuupokea. Lakini bila msaada wa Malaika, nguvu ya kutenda mema haitafanya kazi.

Kadhalika mashetani hawana uwezo wowote wa kutushurutisha kutenda maovu, ila tu wanatusaidia kutenda mabaya: Watatushawishi tupokee msaada wao ili kutenda maovu. Bila ya kusaidiwa na Shetani ovu halitendeki. Lakini mtu anayo hiari ya kupokea msaada wake au kukataa. Maombi ya kulindwa na shari za Shetani maana yake ni kuwa tulindwe tusije tukapokea msaada wake ili kutenda uovu kwa kushawishiwa naye. Siku ya Kiyama Shetani atasema:

> "Wala sikuwa na mamlaka juu yenu isipokuwa niliwaiteni nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu, bali jilaumuni." (Ibraahiim 14:23)

Ijulikane kuwa malaika na shetani ni viumbe tofauti kabisa. Malaika ni wema tu; na mashetani ni wabaya tu.

Mara nyingi husikika 'majini wema' na 'majini wabaya.' Kwa hakika maana yake ni malaika na mashetani; malaika ni majini wema, na mashetani ndio majini wabaya. Na sababu ya kusema hivyo ni kwamba neno

*Jinn* maana yake ni kitu kisichoonekana. Kwa kuwa malaika hawaonekani kwa macho haya na pia mashetani – kwa sababu ya kuwa kwenye *frikwensi* nyingine – kwa hiyo wanaweza kuitwa *Jinn* kwa Kiarabu. Zaidi ya hayo, Kurani haikubali wale majini ambao wameitwa 'pepo wachafu' katika Injili kwamba wanakuwapo ambao wanawaingia binadamu na kuwasumbua mpaka 'mafundi' wanaitwa kuwatoa kwa kusema 'Tawireni au Taileni' ama kutoa kwa "jina la baba, mwana na roho mtakatifu."

Mungu ni Mwumbaji Ameumba viumbe vya aina ngapi, hatujui; lakini kwa vyovyote hatukuambiwa ndani ya Kurani kuhusu majini au 'pepo' wanaowashika watu.

**Majini Walisilimu!**

Kama tulivyoeleza juu, kwa Kiarabu *Jinn*, au tuseme kila neno lenye J, N, N (J moja na N mbili) lina maana ya uficho ndani yake. Kwa mfano '*Janin'* maana yake ni mimba, kwani haionekani kwa urahisi kwa macho matupu. '*Junainah'* maana yake ni bustani (la wanyama), kwani huwezi kuingia ndani mpaka ununue tiketi. '*Jannah'* ni Pepo kwani haionekani ila siku ya Kiyama, pia maana yake ni bustani yenye miti mingi yenye kivuli kingi mpaka ardhi inafichikana kwa vivuli hivyo vya miti hiyo.

Kwa sababu hiyo, kila kitu kisichoonekana kwa urahisi huweza kuitwa *Jinn* kwa Kiarabu. Katika hii maana

Mtume[saw] alitumia neno *Jinn* kwa ajili ya vijidudu vidogo sana visivyoonekana kwa macho mara moja. Kadhalika na watu wakubwa ambao ni taabu kuonekana kwa ajili ya kulindwa na walinzi, huitwa *Jinn*; na kinyume chake neno *Naas* (watu) maana yake ni watu wa kawaida. Ile aya isemayo kuwa mtu ajikinge kwa Mungu katika shari ya majini na watu, maana yake ni kulindwa na taabu anazoweza kupata kutoka kwa watu wakubwa kama vile watawala na pia watu wa kawaida. Watawala wakiwa wadhalimu wanawasumbua raia, na pia watu wa kawaida wanaweza kuleta udhia mwingi.

Ndani ya Kurani Tukufu, neno *Jinn* limetumika mara nyingi kwa ajili ya binadamu. Katika sura Al-Jinn (sura 72), imeelezwa ya kuwa kundi moja la *Jinn* likawahi kusikia Kurani na likasilimu. Bali majini hao waliporudi kwao wakawahubiria wenzao ukweli wa Islam. Hao kwa kweli walikuwa Wayahudi wa Nasibin waliofika kwa Mtume[saw] kisirisiri ili wasisumbuliwe na Wapagani wa Makka; wakasilimu na wakarudi kwao kuhubiri. Kwa ajili ya kusilimu kisirisiri wameitwa majini.

## Wenye Hasira Kali

Watu wenye hasira kali nao huitwa *Jinn*, kwani kwa ajili ya ghadhabu kali mno mtu anatenda lisilofaa kwa sababu ya hulka njema 'kufichikana' kwake. Mtu wa aina hii anahamaki kwa jambo dogo tu lililo kinyume cha

upendo wake, na anachemka haraka. Kwa hiyo Kurani imetumia neno kuumbwa kwa 'ulimi wa moto'; yaani mtu wa aina hii huweza kuitwa kana kwamba ameumbwa na moto. Yaani, ni tabia yake kuchemka upesi. Kurani inasema 'binadamu ameumbwa katika haraka,' yaani tabia ya binadamu ni kufanya haraka.

Basi padre asishangae juu ya majini kuumbwa na ulimi na moto, kwani muradi wake ni wale wanadamu wenye tabia ya kukasirika haraka sana. Kwa Kiingereza pia mtu mwenye hasira kali sana huitwa 'Fire Brand'. Ni uzuri wa lugha kueleza kwa njia ya mifano. Wakati mwingine jitu kubwa huitwa jini pia. Katika Historia ya Ukristo, kilichoandikwa na Robert M. Glen, J. III. William Robertson Smith ameelezwa kuwa "alikuwa kama **jini** lile baya la kuwatisha watu." (uk. 98)

## Somo 17. Mungu na Kaisari

Padre amedhani ya kwamba dini ya Kiislamu inalazimisha kuchanganya dini na utawala (uk. 156). Hili ni kosa kubwa sana. Dini ya Kiislamu inaruhusu sawa na hali kwamba utawala na dini viandamane au viwe mbalimbali. Hii inategemea hali ya zama. Katika zama za Mtume[saw] na baadaye katika zama za Ukhalifa, dini na utawala viliandamana pamoja. Na sasa tunaona nchi kadha zenye Waislamu wengi zina dini na utawala mbalimbali.

Kwa kweli, Nabii mwenye sheria mpya anapotokea duniani, mara nyingi Mwenyezi Mungu huwa Anampa utawala katika maisha yake, ili sheria mpya iweze kubainika (utekelezaji wake). Na hii ni muhimu sana, kwani sheria za Mungu zinaenea juu ya maisha ya dunia na ya roho ya binadamu. Lakini baada ya muda shabaha hii inapokwisha kutimia, haiwi lazima tena kuchanganya utawala na dini.

Na manabii wasio na sheria mpya wanapokuja, ambao kazi yao ni kueneza sheria iliyopo mapema, mara nyingi siyo lazima hao wajaaliwe utawala. Kwa mfano, sawa na imani ya Kiislamu, Nabii Isa (yaani Yesu) hakuwa nabii mwenye sheria mpya, bali alikuja kueneza sheria ya Torati; hivyo haikuwa lazima ajaaliwe utawala wa dunia. Na si jambo la kushangaza kama Yesu alisema:

> "Vya Kaisari mpeni Kaisari; na vya Mungu mpeni Mungu" (Luka 20:25).

Lazima angesema hivyo, kwani njia nyingine hakuna. Kama angeupinga utawala, angeweza kutundikwa msalabani mapema zaidi. Basi akaona njia ya usalama ni kutamka hivyo.

Khalifa wa pili wa Seyidna Ahmad[asw] alisema waziwazi ya kuwa:

> "Katika zama za mwanzo wa Islam, Ukhalifa na utawala viliandamana pamoja, na ilipaswa kuwa

> hivyo kwani utekelezaji wa sheria ulikuwa haujabainika. Kwa ajili ya utekelezaji huo, ukhalifa na utawala vilichanganywa. Na sawa na imani yetu inajuzu kuchanganya ukhalifa na utawala pamoja na pia inajuzu kuvitenganisha." (Alfadhl 12 Desemba 1944, uk. 2)

Basi, padre hakutamka kauli iliyo sawa aliposema kuwa ni lazima dini na utawala viandamane pamoja sawa na imani ya Kiislamu. Bali njia zote mbili zinajuzu sawa na hali.

**Utekelezaji wa Sheria**

Siyo sawa hata kidogo ya kuwa katika serikali ya Kiislamu, iliyochanganya dini na utawala pamoja, kila mwananchi analazimishwa kufuata sheria ya Kiislamu. Sivyo kabisa. Bali wale tu wanaokubali dini ya Kiislamu watalazimika kuifuata. Wasiokuwa Waislamu hawataambiwa kutoa zaka na kutenda mengine yaliyowalazimu Waislamu. Hao watalazimika kufuata sheria za kawaida za nchi huku wakiwa na uhuru wa kuzifuata dini zao bila wasiwasi. Na ndivyo ilivyokuwa katika zama zilizopita. Wayahudi, Wakristo na Wapagani waliishi vizuri katika utawala wa Kiislamu. Bali kwa muda Waislamu walipolazimika kutoka nchini Palestina, Wakristo (wenyeji) waliwasindikiza hao Waislamu kwa huzuni na machozi, huku wakisema kuwa Waislamu wametutendea vizuri kuliko utawala wa Wakristo wenzetu.

Na ile habari ya kupigana vita, tumeisha eleza hapo nyuma ya kuwa vita haisihi kwa kueneza dini; lakini vita inaweza kupiganwa kwa sababu kadha wa kadha. Aya za vita alizoeleza padre zinasema waziwazi ya kuwa "piganeni na wale wanaopigana nanyi."

Padre pia amesema kuwa 'zaka' siku hizi ingeitwa kodi. Hatugeuzi sheria walivyofanya 'watu wa kitabu'. Zaka itabaki kuwa zaka; ina kiwango na kima maalumu. Kodi ni kitu kingine na kima chake na kiwango chake chaweza kubadilishwa na serikali sawa na hali.

Ni sawa ya kuwa Biblia inamtambulisha Mungu kuwa Mungu wa Israeli; lakini Mungu Aliyetambulishwa na Islam ni *Rabbul Aalamina*; ni Mungu wa walimwengu, ni *Rabun-Naas*; Mola wa watu wote; ni *Rabbul-Khalq*, Mola wa viumbe vyote, si tu Mungu wa Muhammad[saw].

**Utawala wa Kikristo**

Padre amesema kuwa Wakristo waliotaka utawala wa kidini katika karne zilizopita hawakufanya vile kwa agizo la Yesu (uk. 157). Ndiyo kusema kwamba waliuasi Ukristo, na hao waasi ndio waliowahi kuueneza Ukristo duniani, tulivyoisha eleza nyuma. Siku zote Kanisa na Serikali viliungana pamoja na kueneza Ukristo.

Padre amesema kuwa siku hizi ni Hispania tu iliyo nchi ya Kikristo. Lakini wote wanajua ya kuwa Uingereza inayo dini ya Kikristo kuwa dini ya serikali,

na malkia ni kiongozi wa kanisa pia. Ni sawa kuwa upo uhuru kwa watu wote; lakini pia ni sawa ya kuwa hao Wakristo wanajaribu kuwalazimisha wengine kufuata desturi za Kikristo. Kwa mfano, William Whitelaw aliwasihi wahamiaji kuishi kizungu; na akieleza maisha ya kizungu akasema:

> "Kwa mfano, ninafikiri haiwezekani kukubali hali iliyopo sasa ya kuwa na wake wawili, ilhali 'mke mmoja' ndiyo sheria."

(Daily News, Tanzania, la tarehe 14.2.1977)

Pia ijulikane kwamba kwa kweli haiwezi kupatikana serikali ya Kikristo kwani katika Ukristo hakuna sheria imhusuyo binadamu katika maisha ya kila siku kama vile ndoa, talaka, urithi n.k.w.k. Hivyo, hata zikipatikana serikali za Kikristo, zitakuwa za bandia tu. Sheria ya kupenda jirani haiwezi kutosha kuendesha serikali – ambayo sheria hiyo nayo imo katika Agano la Kale na pia Kurani Tukufu. Kutenganisha utawala na dini ni kwa sababu ya Ukristo kushindwa kuwapa watu katiba kamili kwa kuendesha serikali.

## Kutumia Nguvu

Padre ameeleza sana juu ya sheria ya Ukristo kuhusu uhuru na upole. Lakini hakika yenyewe sawa na maelezo ya Injili ni kwamba Yesu hakuwapa wengine uhuru wa dini bali akatumia nguvu:

> "Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akizipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa" (Mt. 21:12).

Kama dini ya Ukristo ni dini ghairi ya dini ya Kiyahudi, kwa nini Yesu akatumia nguvu kueneza dini yake. Kama kufanya biashara ni haramu katika hekalu sawa na Agano la Kale, lakini Yesu alipokwisha kuondoa *'laana'* ya sheria, kulikuwa na haja gani kuleta mchafuko hekaluni kwa kuzipindua meza na kuwafukuza watu na kutupa viti vyao? Si anataka kueneza matakwa yake kwa kutumia nguvu. Hii ndiyo hali ya Yesu pasipokuwa na utawala; kama angekuwa na utawala bila shaka angewasumbua sana watu na kueneza fikara zake kwa upanga. Mungu Ametumia hekima kubwa sana kumnyima Yesu utawala wa dunia!

## Somo 18. Dini ya Moyo na ya Maungo

Padre amedai kuwa Ukristo ni dini ya moyo zaidi kuliko Uislamu (uk 160). Kwa hakika kila dini katika hali yake ya asili ni dini ya moyo, lakini baadaye watu wanaanza kuichafua. Ukristo wa asili bila shaka ni dini ya Kiyahudi nayo ilikuwa ya moyo, lakini wafuasi wake wa baadaye wakaifanya iwe dini ya dhahiri tu siyo ya matendo. Kwani waliitegemea damu ya Yesu na wakawa na ruhusa ya kutenda lolote kwa sababu mzigo wa unajisi wa dhambi umekwisha kutwishwa kichwani pa Yesu.

Kwa Waislamu imani na vitendo ni mambo ya lazima: Matendo bila imani au imani bila matendo ni bure. Kurani inasema:

> "Na wabashirie walioamini na kufanya vitendo vizuri, kwamba watapata bustani zipitazo mito chini yake." (Al-Baqara 2:26)

Aya hii inaeleza kwa uwazi kuwa imani na vitendo vizuri, matokeo yake ni bustani na mito chini yake. Ndiyo kusema kwamba jinsi bustani inavyohitaji maji kwa ustawi, ndivyo imani inavyohitaji vitendo vizuri; la sivyo imani itakauka jinsi bustani ikaukavyo bila maji.

Kwa hiyo Uislamu ni dini ya moyo; imani na vitendo vizuri ni vya lazima kwa kuistawisha. Na vitendo vizuri huelezwa na sheria ambayo kwetu siyo *'laana'*.

Juu ya Sala tumeisha eleza nyuma pamoja na kutawadha. Ni kweli ya kuwa katika ibada, roho iandamane na mwili (sura ya 107 ya Kurani, Al-Maa'uun). Padre amesema kuwa 'sala haina budi kuwa kazi ya upendo kwa Mungu na kwa jirani'. Lakini Islam inasema siyo tu kumpenda Mungu na jirani; bali upendo wa Mungu pamoja na upendo wa viumbe vyote, si jirani tu pekee.

Juu ya kufunga saumu pia tumeisha eleza hapo kabla. Padre amesema kuwa Mkristo anashauriwa **sana** kufunga. Lakini, je Wakristo kweli wanafunga **sana**? Au wanawacheka wanaofunga? Padre amesema kuwa 'lakini kufunga chakula siyo kiini cha mafungo.' Hii ni sawa; hata

Islam inafundisha kuwa na kiini cha kufunga, bali kiini cha kila kitendo chema, ni kupata ukaribu na Mungu.

Padre amesema kuwa Mwislamu ni rahisi kutambulika kuliko Mkristo, kwani Mwislamu anafuata sana mambo ya dhahiri, kama vile kuvaa mavazi maalumu na kofia n.k.w.k. Hii ni vizuri kuwa mtu ajulikane kuwa ni wa aina fulani. Lakini ieleweke kuwa vazi la aina fulani sio vazi la Kiislamu; bali kila vazi linalomsitiri mtu vizuri ndilo vazi la Kiislamu. Waweza kuvaa suruale, au shuka; kanzu au shati; ni sawa tu. Lakini tunauliza kuwa je Wakristo nao hawakujizushia mila ya kuvaa 'mslaba'? Je si nao wanajulikana kwa huo? Kwa kweli kuvaa kofia na vazi ni kitu cha maana na faida; lakini kuvaa kijisalaba shingoni ni kitendo cha dhahiri kabisa. Msalaba uliomsumbua Yesu ungekuwa ni adui kwa Mkristo mwenye imani; lakini kinyume chake anaupenda. Ni uchoyo wa hali ya mwisho kukipenda kitu kwa 'faida' yako kilichomdhuru mpendwa wako. Basi upendo huo ni wa dhahiri tu na wa bandia; ni kujipenda kuliko kumpenda Yesu.

**Imani**

Padre amesema kuwa kwa madhehebu ya Kishia kuficha imani (*takiyya*) kunajuzu. Kwa kweli *takiyya* haijuzu katika Islam waila Waislamu wasingeuawa! Lakini padre atasemaje kwa Paulo aliyeeneza Ukristo kwa kusema **Uwongo:**

"Lakini ikiwa kweli ya Mungu imezidi

> kudhihirisha utukufu wake kwa sababu ya uwongo wangu, mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa ni mwenye dhambi." (Warumi 3:7)

Padre ametumia uwongo wa Kipaulo ili kueneza Ukristo alipoandika ya kuwa "Mwislamu anaambiwa kuwa na Imani; bali Mkristo anapaswa kuwa na matendo na imani." (uk. 163). Tumeisha eleza juu ya kuwa katika Islam imani na vitendo vizuri ni mambo yasiyoweza kutengwa.

Padre atambue ya kuwa 'kusadiki Mungu na Muhammad' kwa moyo ndiyo kutenda mema yote yale yaliyo katika uwezo wa mtu.

**Mti wa Kiislamu**

Padre amesema kuwa Mwislamu amepewa mti mzima ambao unaweza kung'olewa na dhoruba na pepo katika siku zijazo. Tunamwelekeza kusoma aya hii ifuatayo ya Kurani Tukufu:

> "Je, hukuona jinsi Mwenyezi Mungu Alivyopiga mfano wa neno zuri? Ni kama **Mti** mzuri ambao mzizi wake ni imara na kila tawi lake lafika mbinguni. Hutoa matunda yake kila wakati kwa idhini ya Mola wake. Na Mwenyezi Mungu Huwapigia watu mifano ili wapate kudhukuru." (Ibraahiim 14:25-26)

Aya hii inamjibu padre ya kuwa **Mti** wa Kiislamu hauwezi kung'olewa na dhoruba kali ya mabadiliko ya hali ya dunia; bali ni mti ambao mzizi wake ni imara kabisa. Tena haukauki mti huu, kwani matawi yake hufika hadi mbinguni na kupata maji kutoka mawinguni pia pamoja na maji ya ardhini kwani mzizi wake umo ndani sana ya ardhi. Huleta matunda daima. Kila wakati katika Islam wanapatikana watawa ambao humfikia Mungu na kuungana naye kwa njia ya mti huu.

Lakini mti wa sheria umekwisha laaniwa na Wakristo, hivyo hawafiki popote 'Bidii yao imepotea katika maisha ya duniani' (Al-Kahf 18:105).

Someni kitabu chetu *"Uislamu na dini nyingine"* mkaelewe jinsi Islam ilivyokamilika tena kwa wakati wote hadi Kiyama.

## Somo 19. Mwanadamu katika Taifa

Padre amesema kuwa katika nchi tunaishi watu wa imani mbalimbali; lakini ni muhimu kuondoa utengano kama udini na ukabila. Tunakubaliana naye. Lakini anasemaje juu ya Yesu aliyefunza kuwa wasio Waisraeli ni kama 'mbwa' (Mt. 15:26). Je huo sio ukabila? Ingawa padre ametoa shauri zuri lakini amempinga Mwana wa Mungu.

Padre atambue ya kwamba kila sheria inayompatia binadamu haki zake ni nzuri kwetu sisi Waislamu.

Kisha ameandika juu ya aina za serikali; habari hii tumeisha eleza nyuma.

### Kujitolea kwa Wenzake

Padre amesema kuwa Kurani haifunzi kujitolea kwa mwingine kiasi hiki kwamba mwenye kujitolea aone taabu kwa ajili ya mwenzake. Padre anaelekezwa kusoma aya hii:

> "Na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo." (Al-Hashr 59:10)

*Kuendelea Pamoja*: Padre anajulishwa ya kuwa Islam inafunza kuwa wote waendelee pamoja kwa njia ya sala ambayo husaliwa pamoja, lakini Ukristo haufunzi kusali pamoja alivyosema padre, ila tu ni amri ya Kanisa.

### Kuwatendea Wengine

Padre amesema kwamba Islam haina mengi juu ya uhusiano kati ya Waislamu na watu wa dini nyingine (uk. 168). Kurani inasema:

> "Semeni na watu kwa wema." (Al-Baqara 2:84)

Yaani kuwatendea watu wote sio Waislamu tu. Tena:

> "Enyi mlioamini, kuweni wasimamizi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoao shahada kwa adili. Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa." (Al-Maaida 5:9)

Ile aya isemayo kuwa waaminio wasifanye urafiki na makafiri, maana yake ni wale makafiri wanaopigana na Waislamu. Na Pia imeelezwa kutokufanya urafiki nao kwa kuwaacha waaminio bali wafanye urafiki na wote.

## Somo 20. Kujenga Ujamaa

Padre anasema kwamba katika ujamaa wa Kiislamu hakuna awezaye kuingia ila tu aliyesilimu; hakuna nafasi kwa mwingine. Na kisha alipoeleza ujamaa wa Kikristo ameeleza kwamba katika ujamaa huo wote wanaingia kwa kubatizwa na kuamini kuwa Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Je siyo maana yake kuwa ujamaa wa Kikristo unawahusu Wakristo tu? Kwa nini tena kuilaumu Islam?

Kwa kweli wasiokuwa Waislamu wanaweza kuishi vizuri katika ujamaa wa Waislamu, kwani watakuwa na uhuru wa kuabudu na watapata amani na ulinzi kamili.

### Matendo ya Kujenga Ujamaa

Kwa kweli sala ni tendo kubwa la kufunza ujamaa, kwani Islam inalazimisha kusali pamoja ila kwa udhuru maalumu tu. Padre amesema kuwa sala ya Ijumaa si tendo la lazima kwa Waislamu. Hapo amekosea sana. Kwani sala ya Ijumaa ni faradhi kabisa iliyolazimishwa ndani ya Kurani tukufu (Sura ya 62, Al-Jumu‘a).

Katika Ukristo hakuna tendo la ujamaa; kwani hata hii Jumapili limeizusha Kanisa, sio Ukristo wenyewe.

Kufunga saumu pia ni kitendo cha ujamaa, kwani huwa wanafunga pamoja yaani katika mwezi mmoja maalumu. Padre amepotea aliposema kuwa Ramadhani ni mwezi wa mwisho kwa mwaka; huo kwa kweli ni mwezi wa 9 katika kalenda ya Kiislamu; mwezi wa mwisho ni Dhul-haji.

**Sikukuu**

Mtume[saw] ametuwekea sikukuu mbili tu: Idul Fitri na Idul Haji. Sikukuu zingine zimezushwa na watu. Tunamsahihisha padre ya kuwa Idul Haji sio ukumbusho wa Mtume Muhammad[saw] kuhamia Madina; bali Idi kubwa ni ukumbusho wa dhabihu ya Nabii Ibrahimu na Nabii Ismaili na Bi Hajira. Nabii Ibrahimu kwa amri ya Mungu (si kwa kuchochewa na Sara) alipowapeleka Ismail na Hajira huko kunako Makka siku hizi, Ibrahimu alipomlaza Ismaili kumchinja kwa sababu ya ndoto yake, Bi Hajira alipokimbia-kimbia baina ya vilima Safaa na Marwah ili kutafuta maji, Ismaili alipojitolea ambaye katika kizazi chake Mtume[saw] alitokea kwa kuhubiri mataifa, kwa jumla ni ukumbusho wa kujitolea kwa hao wacha-Mungu.

Ieleweke ya kuwa mahali panapoitwa Marwah ambako Ismaili alitakiwa kutolewa dhabihu pamegeuzwa kuwa 'Moria' ndani ya Biblia (Mwanzo 22:2); na badala ya Ismaili wameandika Isaka.

## Sikukuu za Wakristo

Jinsi isivyokamilika dini ya Kikristo inajulikana tunapoona kuwa wafuasi wake hawakuwekewa sikukuu yoyote bali wafuasi wenyewe wamehangaika kuzitafuta kwa ajili yao. Padre amesema 'maulidi ya Yesu' ni 'Sikukuu ya Kikristo'. Ukweli ni kuwa siku ya kuzaliwa Yesu haijulikani (The Wycliffe Bible Commentary, uk. 1032). Hii tarehe 25 Desemba ilikuwa sikukuu fulani ya Kipagani iliyochukuliwa kama siku ya Krismasi:

> "Yaonekana kwamba desturi hiyo ya siku ya kuzaliwa kwake Yesu kushikwa mwisho wa Desemba ilipata nguvu kwa kufuatana na sikukuu fulani ya dini ya Upagani ya wakati ule. Maana watu walipoona kwamba pengo lilikuwapo kwa kuacha sikukuu hiyo ya kitaifa walilijaza na sikukuu ya kanisa ya kuzaliwa kwake Yesu Kristo."
>
> (Historia ya Ukristo J I, uk. 63, na Dean A. Peterson)

Sikukuu zingine alizoeleza padre nazo hazionekani katika Biblia wala Yesu hakuweka hizo. Lakini ni jambo la ajabu kuwa sikukuu ya wafanyakazi (tarehe 1 Mei) imehesabiwa kuwa sikukuu ya Kikristo.

## Kuhiji

Padre amekubali kuwa ibada ya Hija inawaunganisha watu pamoja. Kisha ameeleza kuwa Wakristo nao

wanahiji mahala fulani na fulani. Huku ni kuiga tu dini nyingine kwani Yesu hakufunza kwenda kuhiji mahali fulani, na mambo ya Wayahudi yanawachukiza Wakristo. Basi wamelazimika tu kuwaiga wengine ambao wamewekewa mambo hayo na Mungu.

**Fadhila za Ujamaa**

Padre amesema kuwa fadhila za Ujamaa ni 'adabu njema'. Kisha anasema kuwa Yesu alikuwa na heshima kwa mama yake. Anasema kuwa Waislamu wanadhani kwamba Yesu alimdharau mama yake alipomwambia: "Bi mkubwa, twashiriki nini?"

Kweli tunasema kuwa Yesu alimdharau mamaake mzazi; kwani hakuna anayeweza kumwambia mama yake mzazi: 'mwanamke'. Kwa kuogopa lawana yetu, Wakristo wamegeuza tafsiri ya Biblia yao; wameandika: "Mama, tuna nini mimi nawe?" (Yohana 2:4); lakini hata hivyo hayo yanahakikisha kuwa Yesu anaonyesha hahusiani na mama. Bali mpaka leo hii katika Biblia ya Kiingereza imeandikwa: "Woman, what have I to do with thee" (Yn. 2:4): Mwanamke, mimi nina nini nawe. Hata katika Biblia za Kiurdu na Kiarabu imeandikwa kabisa hivi: Mwanamke, nina nini mimi nawe? Basi ujamaa wa Kikristo umefunza adabu nzuri za aina hii ya kumheshimu mzazi kwa kusema: Mwanamke; lahaula!

Kwa hiyo, maneno mengi juu ya heshima aliyojaza padre katika somo hili ni bure wala hayastahili tuandike lo lote juu yake.

Islam imefunza kuwaheshimu wazazi; tumeisha eleza nyuma. Pia inamlazimisha kila mmoja kumhurumia mdogo (Abu Daud). Khalifa wa pili akisihi wanajumuiya alisema:

*Mwaweza kujiheshimu*
*Bali pia nakalimu*
*Msitahi binadamu*
*Kwa staha ipasayo.*

Mtume[saw] alisema kuwa Mwarabu hana ubora juu ya asiye Mwarabu. Yesu aliwafunza kuwahesabu Waisraeli kuwa watoto lakini wengine kama 'mbwa'. Hii ndiyo hali ya usawa uliofunzwa na Ukristo. Mpaka leo hii ukabila na ubaguzi wa rangi hauwatoki watawala wa Kikristo huko Rhodesia na South Africa. Hayo, inaelekea, ni matokeo ya Yesu kumtenda yule mwanamke Mkananayo.

## Kusaidiana

Padre amedokeza kuwa Waislamu wanaambiwa kuwasaidia Waislamu tu wenzao. Hakika ni kuwa tunafunzwa: "Na huwalisha chakula maskini na yatima na mfungwa kwa mapenzi yake (Mungu)" (Ad-Dahr 76:9).

Hakuna ubaguzi wowote. Kila anayestahili anasaidiwa bila kuambiwa 'mbwa.'

## Somo 21. Hali ya Wanawake

Padre amesema sawa kabisa ya kuwa hali ya wanawake duniani ni tofauti na hali ya wanaume. Kisha anauliza swali ya kuwa je hiyo imesababishwa na dini? Hebu tuchunguze vitabu vya dini zetu.

Kwanza kabisa tujue ya kwamba padre amekubali ya kuwa Kurani ilipandisha cheo cha wanawake. (uk. 176). Na kwamba "Muhammad alimpa mwanamke usawa na mume mbele ya Mungu" (uk. 178). Lakini amedai pia ya kuwa Islam haikumpa mwanamke usawa mbele ya watu. Vilevile amejigamba kuwa Yesu alitia msingi wa usawa alipofanya mume na mke kuwa 'mtu mmoja' katika hali ya ndoa. (uk. 176)

### Kuwa Mwili Mmoja

Padre amemsifu bure kabisa Yesu kwa ajili ya kufanya mume na mke kuwa 'mtu mmoja.' Kwa kweli hii ilinenwa tangu ilipoumbwa dunia hii. Kitabu cha Mwanzo kinasema:

> "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa **Mwili Mmoja**" (Mwa. 2:24).

Kwa hiyo, hili ni funzo la Agano la Kale analochukia padre; bali amesema mara kwa mara ya kuwa Kurani

inafanana na Agano la Kale na inaturudisha kwalo ilhali tumo katika Agano Jipya. Kwa kweli hakuna mafunzo ya maana katika Agano Jipya juu ya hali ya wanawake, kwa hiyo padre amelazimika kulitaja hili fundisho la zamani na kulinasibisha kwa Yesu.

> "Na wanapenda kusifiwa kwa yale wasiyoyafanya." (Aali 'Imraan 3:189)

Padre amesema pia ya kuwa Kurani na Biblia vinapatana juu ya jambo hili kwamba wanawake na wanaume wana hali moja mbele ya Mungu (uk. 177). Amesema kuwa hiyo imeelezwa katika Kurani, Al-Ahzaab 33:36; lakini hakuonyesha wapi Biblia imeeleza habari hiyo: Hali ya wanawake ilivyoelezwa katika Biblia ndiyo ifuatayo:

## Mwanamume Bora Kuliko Mwanamke

Ubora wa mwanamume juu ya mwanamke umeelezwa katika Biblia waziwazi:

> "Kichwa cha kila mwanamume ni Kristo, na kichwa cha mwanamke ni mwanamume, na kichwa cha Kristo ni Mungu." (1 Wakorintho 11:3)

Ndiyo kusema kwamba Mkuu ni Mungu, daraja ya pili ni ya Kristo, ya tatu ni ya mwanamume na daraja ya chini kabisa ni kwa mwanamke.

Usawa wa Kikristo baina ya mume na mke umeelezwa hivi: "Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala

**kumtawala** mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia hali ya kukosa" (1 Timotheo 2:12-14).

Pia wanawake wamekatazwa kuvaa nguo nzuri na mapambo na kusuka nyewele (1 Petro 3:3; 1 Timotheo 2:8-10). "Kama vile Kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika **Kila Jambo**." (Waefeso 5:24)

Hiyo ndiyo hali ya mwanamke sawa na mafunzo ya Agano Jipya. Ingawa Agano la Kale pia limeeleza hali za wanawake, lakini hatukutaja, kwani padre ameisha jitenga nalo. Na hayo yote yanahakikisha kuwa hakuna usawa wa aina yoyote baina ya wanawake na wanaume katika Ukristo. Kama siku hizi wanapiga kelele za usawa, basi ni uzushi wao wenyewe, lakini Agano Jipya halifundishi hivyo. Mpaka sasa Kanisa halijakubali usawa kati ya wanawake na wanaume. Hivi majuzi tu Papa Paulo ametangaza kuwa wanawake hawana haki ya kuteuliwa kuwa mapadre, kwani Yesu kwa kitendo alifundisha kuwachagua wanaume tu kuwa mitume.

(Daily News, Tanzania, tarehe 31.1.1977)

Na kile "Chama cha Yesu" ambacho kikawa 'chama kamili katika Kanisa Katoliki' kwa ruhusa ya Papa katika

mwaka 1940, nacho chaendelea mpaka hivi leo kuwa ni ‘chama kimojawapo chenye kupata sifa kubwa katika kazi yao ya elimu na uenezi wa Injili’ kiliwanyima wanawake nafasi ya kuingia katika chama chao.

(Historia ya Ukristo, J. 2, uk. 155, na Dean A. Peterson)

## Islam na Wanawake

Dini Tukufu ya Kiislamu inamweka mwanamke sawa na mwanamume:

> Bila shaka wanaume wanaojisalimisha na wanawake wanaojisalimisha, na wanaume wanaoamini na wanawake wanaoamini, na wanaume wanaotii na wanawake wanaotii, na wanaume wasemao kweli na wanawake wasemao kweli, na wanaume wanaosubiri na wanawake wanaosubiri, na wanaume wanaonyenyekea na wanawake wanaonyenyekea, na wanaume wanaotoa sadaka na wanawake wanaotoa sadaka, na wanaume wanaofunga saumu na wanawake wanaofunga saumu, na wanaume wanaolinda tupu zao na wanawake wanaolinda tupu zao, na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi na wanawake wanaomtaja – Mwenyezi Mungu Amewaandalia msamaha na ujira mkubwa.” (Al-Ahzaab 33:36)

Aya hii inaeleza usawa wa ajabu baina ya wanaume na wanawake ambao mfano wake hauonekani katika dini yoyote iwayo.

## Usawa Katika Ndoa

Padre alieleza usawa wa aina moja tu unaoelezwa katika Ukristo, yaani usawa katika ndoa, kwa kusema kwamba mke na mume wanakuwa 'mwili mmoja'. Tumeisha thibitisha nyuma kuwa fundisho hili nalo si la Yesu bali ni la Agano la Kale; lakini hata hivyo sawa na fundisho la Agano Jipya ni wazi kuwa hakuna usawa katika ndoa, kwani mwanamke ameumbwa kwa ajili ya mwanamume, sio mwanamume kwa ajili ya mwanamke (1 Wakorintho 11:9)

Lakini Kurani Tukufu inafunza:

> "Wake ni nguo kwa waume; na waume ni nguo kwa wake." (Al-Baqara 2:188)

Huu ndio usawa katika maisha ya ndoa.

## Tofauti za Dhahiri

Ni dhahiri ya kuwa kuna tofauti katika umbo la mwanamume na la mwanamke; na tofauti hii yaonyesha kuwa wanawake na wanaume wameumbwa kwa ajili ya wajibu tofauti kidogo. Katika Islam mwanamke anaweza kufanya kazi na kujichumia riziki sharti asichanganyike na wanaume, lakini imependelewa kwamba mume ashike kazi ya uchumi, na mke awe msimamizi wa upande wa matumizi.

Hata katika serikali, ziko idara mbalimbali za uchumi na matumizi. Zikichanganywa, vurugu linatokea. Huku ni

kugawana tu kazi katika maisha. Sawa na umbo linaloweza kuvumilia taabu na magumu, mwanamume amepewa wajibu wa kuchuma riziki. Na wajibu wa kuendesha mambo ya nyumbani, ambao pia ni wajibu wa muhimu kabisa, amepewa mwanamke. Baada ya ndoa watoto wanazaliwa ambao hupaswa kulelewa vizuri ili wafae baadaye kwa dini na taifa. Mama kwa ajili ya upole wa tabia yake anafaa zaidi kufanya kazi ya ulezi wa watoto kuliko mwanamume. Basi mwanamke hakuachwa bila kupewa kazi katika jamii kwani yeye naye anashughulika kuwalea watoto ambao baadaye watakuwa fahari ya taifa wakipata ulezi bora, na kwa ajili ya kulelewa vizuri watakuwa na ari ya kulilinda taifa, na watalitumikia hata kutoa uhai wao.

Na kwa ajili ya wanawake na wanaume kuchanganyika kazini hulka zao zitarudi nyuma, bali na kazi pia zitasinzia kwani wavulana na wasichana badala ya kutumia nafasi zote katika kazi wataahughulikia zaidi kuongea pamoja na kubadilishana maneno ya 'mapenzi'.

Kwa hiyo, hii sheria ya Islam ya kuwa wanaume na wanawake wasichanganyike pamoja ni kwa ajili ya faida na maendeleo ya taifa na hulka bora.

## Wanaume ni Wasimamizi

Idara yoyote au hata serikali yoyote haiwezi kuendelea kama wako maraisi wawili. Lazima raisi awe mmoja, lakini anaweza kuwa na makamu wake. Basi Islam

inafunza ya kuwa mwanamume ni msimamizi na mwanamke ni makamu wake. Kama huku ndiko kumshusha mwanamke, basi je wananchi wanashushwa hadhi wanapokuwa na Rais mmoja anayesimamia maendeleo ya nchi? La, hasha!

Lazima msimamizi awe mmoja tu; mwanamke au mwanamume. Mwanamume amechaguliwa kwa ajili ya hali yake ya maumbile, kwani anaweza kukabiliana na mashaka na magumu ya dunia zaidi. Si upendeleo, bali ni kwa sababu ya tofauti yenyewe katika hali yao ya maumbile.

**Shungi**

Padre ameilaumu Islam kwa sababu imemlazimisha mwanamke kuvaa shungi. Kwa hakika fundisho la Islam lina hekima ndani yake. Mwili wa mwanamke unamvutia mwanamume zaidi kuliko mwanamke kuvutika kwa mwanamume. Hivyo, mwanamke ameambiwa kuvaa shungi. Hata Biblia ya padre inatoa amri ya wanawake kuvaa shungi; bali asiyevaa adhabu yake imeelezwa ni kuwa mwanamke huyo anyolewe nywele zake (1 Wakorintho 11:6).

Basi padre ametumia ujeuri alipochora picha ya mwanamke ndani ya jela na chini yake akaandika aya ya Kurani ya kwamba wanaume ni walinzi wa wanawake. Mwanamke wa Kiislamu anaruhusiwa kutoka nje kwa shughuli zake, lakini avae shungi akitoka.

Padre amesema, Kurani inaeleza mwanamke kuwa njia ya kumzalia mwanamume watoto. Lakini ebu some Biblia ikisema:

> "Mwanamke alidanganywa kabisa na akaingia katika hali ya kukosa. Walakini ataokolewa kwa uzazi wake." (1 Timotheo 2:14-15)

Ndiyo kusema kwamba mwanamke anaambiwa kuokolewa kwa njia ya watoto wake. Yaani lazima azae – ndiyo kazi yake maalumu – kama anataka kuokolewa; asipozaa kwa sababu ya kuwa tasa au kuwa 'mtawa', hawezi kuokolewa. Tasa hawezi kabisa, lakini 'mtawa' anayo 'nafasi' ya kuzaa ili kupata wokovu, sharti watoto hao wakishika wema.

Padre amesema tena ya kuwa Islam inamhesabu mwanamke kuwa 'mali' ya mwanamume. Huu ni uwongo dhahiri. Bali Paulo anafundisha hivyo:

> "Inampasa mwanamke awe na dalili ya **Kumilikiwa** kichwani." (1 Wakorintho 11:10).

Mwanamke kuwa kama shamba kwa mume (Al-Baqara 2:224) maana yake ni kuwa mwanamume analazimika kumtunza vizuri mkewe. Siyo maana yake kuwa mke ni milki ya mume. Kama angekuwa milki yake, hangeweza kupewa haki ya kuachana na mumewe. Islam inamruhusu mume kuachana na mke na pia mke

kuachana na mume. Ziko sharti kadha wa kadha za talaka, siyo kutoa talaka ovyo.

Padre akieleza hali ya wanawake wa Kiarabu kabla ya lslam anawadanganya wasomaji kwa kuwaambia kana kwamba ndiyo Islam iliyosababisha hali hiyo. Neno *Ba΄l*, maana yake ni mume wala siyo ‘mwenye mali’.

Padre anafikiri kuwa mitara ni kinyume na heshima ya mwanamke. Tumeisha eleza kuoa wake zaidi ya mmoja hapo nyuma. Juu ya mahari pia ameandika kana kwamba ni kununua mke. Akili haikubali dalili hii ya padre. Mahari anapewa mke; kama mke ni mali, fedha za mahari angepewa mwuzaji wa mali hiyo, yaani mzazi wa mke. Lakini sivyo, mke anapata mahari katika Islam. Mahari ni zawadi ya arusi anayopewa mwanamke. Hii ndiyo heshima, wala siyo dharau.

**Daraja Moja Zaidi**

Ni sawa aliyosema padre ya kuwa Kurani imesema kuwa wanaume wana daraja moja zaidi kuliko wanawake. Yaani wanaume ndio wasimamizi. Lazima mmojawapo awe msimamizi ili nidhamu iendelee vizuri. Biblia pia inasema;

> “Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe.” (Waefeso 5:22-23)

Kama wanaume hawana daraja moja zaidi ya wanawake mbona wanawake wameambiwa kuwatii waume, lakini waume hawakuambiwa kuwatii wake. Tena mume ni kichwa cha mkewe!

**Talaka**

Ni dhahiri ya kuwa baadhi ya wakati hitilafu kati ya mke na mume inazidi kiasi hiki ya kuwa mmoja anakuwa adui wa mwenzake. Kila jaribio la kuwapatanisha linashindwa. Bali hata inahofiwa isije mmoja akampa mwenzake sumu ili kumwua. Kama hali inakuwa mbaya kiasi hicho, bora waachane kisheria. Islam imeweka nafasi hiyo pamoja na kuonya ya kuwa anayeachana bila sababu za haki za kutosha atakasirikiwa na Mungu. Lakini Yesu anasema kuachana ni mwiko ila kama mke amezini (Mt. 19:9). Ni dhahiri ya kuwa fundisho hili ni pungufu sana. Uasherati tu sio sababu ya kuachana; bali ziko sababu nyingine pia ambazo zinafanya maisha yawe ni adhabu kubwa kabisa.

Kama mke hakuzini, lakini ni mwenye mdomo mchafu, ni mkali wa hali ya juu na kila aibu imo ndani yake, amekuwa ni adui wa mumewe, je wakiachana wamekosea? Hapana.

Ndoa maana yake ni kuwa hao waishi maisha mema ya utulivu. Lakini kama mmoja amekuwa ni sababu ya udhia kwa mwenzake, bila shaka shabaha ya ndoa imebatilika tayari. Hivyo wanaweza kuachana.

Tena mume tu ameambiwa na Ukristo kuachana na mkewe kama mke amezini. Lakini kama mume ni mzinzi, mke hakuambiwa lo lote.

Uhakika ni kuwa fundisho la Islam lina hekima; lakini lililoelezwa katika Injili halina busara.

Yesu alimwambia mwanamke mzinzi:

> "Enenda zako, wala usitende dhambi tena." (Yn. 8:11)

Kwa kweli hiyo siyo dawa kwa kufuta uasherati katika jamii, bali ni kuwahimiza wengine nao watende uovu huo, kwani wanajua wataambiwa tu: "Enenda zako."

**Kuolewa na Kutokuolewa**

Padre amesema kuwa ubikira ni jambo la hiari. Lakini Islam inafunza ya kuwa lazima mtu aoe au aolewe kama hakuna kizuizi maalumu kisichoweza kuepukika. Hakuna useja katika Islam. Paulo amesema kuwa kuolewa na kutokuolewa ni mamoja, lakini Yesu hakusema hivyo.

Padre amepotoka aliposema kuwa: "Kwa bahati mbaya, Muhammad hakuona faida ya mtu kujiweka wakfu kwa ajili ya Mungu..." (uk. 181)

Ndiyo kusema kwamba kwa padre kutokuoa au kutokuolewa ndiyo kujiweka wakfu kwa Mungu. Wazo hili limehesabiwa batili katika Islam, kwani katika hali ya useja mtu ataangukia dhambi kwa ajili ya hali ya

maumbile na badala ya kutumikia ufalme wa Mungu atauchafua. Hao 'watawa' wenyewe wanajua sana hali zao, hatuna haja ya kueleza. Dini inayofunza kinyume na tabia ya asili ya binadamu haiwezi kuwaongoza watu katika njia ya wema.

## Kutunza Mali

Padre amepotosha aliposema kuwa mahari inamwezesha mwanamke kujimudu pindi apewapo talaka. Kwa kweli, mahari ni zawadi ya arusi, wala siyo shabaha yake ya kuwa imsaidie mke atakapotalakiwa. Talaka hupatikana kwa bahati mbaya tu. Mke anaweza kuitumia mali ya mahari jinsi apendavyo.

Padre amedai kuwa Wakristo hawana fikira ya talaka wanapooa. Ijulikane kuwa na Waislamu pia hawana fikira hiyo wakati wa kuoa. Naam, haja ikipatikana mke au mume anaachana; katika Ukristo pia haja ikipatikana wanashika njia mbalimbali, ila tu haiitwi talaka.

## Alama ya Unyonge

Pole pole padre amezidi kujasiri hata akasema kuwa kuvaa shungi ni alama ya unyonge wa wanawake. Ameonyesha kuwa hana elimu kabisa alipoandika ya kuwa kuvaa shungi ni desturi ya wanawake wa Kiarabu. Hakika ni kuwa wanawake wa Kiarabu hawakuwa na desturi ya aina hii. Aya ya kuvaa shungi ilishuka baada

ya Mtume[saw] kuhamia Madina, ndipo wanawake wa Kiislamu wakaanza kuvaa hivyo. Tumeisha eleza hapo kabla ya kuwa hata Paulo aliwalazimisha wanawake kuvaa shungi. Padre amempinga hata Paulo kwa kumtaja (uk. 182). Lakini Paulo amejibu vizuri akisema:

> "Lakini mtu yeyote akitaka kuleta fitina, sisi hatuna desturi kama hiyo, wala makanisa ya Mungu." (1 Wakorintho 11:16)

Basi padre akileta fitina juu ya habari hiyo, ajue ya kuwa kuvaa shungi ndiyo desturi ya 'makanisa ya Mungu'.

## Bikira Maria

Padre amesema kuwa ingawa Waislamu hawapendelei ubikira, lakini wanamheshimu sana Bikira Maria. Kwa kweli, tunamheshimu Maria kama wanawake wengine waliokuwa wema sana; lakini heshima hiyo siyo kwa ajili ya ubikira wake, bali ni kwa ajili ya wema wake. Na kwa vyovyote ubikira haupendezi katika Islam. Kwa kweli padre pamoja na wafuasi wa makanisa wamepotoka kutuelewa vibaya sisi Waislamu. Ingawa imani yetu ni kuwa Yesu alizaliwa bila baba, yaani Maria alipokuwa bado bikira, lakini hatuamini kabisa ya kuwa yeye alibaki bikira maisha mazima.

Yule anayependelea useja bila kizuizi kisichoepukika, hawezi kuheshimiwa kwetu Waislamu. Bali tunaamini ya kuwa baada ya kumzaa Yesu, Maria alikaa na Yusuf

seremala kama mke na mume, na akazaa pia watoto wengine kwa Yusuf. Injili inatuambia:

> "(Yusufu) akamchukua mkewe; asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe; akaitwa jina lake Yesu." (Mathayo 1:24-25)

Ndiyo kusema kwamba baada ya Yesu kuzaliwa, Yusufu alimwingilia Maria, na ubikira wake ulikwisha.

Katika tafsiri ya Biblia kwa Kiswahili, wafasiri wamefanya hiana kwa kuandika tu "asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe", badala ya kuandika hata alipomzaa mwanawe wa kwanza", kama ilivyoandikwa katika tafsiri za Kiarabu na Kiingereza. Lakini kwa vyovyote inajulikana dhahiri kwa maneno ya Mathayo ya kuwa Yusufu alikaa na Maria kama mumewe na kwa hiyo hakubaki tena bikira.

Chini ya aya hiyo ya Mathayo, imeandikwa katika 'The Wycliffe Bible Commentary' ya kuwa maneno hayo yanaonyesha kuwa baada ya Yesu kuzaliwa Yusufu alimjua Maria, ila ni shauri lingine kama mtu ang'ang'anie imani yake ya kuwa Maria alikuwa bikira maisha mazima. Na katika 'The New Bible Commentary' tunasoma ya kwamba maneno 'mwanaye wa kwanza' yanaonyesha ya kuwa Maria alizaa watoto wengine pia baada ya Yesu, na kwamba hakuna mushikili kuamini hivyo kwani hata majina ya nduguze Yesu yametajwa katika (Marko 6:3).

Ile sehemu ya Marko iliyodokezwa juu yasema hivi:

> "Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu, na ndugu zao Yakobo, na Yuda na Simoni? na maumbu yake hawapo hapa petu?" (Marko 6:3)

**Kuzaliwa Bila Baba**

Ieleweke hapa ya kuwa ingawaje Yesu alizaliwa bila baba, lakini jambo hili haliwezi kumfanya yeye awe Mungu au mwana wa Mungu. Bali katika zama zetu hizi za elimu habari hii imeisha kubaliwa na wajuzi wa elimu ya utibabu ya kwamba mwanamke anaweza kuzaa bila kuguswa na mwanamume. Kitabu kiitwacho 'Anomalies and Curiosities of Medicine' kilichotolewa na W.B. Saunders & Co., London, kinaeleza kwa urefu habari ya kuzaliwa bila baba kwamba inawezekana. Vilevile katika Encyclopaedia Britannica chini ya neno 'Virgin Birth' (yaani kuzaliwa bila baba) habari hiyo imeelezwa, bali majina ya baadhi ya watu mashuhuri wa zamani yametajwa ambao walizaliwa bila baba.

Ni sawa ya kuwa Yesu alizaliwa kwa amri ya Mungu, lakini amri hiyo ilipata kutekelezwa kwa njia ya kanuni fulani. Na maelezo yake yaliyotolewa na wataalamu wa utibabu – kuhusu kuzaliwa bila baba — ni kwamba baadhi ya wanawake kwa sababu kadha wa kadha wanapata 'tumour' (kivimbe) ya aina fulani katika sehemu ya nyonga zao. Kivimbe hicho kinachoitwa '*arrhenoblastoma*' kinaweza kuzalisha 'mbegu' ambayo

mbegu hiyo inamfanya msichana kupata mimba bila kugusana na mwanamume au bila kuingizwa mbegu kwa msaada wa daktari. Basi na kuzaliwa kwa Yesu bila baba kunaweza kutokea kwa njia hiyo. Kwa kuwa habari hiyo haikujulikana katika zama zilizopita, hivyo Wakristo walilichukua jambo hilo kuwa tukufu kiasi hiki hata kwamba Yesu akapewa uungu. Na Wayahudi, kwa kuwa walimkataa Yesu, walifikiri kwamba Yesu alizaliwa kwa njia isiyo halali. Katika daftari ya kuandikia uzazi wa ukoo wake, kuzaliwa kwa Yesu kumeandikwa kuwa kwa haramu (Talmud).

Kwa vyovyote Kurani inakubali kwamba Yesu alizaliwa bila baba bila kulihesabu jambo hilo kuwa lenye kumpatia Yesu uungu. Mbegu ya uzazi iingie ndani ya mwanamke kwa njia ya mwanamume kumgusa au kwa vyombo vya hospitali au mbegu izalike mumo humo ndani ya mwanamke, mimba itapatikana, na mtoto atazaliwa na mtoto huyo atakuwa ni binadamu tu kabisa.

## Somo 22. Mwanadamu na Viumbe Wengine

Padre amesema ya kwamba hakuna dini inayoruhusu kuabudu viumbe. Ni sawa; lakini mbona Wakristo wanamwabudu kiumbe dhaifu sana aliyeitwa Yesu? Padre ameeleza ya kuwa vitu vyote vimeumbwa kwa manufaa ya binadamu, lakini hakuweza kutuambia aya yoyote ya Agano Jipya kuhakikisha habari hii, bali

amekimbilia Angalo la Kale (Zaburi). Lakini Kurani Tukufu inafunza waziwazi kwamba:

> "Na amewatiishieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini." (Al-Jaathiya 45:13)

Lakini ieleweke kuwa hii haina maana ya kuwa vitu vyote ni vyakula kwetu; bali tunapaswa kuvitumia ipasavyo.

Padre amehangaika bure kutuhakikishia kwamba Ukristo unafunza kuistawisha dunia hii. Hakueleza kutoka katika Injili habari hiyo, bali kataja Agano la Kale ambalo kwa imani ya padre halitakiwi baada ya ujaji wa Injili.

Padre ameitania Kurani eti inafunza kwamba maisha ya dunia ni upuuzi na mchezo (Al-Hadiid 57:21), kwa hiyo haina maana mtu atie bidii kuistawisha hii dunia. Ukweli ni kwamba Kurani inaeleza ya kuwa vyote vilivyoumbwa ni kwa ajili ya binadamu, kwa hiyo ni dhahiri kwamba mtu anapaswa kujaribu kujipatia manufaa katika hivyo vyote. Ile aya isemayo kuwa maisha ya dunia ni upuuzi na mchezo, inamaanisha ya kuwa maisha ya dunia yanapaswa kutumiwa ili mtu ajikuzie vipawa vyake vya mwili na roho na aungane na Mwumba wa dunia, lakini ni bahati mbaya ya kuwa mtu anasahau shabaha hiyo na kwa hiyo anayafanya maisha yake kuwa upuuzi na mchezo.

Padre hakumbuki maneno ya Yesu aliyomwambia tajiri kwamba:

> "Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote." (Marko 10:21)

Je huku ndiko kuistawisha hii dunia? Lakini Yesu amesema sawa, kwani huyo tajiri alikuwa mpenda mali kiasi hiki hata kwamba maisha yake yakawa ya kipuuzi, na ili kumtibu ilibidi huyo ajitenge na mali yake yote. Basi Kurani inaposema kuwa maisha ya dunia ni upuuzi na mchezo, inamaanisha maisha ya mtu kama huyo tajiri.

**Safi na Najisi**

Padre amesema kwamba:

> "Waislamu hawajafaulu kufuta tofauti iliyokuwa zamani kati ya vitu safi na vitu najisi." (uk. 188)

Jibu lake ni kwamba binadamu hana madaraka ya kugeuza sheria ya Mungu. Waislamu hawajajasiri kuihesabu sheria kuwa *'laana'* kama Wakristo walivyofanya kwa sababu ya ndoto ya mtu aliyezimia kwa njaa. Ndoto iliyootwa katika hali ya kuzimia haiwezi kuaminika.

**Hatima**

Mwishoni mwa kitabu chake, padre amelinganisha Kurani na Injili katika baadhi ya mambo fulani kuhusu Maria na Yesu. Katika sehemu hiyo padre amesema ya kuwa Kurani inamwita Maria mzaa Yesu

kuwa Binti Imran, na dadaake Haruni. Na kisha anapinga kuwa Kurani imechanganya Maria mamaake Yesu na Maria aliyekuwa dadaake Haruni aliyepita miaka 1400 kabla ya Yesu. Kwa kweli msomaji wa Kurani anaelewa sana ya kuwa Kurani inatambua vizuri kabisa tofauti ya zama za Nabii Musa na Haruni na Nabii Yesu. Kurani inaeleza mara kwa mara hali za watu wa zama za Nuhu, Ibrahimu, Musa, Haruni na manabii wengine na mwishowe Yesu pia. Kwa hiyo haina maana kusema kuwa Kurani haitambui historia na zama za Haruni na Yesu.

Hakika yenyewe ni kuwa Kurani inaeleza ya kwamba Wayahudi walipomwona Maria pamoja na Yesu wakamwambia kwa utani:

> "Ewe dada wa Haruni, baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa mwasherati." (Maryam 19:29)

Na sababu ya kumtania ni kuwa ndani ya Biblia Harun amehesabiwa kuwa Kuhani, na Maria naye alitolewa wakfu kwa hekalu. Basi watu walipoona kuwa Maria amejifungua bila ndoa, wakamtania kwamba 'wewe ulipojitolea kama Harun, ukajifanya dada wa Haruni, lakini mbona umemzaa mtoto?' Hivyo, siyo maana yake kwamba Wayahudi walimdhania kuwa dada hasa wa Haruni, ila walimtania tu.

Na vilevile sababu ya kumwita dadaake Haruni ni kwamba sawa na Agano la Kale (Hesabu 12:1-16) kulikuwa na dadaake Haruni aliyeitwa Mariamu ambaye alimsingizia Nabii Musa kwa sababu ya yeye kumwoa mwanamke Mkushi. Kwa hiyo Mungu Akamkasirikia huyo Mariamu na pale pale Mariamu akapata ukoma. Kisha kwa sababu ya maombi ya Musa, mama huyo akasamehewa na akapona baada ya siku saba. (Hesabu mlango wa 12). Basi, Wayahudi walipomwita mamaake Yesu kuwa dadaake Haruni walikuwa na maana ya kuwa yeye amejifanya kama yule Mariamu aliyefanya dhambi mbaya ya kumsingizia Musa na akaadhibiwa. Yaani yule Mariamu dadaake Haruni alitenda dhambi mbaya sana, nawe pia huitwa Mariamu uliyetenda vilevile dhambi mbaya kabisa ya kuzaa kwa njia isiyo halali; na kwa hiyo utaadhibiwa na Mungu jinsi alivyoadhibiwa mwenzako Mariamu aliyekuwa dadaake Haruni. Kwa hiyo, Wayahudi walimwita kama dada wa Haruni kwa utani siyo kwamba walimdhania yu dada hasa wa Haruni.

Ieleweke ya kuwa katika Biblia ya Kiingereza na Kiswahili yule dadaake Haruni ameitwa Miriamu, lakini tumesema Mariamu kwa kweli ni jina lile lile moja ila matamshi ni mbalimbali, kama vile Mariamu pia huitwa Maria. Hii ndiyo sababu katika Biblia ya Kiarabu na Kiurdu jina Mariamu limeandikwa katika

(Hesabu 12:1), baada ya Miriamu kama lilivyo katika Biblia ya Kiswahili na Kiingereza.

Pia ijulikane ya kuwa Biblia inasema kuwa Haruni na Mariamu wote wawili walimsingizia Musa. Hapo bila shaka Biblia imekosea, kwani Haruni sawa na Kurani alikuwa nabii wa Mungu, na nabii hawezi kufanya dhambi. Na usemi wetu ni sawa, kwani Biblia inaeleza ya kuwa Mungu Alipokasirika kwa sababu ya masingizio hayo, Akamwadhibu Mariamu tu wala si Haruni pia. Na Bibilia inaeleza ya kwamba Haruni alimwomba Musa kumwombea mama huyo ili apone. Hayo yanahakikisha ya kwamba Haruni hakuungana na Mariamu katika dhambi hiyo, waila wote wawili wangeliadhibiwa.

Padre Sale ameeleza ya kwamba Kurani imemwita Maria kuwa binti Imran kwa sababu Elizabeth, mamaake Mariamu, alitokana na ukoo wa Imrani. Hili pia ni sawa, bali tunamsifu Padre Sale aliyejaribu kutafuta sababu ya Kurani kumwita Mariamu kuwa Binti Imrani. Lakini Padre Anglars hakujifunza hata kutoka kwa padre mwenzake.

**Mwujiza?**

Padre amesema ya kwamba Kurani Tukufu inaeleza mwujiza wa Yesu alipozungumza katika utoto:

> "Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima." (Aali 'Imraan 3:47)


Kwa kweli kuzungumza huku katika utoto maana yake ni kusema maneno yenye hekima katika umri mdogo kuliko umri wa wataalam wa Biblia wa zama hizo. Siyo maana yake utoto hasa; bali umri mdogo kuliko Mafarisayo wa zama zake. Hata Mtume[saw] aliambiwa na wazee kuwa "mtoto". Tena kama huu ndio mwujiza kuzungumza katika utoto, mbona Kurani inaongeza kusema "na katika utu uzima." Je kuzungumza katika utu uzima pia ni mwujiza? Je watu wa kawaida hawazungumzi katika utu uzima? Kama wanazungumza, basi sio mwujiza. Bali maana yake ni kuwa Yesu alisema maneno ya hekima na busara katika udogo na utu uzima. Hivyo Yesu hakupaa mbinguni katika umri wa miaka 33, bali alizungumza katika utu uzima pia. Na hii ni sawa kabisa, kwani Wakristo wa karne ya pili walichora picha za Yesu zinazoonyesha kuwa Yesu hadi uzee katika dunia hii. Picha hizo zimechapishwa na wenyewe katika kitabu mashuhuri sana kiitwacho 'Encyclopaedia Britannica', jalada la 14. Tunazitia hapa chihi hizo picha kutoka kitabu hicho.



Yesu katika ujana



Yesu katika utu uzima




Yesu katika uzee

Picha iliyo kwenye uk. 266 tumechukua kutoka katika kitabu 'Das Linnen Kurt Berna Stultgrat' kilichotungwa na Hanas Naber Verlag. Wanasayansi wa Kikristo wa Kijerumani wamepiga hii picha kutoka katika 'sanda' alimofunikwa Yesu baada ya kuteremshwa kutoka msalabani. Kwa ajili ya joto la uhai zile dawa alizopakwa Yesu kabla ya kufunikwa katika hiyo shuka zikatia picha hiyo mle ndani ya 'sanda'. Hii inahakikisha kuwa Yesu alikuwa hai alipoteremshwa kutoka msalabani, la sivyo hiyo picha haingeweza kupatikana ndani ya shuka hiyo. Na huu ni uamuzi wa hao wanasayansi. Papa Pius IX alipoona hii picha akatamka:

“Picha hii haikuchorwa, na mkono wa binadamu.”

‘Sanda’ hiyo ipo hadi leo katika Kanisa la huko Turin, Italia. Kwa njia hii ukweli wa Kurani umedhihirika kwamba Yesu hakufia msalabani



Sura ya Yesu ndani ya ‘Sanda’

Padre amesema kuwa Kurani inamkubali Yesu kuwa Masiha. Ni sawa, lakini maana yake ni kwamba yeye alikuwa Nabii chini ya sheria ya nabii mwingine aliye mkubwa kuliko yeye, yaani Musa. Hata Seyidna Ahmad, mwanzishaji wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, ni Masihi naye yuko chini ya sheria ya Mtume Muhammad[saw], yaani ni mdogo kuliko yeye.

# LULU ZENYE THAMNI

Mishowe natoa tenzi zifuatazo zilizotungwa na Seyidna Ahmad[as] kwa lugha ya Kiurdu ambazo nimezifasiri kwa tenzi za Kiswahili.

## Muhammad ni Nuru

1. Muhammadi muongozi, ndiye wetu kiongozi,
   aloleta nuru hizi, yu mpenzi wangu miye.
2. Walotumwa na Latifu, wapitana kitukufu,
   bali mbele ya Raufu, kiumbe bora, ni yeye.
3. Waja wote wa zamani, kawapita kwa yakini,
   kwa uzuri na hisani, ndiye mbalamwezi yeye.
4. Ndiye mwezi kwa uzuri, na kizani yu baduri,
   kulla jicho lakhafiri, kivutika na nuruye.
5. Wote kachoka ndiani, katuvukisha ng'amboni,
   yu nahodha mwenye shani, kwake najitoa miye.
6. Mapazia kaondoa, kaonyesha kulla ndia,
   katuunga na Jalia, ndiye yeye mpenziye.
7. Mpenzi asooneka, na yule alofichika,
   katuonyesha hakika, si mwongozi ghairiye.
8. Yu mfalme wa dini, taji la murisalini,
   yu tayibu na amini, hiyo kweli ni sifaye.
9. Za Mungu zote amuri, katekeleza kwa ari,
   kabaini kulla siri, neema bora ni yeye.

10. Jicho lake darubini, moyo upo kwa Manani,
Kashika mwenge wa dini, chanzo cha nuru dhatiye.

11. Na siri kubwa za dini, hakuacha ufichoni,
utajiri wa rohoni, ndiye yeye atoaye.

12. Nuru huyu Muhamadi, najitolea fuadi,
yeye ndiye ninanadi, si kitu miye mbeleye.

☆ ☆ ☆

## Kazi Yetu ni Kunadi

1. Sisi tu shujaa watu, sojali bughudha katu,
   nyoyo zetu madhubutu, uchungu twavumilia.
2. Loungana na Kahari, kumsai siyo heri,
   Sikere simba wa pori, we bweha duni sikia.
3. Na katika njia yangu, Alinda Mwenyewe Mungu,
   sishinde njiani mwangu, washari kunivizia.
4. Nani ndiye mtukufu, na yupi mla nyamafu,
   ni suna yake Raufu, Hakosi kupambanua.
5. Kweli miye namuona, paziani Maulana,
   Kashika mkali sana, upanga kuuchomoa.
6. Adui loghafilika, kama angelizinduka,
   angeona pasi shaka, mkono wake Jalia.
7. Mkono wake Rabuka, na silaha aloshika,
   kwa adui ngeoneka; fahamuye ngepotea.
8. Angepotewa fahamu, na kusahau shutumu,
   angetokwa yote hamu, hamu ya kubishania.
9. Je katika ulimwengu, hakuna hakimu Mungu,
   dhalimu mpika jungu, wapi tapokimbilia.
10. Mbona mnaajabika, kwani Mola mtajika,
    Umasihi kanivika, ni kazi yake Jalia.
11. Zama muhimu za leo, zahitaji kwa kilio,
    afike kimbio-mbio, Masihi wake Rasua.
12. Nashuhudia mbinguni, jazba iso kifani,
    kuwaita insani, ukweli kuupokea.

13. Malaika wa Karima, wanawashukia wema,
walo na tabia njema, ili kuongoza ndia.

14. Wayoropa walo huru, welekea kwenye nuru,
Mungu Atawanusuru, wafu Anawazindua.

15. Wale wanotafakari, waiambia 'kwaheri'.
imani ya kikafiri, utatu waukimbia.

16. Utatu wakiritadi, wajitolea fuadi,
kwa shauku ilozidi, chemchem ya Umoya.

17. La shaka bustanini, mwa dini ya Rahmani,
ua zuri lenye shani, limepata kuchanua.

18. Kwani upepo wavuma, ulo wa harufu njema,
wenye kuleta uzima, upepo wa sharikia.

19. Miye napata harufu, ya wangu huyo Yusufu,
waona ni mpumbafu, bali ninamngojea.

20. Tazameni pande zote, duniani kote kote,
kwabudu sanamu kote, kunapata kufifia.

21. Kuwaabudu viumbe, hakuna heshima chembe,
walowasujudu kumbe, sasa wanaichukia.

22. Upepo toka mbinguni, wa Umoja wa Manani,
umevuma duniani, binadamu kuokoa.

23. Mioyo yao unasi, inaungana na sisi,
japo miyomo yatusi, inazidi kubwabwaya.

24. Sauti sikilizeni, isikikayo mbinguni,
inenayo kwa yakini, ‘kaja kaja Masihia.’

25. Na tegeni masikiyo, kwa ardhi inenayo,
kwa nguvu itangazayo, 'yuafika Mahadia.'

26. Mbingu inazimimimina, ishara za Subhana,
ardhi nayo yanena , ni zama za Masihia.

27. Ardhi pia na mbingu, hizi ni shahidi wangu,
sikilizeni wenzangu, kwa nguvu ninanadia.

28. Sasa hili bustani, ni pa raha kwa nsani,
haraka liingieni, porini loyuayua.

29. Baada muda madidi, kaja upepo baridi,
je hizi zama tarudi, Mungu ndiye Yuajua.

30 Kazi yetu ni kunadi, pande zote kwa juhudi,
mtu mwema hana budi, mwisho tanikimbilia.

☆ ☆ ☆

## Msaada Wenye Shani

1. Nisikieni jamani, hawaipati auni,
mlangoni pa Manani, rohoni walochafuka.

2. Hakika wetu Mwenyezi, katu Hawaangamizi,
waja wake Mwenye ezi, wale walotakasika.

3. Nao waliopotea, ndani ya Huyo Jalia,
ndio walokurubia, kwa Mola Alotukuka.

4. Wenye kiburi jamani, hawapenyi asilani,
barazani mwa Manani, baraza loheshimika.

5. Ombeni enyi wapenzi, kwa mengi mengi majonzi,
mwungane na Mwenye enzi, ndiyo hila sopotoka.

6. Tafuta wake mkono, kwa yote yote maono,
bila hata majivuno, wacha yote hilo shika.

7. Waja wake watukufu, Huwaauni Raufu,
Msaada maradufu, ajabu wamiminika.

8. Msaada wenye shani, ujapo kuwaauni,
watumishi wa Hannani, dunia yafadhaika.

9. Kama dhoruba wavuma, msaada wa Karima,
njiaye musitakima, husafika takataka.

10. Na pengine wadhihiri, kwa sura yenye hatari,
ndiyo adhabu ya nari, adui wateketeka.

11. Wageuka kuwa vumbi, langukia wenye dhambi,
kichwani pa wenye timbi, ndipo wakadhalilika.

12. Pengine huwa mawimbi, ya bahari na mafumbi,
hughariki wenye dhambi, waifanyao dhihaka.

13. Gharadhi kazi za Mungu, hawashindi walimwengu,
hata wapike majungu, wa viumbe Yu Rabuka.

☆ ☆ ☆

# FAHARASA

Faharasa hii imetengenezwa na vijana wetu wawili, Bwana Amiri Amri Abedi na Bwana Salum Muhammed Kungulilo, ambao wote hao ni wanafunzi wa kidato cha tatu.

Tarakimu zilizoandikwa mbele ya neno fulani ni ukurasa linapopatikana neno hilo.


**A**

*Adamu:*

- Si sawa na Mungu 177

*Adhabu:*

- imani ya Wakristo 200-201
- – kwa wahalifu 208
- – siku ya 205
- – ya ahera 206
- – ya moto 210

*Ahera:*

- frikwensi huko 218
- maisha ya 214
- miili huko 213
- wanawake huko 215

*Ahmad:*

- amtetea Muhammad[saw] 136
- ndiye Yesu 207

**B**

*Badr:*

- vita ya 25, 28, 180

*Bikira Maria:*

- alimzaa Yesu 257
- hakuwa bikira maisha yote 257
- alizaa watoto wengine 258

*Binadamu:*

- anayo mamlaka 153
- anapandishwa cheo 157
- asili ya sala 164-165
- awe mnyenyekevu 164
- katika taifa 237
- kuumbwa kwa – 228
- maadui wa – 224
- – na viumbe wengine 260
- usafi wa – 169

- wasaidizi wa – 224

*Bishara:*

- ya Ezekieli 54
- ya Mathayo 50
- ya Musa 23
- ya Yohana 54

**D**

*Dhambi:*

- husamehewa 199
- za moyoni 196
- za roho na mwili 175

**G**

*Galileo Galilei:* 47

**H**

*Hajira:* 1

- wa ukoo wa kifalme 1
- mamaake Ismaili 1
- mkewe Ibrahimu 150
- kujitolea kwake 240

*Haruni:*

- mtume na nabii 46

- ni kuhani katika Biblia 46
- hakuleta sheria mpya 46

*Hudaibiya:* 29

**I**

*Ibilisi:*

- hakuwa malaika 162

*Ibrahimu:*

- maagizo ya 164
- wazao wa 3
- na tohara 6

*Injili:*

- imevurugwa 68
- juu ya maradhi 221-222
- mafunzo kuhusu adhabu 208
- si maneno ya Mungu wala ya Yesu 68
- si sawa na Kurani 68

*Isaka:*

- si mtoto wa kwanza 2
- hakutolewa dhabihu 2

*Islam:*

- na kuwatendea wengine 238

- na heshima 242-243
- na kusaidiana 244
- na wanawake 244
- ujamaa wa 80, 239
- utimilifu wa vitabu vyote 81
- na sheria ya upendo 83
- na usafi 84, 170-171
- katika Afrika Mashariki 96
- haikuenea kwa vita 97
- haifundishi hirizi 102-103
- na upendo wa Mungu 147
- yakataza pombe 171
- yakataza nguruwe 171
- na talaka 121, 253
- na ujinga, umaskini, ufukara 181
- na utawala 228
- na utumwa 103

*Ismaili:*

- si mtoto wa mjakazi 1
- alitolewa dhabihu 2
- abarikiwa 3

**J**

*Jahanamu:*

- si ya milele 208
- maelezo ya 211, 215

*Jahangir:* 102

Jini:

- maana ya 226-227
- walisilimu 226

*Jiwe Kuu:*

- la pembeni 4, 49-50

**K**

*Kanisa:*

- na utumwa 104

*Kiyama:*

- hukumu ya 205

*Kurani:*

- imekuja kuokoa 188
- na radhi ya Mungu 192-193
- na kumpenda Mungu 147
- mpango wa 74

- usahihi wa 77
- yataja utatu 138
- juu ya utumwa 106-107

**M**

*Mahari:* 255

*Malaika:*

- kwa nini hawaonekani 212
- washauri wema 224

*Maria Kibtiya:*

- mkewe Mtume[saw] 39

*Mariamu:*

- mama wa Mungu? 144
- dadake Harun? 262

*Marwah:* 241

*Mauti:*

- ya mwili 188
- ya roho 188

*Mitume:*

- wamepita wengi 47
- idadi ya 47

- hawatendi dhambi 87
- waliteseka 134
- katika Biblia 135
- kazi ya 190

*Mkristo:*

- hana haja ya kulima 160
- hafuati agizo la Ibrahimu 164

*Muhammad[saw]*:

- hakutenda dhambi 86
- Mtume kwa wote 55, 87, 132, 134, 191
- katika Biblia 49-50, 80, 135
- Roho wa kweli 54, 60, 144
- na kuombaomba 187
- hakuiga Wayahudi 9
- na Wakristo 19
- mkubwa kuliko Yesu 20
- si mtume mgeni 23
- vita vyake 24
- ndoa za 30
- si kuhani 46

- afanana na Musa 51-52
- hakulelewa kipagani 85

*Mungu:*

- Habadili nia 22, 133, 172-173, 194
- watumwa wa 59
- Anayo mamlaka 87
- Husamehe dhambi zote 152, 199-200
- kadiri ya 147, 201
- neema za 180
- kukutana na 209
- wa Israeli 231
- wa Islam 231

*Musa:*

- biashara ya 23
- alifunza msamaha 65-66
- na kafara 155

**N**

*Ndoa:*

- ndani ya Agano la Kale 30
- Islam na 254
- mitara 30
- Yesu na 31-32

**P**

*Papa Leo II:*

- na utumwa 105

*Paulo*: 162, 236

*Pepo Mchafu*: 182, 226

*Petro*: 38

- ndoto ya 174

**S**

*Sala*: 164, 234

*Sara*: 4-5, 240

*Saumu:* 122, 172

- na Waislamu 198-199
- na Wakristo 198-199

*Shetani:*

- mshauri mbaya 224-225

*Shungi:*

- ni mtindo mzuri 43-44
- si alama ya unyonge 256
- katika Biblia 250-251

**T**

*Talaka*: 253

**U**

*Ukristo:*

- aina za 12
- hausamehi dhambi zote 200-201
- na Kadiri 201
- katika India 102
- na uhuru wa dini 232-233
- ujamaa wa 239
- na wanawake 245-246
- sikukuu za 241

*Utumwa*: 97, 103

Waisraeli na 9

**Y**

*Yesu:*

- alifunga saumu 198
- mtoaji pepo mchafu 220
- na ahera 86
- na amani 181
- na elimu 182
- kaburi la 126

- si kwa watu wote 54, 190
- mbele ya Mungu 194
- alijaribiwa na shetani 221
- picha za 266-268
- ujaji wa 207

**Z**

*Zaid:*

- amwoa Zainabu 34
- amwacha Zainabu 35
- mwana wa kupanga 33

*Zainabu:*

aolewa na Mtume[saw] 35